Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 27 Mei, 2014

*(Mkutano Ulianza Saa tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kwa Mwaka 2012/2013 *(The Annual Report and Accounts of Arusha International Conference Centre for the Year 2012/2013)*.

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. BETTY E. MACHANGU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Maoni ya Kamati

Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. PAULINE P. GEKUL (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 130

### Mbunge/Diwani Kutekeleza Ahadi Zake Wakati wa Uchaguzi Mdogo

**MHE. PAULINE P. GEKUL** aliuliza:-

Je, kwa mujibu wa Sheria wakati wa Uchaguzi Mdogo kwenye kijiji, mtaa au Kata, Mbunge au Diwani anaruhusiwa kutekeleza ahadi aliyotoa siku za nyuma wakati Kampeni zikiendelea?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi wakati wa Uchaguzi Mkuu wagombea wa Ubunge au Diwani wanaruhusiwa kufanya kampeni kwa madhumuni ya kuwashawishi Wapiga Kura wawachague. Katika kuwashawishi wapiga kura wagombea wanaweza kutoa ahadi ambazo watatakiwa wazitekeleze. Inawezekana wakati wagombea waliochaguliwa Wabunge au Madiwani wanatekeleza ahadi zao katika Jimbo/Kata pakatokea uchaguzi mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria za uchaguzi hazikatazi Wabunge na Madiwani kutekeleza ahadi zao wakati wa uchaguzi mdogo pamoja na kwamba Sheria za Uchaguzi hazikatazi, Wabunge na Madiwani kutekeleza ahadi wakati wa Uchaguzi Mdogo. Inashauriwa kwamba hekima na busara zitumike katika utekelezaji wa ahadi hizo ili isitafsiriwe kuwa mgombea au chama husika kinatoa rushwa kwa Wapiga Kura.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Mheshimiwa Waziri nakushukuru kwa majibu yako. Lakini najiuliza ni kwa nini umepotosha na unadanganya Bunge wakati Sheria ya Gharama za Uchaguzi Namba 16 ya Mwaka 2010. Ninayo hapa hiyo Sheria, *Section* ya 21 Sehemu ya 5 inasema vitendo vinavyokatazwa. Naomba ni-*quote section* ndogo Mheshimiwa Waziri inasema hivi:-

"Miradi ya kijamii au ahadi mbalimbali katika Jimbo yanaweza yakafanyika kabla ya mchakato wa Uchaguzi na kampeni kuanza. *Section* Namba *21 Section* ndogo ya tatu, inakataza wapiga kura kusombwa kupelekwa kwenye vituo vya kupiga kura. Inakataza ahadi hizo za Wabunge na Madiwani kutekelezwa wakati kampeni zimeanza". Mheshimiwa Waziri, kwa nini unasema hekima itumike wakati unajua ni Sheria na imekataza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa chaguzi tulizo nazo sasa katika nchi yetu, kuna chaguzi za Serikali za Mitaa, na Uchaguzi Mkuu ambako ni Madiwani, Wabunge na Rais. Chaguzi hizi zinaongozwa na Sheria mbili tofauti. Katika Chaguzi za Serikali za Mitaa vitambulisho vya kupiga kura au vya mpiga kura havitumiki.

Mheshimiwa Waziri huoni kwamba sasa ni wakati muafaka kuleta hizo Sheria mbili zirekebishwe ili hata katika chaguzi za Serikali za Mitaa vitambulisho vya mpiga kura vitumike? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri wewe ndiyo umechanganya. Mimi sijadanganya. Kwa sababu aidha kwanza kuna chaguzi za aina mbili. Chaguzi ya kwanza ni ile inayoitishwa ya miaka mitano na Tume ya Uchaguzi. Wakati ule tunafanya uchaguzi ule katika kipindi cha Uchaguzi Ukuu kunakuwa na *referee,* Kanuni zinatolewa na Tume ya Uchaguzi inasimamia wote tunajua. *(Makofi)*

Mambo gani yanatakiwa na mambo gani hayatakiwi. Kwa hiyo, huo uchaguzi wakati huo hakuna Mbunge katika Jimbo. Hakuna Diwani kwenye Kata. Wote tunasimamiwa na Tume ya Uchaguzi. Chaguzi ya pili mtu kafa, mtu kafukuzwa, Mwenyekiti wa Kijiji kafukuzwa. Mimi Mbunge wa Jimbo la Isimani, Mwenyekiti kafukuzwa, ninakatazwa nini kwenda kutekeleza ahadi kwenye Jimbo langu, kwani mimi ndiyo nachaguliwa? *(Makofi)*

Diwani kafa, kafukuzwa, mimi Mbunge nitasimama kufanya shughuli zangu katika eneo pana kwa sababu Diwani kafukuzwa haiwezekani. Juzi hapa Igunga mlishitaki kesi kwamba Serikali imefanya hivi imegawa mahindi. Mbona kesi imeamuliwa tumeshinda. Tumetoa mahindi wakati kuna njaa na Mahakama ya Rufaa imesema Serikali haiwezi kusimama kutekeleza jukumu lake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nafikiri Mheshimiwa Gekul unachanganya mambo mawili. Haiwezekani kuna uchaguzi mdogo katika Kata, Diwani kafa, halafu hatekelezi ahadi zake, inawezekana wapi? Nani huyo atakaetekeleza ahadi zake wakati tunafanya uchaguzi mdogo kwa mtu aliyekufa.

Haiwezekani, kwa hiyo kwa hiyo ni chaguzi umechanganya. Kwenye uchaguzi mkuu haiwezekani, kwa saabu unasimamiwa na Tume ya Uchaguzi na wote tunakuwa hatuna vyeo hivyo. Lakini kwenye chaguzi ndogo inategemea, kwa sababu kama ni uchaguzi wa Kijiji lazima yule Mwenyekiti wa Kijiji au kafa au kafukuzwa. Kwa hiyo hawezi kufufuka kutekeleza ahadi zake. Lakini mwenye eneo kubwa anaweza kufanya hizo kazi zake za ahadi alizofanya. Kwa hiyo Mheshimiwa Gekul nilifikiri hiyo nikuelimishe namna hiyo. *(Makofi)*

Lakini la pili hili la Sheria za Uchaguzi kati ya Serikali, Sheria inayosimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na uchaguzi wa Madiwani na Wabunge. Zoezi tunalokwenda nalo sasa marekebisho ya Katiba itakuwa ndiyo wakati muafaka wa kurekebisha jambo hili. Kwa sababu jambo hili linazungumzwa sana na mmekuwa mnazungumza sana kuanzia kwenye Katiba. Kwa hiyo, mimi ushauri wangu ni kwamba tuanze kwenye Katiba. Tushirikiane wote turudi tutengeneze Katiba nzuri halafu tushirikiane baada ya hapo turekebishe Sheria ya Uchaguzi ili nia yako njema iweze kutimia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mmesikia mrudi kwenye Kikao hapa. Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi. Swali la Mheshimiwa Catherine Valentino Magige. Kwa niaba yake Mheshimiwa Jafo.

Na. 131

**Utaratibu wa Kulipa Kodi ya Nyumba Kwa Mwaka Mzima**

**MHE. SELEMANI S. JAFO (K.n.y. MHE. CATHERINE V. MAGIGE)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzuia utaratibu wa wenye nyumba kulazimisha wapangaji kulipa kodi ya pango la mwaka mzima hali ambayo huwaumiza sana wananchi wengi wanaohitaji nyumba za kupanga?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentino Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1984 Serikali baada ya kutambua kero wanazopata wapangaji hususani wale wa nyumba wamiliki binafsi ikiwemo kudaiwa kodi kubwa sana na kutakiwa kulipa mwaka mzima, ilitunga sheria ya udhibiti na upangaji na kodi za nyumba yaani *The Land Restriction Act No.17* mwaka 1984.

Mwaka 2005 Sheria hiyo ilifutwa kupitia marekebisho ya Sheria Na. 2 ya mwaka 2005 yaani *The Written Laws Miscellaneous Amendment Na. 2 Act of 2005.*Sheria hiyo iliweka utaratibu utakaofuatwa na wenye nyumba kumtoza mpangaji kodi ya pango.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mambo yaliyolalamikiwa ni kuwa Sheria hii iliwapendelea sana wapangaji kuliko wenye nyumba. Aidha, kutokana na hali hiyo, soko la nyumba limeshuka na kusababisha upungufu wa nyumba nchini na hivyo kufanya wahitaji kukubali masharti yoyote watakayopewa na wamiliki ikiwa ni pamoja na kulipa kodi kubwa kwa mwaka au zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ipo haja ya kuweka utaratibu wa ulipaji wa kodi ya nyumba ili wananchi wengi wenye kipato cha chini wasiumie. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu sasa Wizara yangu iko katika hatua ya kuandaa Sheria ya Nyumba itakayosimamia

utekelezaji wa nyumba ikiwa ni pamoja na kusimamia masuala ya upangaji na kodi ya pango.

Namwomba Mheshimiwa Mbunge na wapangaji wote, wavute subira wakati Serikali ikiendelea kulifanyia kazi suala hili. Aidha niwaombe wenye nyumba za kupangisha wote nchini wasipangishe nyumba zao kwa muda wa mwaka au zaidi maana wapangaji wengi wanapata changamoto kubwa kwa kodi za muda mrefu. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nilipenda kujua yafuatayo:-

Kwa kuwa suala la upangaji wa nyumba na suala la bei linatokana na suala zima la *concept* ya *demand in supply* na kwa kuwa tunaangalia wapangaji wengi sana katika nchi yetu hasa walioko katika Jiji la Dar es Salaam changamoto imekuwa kubwa kutokana na uchache wa makazi na kwa kuwa Dar es Salaam iko karibu kabisa na Jimbo la Kisarawe ambao tunaona kwamba wakazi wengi wa Dar es Salaam wanaweza wakaishi Kisarawe pale na kufanya kazi yao Dar es Salaam na kwa kuwa Kisarawe tuna mpango nzuri wa mipango miji kuimarisha mji wetu wa Kisarawe na kuimarisha kuwasaidia watu wa Dar es Salaam.

Je, Serikali kwa kutumia Shirika lake la Nyumba ina mpango gani kujenga nyumba za kupanga katika Wilaya ya Kisarawe katika mpango huu miji ili mradi kuhakikisha wananchi wa Dar es Salaam wasipate tatizo kubwa la kodi ya nyumba iliyokuwa kubwa?

Jambo la pili, kwa kuwa tunajua kwamba changamoto ya bajeti yetu ukiangalia sasa hivi tuna uchache wa fedha na kwa kuwa watu wengi Tanzania hii wanalipa kodi za nyumba lakini kodi zile haziingii katika mapato ya Serikali.

Je, Serikali sasa kupitia Wizara ya Fedha ina mpango gani kuhakikisha kwamba wapangaji wanaolipa kodi za nyumba lakini zile kodi zinakatwa kodi kuingia Serikalini na Serikali iweze kuwahudumia wananchi wake katika mipango mablimbali, kama vile maji, afya na elimu? Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba panapokuwa na uhitaji mkubwa basi panahitaji pia uwepo wa rasilimali hiyo kwa ajili ya kuingia kwenye soko,na ni kweli kwamba Kisarawe ni eneo ambalo lipo karibu na eneo ambalo linahitaji makazi na kwamba *National Housing* wamekuwa wakifanya Shirika letu la Taifa

la Nyumba limekuwa lilkifanya hivyo katika Wilaya mbalimbali nchini na hata wakati wa Bajeti yetu tutaonyesha maeneo ambako *National Housing* wana miradi inayoendelea na mingine imekamilika.

Nichukue nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba kama anatuhakikisha kwamba eneo lipo. Maana changamoto kubwa hapo kwa *National Housing* hua ni maeneo. Wakishakuwa na lengo la kwenda kuwekeza mahali fulani eneo lile linaanza kuuzwa kwa bei kubwa sana na mpaka wanashindwa kupata maeneo. Kwa hiyo, maeneo yapo na kama masharti ya upatikanaji wa maeneo, na ikibidi hata hizi Halmashauri kutusaidia kutupatia maeneo *National Housing* wako tayari kuwekeza katika maeneo husika.

Namba mbili Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika Bajeti pamoja na uchache wa bajeti tulionao, eneo hili la nyumba, sekta ya nyumba lingeweza kuingiza kodi nyingi sana. Lakini shida tulio nao ni kwamba makazi mengi hayajarasimishwa, kwa maana ya kwamba bado maeneo mengi ni *squatter.*

Lakini kwa yale ambayo ni makazi yanayojulikana yenye hati tunajitahidi sana Serikali inakusanya kodi. Lakini nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba iko changamoto, na hapa tukubaliane kwamba kila mpangaji, kila mwenye nyumba anayepangisha, anaopata lile pato basi akumbuke kwamba ni lazima alipie kodi.

Tutajaribu kuona kama Wizara nini tufanye kwa haraka pamoja na changamoto tulizonazo za kielektroniki mtandao wa kisasa ambao tunaujenga sasa katika Wizara ambao utakuwa unahakikisha kwamba nchi nzima inajulikana na makazi yote yanajulikana tuone ni namna gani tnaweza tukasaidia katika kufanya makusanyo haya yawezekane. Lakini kwa sasa bado ni changamoto, na ni lazima kama Serikali tuweke mkakati na sisi kama Wizara tutajaribu kulifanyia kazi jambo hili. *(Makofi)*

**MHE. CECILIA D. PARRESO:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mara nyingi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tumesisitizwa kuundwa kwa Wakala wa Udhibiti wa Kodi za nyumba na makazi.

Lakini pia kutokana na hoja ya Mheshimiwa January Makamba na Bunge lako likapitisha Azimio la kwamba Serikali ilete Muswada wa kuunda mfumo wa kudhibiti kodi za nyumba mwaka 2012 na sasa yapata miaka mitatu majibu ya Wizara ni kwamba wako kwenye mchakato.

Je, Wizara hii kweli ina dhamira ya kuleta Muswada huu kutokana na Azimo la Bunge lako Mheshimiwa Naibu Spika?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia azimio iliyotokana na hoja ya Mheshimiwa Makamba, Serikali ilitoa ahadi kwamba tutaleta hapa marekebisho na kuzingatia yale yaliyoagizwa na Maazimio yale ya Bunge.

Lakini mchakato huu wa kubadilisha Sheria hauanzi tu mara moja ni hadi uweke Sera kwanza vizuri. Kwa hiyo, tumeanza na kutayarisha pia Sera ya Nyumba ambayo Sera iliyokuwepo ya nyumba na makazi lazima irekebishwe ili iweze ku-*accommodate* hiyo *scenario* ambayo ilitokana na agizo hilo lile la Kamati na hii tunaendelea nayo iko katika hatua nzuri.

Lakini pia tunaenda sambamba na uandaaji wa Sheria ya Nyumba na Makazi ambayo itaweza kuweza ku-*accommodate* pia hilo eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge anasema litatuwezesha kuweza kukusanya kodi kutoka katika sekta hii ambayo na mimi nakubaliana na yeye kwamba inaweza kuwa na mchango mkubwa sana katika ukusanyaji wa mapato ya Taifa.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa, Serikali ilipoacha kudhibiti au ku-*control* mambo ya upangaji wa nyumba na kuliachia soko liamue, nyumba zilizjengwa nyingi sana na ikapunguza matatizo ya nyumba takribani nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa kuwa, kama wale wenye nyunba, *Real Estate,* kama wao watapandisha sana soko litaamua na wanaweza wakakosa wapangaji. Je, Serikali haioni itakuwa vibaya sana kama itaingilia tena upangishaji wa nyumba na kodi? Hiyo inaweza ikapunguza ujenzi wa nyumba kwa wale *Real Estate* kama mimi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rita Mlaki, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, kwamba, sababu zilizosababisha kufutwa kwa ile Sheria iliyokuwa inawalinda wapangaji, *The Land Restriction Act*

ya Mwaka 1984, zilikuwa hizo ambazo nimezisema na ambazo Mheshimiwa Mbunge Mwuliza swali anazisema, lakini Mheshimiwa Mbunge unapofanya kitu Dunia na maisha ni *dynamic* lazima yanakwenda mbele.

Tunachokishuhudia sasa baada ya hayo ni kwamba, masikini ndio wanaoumia sana. Sisi Serikali ya Chama cha Mapinduzi hatuwezi kukubali kuona masikini wanaumia, wanapanga kwa gharama kubwa, kwa muda mrefu na hao matajiri wenye nyumba halafu tukasema tuliachie soko liamue, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchumi wa aina ya nchi kama ya kwetu, huwezi kuliachia soko moja kwa moja lika-*dictate* maisha ya kila siku ya watu wetu. Lazima tu-*balance,* tunajua nchi yetu ina watu wa kada zote, ina matajiri wakubwa, ina matajiri wa kati, lakini ina watu masikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukubaliane tu na Mheshimiwa Mbunge na nimshawishi kwamba, tutakuwa waangalifu sana katika kuitunga Sheria hiyo, lakini dhamira yake itakuwa ni nzuri haitaathiri soko na maendeleo yaliyojitokeza baada ya kufutwa kwa Sheria hii kwa maana ya kuongezeka kwa makazi mengi ya watu walioamua kuwekeza katika hii sekta. Tutajaribu ku-*balance* hizo *interest,* lakini masikini lazima walindwe na Serikali. *(Makofi)*

Na. 132

**Upandishwaji Vyeo Askari Polisi**

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED (K.n.y. MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA)** aliuliza:-

Yako malalamiko kwa baadhi ya Askari kutopandishwa Vyeo na wengine kupata Vyeo bila mafao ya vyeo hivyo:-

(a) Je, ni Askari Polisi Wangapi wamepandishwa vyeo kuanzia 2010 hadi 2012?

(b) Kati ya hao waliopandishwa vyeo ni Askari wangapi wamepewa maslahi yao kulingana na vyeo vyao?

(c) Je, ni Askari wangapi katika Mkoa wa Kaskazini Pemba wamepandishwa vyeo kuanzia 2010 hadi 2013?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Konde, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha mwaka 2010 hadi 2012 Maofisa waliopandishwa vyeo ni 623, Wakaguzi 847 na Askari wa Vyeo vya Chini 7,949.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya Askari 7,949 wa Vyeo vya chini waliopandishwa vyeo, 6,598 hawajarekebishiwa mishahara kulingana na Vyeo vyao. Aidha, Wakaguzi 907 na Maafisa 199 pia bado hawajapewa maslahi yao kulingana na nafasi zao mpya.

Hivi sasa zoezi la kuhuisha kumbukumbu litakalohitimishwa na urekebishaji wa mishahara linaendelea. Kukamilika kwa zoezi hili kutafanya kila Askari kuwa na kumbukumbu sahihi, ikiwa ni pamoja na kulipwa mshahara kulingana na vyeo vyao.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi kuanzia 2010 hadi 2013 jumla ya Maafisa, Wakaguzi na Askari 128 walipandishwa vyeo mbalimbali kutoka Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa mchanganuo ufuataoo:- Maafisa 7, Wakaguzi 18 na Askari 103. *(Makofi)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni jambo la kusikitisha kuona zaidi ya 80% ya Askari ambao walipandishwa vyeo mpaka leo hawajapatiwa mafao yao. Na ni Bunge lililopita tu la 14 Mhesimiwa Waziri huyuhuyu, alitujibu hapa kwamba, hakuna Askari ambaye hajatengenezewa malipo yake kati ya Askari ambao wamepandishwa vyeo. Leo anatujia na majibu ya aina hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize maswali zaidi ya matatu ikiwa itawezekana:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza; nilitaka *commitment* ya Serikali ni lini askari hawa sasa watarekebishiwa mishahara yao?

Hasa tukizingatia lugha ambazo sasa hivi zimekuwa zikitolewa na badhi ya Viongozi kutishia wananchi pale wanaposema kwamba, ikiwa tutakuwa na Mfumo wa Serikali Tatu, basi Wanajeshi pamoja na Vikosi hivi vitavua magwanda na kupindua Serikali.

Je, ili Askari hawa wasivue magwanda kupindua Serikali yenu ninyi *CCM* nini *commitment* ya Serikali katika hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali sijui matatu au moja ya Mheshimiwa Rajab, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina kumbukumbu za kuwa nilisema hakuna Askari anayetudai. Nakumbuka mara nyingi nikisimama hapa nawaomba tusaidie Bajeti iongezeke, ili kuondosha mashaka makubwa waliyonayo Askari wetu. Leo nimesema na nikatoa *figures* kwamba, hicho nilichosema ndio ambaco kipo kwenye maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali ni lini tutapandisha Vyeo?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu yangu ya msingi nilisema kwamba, kuna kumbukumbu ambazo zinarekebishwa. Kuna michakato miwili katika kupandisha Cheo cha Wakubwa na Wadogo. Wadogo kunatoka *Force Order* ambayo ikitoka inakwenda kwa ma-*RPC* na *RPC* lazima wazifanyie kazi kule Mikoani na kisha wazirejeshe kwa *IGP*. Hizo ndiyo sasa zitaanza kufanyiwa kazi kupitia Hazina na *authorities* nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna Maafisa ambao ni Wakaguzi kwenda juu, ambao kuna Tume ya Utumishi wa Magereza na Polisi ndio wanafanya. Hao wanawapa moja kwa moja barua zao Maafisa wahusika.

Kwa hiyo, mimi naamini kwamba, kama nilivyosema mchakato huu utakapomalizika na mchakato hasa wa kuweka kumbukumbu sawa na kuweka kwenye mitandao, utasaidia sana katika kuhakikisha kwamba, Jeshi litalipa mafao yao kwa wakati na hakutakuwa na uwoga wa kusema kwamba, Serikali itakuja kupinduliwa na hawa Askari wetu. *(Makofi)*

Na. 133

**Makazi Bora kwa Askari Polisi Zanzibar**

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE** aliuliza:-

Malengo ya Serikali kwa Jeshi la Polisi ni uboreshaji wa makazi bora kwa Askari Polisi.

Je, lengo hili limetekelezwa kwa kiasi gani kwa upande wa Tanzania Visiwani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda nijibu swali la Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mbunge wa Jang'ombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya Mpango wa Maboresho wa Jeshi la Polisi Nchini, Serikali imekuwa ikiboresha makazi ya Askari sehemu mbalimbali kama inavyoonekana. Aidha, kupitia njia ya ushirikishwaji umma wananchi wamekuwa wakichangia gharama za ujenzi wa Vituo na Nyumba za askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa Serikali imekamilisha ujenzi wa majengo mawili ya ghorofa 3 kila moja ambapo eneo la Unguja (Ziwani), Mkoa wa Mjini Magharibi kuna jengo moja na upande wa Pemba (Limbani). Mkoa wa Kaskazini Pemba kuna jengo moja.

Serikali ina mpango wa kuendeleza majengo mengine ya aina hii kama yatakavyojengwa sehemu mbalimbali za Zanzibar na nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla ambao wanashirikiana na Serikali katika kutatua kero za makazi bora kwa Askari wetu. Nitoe wito kwa wadau wengine nchini kuendelea kushirikiana na Serikali katika ujenzi wa nyumba na miundombinu mingine ya Askari Polisi.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na maghorofa yaliyoelezwa kuwa yamejengwa, mahitaji ya nyumba za Askari Polisi ni makubwa mno, bado wanaishi uraiani.

Je, Serikali haioni kuwa, hili ni tatizo kwa kazi za ulinzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; nyumba za askari zilizojengwa zilizobakia Ziwani bado zina matatizo, nyingine ni hatarishi hata kwa familia zao. Kwa hivyo, nilikuwa naomba Serikali ina mpango gani kuhusu hali hii iliyokuwepo Ziwani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge wa Jang'ombe, Mheshimiwa Mzee, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni kwamba, katika hali ya kawaida Askari wote wanatakiwa wakae Kambini. Hilo ndilo ambalo litaleta mazingira

halisi na bora katika kufanya kazi yao. Kuishi uraiani ni tatizo na sisi tunalifahamu, ikitokea dharura kutafutana sio rahisi; wengine wamelala nyumba ya tatu, wengine kubwa, wengine ndogo, na kadhalika. Kuwakusanya ukawaambia twendeni kazini, itakuwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, kukaa uraiani Askari kunapoteza, pamoja na haja ya kuwaweka karibu na wananchi, lakini tabia za Askari zinabadilika na nyingine zinakuwa si za kawaida. Kwa hiyo, hilo nalo tunaliona, lakini pia kuna tatizo la kiusalama; siku hizi za karibuni kumekuwa na uvamizi kukiwa na tatizo la korosho, Askari mbao wako karibu wanakatwa vichwa, familia zao zinateseka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tatizo ni kubwa nan i *priority* kwetu kuhakikisha kwamba, tunalirekebisha. Hata hivyo, nia ni tofauti na matokeo, tutaendelea kulielewa hili kwamba, ni tatizo kubwa na tutashirikiana katika kuhakikisha kwamba, tunalitatua na siku moja Askari wakae kwenye maeneo ya Kambi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kwamba, pale Ziwani kuna majengo aina nyingi. Kuna majengo ambayo yalijengwa enzi za ukoloni, majengo haya pamoja na kuwa ni ya zamani ni majengo bado yanafaa, madhubuti. Yana matatizo madogo madogo ambayo tunaendelea kuyarekebisha na ni majengo ya kutegemea kuliko yale mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna majengo mengine yalijengwa, nafikiri katika wanaita Ngazi Nje na Ndani, yalijengwa na Serikali ya Mapinduzi.

Haya ni majengo ambayo yamejengwa karibuni, lakini ndio yenye matatizo makubwa ya kuhatarisha maisha. Majengo yale tumeamua tuyavunje yote na ikiwezekana hayo mapya yatakayokuja tutajenga pale.

Mwisho ni majengo yale mapya ambayo ndio mfano kwa sasa. Ni mapya na tutaendelea kuyaendeleza yale hata pale tutakapovunja.

Na. 134

**Fursa ya Elimu kwa Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. NAMELOCK E. SOKOINE** aliuliza:-

Ibara ya 11(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka utaratibu wa fursa sawa kwa watu wote kupata elimu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa, wale wanafunzi wenye ulemavu wenye nia ya kusoma, lakini kutokana na umbali wa shule au kutokuwepo kwa mazingira rafiki kwa ajili ya hali zao wameshindwa kuendelea na masomo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Namelock Edward Sokoine, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua haki ya wanafunzi wenye ulemavu kupata elimu kwa usawa kabisa kama ambavyo wanafunzi wengine wanavyopata elimu. Kwa kutambua hilo, Serikali imetenga Shule za Msingi 37, Shule za Sekondari 39 na Vitengo 216 kwa ajili ya kutoa elimu maalum nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kutenga Shule Maalum zenye mabweni na vifaa maalum kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum, ambao wanakabiliwa na mazingira yasiyo rafiki kwa upatikanaji wa elimu, ikiwemo umbali, Serikali imekuwa ikiwatumia Viongozi kama Maafisa Elimu, Waratibu wa Elimu Kata, pamoja na Wanasiasa kupitia Vikao mbalimbali katika maeneo yao, lengo ni kusaidiana katika kuwabaini wanafunzi hao na kuwapeleka katika shule zenye miundombinu rafiki katika kuwapatia elimu bora.

Sambamba na hilo, kila ifikapo Mwezi Septemba ya kila mwaka Serikali kwa kuwatumia Walimu wa Shule za Msingi hufanya sensa ya nyumba kwa nyumba, ili kuwabaini watoto waliofikisha umri wa kuanza darasa la kwanza wakiwemo watoto wenye ulemavu na wanaotakiwa kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Elimu Jumuishi wa mwaka 2009 – 2017 wenye lengo la kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Sanjari na mpango huu, Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kukarabati majengo ya shule, ili yawe rafiki kwa wanafunzi wote. Vilevile Serikali imetoa Mwongozo wa Ujenzi wa Majengo yanayozingatia mahitaji maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kuwahamasisha wazazi na walezi wanaoishi na watoto wenye mahitaji maalum, wakiwemo wenye ulemavu, kuwapeleka kwenye shule zilizo karibunao kwa kuzingatia kiwango cha ulemavu. Natoa wito kwa Mamlaka zote za Elimu katika ngazi za Halmashauri, kuhakikisha kuwa fursa za

Elimu zinapatikana karibu na rafiki kwa wanafunzi wote na kwa wakati unaotakiwa.

**MHE. NAMELOCK E. SOKOINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa, bado wapo vijana wengi walemavu wa ngozi, hasa albino, wameshindwa kuendelea na masomo yao kwa sababu, ya kunyanyaswa.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kushirikiana na mimi kuhakikisha vijana hao tuanwasaidia, ili waweze kupata Vyuo vya Ufundi, ili waweze kusoma mwisho kujiajiri?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, bado wapo vijana wengi ambao wamefaulu kwenda Sekondari, hasa Shule za Kata, ambazo hizo ndio hazina kabisa mazingira rafiki ya kuwawezesha kuweza kupata elimu.

Je, Serikali inawasaidiaje watoto wa aina hiyo na hasa wengi waliopo vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Namelock kwa jinsi ambavyo anakumbuka pia, watoto hawa wenye ulemavu katika nchi ya Tanzania kuweza kuhakikisha wanapatiwa elimu. Naomba nimpongeze sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nakubaliana na Mheshimiwa Namelock kwamba, kuna haja ya kutizama kwa undani watoto hao wenye ulemavu na hasa hawa watoto wenye ulemavu wa ngozi, yaani albino, ni namna gani Serikali inaweza kuwasaidia kupata elimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe wito kwa Walimu wote na watoaji wa elimu katika maeneo yote ni marufuku kuwanyanyasa watoto wenye ulemavu wa aina yoyote wawapo katika maeneo yao na hasa wanapohudhuria masomo.

Hiyo ni marufuku, watoto hao wanatakiwa wapate haki sawa ya elimu kwa hiyo, kuwatendea jambo lolote la unyanyasaji ni kwenda kinyume na utoaji wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama anawatambua na kuwafahamu watoto hawa wenye ulemavu wa ngozi ambao wanataka kuendelea na masomo yao katika vyuo vya ufundi Serikali iko tayari kushirikiana nae na kushirikiana na Wabunge wote kuwabaini watoto hao na hivyo basi kuwatafutia vyuo ambavyo vitakuwa ni rafiki kwa

mazingira yao yenye usalama, wakaenda huko na wakaendelea na elimu ya mafunzo ya ufundi kwa faida yao na kwa faida ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili; Mheshimiwa Mbunge ametaka kujua Serikali inafanya nini, ili kuwasaidia watoto wale wanaofaulu na kwenda kwenye Shule za Kata, lakini wana ulemavu wa namna tofauti na hasa ulemavu wa viungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama nilivyojibu katika swali la msingi, tumetenga Shule Maalum za Msingi, tumetenga Shule Maalum za Sekondari na tuna Vituo Maalum 216.

Kwa hiyo, tunawaomba sana Waheshimiwa Wabunge kupitia Halmashauri zetu tupatiwe taarifa hizo na watoto hao tutawapeleka katika hizo shule tulizozitenga na wana haki ya kupatiwa elimu na tutashirikiana na ni lazima watoto hao wote wapatiwe elimu, hata kama ni Walemavu wana haki ya kupata elimu katika nchi yao ya Tanzania. *(Makofi)*

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itakubaliana na mimi sasa kwamba, pale ambapo kunakuwa na fursa za *Hostel,* wanafunzi wenye ulemavu wapewe kipaumbele?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimkubalie kabisa Mheshimiwa Al-Shamaa kwamba Serikali imeweka kipaumbele hicho na shule yetu kwa mfano ya Sekondari ya Pugu kipaumbele kimewekwa kwa ajili ya watoto wenye ulemavu kwa hiyo tuwasiliane tu kama anaona kuna tatizo mahali popote na Serikali itazingatia hilo na inaendelea kuzingatia. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nimefuatilia kwa makini sana majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kubwa ambalo amesema ni kwamba Serikali inajitahidi kukarabati shule mbalimbali ili kuhakikisha kwamba shule hizo zinakuwa na mazingira rafiki kwa walemavu.

Lakini utakubaliana nami kwamba hata shule zinazojengwa sasa hivi bado kabisa hazizingatii mazingira rafiki kwa maana ya kwamba watoto wenye ulemavu wanashindwa kabisa kuingia kwenye madarasa hayo, kwa sababu tu pale mlangoni kwenye kile kizingiti cha kupanda ni parefu sana. Sasa nataka kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri wanatoa tamko gani kuhusiana na shule ambazo zinajengwa sasa hivi kuhakikisha kwamba mazingira hayo yanakuwa rafiki ili wanafunzi wote wenye ulemavu wa aina yoyote ile waweze kuweza kuingia madarasani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu spika, ni kweli kabisa kwa muda mrefu majengo mengi yaliyojengwa katika shule zetu mbalimbali na hata katika vyuo vyetu vikuu na vyuo vingine hayakuwa rafiki kabisa ili kuwawezesha wanafunzi ama watoto wenye ulemavu kuweza kupata elimu kwa kutumia miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa ujenzi wa majengo ya shule zetu na hasa mpango wa ujenzi katika Elimu ya Sekondari yaani MES II sasa hivi kipaumbele kimewekwa na maagizo makali yametolewa ya kwamba kila jengo litakalojengwa ni lazima lizingatie mahitaji ya wanafunzi ama watoto wenye ulemevu.

Hivyo naomba kutumia Bunge lako Tukufu kuwatangazia wakandarasi wote na wadau wote wa elimu wanaoendelea kujenga majengo yoyote kuanzia sasa lazima wakumbuke kuhakikisha wanatengeneza miundombinu hiyo ikiwa ni rafiki kwa ajili ya watoto wetu wenye ulemavu na kutokufanya hivyo itakuwa ni kukiuka kabisa maagizo ya Serikali na kukiuka kuwatendea haki wtoto wetu wenye ulemavu nchini.

Kwa hiyo, wanisikilize hapa na wazingatie hilo na sisi kama wenye dhamana kwa maana ya Serikali tutajitahidi sana sasa kukagua na kuhakikisha kwamba agizo hilo linatekelezwa kwa manufaa ya watoto wetu kwa ujumla na hasa hawa walemavu.

Na. 135

**Gharama za Mbio za Mwenge wa Uhuru Nchini**

**MHE. JOHN J. MNYIKA (K.n.y LUCY F. OWENYA)** aliuliza:-

Kila mwaka kumekuwepo na mbio za mwenge katika kila Wilaya hapa nchini.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha hutumika kwa kila Wilaya kwa ajili ya mbio za mwenge na mwenge huo unagharimu kiasi gani kuuwasha na kuuzima?

(b) Je, ni faida gani zinazopatikana kwa kuwa na mbio za mwenge?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuu hutenga kiasi cha fedha kulingana na mahitaji na gharama halisi ya wakati husika kwa mfano mwaka 2012 jumla ya shilingi milioni 650 zilitengwa kwa ajili ya kuadhimisha uzinduzi na kilele cha mbio za mwenge wa uhuru. Kati ya hizo milioni 450 zilitumika na Wizara na shilingi milioni 200 zilitumika na Mkoa uliokuwa mwenyeji wa Sherehe za kilele cha mbio za Mwenge wa uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kiasi cha fedha zinazotumiwa na Wilaya ni kwamba zinatofautiana kulingana na michango ya wananchi katika Wilaya husika kwani michango hiyo ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo pambayo huzinduliwa wakati wa mbio za mwenge kwa ujumla mwaka 2012 wananchi walichangia kiasi cha shilingi bilioni 11,500,846,850.

Halmashauri za Wilaya na Manispaa zilichangia shilingi bilioni 45, wahisani na watu binafsi shilingi milioni 52,340,862 na Serikali kuu shilingi bilioni 49,154,437,995. Jumla ya michango yote ni shilingibilioni 158, 837,117,855.

Faida zinazopatikana kutokana na mbio za mwenge wa uhuru nchini ni pamoja na kuendelea kutunza historia na falsafa ya ukombozi wa taifa letu, kuhamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuendelea kuienzi amani, mshikamani, upendo na zaidi kupambana na aina yoyote ile ya kuwabagua Watanzania kwa rangi, dini au makabila yao na kuendelea kuhamasisha kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali na kujiletea maendeleo.

Mbio za mwenge wa uhuru hutumika kuhimuza miradi mbalimbali kwa njia ya kuweka mawe ya msingi au kuzindua miradi iliyowekewa jiwe la msingi mwaka uliopita na mwisho ni kuhamasisha moyo wa uzalendo na kujitolea kwa vijana na hasa kuonyesha umuhimu na nafasi yao katika kudumisha historia ya nchi yao, kulinda uhuru wa nchi yao na kuleta maendeleo ya nchi yao.

**NAIBU SPIKA:** Jamaa zangu mbona mwenge mmeunyanyukia namna hii. Mheshimiwa Mbunge wa Ubungo swali la nyongeza.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Nashukuru mwuliza swali hajajibu maswali ya msingi kwa sababu hajaketa orodha kwa kila Wilaya cha kiwango cha amechanganya fedha za kawaida za mbio za mwenge na fedha za miradi ya maendeleo za Serikali kuu na Halmashauri na watu binafsi ili ionekane kama vile mwenge una tija kubwa. Katika mazingira kama hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitabu cha taarifa ya miaka hamsini ya uhuru wa Tanzania bara mwaka 1961-2011 kinasema mwenge wa uhuru uliwashwa ili

umulike ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu kama ishara ya kuwapa matumaini waliokata tamaa, heshima palipo na dharau na upendo palipo na chuki. Sasa maswali mawili.

Je, Serikali iko tayari kutoa kauli kwa manufaa ya wananchi waliokata tamaa na ugumu wa maisha kupiga marufuku michango yote ambayo wananchi wanachangishwa kwenye mbio za mwenge wakati Serikali inatenga pesa za Bajeti kwa ajili ya mbio za mwenge?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili mbio za mwenge za mwaka huu na mimi mwenyewe nimeshudia kwenye televisheni ya Taifa na vyombo vingine zinatumiwa na wakimbiza mwenge kama jukwaa la kufanya propaganda ya Serikali mbili na kueneza chuki kwa Watanzania. Nauliza je, Serikali iko tayari kuwapiga marufuku wakimbiza mwenge wanaoendelea hivi sasa kuzunguka nchini na kufanya propaganda badala ya kuleta matumaini kwa Watanzania na kutimiza misingi ya mwenge na kama hilo halifanyiki basi mwenge huu uzuiwe na ufutwe. Naomba majibu kutoka kwa Serikali. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA UTAMADUNI NA MICHEZO**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mnyika Mbunge wa Ubungo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme tu kwamba Serikali haiko tayari kutoa tamko la kupiga marufuku michango na nisisitize kwamba suala la michango ni imani kubwa waliyonayo Watanzania kwa mbio za mwenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwamba Serikali inatumia mbio za mwenge kwa ajili ya kuhamasisha Watanzania kuhusu suala la Katiba na Serikali mbili, nataka niseme tu na Mheshimiwa Mnyika unielewe vizuri sana kwamba mbio za mwenge zinatumika kwa Watanzania kuleta amani, umoja na mshikamano lakini pili si wakimbiza mwenge tu wanaohimiza amani pengine wakimbiza mwenge wanatumia fursa nzuri zaidi wanapokutana na wananchi katika maeneo yote bila kujali itikadi zao za vyama, dini zao, wala makabila yao.

Pengine inakuwa tofauti zaidi wakimbiza mwenge wanafanya kazi nzuri zaidi kuliko wanavyofanya UKAWA kwa sababu UKAWA siyo wakimbiza mwenge lakini wapo wanazunguka nchi nzima na wao wakishinikiza suala hilo. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa naibu Spika, asante kwanza naomba nimtaarifu Naibu Waziri kwamba Spika alikataza UKAWA kutajwa humu lakini kwa sababu yeye amehitaja halafu hamjamzuia kuanzia leo tutaendelea kui-*mention* UKAWA ndani ya Bunge kila tutakapopata nafasi ya kufanya hivyo. Lakini niongezee alipoongea Mheshimiwa Mnyika kuhusiana na kuwalazimisha wananchi michango *particularly* walimu.

Walimu wamekuwa wanalalamika sana kwamba Serikali inawalazimisha kuchangia mbio za mwenge wakati ni wazi kwamba walimu wengi hawataki. Sasa mnakuwaje, mnatoa wapi utu wa kuwakata walimu kinguvu wakati walimu hao hao mnashindwa kuwalipa vizuri na wanalalamika kila siku.

Sasa ni lini Serikali itaacha kuwalazimisha walimu kuchangia na wakati huo huo kwa sababu Serikali ni moja hata kama wewe siyo Waziri wa Walimu niseme kwamba kwa kutumia nafasi hii kwamba mrudishe posho ya walimu ya kufundisha kwa sababu walimu hawana kipato cha kutosha nab ado mnawalazimisha kuchangia michango kama ya mwenge ambayo haina tija kwao?

**NAIBU SPIKA:** Kabla ya kumruhusu Mheshimiwa Naibu Waziri kujibu swali hili nifafanue tu kwamba Mheshimiwa Waziri nifafanue tu jambo moja. Alichokipiga marufuku Mheshimiwa Spika, ni kambi Rasmi ya Upinzani humu Bungeni kujibandika jina ambalo halipo katika Kanuni zetu. Alichokisema Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba kuna kikundi kinazunguka nchini na wala siyo siri, chenye jina hilo. Kwa hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri yuko sahihi kabisa. Majibu ya swali la nyongeza. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbilinyi Joseph, Mbunge wa Mbeya Jiji kwa niaba ya Waziri wa Habari. Michango inayotolewa na wananchi kwa ajili ya shughuli za maendeleo, michango inayotolewa kwa shughuli mbalimbali za maendeleo tumeshatoa ufafanuzi mara nyingi huwa inakuwa ni makubaliano yanayofanywa na wachangaji wenyewe na katika mwenge wa uhuru moja ya jukumu kubwa mwenge wa uhuru mara nyingi unahamasisha shughuli za maendeleo katika Wilaya mbali mbali.

Kwa hiyo, kama wananchi wamekubaliana kuchangia ujenzi wa shule na miradi Fulani Fulani ya maendeleo kwa kuchangia kwa hiari hilo ni jambo jema na Serikali haiwezi kuzuia.

Siku zote tumesema hakuna michango ya kulazimishana, Serikali imeshawahi kusema siku zote tumeshasema hii siyo mara ya kwanza hatujawahi kumkamata mtu kwa sababu ameshindwa kuchanga mchango. Kwa hiyo Serikali itaendelea kuhimiza wananchi kuchangia shughuli zao za maendeleo

bila kujali ni wakati wa mwenge, wakati mwingine wowote ili mradi michango hiyo iwe ni hiari na michango hiyo ionyeshe shughuli zinazofanywa na taarifa zitolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa yenu michango hii hainunui mafuta ya kuendesha chombo kile. Hailipi posho ya wale wakimbiza mwenge. Kwa hiyo michango itaendelea kutolewa, ili mradi tu iwe ya hiari, siyo ya lazima na kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Inaweza kuhamasishwa kupitia mwenge, inaweza kuhamasishwa kupitia vijiji, inaweza kuhamasishwa na viongozi wowote katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI SULEIMAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nishukuru sana Serikali yetu kwa kuendelea kuenzi mwenge na mbio za mwenge.
Lakini niwashukuru pia Watanzania wote wanaoendelea kuchangia na kushiriki katika mbio hizi Tukufu za mwenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali sisi wananchi wa Kishapu na leo nina baraza la Madiwani lote la Kishapu hapa pamoja na Madiwani wengine wa vyama vya upinzani tunaiomba Serikali kwa kuwa tunathamini na kuenzi Mwenge na mbio za mwenge hasa katika shughuli za Maendeleo, kudumisha amani na utulivu na upendo wa nchi yetu.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri uko tayari kutuongezea wigo wa mbio za mwenge katika vijiji zaidi vya jimbo la Kishapu ili wananchi wa kishapu waweze kupata fursa ya kuuenzi na kuuona na kupokea ujumbe wa mwenge hata katika vijiji vyote 122 vya jimbo la Kishapu?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA UTAMADUNI NA MICHEZO**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nchambi, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikupongeze sana wewe na Halmashauri yako na wananchi wote wa Wilaya yako na Mkoa mzima wa Shinyanga kwa kuelewa na kutambua umuhimu wa mbio za mwenge. Si mwenge huu wa uhuru tu unaokimbizwa Tanzania tunaoufahamu, uko mwenge wa *Olympic* ambao unakimbizwa dunia nzima, kiko kifimbo cha Malkia ambacho pia kinakimbizwa katika nchi zote za *Commonwealth* lengo ni kuleta mshikamano wa Taifa na Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala lako la kuongeza wigo wa mwnge ili ukimbizwe zaidi katika Wilaya yako ya Kishapu tumelichukua tutalifanyia kazi, asante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nisimame tu kwa sababu jambo lenyewe kubwa hili lakini naona kama vile tunataka kulifanya dogo sana, halina maana kwa taifa letu jambo ambalo siyo zuri sana. Wakumbuke Waheshimiwa Wabunge kwamba mwenge huu unapokimbizwa nchini kila mwaka kuna kauli mbiu yake na hizi kauli mbiu ni kwa sababu mwenge una fursa ya kupita maeneo mengi.

Kwa hiyo, tunatumia muda ule vile vile kutoa elimu katika masuala yale mazito ya nchi jambo ambalo ni zuri sana na linatakiwa kwa kweli kila mmoja kuona Serikali ilichokifanya ni sahihi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili naelewa inawezekana kabisa wenzetu upande wa kambi ya upinzani hili lisiwapendeze sana. Lakini kupitia mwenge huu tunahamasisha jamii iweze kuona umuhimu wa kujitolea katika shughuli za maendeleo katika maeneo yao mbalimbali na ndiyo maana katika kila tunapokimbiza mwenge ni lazima tuseme ni miradi mingapi, yenye thamani gani, wananchi wamechangia kiasi gani ili kuamsha tu moyo wa Watanzania kuenzi suala hili la watu katika shughuli hizi ambazo ni za jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi sioni kwamba hili jambo lina ukakasi hata kidogo. Sasa naelewa hoja yenu ni kitu kinaitwa michango. Mimi nazungumza michango, kama ambavyo wenzangu wamesema michango wakati wa mwenge inategemea mwenge huo kama unakuja kulala kibaoni kwangu kijijini kinachofanyika ni watu kutambua tu kwamba watakuwa na ugeni mkubwa huu wa watu ambao wanafanya kazi nzuri ndiyo.

Kwa hiyo, yule ambaye ananafasi ya kuchangia kuku, mwenye nafasi ya kuchangia bata, anaweza kufanya hivyo na hii si dhambi na nataka nionyeshe tu kwamba Watanzania kwenye jambo hili ni wakarimu sana wamefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

Na. 136

**Taarifa za Kuwepo kwa Madini ya Urani Wilaya ya Bahi**

**MHE. OMARY AHMAD BADWEL** aliuliza:-

Kumekuwepo na taarifa zisizo rasmi za kuwepo kwa Madini aina *Uranium* katika Wilaya ya Bahi:-

(a) Je, ni lini Serikali itatoa tamko rasmi kwa viongozi na wananchi wa Bahi juu ya kuwepo kwa madini hayo na ni lini yataanza kuchimbwa?

(b) Kama uchimbaji utaanza. Je, Serikali imefanya maandalizi gani hadi sasa ya kutoa elimu na utaratibu wa fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yatachukuliwa na mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mhesimiwa Ahmed Badwel, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wakijiofizikia yaani *airborne geophysical survey* uliofanywa miaka ya 1979 hadi mwaka 1982 ulionyesha uwezekano wa kuwepo kwa mashapu yenye madini ya urani katika baadhi ya maeneo nchini katika wilaya ya Bahi. Madini ya Urani yamegundulika kuwepo katika maeneo ya mbuga ya Bahi, mbuga ya Chimendeli, Chali Igongo na maeneo yanayopakana na wilaya ya Manyoni yaani Kigwe yaani Bunga ya Ilindi, Bahi Kaskazini, Bahi Kusini, mbuga ya Kibuga, Mbuga ya Issuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Serikali imetoa leseni sita kwa ajili ya utafutaji wa madini ya urani katika eneo la Bahi kwa kampuni mbalimbali. Kwa nyakati tofauti kampuni hizo hususan *Tanzoz Uranium Limited na Mantra na mantra Tanzania Limited* zimefanya utafiti wa urani na matokeo yake yanaonyesha kuwepo kwa madini ya urani katika eneo hilo. Kampuni ya *Tanzoz* imefanya uchorongaji na kwa sasa wanasubiri majibu ya maabara. Utafutaji wa madini unaofanywa na kampuni hizo bado unaendelea na utakapokamilika Serikali itawafahamisha wanai wa Bahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kutoa elimu kwa makundi mbalimbali wakiwemo wananchi wanaoishi maeneo ambayo utafiti wa madini hayo unaendelea hapa nchini. Ili kuondoa hofu ya madhara ya uchimbaji wa madini hayo mfano Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Adam Malima, aliwahi kutembelea Wilaya ya Bahi, Manyoni na Namtumbo, akiongozana na wataalam wa Madini kwa ajili ya kutoa elimu ya juu ya mpango wa Serikali katika utafutaji na uchimbaji, usafirishaji wa Madini ya Urani nje ya nchi.

Aidha, wadau wengine zikiwemo kampuni za utafiti na taasisi zisizo za kiserikali wamekuwa wakitoa elimu hiyo katika maeneo mbalimbali yenye utafiti wa madini haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ulipaji wa fidia wananchi ili kupisha shughuli za mradi huo, kazi hii itafanyika pale tu kampuni husika itakapojiridhisha kuwepo kwa mashapo ya urani yanayoweza kuchimbwa kwa faida. *(Makofi)*

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa Bahi wamesubiri sasa kwa muda mrefu juu ya matokeo ya utafiti wa upatikanaji wa madini ya *uranium* katika maeneo hayo mbalimbali ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyataja na wakati wananchi hawa wanasubiri matokeo hayo wengi wa wananchi hao wameshindwa kuendeleza maeneo yao ama mashamba ama ujenzi kutokana na hofu kwamba heunda maeneo yao yakaingia katika uchimbaji wa madini ya *uranium*. Sasa ni lini Serikali inawaambia wananchi wa Bahi kwamba itasimamia zoezi la utafiti liweze kukamilika mapema na wananchi wale wa Bahi na maeneo mengine waweze kujua hatima ya maeneo yao?

Kwa kuwa, watafiti ambao amewataja Mheshimiwa Naibu Waziri ambao wamekuja katika wilaya ya Bahi kufanya utafiti wakati mwingine wamekuwa wakiingia katika maeneo ya mashamba maeneo mengine yanayomilikiwa na wananchi bila taarifa na kufanya utafiti wao ambao wanaruhusiwa kuchimba katika maeneo yale bila kuwaarifu wenyewe na kuleta migogoro au hata kuwalipa au kulipa chochote kwa ajili ya kufidia wakati wakiondoka waweze kutengeneza yale maeneo.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema nini juu ya watafiti hao wanaokuja bila taarifa kwa Serikali au watu wanaohusika na maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba shughuli za utafiti wa madini zinafanywa kwa mujibu wa sheria ya madini ya 2010 na katika sheria ya madini inaelekeza kabisa kwamba kampuni yoyote inayofanya utafiti ambayo inamiliki leseni ya utafiti inapaswa kurejesha ripoti, *quarterly report* katika Wizara ya Nishati na Madini, ambazo ripoti zile ndiyo tunazifanyia *assessment* na kuona maendeleo ya utafiti katika eneo husika.

Haya ni masharti ya leseni, kampuni yoyote ambayo haitekelezi masharti haya Serikali huifutia leseni kampuni hizo na hivyo katika eneo la Bahi, kampuni zinazofanya utafiti pale zimekuwa zikileta ripoti na ripoti inaonyesha bado kuna kazi ya uchorongaji zaidi inahitajika ili kuweza kuthibitisha madini ya mashapo ambayo yako pale chini na kuweza kuruhusu uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tena sheria ya madini haswa kwenye eneo hili la kutoa taarifa kwenye mamlaka husika *section 95* ya sheria yetu ya madini inaelekeza kampuni zote ama mtu yeyote anayemiliki leseni ya madini ni lazima afike kwenye maeneo na mamlaka husika atoe taarifa kwamba anaendeleza shughuli za utafiti katika maeneo husika.

Hivyo, nitumie nafasi hii kuyaagiza makampuni yote ambayo yanamiliki leseni za utafiti waweze kutoa taarifa kwenye mamlaka husika ikiwemo ofisi za wakuu wa mkoa, ofisi za wakuu wa wilaya pamoja na halmashauri zetu, ili wananchi pamoja na viongozi wa maeneo wahusika wajue shughuli zinazoendelea kwenye maeneo yao.

Kuhusu suala la tozo hili kwa mujibu wa sheria zetu za Serikali za Mitaa zinaeleza wazi sheria ya fedha ya Serikali za mitaa ya mwaka 82 kwamba Serikali inapasa ilipwe asilimia 0.3 ya mapato ya kampuni inayofanya shughuli katika eneo husika. Hivyo pindi kampuni hizi zinazotafiti eneo la Bahi zitakapoanza kuzalisha basi zitapaswa kulipa kulingana na sheria hiyo.

Wito wangu kwa wananchi wa Bahi, hususan halmashauri wahakikishe wanaandaa bylaws zao mapema ili kuepuka migogoro ambayo tuliipata katika maeneo mengine ya uchimbaji na hivi sasa tumefaulu kurudisha asilimia 0.3 kwa maeneo ambayo *African Barrick* wanachimba, kwa hiyo Bahi pia ni vizuri mkajiandaa mapema. *(Makofi)*

Na. 137

**Hitaji la Umeme wa Solar Tarafa ya Lukula**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza:-

Serikali kupitia *REA* imeahidi kupeleka umeme maeneo ya kata ya Kipiri kwenye Vijiji vya Kiyombo na Kilumbi:-

Je, Serikali kupitia *REA* inaweza kupeleka umeme wa *solar* kwenye Makao Mkuu ya Tarafa pale Lukula, Kata ya Kitunda?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia wakala wa Nishati vijijini *REA* itatekeleza mradi wa awamu ya pili wa kufunga mifumo ya umeme jua kwenye taasisi za umma kwenye wilaya ya Sikonge. Utafiti wa vijiji pamoja na taasisi zitakazonufaika na mradi huo ulifanyika mwaka 2010 mradi huu utahusisha kata za Chabutwa, Igigwa, Ipole, Kiloleli, Kipanga, Kipiri, Kitunda, Pangale, Sikonge na Tutuo katika wilaya hii ya Sikonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unatarajiwa kuanza wakati wowote mwaka huu wa 2014 na utakamilika mwaka 2018 kwa gharama ya dola za Marekani milioni 15. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa zoezi la kufunga mifumo ya umeme jua kwenye maeneo yaliyo nje ya miundombinu umeme kutoka kwenye *grid* ya Taifa ni endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wilaya nyingine zitakazonufaika na mradi ni Biharamulo, Chato, Bukombe, Kasulu, Kibondo, Tunduru na Namtumbo. Majadiliano na mkandarasi yatafanyika mara tutakapopata *no objection* kutoka Benki ya Dunia hivyo tunaomba uvumilivu wakati huu Serikali ikitafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa miradi ya umeme jua kwenye maeneo ambayo hayapo katika huduma ya umeme ya *grid*.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize maswali mawili. Kwa kuwa vipo vijiji vya kata ya Kisanga na vijiji vya kata ya Kiloli ambavyo havimo kwenye mfumo aidha wa grid ya Taifa au ule wa mfumo wa jua kwa maana ya *solar.* Je, sasa Wizara na *REA* wako tayari kuziingiza kata hizo katika awamu zijazo?

La pili, kupitia *REA* wilaya ya Sikonge inapata umeme kwenye vijiji 18, lakini wananchi wamekuwa wanasubiri kwa muda mrefu sana zoezi hili halijaanza yakiwemo na maeneo mengine kama Mvomero na baadhi ya maeneo mengine ambayo yamekwishaahidiwa kwa muda mrefu.

Je, Waziri anaweza kuniambia hapa kwamba ni lini kazi hiyo itaanza rasmi kwa haraka na kasi zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kijiji cha Kisanga hakiko katika mpango wa *REA* sasa hivi.

Lakini kama nilivyokuwa nikijibu hapo awali ni kwamba Serikali ina mpango wa kuhakikisha kwamba vijiji vyote katika nchi yetu vinapatiwa umeme. Lakini hatua hii itakwenda awamu kulingana na pesa zitakavyokuwa zikipatikana. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu kwamba kijiji cha

Kisanga kitaingizwa katika mpango pale ambapo pesa zitapatikana hapo mbeleni.

Kuhusu vijiji 18 katika Jimbo la Sikonge pamoja na Mvomero, niseme tu kwamba nimhakikishie wakandarasi sasa hivi wako Mvomero, wako Mkoa wa Tabora na vilevile watafika katika wilaya ya Sikonge na nimhakikishie tu kwamba *REA No. II* imeshaanza na tunatarajia kwamba ifikapo tarehe 30 Juni, 2015 mradi huu utakuwa umekamilika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda tuishie hapa maswali yaliyobaki yatapangiwa wakati mwingine, ambayo ni swali Namba 138 na 139. Kwa sababu leo ni siku ambayo imebana sana mambo yetu ni mengi sana, inabidi twende kwa wakati.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitoe matangazo kwa haraka haraka. Wako wageni wa Mheshimiwa Benard Membe, Waziri wa Mambo ya Nje ya ushirikiano wa Kimataifa ambao ni Mama Dorcas Membe mke wake, asimame pale alipo, karibu sana. Wako watoto wake watatu wa Mheshimiwa Membe ambao ni Ndugu Cecilia, Richard na Esther, ambao wameambatana na Ndugu watano wa familia karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni ya kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Ndugu John Haule, Katibu Mkuu wa Wizara, ahsante karibu, Ndugu Rajab Gamaha, Naibu Katibu Mkuu, karibu Ndugu Christopher Liundi, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha *AICC*.

Ndugu Elishilia Kaaya, Mkurugenzi Mtendaji Kituo cha Mikutano cha Kimataifa *(AICC),* Ndugu Twalibu Mahundi, Katibu wa Chuo cha Diplomasia, Balozi Mohamed Mahundi, Mkuu wa Chuo cha Diplomasia. Pia wako Wakuu wa Idara na Vitengo vya Wizara ya Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Kimataifa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge pia miongoni mwa wageni wa Mheshimiwa Benard Membe ni Katibu Mkuu wa *SADC* Dkt. Stagomena Tax, yuko wapi Katibu Mkuu huyo hajafika? Ahsante sana na tunakupongeza sana sidhani toka umeteuliwa kuwa Katibu Mkuu umeshafika hapa Bungeni. Dkt. Charles Mubita, Msaidizi wake, Mheshimiwa Juma Khalfan Mpango Balozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na wakuu wa Mabalozi nchini Tanzania, karibu sana.

Mama Sinika Antila, Balozi wa Finland nchini Tanzania, pale mlipo, Ndugu Zakaria Ashall Balozi wa Indonesia nchini Tanzania, Ndugu Medghji Agah Safar balozi wa Iran nchi Tanzania, Ndugu Ismail Noleat balozi wa Libya Tanzania, Dkt.

Hamada Badui Mohamed Faki Balozi wa Comorro Tanzania, Ndugu Hyasinta Magumu Kaimu Balozi wa Msumbiji nchini Tanzania, Ndugu Lambet Sano, Kaimu Balozi wa Rwanda nchini Tanzania, Ndugu Mussa Kaimu Balozi wa Nigeria Tanzania, Ndugu Mendesi Bomu Kaimu Balozi wa Angola nchini Tanzania, Mr. Chu Hang naibu Balozi wa China nchini Tanzania, mama Marvis Tungulu afisa balozi wa Namibia nchini Tanzania na Ndugu Nikita, afisa ubalozi Urusi nchini Tanzania. *(Makofi)*

Pia katika wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni wanafunzi 55 kutoka chuo Kikuu cha Kidepromasia Dar es Salaam, simameni pale mlipo, ahsante sana karibu sana wanafunzi kutoka chuo chetu cha Diplomasia karibu Bungeni mjifunze namna Bunge lenu linavyofanya kazi.

Tuna wanafunzi 25 kutoka chuo kikuu cha Dodoma, (*UDOM),* karibuni sana wanafunzi kutoka chuo Kikuu cha Dodoma hapa Bungeni, wanafunzi 25 kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe, wanafunzi 25 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, karibuni sana. Wanafunzi wa kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mlimani, Wanafunzi sita (6) kutoka chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine, karibuni sana kutoka Chuo kikuu cha Augustine, sijui *campus* ya wapi. Wanafunzi kumi kutoka vyuo vikuu mbalimbali vya Zanzibar, karibuni sana Dodoma. Wageni 12 wa Mheshimiwa Waziri wakiongozwa na Ndugu Jack Gotham, karibuni sana wageni wote. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wa Mheshimiwa Samwel Sitta, Waziri wa Ushirikano wa Afrika Mashariki, ambao ni Ndugu Hussein Kim, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Wilaya ya Nyamagana - Mwanza. Karibuni sana Bungeni, tupelekee salaam Nyamagana pale. Naona Mheshimiwa Wenje ananiangalia hapa. *(Makofi)*

Ndugu Anitha Kagemulo, Mwenyekiti wa Chama cha Wasanii Mwanza na Ndugu Kulwa Kikumba, msanii maarufu wa *Bongo movie Dude*, karibu sana. *(Makofi)*

Lakini pia tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, kutoka Nyakagomba Butundwe karibuni sana. Wageni watano (5) wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, ambao ni Wanakamati wa Mji Mpya wa Kigamboni, wakiongozwa na Ndugu Exaud Mmari, karibuni wana Kigombani leo mambo yenu ya Ardhi yataingia hapa. Wageni sita (6) wa Mheshimiwa Tundu Lissu kutoka soko la Rehema Nchimbi – Dodoma, wakiongozwa na Ndugu Peter Mboya, karibuni sana.

Wageni wa Mheshimiwa Celina Kombani - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ambao ni wanafunzi sita (6) kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)*, karibuni sana. Wageni wa Mheshimiwa Godbless Lema, kutoka Arusha ambao ni Ndugu Mathew Kishiri, Katibu na Ndugu Gibson Mesiaki, Diwani wa Arumeru Magharibi. *(Makofi)*

Wageni wa 15 wa Mheshimiwa Suleman Jafo, Mbunge wa Kisarawe Mkoa wa Pwani ambao ni Wajumbe wa Kamati ya CCM Wilaya ya Kisarawe wakiongozwa na Ndugu Khalfan Miembe, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kutoka Wilaya ya Kisarawe, karibuni sana Wajumbe wa Kisarawe, karibuni hapa Bungeni.

Mchungaji Gerald Ongiri na Askofu Raphael Okeyo kutoka Mara, Wilaya ya Rorya karibuni sana pale mlipo. Wageni wa Mheshimiwa Felister Bura, ambao ni wanawake 20 wajasiriamali wa Kanisa la *Adventist* Wasabato Kikuyu - Dodoma wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mama Mbwambo, wageni wa Mheshimiwa Felister Bura, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wa Mheshimiwa Seleman Nchambi, Mbunge wa Kishapu ambao ni Madiwani 26 kutoka Wilaya ya Kishapu, naomba Madiwani wale wasimame kutoka Wilaya ya Kishapu, karibuni sana Waheshimiwa Madiwani karibuni mjifunze namna Bunge linavyoendeshwa na hii itawarahisishia na ninyi kuona namna gani mnavyoweza kuendesha vikao vyenu vya Madiwani huko Kishapu.

Lakini pia yupo Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Ndugu Mkambaku, karibuni sana Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya. Pia yuko Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Justine Sheka, karibu sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya. Wako viongozi watano (5) wa CCM wa Wilaya ya Kishapu tusimame viongozi wa CCM pale mlipo karibuni sana. *(Makofi)*

Wako Watendaji 12 wa Wilaya ya Kishapu wakiongozwa na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na Watendaji kutoka Kishapu, ahsante sana sana. Watendaji hawa wanaongozwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kishapu, Dada Jane, ahsante sana. Tunakupongeza kwa nafasi hiyo ya Ukurugenzi katika Wilaya hiyo ya Kishapu. *(Makofi)*

Wapo pia Makatibu wa Jumuiya za Wazazi na Vijana wa Wilaya ya Kishapu; karibuni sana Makatibu.

Pia wapo *Greenguard Kishapu;* simameni, tunawashukuru sana, karibuni sana. Mbunge wenu Mheshimiwa Nchambi, anafanya kazi nzuri sana hapa Bungeni, tunaomba mwendelee kumlea.

Baada ya matangazo hayo, sasa matangazo ya kazi, liko moja tu. Tunawajulisha Waheshimiwa Wabunge kwamba, ile ahadi ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Samwel Sitta, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwamba, italetwa orodha ya Maafisa Viungo, *Focal Point,* wa masaula ya Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kama ilivyoahidiwa naye, sasa orodha hiyo, itagawanywa kwenu muda si mrefu ujao, ambayo inaonesha Maafisa ambao watakuwa ndiyo viungo katika masuala ya Mtangamano wa Afrika Mashariki. Nimeangalia orodha hii Mheshimiwa Waziri, Kongwa haimo! Sasa hapo umeniacha, kwa hiyo na mimi nitaomba baadaye nijue *focal point* wetu kule ni nani maana tuna Soko la Kimataifa ambalo tunataka liingie katika shughuli za Afrika Mashariki na biashara kwa ujumla.

Katibu, tuendelee!

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Jamani, muda leo muda wetu mdogo sana, haya nitajieni wenyewe, Mheshimiwa Ezekia Wenje, Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Pauline Gekul na Mheshimiwa Susan Kiwanga, dakika moja moja. Mheshimiwa Wenje!

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Katika kipindi cha maswali na majibu, kwenye suala la Mwenge, naomba muongozo wako kwa sababu ni kweli kwamba, kuna watu wanalazimishwa kutoa mchango wa Mwenge na kuna watu wanakamatwa. Ikifika kipindi cha Mwenge, Mkuu wa Mkoa anaita wafanyabiashara wote na anawaagiza kutoa mchango wa Mwenge. Kuna vijiji vingine mpaka mtu anachukuliwa mbuzi, anachukuliwa ng'ombe au kuku, pale ambapo anashindwa kutoa mchango wa Mwenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachohitaji kutoka kwenye Kiti chako; Serikali itueleze kupitia Kiti chako kwamba, ni sheria gani wanatumia kulazimisha watu kutoa mchango wa Mwenge mpaka wengine wanafungwa na wengine wanapigwa fine na inakamatwa mpaka mifugo yao? Sheria gani inatumika hapa? Sheria namba ngapi ya nchi hii inayolazimisha watu kunyanyaswa kwa sababu ya mchango wa Mwenge? Naomba mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wenje, kabla hatujaendelea sana, una ushahidi wowote wa kuweka mezani wa watu waliofungwa, waliokamatiwa mifugo au unasikia?

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu, tupo tayari kuleta ushahidi huo ukitupa muda. *(Makofi)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) nami kuomba Mwongozo kuhusiana na suala hili hili la Mwenge lakini katika mtazamo mwingine kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati maelezo nayaendelea kutolewa na Serikali kuhusiana na kero ya Wananchi kulazimishwa kuchangia michango mbalimbali, nimepokea ujumbe tena hapa ukisema kwamba, naomba ninukuu ni mfupi sana: "Mwananchi mmoja anasema, nimesikia suala la michango ya Mwenge, Waziri amesema …

**MHE. SULEIMAN NCHAMBI SULEIMAN:** Kuhusu Utaratibu. Ni muhimu sana Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Machali, tulia kidogo nitakupa nafasi!

**MHE. SULEIMAN NCHAMBI SULEIMAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wangu, simu humu ndani haziruhusiwi, ujumbe huu ameupokea kwa utaratibu upi? Atueleze!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Machali, dakika zako zinaisha tafadhali!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ujumbe huu unasema kwamba, nimesikia suala la michango ya Mwenge Waziri amesema ni makubaliano kuchangia Mwenge. Mbona *DC* Kasulu ametishia kuwafukuza kazi wasimamizi wa vituo vya kazi wasipowasilisha michango yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, *DCs* na Viongozi wengine wa aina hiyo, wanapata wapi uhalali wa kuwalazimisha watu wakati walimu wanalalamika na ndiyo imekuwa ni watu ambao kila mwaka wanatozwa michango hii pasipo hiari yao. Sasa kauli kama hizi ni wazi kwamba, suala hili la michango kuna watu wanalazimishwa na siyo hiali kama Waziri alivyosema. Nini mwongozo wako kuhusiana na hili?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana, ni lile lile la Mheshimiwa Wenje, kwa hiyo, tusichukue muda mrefu sana. Natumaini hawa wengine mna

mambo mengine na siyo hili la Mwenge, kama ni hilo hilo basi tusonge mbele. Mheshimiwa Gekul!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Natumia hiyo Kanuni ya 68(7), lakini kuhusu Kanuni iliyokiukwa ya 46 kwamba, Waziri anatakiwa ajibu maswali kikamirifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nauliza swali langu asubuhi kuhusu rushwa au vitendo vinavyotekelezwa aidha na Chama, Wakala, Mbunge au Diwani, kwenye uchaguzi wowote mdogo ule. Kwamba, Mbunge anakwenda pale au Chama chochote, anakwenda kutekeleza kampeni zinaendelea. Nimeuliza na nikamwonesha Mheshimiwa William Lukuvi, Sheria niliyonayo. Naomba mwongozo wako, Waziri Lukuvi anatumia Sheria gani kwa sababu swali langu linatumia Sheria Namba Sita ya mwaka 2010 ya gharama za uchaguzi na naomba ni-*quote*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul, samahani kidogo, unachobisha ni kitu gani kwa sababu maelezo yametolewa hapa na wote tumeelewa? Maelezo yaliyotolewa ni kwamba, kama kuna nafasi ambayo iko wazi, lakini katika nafasi hiyo iliyo wazi tuseme Serikali ya Kijiji, lakini tukumbuke kuna Viongozi wengine ambao wako, mfano Diwani, Mbunge na Wengine; kwa hiyo, hoja yako wewe ni kwamba, Mbunge na Diwani wasitekeleze Ilani kwa sababu kuna Mwenyekiti ambaye hayupo au hoja yako ni nini?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu naomba ninukuu Kanuni ya 21(3) inasema hivi: "Kwa madhumuni ya kifungu hiki, tendo au shughuli hakitachukuliwa kuwa ni kitendo kinachokatazwa kama itathibitika ilikuwa inakusudia kuleta faida katika kuchangisha fedha kwa jamii, kusaidia kujitegemea au miradi ya kijamii ndani ya jimbo na ambacho kimefanyika kabla ya mchakato wa uteuzi au Kampeni za uchaguzi kuanza." Kabla ya mchakato, uteuzi na uchaguzi haujaanza. Nakubaliana…

**NAIBU SPIKA:** Sasa maneno haya yanamzuiaje Mbunge, Diwani au mtu mwingine ambaye yupo katika eneo hilo kufanya kazi yake?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie. Mheshimiwa Lukuvi anasema, wakati uchaguzi unaendelea inaruhusiwa Mbunge, Chama chochote au Wakala yeyote kutekeleza ahadi. Sheria inasema hairuhusiwi. Naomba mwongozo wako, Mheshimiwa Lukuvi aniambie ni Sheria ipi ameitumia kunijibu majibu yake haya wakati Sheria inakataza mchakato unapoendelea Wabunge wasiende pale wala Chama wala

Wakala? Nina Sheria ya Mwaka 2010. Naomba mwongozo wako kwa nini Mheshimiwa Lukuvi analipotosha Bunge hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul, nakupa nafasi nyingine, Wabunge wote naomba tumsikilize, isome hiyo Sheria inayokataza watu wengine wenye madaraka wasifanye kazi katika eneo ambalo lina uchaguzi. Isome tuisikilize Wabunge wote tuone nani anayepotoka kati yako na Mheshimiwa Lukuvi.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Sheria niliyonayo naomba tu niiseme ni ya tarehe 9 Julai, 2010, Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya Mwaka 2010. Ninasoma sehemu ya tano ambayo inasema, vitendo vinavyokatazwa. Katika vitendo vinavyokatazwa kwenye Sheria hii, ukurasa wa 18, *section* 21(3) inasema hivi; Kwa madhumuni ya kifungu hiki, tendo au shughuli, hakitachukuliwa kuwa ni kitendo kinachokatazwa kama ikithibitika yalikuwa yanakusudia kuleta faida katika kuchangisha fedha kwa jamii, kujisaidia, kujitegemea au miradi ya jamii ndani ya Jimbo na ambacho kimefanyika kabla ya mchakato wa uteuzi au kampeni za uchaguzi. Tunatofautiana na Mheshimiwa Lukuvi kwamba, yeye anasema wakati kampeni zinaendelea, mahindi ya njaa kama Igunga yanaweza yakapelekwa, lakini sheria inasema kabla hayo yafanyike na hili limefanyika…

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea kwa ajili ya muda, Mheshimiwa Susan Kiwanga!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naib Spika, naomba nimalizie.

**NAIBU SPIKA:** Umeshaeleweka, nilitaka usome tu hiyo Sheria basi.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nisisitize.

**NAIBU SPIKA:** Umeshaeleweka, nilitaka usome hiyo Sheria tu basi. Mheshimiwa Suzan Kiwanga!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Lukuvi anapotosha, naomba arekebishe kauli yake na anijibu! *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suzan Kiwanga ninakufuta huku; umejitoa au?

**MHE. SUZAN L. A. KIWANGA:** Sijajitoa!

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasimama kwa Kanuni namba 68(7), nashukuru kwa kunipa ruhusa, lakini hapa nina *message* nyingi sana kutoka kwa Wananchi. Naomba mwongozo wako, naongezea kwa Mheshimiwa Wenje, ushahidi ninao, Katibu Tarafa wa Mang'ula ametoa tamko watu wote wachangie kwa lazima.

**NAIBU SPIKA:** Hapana, hapana, Mheshimiwa Suzan Kiwanga, naomba ukae, akishakuwa ameongea mtu mmoja inatosha. Haya mengine mengine nitayatolea utaratibu baadaye, labda kidogo tu kwa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, kama ana nyongeza yoyote katika yaliyosemwa hapa au Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari!

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kusema tu, nasisitiza yale ambayo nimetoa majibu pale mezani kwenye *podium* na Waziri Mkuu ameshalisemea hili, kwa hiyo, msimamo wa Serikali uko pale pale. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa upande wangu, mengine tutazungumza mbele ya safari. Katibu tuendelee!

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadilio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 - Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

### Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Kama Ilivyosomwa Bungeni

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako kutokana na ufinyu wa muda, naomba kuwasilisha kwa kifupi maeneo makuu yaliyoko kwenye Kitabu cha Hotuba ya Wizara yangu ambayo imesambazwa kwa Waheshimiwa

Wabunge. Hata hivyo, naomba Hotuba nzima kama ilivyo kwenye Kitabu, itambuliwe na kuingizwa kwenye kumbukumbu za *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa pole kwa familia, kwako binafsi na kwa Bunge lako Tukufu, kwa misiba ya Mheshimiwa William Augustao Mgimwa, aliyekuwa Mbunge wa Kalenga na Mheshimiwa Saidi Ramadhani Bwanamdogo, aliyekuwa Mbunge wa Chalinze. Taifa limepoteza watu waliokuwa na mchango mkubwa kwa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi hii napenda nitoe shukrani kwa Viongozi na Watanzania wote, walioisaidia Wizara yangu wakati ilipopata msiba wa ghalfa wa aliyekuwa Balozi wa Malawi hapa nchini, Marehemu Flossie Gomile Chidyaonga, uliotokea tarehe 9 Mei, 2014. Napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutoa usafiri wa ndege wa kusafirisha mwili wa marehemu kwenda nyumbani kwao Blantyre, Malawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, wakati kumbukumbu ya kifo cha Mzee Nelson Rolihlahla Mandela bado ingalipo, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Watanzania wote na Waheshimiwa Wabunge, kwa maom,bolezo hayo. Pia, kumshukuru tena Mheshimiwa Rais wetu kwa hotuba aliyoitoa kwenye mazishi yale kwa niaba ya Watanzania wote, iliyogusa sana nyoyo za ndugu zetu wa Afrika Kusini, hadi kupelekea Serikali yao kututumia salamu rasmi za upendo na shukrani, kwa yote ambayo Tanzania imeyafanya huko nyuma wakati wa vuguvugu la ukombozi na wakati wa kipindi cha msiba huo. Mwenyezi Mungu, aziweke roho za marehemu wote mahala pema peponi, amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa shukrani kwa Viongozi Wakuu wa wa nchi wakiongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi thabiti ambao umeendelea kuifanya nchi yetu ishamili nje ya mipaka yetu na kutuletea heshima kubwa na maendeleo ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mwenyekiti wa Kamati na Makamu wake, Mheshimiwa Azzan Zungu kwa kazi nzuri na msaada mkubwa ambao wameendelea kuipatia Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Yusuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani, Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga na Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge wa Chalinze, kwa kuchaguliwa kuwawakilisha wa Wananchi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitoe tathmini ya hali ya Dunia. Hali ya Dunia kwa sehemu kubwa ni shwari, ingawa bado kuna changamoto kubwa ya vitendo vya kigaidi Duniani. Mbali na changamoto hiyo, Viongozi Duniani pamoja na Jumuiya za Kimataifa, wanaendelea kupambana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaathiri sana maisha ya walimwengu. Kwa upande wa maendeleo na kuboresha maisha ya watu, nchi nyingi Duniani zinajitahidi kufikia Malengo ya Milenia ambayo yanakoma mwakani, lakini Umoja wa Mataifa utaendeleza baadhi ya Malengo hayo baada ya mwaka 2015 ili Dunia iwe na malengo endelevu ya maendeleo. Aidha, amani Duniani ipo lakini usalama wake umeathirika kwa kiwango kikubwa na migogoro ya vita vya wenyewe kwenye baadhi ya nchi.

Napenda kwa nafasi hii, kutoa tathmini ya maeneo machache ya Dunia ambayo kwa namna moja au nyingine yanatuhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa Syria. Kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu kwenye Hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2013/2014 kuhusu mgogoro wa Syria, hali imeendelea kuwa mbaya na hivyo kusababisha vifo vingi, wakimbizi wa ndani na nje na uharibifu mkubwa wa mali. Hali hii inazidi kuwa mbaya zaidi baada ya msuluhishi aliyechukua nafasi ya Bwana Kofi Annan, Mheshimiwa Lakhdar Brahimi naye kuomba kujiuzulu nafasi hiyo mwezi huu. Tanzania inaiomba Jumuiya ya Kimataifa kuendelea na jitihada za makusudi ili kuhakikisha mgogoro huo unapatiwa ufumbuzi, hususan kwa njia ya mazungumzo na hivyo kurejesha amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko Ukraine, kama mnavyofahamu, pamekuwepo na mgogoro nchini Ukraine uliopelekea kujitenga kwa jimbo lake moja la Crimea na mengine kutaka kufanya hivyo. Mgogoro huo umetishia kuigawa Dunia pande mbili, zile zinazounga mkono kujitenga zikiongozwa na Urusi na zile zinazopinga zikiongozwa na Mataifa ya Ulaya na Marekani. Msimamo wetu sisi Watanzania ni wa kutofungamana na upande wowote katika suala hili ili kuepuka kuingia kwenye mgogoro huo unaotishia amani na usalama wa Dunia kwa kuirudisha tena kwenye vita baridi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya amani na usalama Barani Afrika kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 imezidi kuimarika. Baadhi ya migogoro kama vile ya Liberia, Ivory Coast, Burundi, Guinea na Madagascar, imepatiwa ufumbuzi wa

kudumu. Jitihada zinaendelea ili kutafuta suluhu kwenye migogoro ya kisiasa inayoendelea kwenye nchi kama Somalia, Sudan Kusini, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Misri na Libya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Somalia katika kipindi cha mwaka 2013/2014, hali ya usalama nchini kwao imeendelea kuimarika ambapo mashambulizi ya kikundi cha Al Shaabab dhidi ya Vikosi vya Serikali na Umoja wa Afrika yamepungua kwa kiasi kikubwa. Hali hiyo imefanya usalama wa raia kuimarika zaidi. Vilevile matukio ya uharamia katika Pwani ya Afrika Mashariki yamepungua sana. Tanzania inaipongeza Serikali ya Somalia kwa juhudi zake kubwa za kuimarisha hali ya usalama nchini humo. Aidha, tunapongeza Umoja wa Afrika na Jeshi la Afrika la kulinda amani nchini Somalia (AMISOM), na hasa majeshi ya Kenya ambayo yaliingia hadi Kismayu na kuiteka kabisa ngome ya Maharamia. Tanzania itaendelea kutumia ushiriki wake kwenye Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kuhakikisha kuwa amani na usalama nchini Somalia vinazidi kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dunia ilipatwa na mfadhaiko mkubwa mwezi Desemba 2013 baada ya taifa jipya na changa la Sudan Kusini kuingia kwenye mapigano makali ya wenyewe kwa wenyewe. Mapigano hayo yaliyoanza mwezi Julai, 2013 yalisababishwa na kutoelewana kati ya Mheshimiwa Salva Kiir, Rais wa Jamhuri ya Sudan Kusini na aliyekuwa Makamu wake, Bwana Riek Machar. Hali hii ilitokea baada ya Rais Kiir kumfuta kazi Makamu wake huyo na baadhi ya Viongozi wengine waandamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kuibuka kwa mapigano hayo, tarehe 24 Desemba, 2013, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilipitisha azimio la kuongeza askari kwenye kikosi chake kilichopo Sudan Kusini. Kufuatia kazi nzuri iliyofanywa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi kule Darfur, Lebanon na hasa *DRC*, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa limeiomba Tanzania kupeleka Kikosi Darfur na pia tumeombwa kupeleka kikosi cha kulinda Amani Sudan ya Kusini na Serikali yetu tayari imeridhia maombi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tarehe 25 Aprili, 2014, Serikali ya Sudan Kusini iliwaachia huru wafuasi wanne wa Bwana Machar waliokuwa bado wakishikiliwa na Serikali. Kufuatia uamuzi huo wa Serikali, tarehe 9 Mei, 2014 Rais Kiir na Bwana Machar, walifanya mazungumzo ya ana kwa ana, mjini Addis Ababa kwa mara ya kwanza tangu kuibuka kwa mgogoro huo na kuweka saini makubaliano ya kusitisha mapigano.

Mheshimiwa Naibu Spika, makubaliano yaliyofikiwa kati ya pande mbili zinazogombana katika kikao hicho cha Addis Ababa ni kwamba; kwanza, pande zote mbili ziache mapigano; pili, pande zote ziruhusu mashirika ya utoaji

huduma za madawa, tiba na chakula, kuwafikia waathirika ili kuwapa misaada hiyo; tatu, kuchuja askari ili wale watiifu wasajiliwe na kuingizwa kwenye Jeshi la Taifa; nne kuunda Serikali ya Mseto na ya Mpito; na tano, kutengeneza Katiba mpya. Kutokana na makubaliano hayo, uchaguzi ambao ulitakiwa kufanyika mwakani (mwaka 2015), sasa umeahirishwa, uchaguzi sasa utafanyika baada ya mwaka 2017. Tanzania inaunga mkono makubaliano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama itakavyokumbukwa, nchi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati, iliingia kwenye mgogoro baada ya waasi wa Kikundi cha *SELEKA* kufanya mapinduzi yaliyomwondoa madarakani aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Bwana Francios Bozize mwezi Machi 2013. Kiongozi wa Kikundi cha *SELEKA* Bwana Michel Djotodia alichukua madaraka, lakini uongozi wake ulishindwa kurejesha utulivu nchini humo. Hali ya usalama ilizidi kudorora zaidi mwezi Desemba 2013 baada ya kuanza kwa mapigano makali yaliyosababisha hasara na mauaji ya raia.

Kutokana na kuendelea kwa mapigano hayo, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa liliridhia uamuzi wa kupelekwa kwa vikosi hivyo vyenye askari 6,000 tarehe 5 Desemba 2013, kuungana na askari wengine 1,200 wa Ufaransa waliokuwemo nchini humo. Vikosi hivyo kwa sasa vinaundwa na askari kutoka Congo, Chad na Rwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuendelea kulegalega kwa uongozi wa Bwana Djotodia, Wakuu wa Nchi wa *ECCAS* walifanya kikao nchini Chad tarehe 11 Januari, 2014. Wakati wa kikao hicho, Bwana Djotodia na Waziri wake Mkuu, Bwana Nicolas Tiengaye, walitangaza kujiuzulu. Tarehe 20 Januari, 2014 Bunge la Mpito la Jamhuri ya Afrika ya Kati lilimteua Bibi Catherine Samba-Panza, aliyekuwa Meya wa Mji wa Bangui, kuwa Rais wa Mpito wa nchi hiyo hadi uchaguzi mkuu wa nchi hiyo utakapofanyika. Tangu kuingia madarakani kwa Serikali mpya na kuwasili kwa vikosi vya *MISCA*, hali ya usalama imeanza kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ikiwa Mjumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika, itaendelea kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Umoja wa Afrika, Umoja wa Mataifa pamoja na wadau wengine ili kuhakikisha suluhu ya kudumu inapatikana nchini Jamhuri ya Afrika ya Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro nchini Misri umeendelea hasa baada ya Rais Mohamed Morsi kuondolewa madarakani mwezi Julai, 2013 ambapo watu wengi wamepoteza maisha kutokana na mgogoro huo. Kwa mujibu wa sheria za Umoja wa Afrika, Serikali yoyote inayoingia madarakani kwa nguvu na kinyume cha Katiba, inapoteza Uanachama wake *AU* na kuwekewa vikwazo. Matumaini yetu ni kuwa baada ya uchaguzi kufanyika mwezi huu na hasa leo,

Misri itachukua tena nafasi yake kwenye Umoja wa Afrika na kwamba hali ya usalama na kisiasa nchini Misri itakuwa na unafuu. Kama maoni ya magazeti na wanasiasa ni sahihi, basi Rais mpya wa Misri anategemewa kuwa Mheshimiwa Mohamed Fatah El Sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usalama nchini Libya bado ni tete. Baada ya kuuawa kwa Kiongozi wa Libya Kanali Muammar Gaddafi miaka mitatu iliyopita na baada ya kuuawa kwa Balozi wa Marekani nchini Libya, miaka miwili iliyopita, mapigano ya wenyewe kwa wenyewe na mauaji ya wageni na raia, yanazidi kushika kasi siku hadi siku. Hali imekuwa mbaya hadi kupelekea Waziri Mkuu kutekwa nyara na baadaye kuachiliwa na Bunge kuvamiwa na kuchomwa moto. Mapigano na mauaji yanayoendelea, yanaifanya nchi ya Libya isitawalike na kusababisha ofisi nyingi za Ubalozi nchini Tripoli na Benghazi kufungwa. Tunashauri Watanzania wanaojisikia kwenda Libya kwa sasa wasifanye hivyo kutokana na hali mbaya ya kiusalama iliyopo mpaka hapo watakaposhauriwa vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kumekuwa na taarifa kuwa kuna mvutano wa Viongozi wa Vyama vya Siasa nchini Burundi. Hali hii inatokana na hofu kwamba, Serikali iliyopo madarakani ya Rais Pierre Nkurunziza, inataka kubadilisha katiba ili kumpatia Rais Nkurunziza nafasi nyingine ya kugombea Urais kwa mara ya tatu.

Wanasiasa, hasa kutoka Kambi ya Upinzani na Viongozi wastaafu wanasema kuwa, kubadili Katiba kutavunja makubaliano ya Arusha ya Amani na Maelewano kwa *Burundi (Arusha Peace and Reconcilliation Agreement for Burundi)* na hivyo kuhatarisha amani na usalama wa nchi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Tanzania tunalo jukumu la kuhakikisha kuwa, ndugu zetu wa Burundi hawatumbukii kwenye matatizo ya kisiasa na usalama. Tunaamini kwamba, Mheshimiwa Pierre Nkurunziza, hana nia wala sababu ya kubadili Katiba ili kumwezesha kuendelea kubaki madarakani. Hivi sasa mawasiliano ya kumaliza tatizo hili yanaendelea kati ya Serikali yetu, Umoja wa Afrika na Viongozi mbalimbali wa Burundi. Tunashawishika kuamini kuwa wale wote wanaoitakia mema Burundi watasaidia katika kulimaliza tatizo hili hasa nchi za jirani zinazoizunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendo vya kigaidi vinavyofanywa na kikundi cha Boko Haram nchini Nigeria na pia kikundi cha Al-Shabaab nchini Kenya ni vitendo vya kulaaniwa na kukomeshwa na wapenda amani wote Duniani. Mauaji ya hivi karibuni ya watu wasiopungua 400 na utekaji wa wanafunzi wasichana zaidi ya 200 nchini Nigeria na vilevile mauaji ya jumla ya watu wasiopungua 100 kwa jirani zetu Kenya, ni ushaidi tosha wa kuitaka Jumuiya ya Kimataifa na Dunia kushirikiana kwa pamoja kupambana na vitendo vya kigaidi

vya aina hii. Serikali yetu tayari imekwishatuma salamu za pole tukilaani vitendo hivi na kutumia fursa hiyo kuwahakikishia wenzetu utayari wetu katika kushirikiana kwenye mapambano dhidi ya ugaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi ya amani na yenye utulivu mkubwa. Pamoja na tofauti zetu tulizonazo, tusikubali wala kushawishika kuzimaliza tofauti zetu kwa njia za kigaidi. Tuendelee na tabia ya kukosoana na kumaliza tofauti zetu kwa mazungumzo na njia zinazokubalika kisheria. Tuwe macho na watu wote wasioitakia mema nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC): Tanzania imeendelea kuwa mstari wa mbele katika kushiriki kulinda amani, usalama na demokrasia kwenye nchi za Afrika na Duniani kwa ujumla na hasa hiyo DRC.

Kutokana na msimamo huo, Tanzania imechangia kikosi kimoja cha askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwenye *Force Intervention Brigade,* inayojulikana kama *FIB,* iliyoko chini ya Kikosi cha Umoja wa Mataifa cha kulinda amani nchini *DRC*. Kama mnavyofahamu, *FIB* inaongozwa na Kamanda Mtanzania, Brig. Gen. James Alois Mwakibolwa, kwa ajili ya kupambana na waasi ndani ya DRC. Ninafurahi kutamka kwamba, askari wetu kwa kushirikiana na majeshi ya DRC na *MONUSCO,* walifanya kazi nzuri ya kukisambaratisha kabisa kikundi cha waasi wa *M23* ambao wamekuwa wakivuruga amani kwa muda mrefu mashariki mwa *DRC* na kupelekea kupatikana kwa amani ambayo ilikuwa imepotea kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkutano wa dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC),* uliofanyika sanjari na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika Jijini Addis Ababa, Ethiopia, tarehe 30 Januari, 2014, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC)* ilitoa taarifa kuhusu hali ya usalama inavyoendelea nchini humo, baada ya kusainiwa kwa makubaliano ya kusitisha mapigano kati ya Serikali na kikundi cha *M23.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwakilishi wa DRC alieleza kuwa, baada ya kutiwa saini makubaliano hayo, hivi sasa Serikali yake imejielekeza katika kuvisambaratisha vikundi vya kijeshi vilivyosalia nchini humo ikianza na *ADF-Nalu* na baadaye *FDLR.* Mwakilishi huyo pia alieleza kuwa, Bunge la nchi hiyo lilikuwa kwenye mchakato wa kutunga Sheria ya Msamaha *(Amnesty Law)* ambayo itafafanua ni waasi gani watanufaika nayo na wale ambao hawataweza kunufaika na sheria hiyo. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Sheria hiyo imekwishapitishwa tangu tarehe 5 Februari 2014. Kwa mujibu wa

Sheria hiyo, walioshiriki katika makosa ya kimbari, makosa ya kivita na jinai dhidi ya ubinadamu *(Genocide, War Crimes and Crimes Against Humanity)* hawatanufaika nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazungumzo ya usuluhishi wa mgogoro wa mpaka kati yetu na Malawi bado yanaendelea. Tarehe 20 na 21 Machi, 2014 tuliitwa Malawi kwenye jopo la usuluhishi lililopo chini ya Uenyekiti wa Rais Mstaafu wa Msumbiji, Joachim Chissano. Wengine ni Rais Mstaafu wa Afrika Kusini, Thabo Mbeki na Rais Mstaafu wa Botswana, Festus Mogae. Pamoja nao kulikuwa na kikosi cha wanasheria sita waliobobea kwenye migogoro ya mipaka duniani.

Baada ya mjadala mkubwa uliotoa fursa kwa kila upande kuwasilisha hoja zake za kisheria mbele ya Jopo, Jopo lilishauri kuwa hoja za kisheria tuziweke pembeni kwanza kwa muda na badala yake kila upande uainishe hoja zisizokuwa za kisheria. Tulitakiwa tujadili hoja zinazogusa maisha ya kila siku ya kijamii. Kwa mfano, wenzetu wa Malawi walitakiwa kueleza hasara watakazozipata endapo itaamriwa kuwa mpaka utapita katikati ya Ziwa na sisi Tanzania tulitakiwa kueleza hasara tutakazozipata endapo itaamriwa kuwa mpaka utapita kwenye ufukwe wa Ziwa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Timu ya Tanzania ambayo inajumuisha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara yangu, sasa inajiandaa kutoa majibu hayo. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Anna Tibaijuka, Mbunge na Mwanasheria Mkuu Jaji Fredrick Werema, kwa kazi nzuri sana wanayoifanya katika kujenga hoja nzito na zenye ushawishi wa kuuweka mpaka katikati ya Ziwa na siyo ufukweni, na huo ndiyo msimamo wa Tanzania, mpaka kati ya Ziwa kati yetu na Malawi unapita katikati. Aidha, kwa kuwa hadi sasa Serikali mpya ya Malawi bado haijatangazwa kama mnavyoambiwa na mnavyosikia, wala kuundwa, Jopo la usuluhishi limesitisha kikao cha pili cha usuluhishi hadi hapo nchi ya Malawi itakapopata Serikali yake mpya. Tanzania inawaombea ndugu zetu wa Malawi waiunde Serikali yao kwa amani na utulivu mapema iwezekanavyo ili tatizo hili la mpaka tulimalize na Serikali mpya inayokuja

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya kisiasa nchini Zimbabwe kwa sasa ni shwari. Zimbabwe ilifanya Uchaguzi wake Mkuu wa Rais tarehe 31 Julai, 2013. Kabla ya uchaguzi huo, Zimbabwe ilifanya mchakato wa kutengeneza Katiba mpya kwa mafanikio makubwa. Tanzania ilishiriki katika uangalizi wa shughuli zote mbili kupitia timu ya uangalizi wa *SADC,* ambayo niliiongoza mimi mwenyewe. Wananchi wa Zimbabwe walitumia nafasi yao ya kidemokrasia katika kuchagua viongozi wao na vyama walivyopenda kwa uhuru na haki. Katika uchaguzi wao huo, Mheshimiwa Robert Gabriel Mugabe, mwenye umri

wa miaka 90 sasa, aliibuka mshindi wa Urais kwa kipindi cha miaka mitano kwa kupata asilimia 61.09 ya kura zote. Aidha, timu ya uangalizi wa *SADC* iliridhika kabisa kwa maandalizi yaliyofanywa na Tume ya Uchaguzi katika mchakato mzima wa uchaguzi nchini Zimbabwe kwa mwaka 2013 na kwamba ulikuwa huru na wa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya jitihada za *SADC* za kuandaa mazingira ya uchaguzi kufanyika nchini Madagascar na baada ya kufanikisha zoezi la kuwaomba viongozi wa zamani; Ravanomanana, Rajoelina, Rasiraka na Mama Ravaromanana kutogombea kwa sababu za kiusalama, Wananchi wa Madagascar hatimaye walipiga kura tarehe 25 Oktoba, 2013 na kurudia Desemba, 2013 ambapo Henry Martial Rakotoarimanana Rajaonarimampianina, alichaguliwa kuwa Rais mpya wa Madagascar. Hali ya kisiasa nchini Madagascar kwa ujumla ni shwari ingawa kuna kutoelewana kati ya Rais aliyeondoka madarakani, yaani Rajoelina na Rais wa sasa, baada ya Rais mpya kukataa pendekezo la Rais Rajoelina la kutaka ateuliwe kuwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia ushindi huo, Wakuu wa Nchi Wanachama wa *SADC* walikubaliana kwa kauli moja, kuiondolea vikwazo nchi ya Madagascar na hivyo kuikaribisha rasmi kushiriki katika shughuli za *SADC*, ikiwemo kuhudhuria vikao vyote kama Wanachama halali. Kufuatia hatua hiyo Rais Rajaonarimampianina pia alikaribishwa rasmi kujumuika na kukalia kiti cha Madagascar katika mikutano ya Umoja wa Afrika *(AU)*. Tuendelee kuwaombea amani ya kudumu Wananchi wa Madagascar ili waweze kuijenga nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara, Idara na Taasisi nyingine, imeendelea kutekeleza Diplomasia ya Uchumi kwa kuvutia wawekezaji wenye vigezo na sifa kuja kuwekeza katika sekta mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi kabisa napenda kuelezea baadhi ya mafanikio tuliyoyapata kwenye sekta mbalimbali ambayo yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa diplomasia ya uchumi:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Kilimo; Mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu mafanikio tuliyoyapata katika kutafuta masoko ya bidhaa zetu za kilimo kwenye soko kubwa la China. Mafanikio hayo ni pamoja na kuingia Mikataba, Makubaliano na Itifaki mbalimbali na Mamlaka pekee ya China inayoruhusu biashara za namna hiyo, ambayo imeruhusu Tanzania kuingiza Zao la Tumbaku nchini China. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, hivi sasa Mamlaka hiyo imeruhusu pia mazao ya baharini kuingia

nchini China. Makubaliano hayo yaliwekwa saini mbele ya Mawaziri Wakuu Mheshimiwa Li Keqiang na Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nchini China mwezi Oktoba, 2013. Hii ni fursa adhimu kwa wavuvi wetu kupata soko la uhakika la bidhaa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kuliwezesha zao la pamba kupata soko nchini China umefikia hatua nzuri, ambapo Mkoa wa Shinyanga na Kampuni ya Dahong ya Jimbo la Jiangsu, zimeingia Mkataba wa kuendeleza Zao la Pamba mkoani humo na kuuza katika viwanda vya Dahong, China. Mkataba huo unajulikana kwa jina la *Agreement On China-Tanzania Modern Agro-Industrial Zone* na ni mmoja kati ya mikataba mitano iliyowekwa saini Oktoba 17, 2013 mbele ya Mawaziri Wakuu Mizengo Pinda na Li Keqiang mjini Beijing.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Wizara kupitia Ubalozi wake Beijing, inafuatilia kwa karibu uingiaji wa Makubaliano na Serikali ya China, yatakayoiwezesha Tanzania kuingiza China Zao la Muhogo kwa ajili ya matumizi ya viwandani ambako wanga wake unahitajika sana. Wizara yangu imeziomba mamlaka za kilimo nchini kuanzisha michakato kama hiyo kwa mazao mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua mchango wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete katika Sekta ya Kilimo, mwezi Septemba, 2013, Chuo Kikuu cha Guelph cha nchini Canada, kilimtunukia Shahada ya Heshima ya Uzamivu *(Honorary Doctorate)* ya Sheria. Mheshimiwa Rais amekuwa Mtanzania wa kwanza kutunukiwa shahada hiyo katika historia ya zaidi ya miaka 100 ya Chuo hicho maarufu kwa utafiti wa kilimo na magonjwa ya wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Nishati: Mwaka huu tumeendelea kupata fursa mbalimbali ikiwa ni pamoja na mpango mpya wa ushirikiano na Serikali ya Marekani kwenye uzalishaji umeme Barani Afrika uitwao *Power Africa Initiative,* uliozinduliwa hapa nchini tarehe 2 Julai, 2013 na Rais Barack Obama wa Marekani pamoja na Rais Jakaya Mrisho Kikwete wa Tanzania. Tanzania ni miongoni mwa nchi sita Barani Afrika zinazonufaika na Mpango huo. Katika mpango huo, Serikali ya Marekani imetenga kiasi cha Dola za Marekani bilioni saba wakati sekta binafsi nchini humo imeahidi kuwekeza kiasi cha Dola za Marekani bilioni tisa za kufanikisha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, aliyoifanya nchini Singapore mwezi Juni, 2013, alikutana na Viongozi wa Makampuni Makubwa ya Biashara. Kufuatia mkutano huo, Kampuni ya *Pavillion Energy* ya nchini Singapore imekubali kuwekeza katika sekta ya gesi nchini, ambapo kwa

kuanzia imenunua asilimia 20 ya hisa za Kampuni ya Ophir Gas kwa kiasi cha Dola za Marekani bilioni 1.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kutafuta fursa mbalimbali za biashara kwa Watanzania nje ya nchi na pia masoko kwa bidhaa zetu nje ya nchi. Balozi zetu zote Duniani zimeendelea kuwezesha upatikanaji wa taarifa juu ya maonesho ya biashara, masoko ya bidhaa na fursa za uwekezaji. Mwaka huu Kampuni ya Dragon Mart ya Dubai imeonesha nia ya kuwekeza nchini kwa kushirikiana na *TANTRADE*. Lengo la ushirikiano huo ni kujenga eneo la kisasa la maonesho ya kimataifa ya biashara nchini ambalo litakuwa linafanya maonesho ya biashara kwa kipindi cha mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Utalii, jitihada za kukuza utalii, Serikali kupitia Ubalozi wetu wa Washington Marekani imefungua Ofisi tisa za Uwakilishi wa Heshima *(Honorary Consulates)* sehemu mbalimbali nchini Marekani. Hatua hiyo inatarajiwa kuongeza idadi ya watalii kutoka Taifa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba, soko kubwa la utalii Duniani lipo China. Wizara yangu kupitia Ubalozi wake nchini China imeanza mazungumzo na mamlaka za Utalii za China kuhusu utangazaji wa vivutio vya utalii hasa vya Tanzania. Aidha, wakati wa Ziara ya Waziri Mkuu nchini China mwezi Oktoba, 2013, kampuni kubwa ya Usafirishaji wa Watalii ya Hong Kong Travels iliahidi kusafirisha watalii wapatao 10,000 kila mwaka kutembelea Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ubalozi wetu Abu Dhabi kupitia Ubalozi Mdogo wa Dubai kwa kushirikiana na Shirika la Taifa la Nyumba, ulifanya vikao kadhaa na wamiliki wa mashirika makubwa ya ujenzi wa majengo ya biashara na ya makazi ambapo walifanikiwa kuwapata wawekezaji wakubwa kwenye Sekta ya Miundombinu na Uchukuzi. Mashirika yaliyokubali kuja kuwekeza Tanzania ni *DAMAC, AL GHURAIR, SOBHA na NAKHIL*. Aidha, kwa kutambua fursa hiyo, Ubalozi umeandaa mkutano wa wawekezaji wa Dubai na Tanzania tarehe 11 Juni mwaka 2014 katika Hoteli ya Jumeirah Emirates Tower Jijini Dubai. Shirika la *National Housing Cooperation* ndiyo wanaoratibu ushiriki wa wawekezaji kutoka Tanzania. Tunawapongeza na kuwaahidi ushirikiano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa sekta za ajira, baada ya Mji wa Dubai kushinda kinyang'anyiro cha kuwa mwenyeji wa Maonesho ya Biashara ya Dunia ya Mwaka 2020, ni wazi fursa nyingi zitapatikana kupitia Maonesho hayo, hasa tukitilia maanani uhusiano mzuri wa kidiplomasia uliopo kati yetu na Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu. Kati ya fursa hizo ni pamoja na

nafasi za ajira milioni mbili na laki nane ambazo Serikali ya *UAE* itajitahidi kuzijaza kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Ubalozi umekutana na Shirika la Emirates ambalo ndiye mmiliki wa Shirika la ndege la Emirates, Danata na Fly Dubai na kuweka mikakati ya kuongeza ajira kwa Watanzania kwa Mashirika yote yaliyo chini ya Emirates. Shirika la Emirate limekubali kuajiri wafanyakazi kutoka Tanzania katika kada za wahudumu wa ndege *(Cabin Crews)* mafundi *(Technicians)* maafisa mipango *(Planning Assistants*), watoa huduma kwa wateja wa masuala ya tiketi *(Costomer Care and Ticketing)*. Napenda kuwasihi Watanzania wote wenye sifa zinazotakiwa, waombe nafasi hizi kwa wingi mara zitakapotangazwa rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Pamoja na Kudumu ya Ushirikiano *(JPC):* Katika kuratibu shughuli za Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano, Wizara imeendelea kufanya vikao vya wadau wa ndani na nje ya nchi ili kutekeleza shughuli hizo. Katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Wizara nyingine, taasisi za umma na sekta binafsi, iliandaa awamu nane ya mikutano ya Tume ya Pamoja ya Ushirikiano kati ya Tanzania na India, uliofanyika katika Hoteli ya Kilimanjaro Hyatt, tarehe 8 hadi 9 Julai, 2013. Maazimio ya mkutano huo yalitiwa saini na mimi mwenyewe na Mheshimiwa Prabit Kaur, Waziri wa Nchi wa Mambo ya nje wa India.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imefanikiwa kutekeleza sehemu ya majukumu yaliyotajwa hapo juu kwa ushirikiano na washirika wa maendeleo kutoka nchi na asasi mbalimbali za kitaifa, kikanda, kimataifa pamoja na sekta binafsi. Naomba kuwashukuru wote kwa pamoja na ni imani yangu kwamba, tutaendelea kusonga mbele pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ndiye msimamizi mkuu wa masuala ya itifaki ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imeendelea kutoa huduma ya itifaki kwenye sherehe zote na maadhimisho ya kitaifa, kuratibu safari za Viongozi wa Kitaifa wanapokwenda nje ya nchi na kuratibu mapokezi ya viongozi wa nje waliotembelea Tanzania.

Wizara imeandaa na kuratibu ziara za kikazi za Viongozi wa Kitaifa katika nchi za Nigeria, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo, Afrika Kusini, Malawi, Namibia, Kenya, Uganda, Oman, Marekani, Canada, Ethiopia, Uingereza, Srilanka, Poland, Kuwait, Ufaransa, Falme za Kiarabu, India, Uholanzi na China.

Mheshimiwa naibu Spika, ziara hizo zimefungua milango mipya ya ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi hizo; kati ya Wananchi wa nchi zetu na kati

ya sekta binafsi kutoka pande zote hizi. Aidha, ziara hizo pia zimechochea na kukuza biashara na kuimarisha mahusiano mazuri. Nitapata muda baadaye mchana huu wa kutoa ufafanuzi kitamwimu zaidi kuhusu jambo hili ambalo kila mara limekuwa linazua maswali hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa viongozi wa kimataifa kutoka nje ya nchi, Wizara iliandaa na kuratibu zaira za kikazi za wakuu wa nchi na Serikali kutoka nchi za Marekani, Thailand, Burundi, Finland, Sweden, Uholanzi, Benin, na Comoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara imehusika sana kikamilifu katika kuandaa na kuratibu ushiriki wa viongozi wakuu wa nchi na Serikali na mashirika ya kikanda na kimataifa kutoka nchi mbalimbali katika Sherehe za Maadhimisho ya Miaka 52 ya Uhuru wa Tanganyika tarehe 9, Desemba mwaka 2013. Sherehe za Maadhimisho aya Miaka 50 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, tarehe 12 Januari, 2014 na Maadhimisho ya Miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, sherehe ambazo zilifanyika tarehe 26 Aprili, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza jukumu la kusimamia mikataba na makubaliano baina ya Tanzania na nchi nyingine na Taasisi mbalimbali za Kimataifa, Wizara iliratibu na kusimamia uwekwaji saini wa mikataba 13 kati ya Tanzania na nchi nyingine *(Bilateral Agreements)* kama inavyoonekana kwenye Kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba hii itasimamiwa na kutekelezwa na kila sekta husika. Wizara yangu itaendelea na jukumu la kuratibu uwekaji saini na kufuatilia utekelezaji wa mikataba na makubaliano mbalimbali baina ya nchi yetu na nchi nyingine pamoja na Mashirika ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu, japo kwa ufupi, mafanikio tunayoyapata kutokana na ushiriki wetu kwenye Mikutano ya Kimataifa na katika Jumuiya mbalimbali ambazo nchi yetu ni mwanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliratibu ushiriki wa nchi yetu kwenye mikutano 68 ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa uliofanyika New York Marekani kuanzia mwezi Septemba hadi Desemba mwaka 2013. Katika mkutano huo, masuala mablimbali yalijadiliwa ikiwa ni pamoja na suala la ajenda ya maendeleo baada ya mwaka 2015, ambapo Malengo ya Maendeleo ya Milenia tunayoyatekeleza sasa yatafikia ukomo.

Katika kujadili ajenda hiyo, mjadala uligusa pia suala la Malengo ya Maendeleo Endelevu ambayo kimkakati ndiyo yanayoandaliwa kuchukua nafasi ya Malengo ya Maendeleo ya Milenia ifikapo mwaka 2015. Tanzania ni

mjumbe wa kikundi cha kazi kati ya nchi 30 kilichoanzishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwa ajili ya kufanya majadiliano ya kuanzishwa kwa Malengo ya Maendeeo Endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha wadau wote wanashirikishwa kikamilifu kwenye mchakato huu, zikiwemo Taasisi za Serikali na Zisizo za serikali, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, tayari imeshafanya makongamano manne; mawili Zanzibar na mawili Tanzania Bara. Makongamano haya yameshirikisha Makatibu Wakuu na Naib Makatibu Wakuu wa Zanzibar na Tanzania Bara, Wakurugenzi wa Sera za Mipango Zanzibar na Bara na Taasisi mbalimbali zisizo za serikali kwa pande zote mbili za muungano. Lengo la makongamano hayo ni kueleza kwa kina maendeleo ya mchakato huo na kupokea maoni na ushauri wa taasisi hizo kuhusu majadiliano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hayo, Mheshimiwa Rais alishiriki kwenye mikutano ya pembeni ya nchi na nchi na mingine, ikiwemo mkutano wa kupambana na ujangili kwenye mbuga za wanyama unaotishia kutoweka kwa baadhi ya wanyama kama vile tembo na faru. Mkutano huu uliweka chachu ya mkutano wa kimataifa kuhusu biashara haramu ya wanyamapori uliofanyika London Uingereza mwezi Februari mwaka 2014, ambao uliratibiwa na Wizara yangu. Mkutano huu uliikutanisha Jumuiya ya Kimataifa kwa lengo la kujadili na kutafuta mbinu za kupambana na hatimaye kutokomeza kabisa biashara haramu za pembe za ndovu na faru.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkutano wa mabadiliko ya tabianchi ulifanyika Warsaw Poland mwezi Novemba mwaka 2013. Pamoja na ujumbe wa Tanzania kushiriki kama nchi, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania. aliwawakilisha Wakuu wa nchi za Bara la Afrika kwa nafasi yake ya Uenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa nchi wa Serikali wa Afrika kuhusu mabadiliko ya tabianchi. Akiwa Warsaw, Mheshimiwa Rais, alifanya kikao na Mawaziri wa Mazingira na *negotiators* wa Afrika na kuweka msimamo wa pamoja wa namna ya kuhakikisha masilahi ya Afrika yanalindwa kwenye mkutano huo na mingine ya mabadiliko ya tabianchi. Mheshimiwa Rais, alisisitiza umuhimu wa kutoa kipaumbele kwenye masuala ya upatikanaji wa fedha, teknolojia na kuijengea Afrika uwezo, ambapo kupitia mkutano huo, nchi tajiri na zenye viwanda Duniani ziliahidi kuchangia kiasi cha Dola za Marekani 100,000,000,000 kila mwaka hadi mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ilichaguliwa tena na Wakuu wa Nchi na Serikali za Jumuiya ya Madola kuendelea kuwa Mjumbe katika kikundi cha kazi cha Mawaziri, yaani *CMAG* cha Jumuiya ya Madola. Mawaziri wanaounda *CMAG* walinipendekeza na kunichagua kwa nafasi yangu kama Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuwa Mwenyekiti wa *CMAG* kwa

mwaka 2013 hadi 2015. Kuchaguliwa kwa Tanzania ni mafanikio kwa diplomasia ya nchi na kumedhihirisha jinsi nchi inavyoheshimika kwenye Jumuiya ya Kimataifa; ikizingatiwa kuwa *CMAG* ni chombo maalum na chenye hadhi ya pekee kwenye muundo wa Jumuiya ya Madola, kinachosimamia kanuni na kuratibu Jumuiya hiyo na kuchukua hatua; kwa kweli ni kitengo ambacho kinafanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumuiya ya Madola itakuwa na mashindano Commonwealth huko Glasgow Uingereza Mwezi Julai, 2014. Katika mashindano hayo ya Commonwealth, vijana wanariadha wa Tanzania watashiriki katika maeneo ya mbio fupi na ndefu pamoja na michezo ya mpira wa meza, ngumi, judo na kadhalika. Vijana wasiopungua 50 wanatarajiwa kushiriki katika mashindano hayo.

Kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Wizara yangu kwa kutumia diplomasia ya mahusiano katika michezo, tumeweza kupeleka vijana 50 pamoja na walimu wao, kwenye makambi ya mafunzo nchini Ethiopia, Uturuki, New Zealand na China. Vijana wapo huko na taarifa tulizonazo hivi sasa, ni kwamba, mazoezi yanakwenda vizuri sana. Ni matumaini yetu kuwa, watakapokuwa huko Glasgow mwezi Julai, vijana wetu watafanya maajabu na kuijengea heshima nchi yetu kwa kutuletea wingi wa medali za dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeendelea kushiriki kikamilifu kwenye Jumuiya za Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika. Mwezi wa nane mwaka 2013, Wizara iliratibu na kushiriki mikutano wa nchi za Serikali za *SADC* uliofanyika Lilongwe Malawi. Kwenye mkutano ule, ulijadili na kufanya maamuzi na kumteua aliyekuwa Rais wa Malawi, Mheshimiwa Joyce Banda kuwa Mwenyekiti wa *SADC,* Mheshimiwa Hifikepunye Pohamba, Rais wa Namibia kuwa Mwenyekiti wa Asasi za *SADC* inayoshughulikia masuala ya siasa, ulinzi na usalama na kumteua Dkt. Stegomena L. Tax kutoka Tanzania kuwa Katibu Mtendaji Mpya wa *SADC*. *(Makofi)*

Uteuzi huo wa Dkt. Tax ni uthibitisho mwingine Mheshimiwa Naibu Spika na umesema, wa kuzidi kushamiri kwa diplomasia ya Tanzania na umeendelea kuijengea heshimia kubwa sana Tanzania na kuitangaza nchi yetu katika medani za kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie Watanzania waishio ughaibuni na suala la uraia pacha *(Dual Citizenship)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutekeleza jukumu lake la kuwashirikisha Watanzania waishio ughaibuni katika maendeleo ya kiuchumi na

ya kijamii ya nchini kwetu. Wizara kwa kutumia kurugenzi yake ya diaspora, inaendelea na utafiti kwa kushirikiana na Balozi zetu Duniani, pamoja na Uongozi wa Jumuiya ya Diaspora ili kubaini idadi kamili ya Watanzania waishio nje, ikiwa ni pamoja na kubaini taaluma zao.

Changamoto na kilio kikubwa cha wana-diaspora cha kutaka Serikali yetu ikubali na kuipitisha sheria ya kuruhusu uraia wa nchi mbili *(dual citizenship)*, inashughulikiwa kikamilifu na Wizara yangu. Wizara tayari imelifikisha suala la uraia wa pacha kwa Tume ya Jaji Warioba na tayari suala hili limewekwa kwenye rasimu ya Katiba mpya na ni matumaini yangu kwamba, tutaijadili kwa nguvu za hoja, na kwamba sasa umefika wakati wa nchi yetu kuwa na sheria ya kuruhusu uraia pacha kwa masilahi na maendeleo ya Taifa letu. Ni matumaini yangu kuwa Bunge hili litaunga mkono pendekezo hilo wakati wa mjadala utakapowasili kwenye Bunge la Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa naibu Spika, katika miaka ya hivi karibuni, Jumuiya ya Kimataifa imeshuhudia Tanzania ikichukua majukumu ya kushiriki moja kwa moja katika harakati za ukombozi na utatuzi wa migogoro barani Afrika na Duniani kote. Mpaka sasa Tanzania imeendelea kushiriki katika utatuzi wa migogoro na ulinzi wa amani, ambapo imekuwa ikichangia vikosi vya kulinda amani katika nchi mablimbali zinazokabiliwa na migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi mwaka 2014, Tanzania tayari imekwishapeleka Duniani wanajeshi 2,259 kwenye maeneo manne ya kulinda amani ya Umoja wa Mataifa. Maeneo hayo ni DRC Kongo, yaani DR Congo, Sudan, Lebanon na Ivory Coast. Hii inaonesha jitihada za Tanzania za kuifanya Dunia kuwa mahala pa kuishi salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tunajivuna kwamba, tarehe 26 Aprili mwaka 2014, Muungano umetimiza miaka 50 tangu kuundwa kwake. Hatua tuliyofikia ni ya kujivunia, kwani katika kipindi hicho zipo nchi nyingi zilizojaribu kufanya hivyo bila mafanikio yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa fesha 2013/2014, Chuo cha Diplomasia kimeendelea kufanya maboresho ili kukidhi masharti ya Baraza la Ithibati ya Elimu ya Ufundi. Chuo kimezidi kutambulika na kuimarika katika utoaji taaluma, ushauri wa kufanya tafiti katika masuala ya utatuzi wa migogoro, itifaki, diplomasia ya uchumi, stratejia na menejiment ya mahusiano ya kidiplomasia. Aidha, Chuo kimeendelea kuishauri Wizara yangu katika masuala ya diplomasia na kutoa mafunzo maalum kwa Watumishi wa Wizara, Mabalozi na wenzi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kuongeza udahiri kutoka wanafunzi 559 katika mwaka wa masomo 2012/2013 na kufikia wanafunzi 881 katika mwaka huu wa masomo. Chuo kipo katika hatua za mwisho za mchakato wa kutoa shahada na kufundisha Lugha ya Kichina kwa Watanzania na Kiswahili kwa wageni kuanzia mwaka ujao wa masomo, ikiwa ni sehemu ya Mpango Mkakati wa Miaka Mitano, yaani mwaka 2012/2013 hadi 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha *(AICC),* kimeendelea kutuwakilisha vyema katika diplomasia ya mikutano na kuvutia utalii nchini kwa njia ya mikutano. Kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Juni, 2013 Kituo kiliweza kuwa mwenyeji wa Mikutano ya Kimataifa 29 na ya Kitaifa 33 iliyoingiza nchini wageni wanaokadiriwa kufikia 15,040. Katika kipindi hicho, Kituo kilipata faida ghafi ya Shilingi 191,331,385,000 na kinaendelea kufanya shughuli zake kwa ufanisi mkubwa na bila kuwa tegemezi kwa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2014/2015, Kituo kimepanga kuingiza mapato ya Shilingi 13,885,707,832 kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato, ikiwemo ya kituo kipya cha Kimataifa cha Julius Nyerere ambacho kilikabidhiwa kwa *AICC* Agosti mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Wizara yangu iliidhinishiwa kutumia kiasi cha Shilingi 138,359,944,221. Kati ya fedha hizo, Shilingi 110,359,944,221 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 28,000,000,000 ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Katika fedha zilizotengwa kwa matumizi ya kawaida *(Recurrent Budget),* Shilingi 104,906,284,719 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(Other Charges)* na Shilingi 5,453,659,502 ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Balozi zake ilitarajia kukusanya kiasi cha Shilingi 16,966,729,300 kama maduhuli ya Serikali. Hadi kufikia tarehe 31 Machi mwaka 2014, Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha Shilingi 12,909,470,376, ikiwa ni makusanyo ya maduhuli Balozini. Kiasi hicho cha makusanyo ya maduhuli ni sawa na asilimia 76 ya makusanyo yote ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 31 Machi mwaka huu wa 2014, Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha Shilingi 117,327,353,962. Kati ya kiasi hicho, Shilingi 106,492,842,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, Shilingi 4,368,705,920 ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi 6,465,800,000 ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014: Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2013/2014, Wizara yangu imekabiliwa na changamoto mbalimbali za kiutawala na bajeti katika utekelezaji wa majukumu yake. Baadhi ya changamoto hizo ni upungufu wa watumishi Makao Makuu ya Wizara na Balozini, upungufu wa vitendea kazi, uchakavu wa majengo ya ofisi na makazi balozini na uchakavu wa magari ya uwakilishi na huduma Ubalozini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuomba kibali Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), cha kuajiri watumishi wapya. Vilevile Wizara imeendelea kununua vitendea kazi vya watumishi kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, Wizara imeendelea kutumia fedha za Bajeti ya Maendeleo zinazopangwa katika Bajeti kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo kwa kuzingatia vipaumbele na kushirikisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika kuingia ubia wa kutekeleza Miradi ya Maendeleo iliyopo Ubalozini. Hali kadhalika, Wizara imepanga kutumia utaratibu wa *higher purchase* katika kufanikisha ununuzi wa magari kwenye Balozi zetu. Utaratibu huu ni mzuri na utapunguza gharama za ununuzi wa magari hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015: Katika Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, pamoja na mambo mengine, shabaha kuu ya kuitangaza nchi yetu kama mahala salama na amani kwa uwekezaji, utalii na biashara ikiwa ni sehemu ya kutekeleza Sera yetu ya Diplomasia ya Uchumi. Aidha, tunaendelea kujikita katika kuwahusisha Watanzania waishioo ughaibuni, yaani Diosphora, katika kujenga nchi yoa na kuwapa nafasi wanayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kumaliza, ninaomba kuchukua nafasi hii niwashukuru kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Dkt. Mahadhi Juma Maalim – Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bwana John Haule – Katibu Mkuu, Balozi Rajab Gamaha – Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Mabalozi na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu waliopo Makao Makuu, Ofisi yetu ya Zanzibar na katika Balozi zetu mbalimbali Duniani, kwa ushirikaino walionipatia na wanaoendelea kunipatia, kwa kazi nzuri na ya kizalendo ya kutetea masilahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, niwashukuru Wananchi na Viongozi wa Mkoa wa Lindi, hususan Viongozi wote wa Mkoa, wa Jimbo la Mtama, wa Tarafa zote na hasa Rondo, kwa kuniunga mkono katika shuguli za maendeleo Jimboni na Mkoani kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani za pekee ziwaendee mke wangu Mama Dorcas Membe na watoto wetu Cecilia, Richard na Denis, kwa kunivumilia sana pale ninapolazimika kuwa mbali na familia kwa muda mrefu na dada zangu Esther Membe na Consolata Membe, ambao kila wiki hunipigia simu na kunitakia kila la heri na dada yangu yuko hapa. Katika kutimiza majukumu yangu na kulitumikia taifa; ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu yaliyotajwa hapo juu, kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 191,919,748,000 na kati ya fedha hizo, Shilingi 161,919,748,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 30,000,000,000 ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, Wizara yangu kupitia Balozi zake, inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi 18,568,222,778 kama maduhuli ya Serikali; na kwa maana ya utekelezaji wa Bajeti, kiasi hiki cha maduhuli tayari kimejumuishwa kama sehemu ya bajeti ya matumizi mengineyo ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nirudie tena takwimu hizi kwa sababu herufi moja ilikuwa haionekani vizuri.

Wizara yangu kupitia Balozi zake inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi 18,568,022,478 kama maduhuli ya Serikali. Kwa maana ya utekelezaji wa Bajeti, kiasi hiki cha maduhuli tayari kimejumuishwa kama sehemu ya bajeti ya matumizi mengineyo ya Wizarra.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Kama Ilivyowasilishwa Mezani**

**H O T U B A Y A WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA, M H E S H I M I W A B E R N A R D K A M I L L I U S M E M B E ( M B . ) , AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA KWA MWAKA**

**WA FEDHA 2014/2015**

**UTANGULIZI**

***Mheshimiwa Spika***, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote naomba niungane na wenzangu walionitangulia kutoa pole kwa familia, kwako binafsi na kwa Bunge lako Tukufu kwa misiba iliyotokea katika mwaka huu wa fedha, ambapo tuliondokewa na wabunge wenzetu wawili; Mheshimiwa William Augustao Mgimwa, aliyekuwa Mbunge wa Kalenga na Mheshimiwa Saidi Ramadhani Bwanamdogo, aliyekuwa Mbunge wa Chalinze. Taifa limepoteza watu waliokuwa na mchango mkubwa kwa maendeleo. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu wote mahali pema peponi. Amina.

***Mheshimiwa Spika,*** kwa nafasi hii napenda nitoe shukrani kwa Viongozi na Watanzania wote walioisaidia Wizara yangu wakati ilipopata msiba wa ghalfa wa aliyekuwa Balozi wa Malawi hapa nchini Marehemu Flossie Gomile Chidyaonga uliotokea tarehe 9 Mei, 2014. Napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa usafiri wa ndege wa kusafirisha mwili wa marehemu kwenda nyumbani kwao Blantyre, Malawi.

***Mheshimiwa Spika,*** wakati kumbukumbu ya kifo cha Mzee Nelson Rolihlahla Mandela bado ingalipo, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Watanzania wote na Waheshimiwa Wabunge kwa maombolezo hayo. Pia, kumshukuru tena Mheshimiwa Rais wetu kwa hotuba aliyoitoa kwenye mazishi yale kwa niaba ya Watanzania wote, iliyogusa sana nyoyo za ndugu zetu wa Afrika Kusini, hadi kupelekea Serikali yao kututumia salamu rasmi za upendo na shukrani kwa yote ambayo Tanzania imeyafanya huko nyuma wakati wa vuguvugu la ukombozi na wakati wa kipindi cha msiba huo.

***Mheshimiwa Spika***, napenda kutumia fursa hii pia kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake mahiri wa Serikali ya Awamu ya Nne. Ni dhahiri kwamba chini ya uongozi wake Taifa letu limeendeleza utamaduni wetu wa kudumisha amani, usalama na mshikamano wa kitaifa pamoja na kuimarisha ushawishi wa Tanzania katika nyanja za Kikanda na Kimataifa kupitia diplomasia thabiti na imara. Pamoja na utendaji wake kuonekana kwetu, mtazamo wa

watu wa nje ya Tanzania pia unadhihirisha hivyo. Tarehe 9 Aprili 2014, Mheshimiwa Rais alitunukiwa tuzo ya kuwa kiongozi mwenye mchango mkubwa zaidi katika maendeleo Barani Afrika kwa mwaka 2013, huko jijini Washington DC. Tuzo hiyo ya heshima kubwa niliyoipokea kwa niaba yake, ilitolewa na jarida maarufu la kimataifa liitwalo *African Leadership Magazine Group*.

***Mheshimiwa Spika***, ninawaomba Watanzania wenzangu, tuendelee kushirikiana na wenzetu duniani kote katika kudumisha demokrasia, amani, usalama, umoja na mshikamano bila kujali rangi, kabila, dini au itikadi zetu za kisiasa. Napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba jumuiya ya kimataifa inatambua na kuthamini mchango wa Tanzania katika maeneo hayo ya utawala bora na hivyo kuichukulia kama mfano wa kuigwa.

***Mheshimiwa Spika***, napenda vilevile kuwashukuru Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Stephen Masato Wassira (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu kwa hotuba zao nzuri. Hotuba zao sio tu zimechambua kwa kina masuala ya kiuchumi, kijamii, kiusalama na kisiasa na kutoa dira ya Taifa letu katika mwaka ujao wa fedha, bali zimegusia pia mambo kadhaa ya msingi yanayohusu Wizara yangu. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote ambao wameshawasilisha hotuba zao, ambazo kwa namna moja au nyingine ziligusa maeneo yanayohusu Wizara yangu. Kama mnavyofahamu, Wizara hii inashughulikia masuala mtambuka ambayo yanagusa na kuguswa na Wizara, Idara na Taasisi zote yanapokuja masuala ya nchi, kanda, kimataifa na mashirika mbalimbali duniani. Wajibu wetu mkubwa ni kuratibu masuala hayo na utekelezaji unabaki kwa Taasisi husika.

***Mheshimiwa Spika***, naomba nitumie fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati na Makamu wake Mheshimiwa Azan Zungu (Mb.) kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuchambua na kushauri Wizara yangu kuhusu bajeti wakati wa vikao vya Kamati. Uchambuzi na ushauri walioutoa utakuwa nguzo muhimu katika utekelezaji wa bajeti hii na majukumu ya Wizara yangu na hivyo kusimamia utekelezaji wa diplomasia ya uchumi kwa ukamilifu zaidi kwa manufaa ya nchi yetu.

***Mheshimiwa Spika,*** pongezi zangu pia kwa Wabunge wapya watatu waliojiunga nasi mwaka huu, ambao ni Mheshimiwa Yusuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani; Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga; na Mheshimiwa Ridhiwan Jakaya Kikwete, Mbunge wa Chalinze. Nawapongeza kwa kuchaguliwa kuwawakilisha wananchi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***Mheshimiwa Spika***, pia nawashukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Mahadhi Juma Maalim (Mb.), Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; Bwana John M. Haule, Katibu Mkuu; Balozi Rajabu H. Gamaha, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi, Mabalozi na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu waliopo Makao Makuu, Ofisi yetu ya Zanzibar na katika Balozi zetu mbalimbali duniani, kwa ushirikiano wanaonipa na kwa kazi nzuri na ya kizalendo ya kutetea maslahi ya Taifa letu.

***Mheshimiwa Spika***, halikadhalika niwashukuru wananchi na viongozi wa Mkoa wa Lindi, hususan wa Jimbo la Mtama kwa kuniunga mkono katika shughuli za maendeleo jimboni na mkoani kwa ujumla. Shukurani za pekee ziwaendee mke wangu Mama Dorcas Membe na watoto wetu kwa kunivumilia pale ninapolazimika kuwa mbali na familia kwa muda mrefu na kunitia moyo katika kutimiza majukumu yangu ya kulitumikia Taifa.

**TATHMINI YA HALI YA DUNIA**

***Mheshimiwa Spika,*** hali ya dunia kwa sehemu kubwa ni shwari ingawaje bado kuna changamoto kubwa ya vitendo vya kigaidi. Mbali na changamoto hiyo, viongozi duniani pamoja na jumuiya za kimataifa wanaendelea kupambana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaathiri sana maisha ya walimwengu. Aidha, amani duniani ipo lakini usalama wake umeathirika kwa kiwango kikubwa na migogoro ya vita vya wenyewe kwa wenyewe kwenye baadhi ya nchi. Kwa upande wa maendeleo na kuboresha maisha ya watu, nchi nyingi duniani zinajitahidi kufikia malengo ya milenia ambayo yanakoma mwakani lakini Umoja wa Mataifa utaendeleza baadhi ya malengo hayo baada ya 2015 ili dunia iwe na malengo endelevu ya maendeleo (SDGs). Napenda kutoa tathmini ya maeneo machache ya dunia ambayo kwa namna moja au nyingine yanatuhusu:-

**Mgogoro wa Syria**

***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu kwenye hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2013/2014 kuhusu mgogoro wa Syria, hali imeendelea kuwa mbaya na hivyo kusababisha vifo vingi, wakimbizi wa ndani na nje na uharibifu mkubwa wa mali. Hali hii inazidi kuwa mbaya zaidi baada ya msuluhishi aliyechukua nafasi ya Kofi Annan, Mheshimiwa Lakhdar Brahimi naye kuomba kujiuzulu nafasi hiyo mwezi huu. Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa masikitiko makubwa amekubali kujiuzulu kwake ifikapo tarehe 31 Mei 2014. Tanzania inaiomba Jumuiya ya Kimataifa kuendelea na jitihada za makusudi kuhakikisha mgogoro huo unapatiwa ufumbuzi, hususan kwa njia ya mazungumzo na hivyo kurejesha amani na utulivu kwa nchi na wananchi wa Syria.

**Mgogoro wa Ukraine**

***Mheshimiwa Spika,*** kama mnavyofahamu, pamekuwepo na mgogoro nchini Ukraine uliopelekea kujitenga kwa jimbo lake moja la Crimea na mengine kutaka kufanya hivyo. Mgogoro huo umetishia kuigawa dunia pande mbili, zile zinazounga mkono kujitenga zikiongozwa na Urusi na zile zinazopinga zikiongozwa na Mataifa ya Ulaya na Marekani. Msimamo wa Tanzania ni kutofungamana na upande wowote ili kuepuka kuingia kwenye mgogoro huo unaotishia amani na usalama wa dunia kwa kuirudisha tena kwenye vita baridi. Tanzania inaendelea kuiomba Jumuiya ya Kimataifa kushughulikia mgogoro huu kwa kutumia hekima na busara ambayo itaiepusha dunia kuingia kwenye vita.

**Hali ya Usalama Barani Afrika**

***Mheshimiwa Spika****,* hali ya amani na usalama Barani Afrika kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 imezidi kuimarika. Baadhi ya migogoro kama vile wa Liberia, Cote d'Ivoire, Burundi, Guinea, na Madagascar imepatiwa ufumbuzi wa kudumu. Jitihada zinaendelea ili kutafuta suluhu kwenye migogoro ya kisiasa inayoendelea kwenye nchi kama Somalia, Sudan Kusini, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Misri na Libya.

**Somalia**

***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2013/2014, hali ya usalama nchini Somalia imeendelea kuimarika ambapo mashambulizi ya kikundi cha Al Shaabab dhidi ya vikosi vya Serikali na Umoja wa Afrika yamepungua kwa kiasi kikubwa. Hali hiyo imefanya usalama wa raia kuimarika zaidi. Vilevile matukio ya uharamia katika Pwani ya Afrika Mashariki yamepungua sana. Tanzania inaipongeza Serikali ya Somalia kwa juhudi zake kubwa za kuimarisha hali ya usalama nchini humo. Aidha, tunapongeza Umoja wa Afrika na Jeshi la Afrika la kulinda amani nchini Somalia (AMISOM), na hasa majeshi ya Kenya ambayo yaliingia hadi Kismayu na kuiteka kabisa ngome ya Maharamia. Tanzania itaendelea kutumia ushiriki wake kwenye Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kuhakikisha kuwa amani na usalama nchini Somalia vinazidi kuimarika.

**Sudan Kusini**

***Mheshimiwa Spika,*** dunia ilipatwa na mfadhaiko mkubwa mwezi Desemba 2013 baada ya taifa jipya na changa la Sudan Kusini kuingia kwenye mapigano makali ya wenyewe kwa wenyewe. Mapigano hayo yaliyoanza mwezi Julai 2013 yalisababishwa na kutoelewana kati ya Mheshimiwa Salva Kiir, Rais wa Jamhuri ya Sudan Kusini na aliyekuwa Makamu wake, Bwana Riek Machar. Hali hii ilitokea baada ya Rais Kiir kumfuta kazi Makamu wake huyo na baadhi ya viongozi wengine waandamizi.

***Mheshimiwa Spika***, mgogoro kati ya viongozi hao ulichukua sura mpya tarehe 14 Desemba, 2013 baada ya Serikali ya Sudan Kusini kutangaza kuwepo kwa jaribio la mapinduzi lililofanywa na wafuasi wa Bw. Machar. Baada ya tangazo hilo, Bw. Machar alikwenda mafichoni lakini wafuasi wake 11 walikamatwa na kufunguliwa mashtaka ya uhaini. Hatua ya kuwakamata wafuasi wa Bw. Machar ilizusha mapigano makali baina ya vikosi vya Serikali na wafuasi wa Bw. Machar, hususan kwenye majimbo ya Jonglei, *Unity* na *Upper Nile*. Kadri muda ulivyokwenda, mapigano yalichukua sura ya ukabila kati ya kabila la Ngok Dinka analotoka Rais Kiir na Nuer la Bwana Machar, ambapo idadi kubwa ya raia wasio na hatia waliuawa na wengine kulazimika kukimbia makazi yao.

***Mheshimiwa Spika***, kufuatia kuibuka kwa mapigano hayo, tarehe 24 Desemba, 2013, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilipitisha azimio la kuongeza askari kwenye kikosi chake kilichopo Sudan Kusini *(United Nations Mission in South Sudan – UNMISS)*. Kufuatia kazi nzuri iliyofanywa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania kule Darfur, Lebanon na hasa DRC, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa limeiomba Tanzania kupeleka Kikosi cha Kulinda Amani Sudan ya Kusini na Serikali yetu tayari imeridhia ombi hilo. Aidha, tarehe 27 Desemba 2013, Wakuu wa Nchi wa IGAD (*the Inter-Governmental Authority on Development)* walifanya mkutano wa dharura mjini Nairobi, Kenya, kujadili mgogoro huo. Tarehe 30 Desemba, 2013 Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika lilifanya kikao mjini Banjul, Gambia, na kuunga mkono jitihada za IGAD kwa kuzitaka pande zinazohusika kuacha mapigano na kuanza mazungumzo.

***Mheshimiwa Spika***, pande zinazohusika na mgogoro nchini Sudan Kusini zilianza mazungumzo mjini Addis Ababa, Ethiopia, tarehe 4 Januari, 2014. Kufuatia majadiliano hayo tarehe 23 Januari, 2014 pande hizo mbili zilitia saini Mkataba wa kusimamisha mapigano baada ya Serikali kukubali kuwaachia huru wafuasi 7 kati 11 wa Bwana Machar. Pande hizo mbili zilianza tena mazungumzo mwezi Februari 2014 ili kutafuta suluhisho la kudumu la mgogoro huo. Hata hivyo, mazungumzo hayo yalikwama na kusitishwa baada ya upande wa Bw. Machar kushinikiza kuachiwa huru kwa wafuasi wanne waliobaki.

***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 25 Aprili 2014, Serikali ya Sudan Kusini iliwaachia huru wafuasi wanne wa Bwana Machar waliokuwa bado wakishikiliwa na Serikali. Kufuatia uamuzi huo wa Serikali, tarehe 9 Mei, 2014 Rais Kiir na Bwana Machar walifanya mazungumzo ya ana kwa ana, mjini Addis Ababa kwa mara ya kwanza tangu kuibuka kwa mgogoro huo na kuweka saini makubaliano ya kusitisha mapigano.

***Mheshimiwa Spika,*** makubaliano yaliyofikiwa kati ya pande mbili zinazogombana katika kikao hicho cha Addis Ababa ni; kwanza pande zote mbili kuacha mapigano; pili, pande zote ziruhusu mashirika ya utoaji huduma za madawa, tiba na chakula kuwafikia waathirika ili kuwapa misaada hiyo; tatu, kuchuja askari ili wale watiifu wasajiliwe na kuingizwa kwenye jeshi la Taifa; nne kuunda Serikali ya Mseto na ya mpito na tano kutengeneza Katiba mpya. Kutokana na makubaliano hayo, uchaguzi ambao ulitakiwa kufanyika mwakani 2015, sasa umeahirishwa. Tanzania inaunga mkono makubaliano hayo.

**Jamhuri ya Afrika ya Kati**

***Mheshimiwa Spika***, kama itakavyokumbukwa nchi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati iliingia kwenye mgogoro baada ya waasi wa Kikundi cha SELEKA kufanya mapinduzi yaliyomwondoa madarakani aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Bwana Francios Bozize mwezi Machi 2013. Kiongozi wa Kikundi cha SELEKA Bwana Michel Djotodia alichukua madaraka lakini uongozi wake ulishindwa kurejesha utulivu nchini humo. Hali ya usalama ilizidi kudorora zaidi mwezi Desemba 2013 baada ya kuanza kwa mapigano makali yaliyochukua sura ya udini, baina ya wanamgambo wa Kundi la SELEKA lenye wafuasi wengi wa Kiislamu na wanamgambo wa Kundi la ANTI-BALAKA lenye wafuasi wengi wa Kikristo. Mapigano hayo yalisababisha madhara makubwa nchini humo, ikiwemo idadi kubwa ya vifo vya raia na maelfu ya watu kukimbia makazi yao.

***Mheshimiwa Spika****,* tangu kuibuka kwa mgogoro nchini Jamhuri ya Afrika ya Kati, Jumuiya ya Kimataifa ikiwemo Umoja wa Afrika (AU), Umoja wa Mataifa na Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika ya Kati *(Economic Community of the Central African States – ECCAS)* na wadau mbalimbali imekuwa ikifanya jitihada za kutatua mgogoro nchini humo. Umoja wa Afrika uliisimamishia uanachama nchi hiyo kwa kuwa Serikali yake iliingia madarakani kinyume cha sheria. Aidha, mwezi Julai 2013, Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika, ambalo Tanzania ni mjumbe, lilipitisha uamuzi wa kupelekwa Kikosi cha Afrika cha Kulinda Amani nchini Jamhuri ya Afrika ya Kati *(Africa-led International Support Mission in the Central African Republic –MISCA)* kuchukua nafasi ya vikosi vya nchi za ECCAS. Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa liliridhia uamuzi wa kupelekwa kwa kikosi hicho chenye askari 6,000 tarehe 5 Desemba 2013, kuungana na askari wengine 1,200 wa Ufaransa waliokuwemo nchini humo. Kikosi hicho kwa sasa kinaundwa na askari kutoka Congo, Chad na Rwanda.

***Mheshimiwa Spika*****,** kutokana na kuendelea kulegalega kwa uongozi wa Bwana Djotodia, Wakuu wa Nchi wa ECCAS walifanya kikao nchini Chad tarehe 11 Januari, 2014. Wakati wa kikao hicho, Bwana Djotodia na Waziri wake Mkuu Bwana Nicolas Tiengaye walitangaza kujiuzulu. Tarehe 20 Januari, 2014

Bunge la Mpito la Jamhuri ya Afrika ya Kati lilimteua Bibi Catherine Samba-Panza, aliyekuwa Meya wa Mji wa Bangui, kuwa Rais wa Mpito wa nchi hiyo hadi uchaguzi mkuu wa nchi hiyo utakapofanyika. Tangu kuingia madarakani kwa Serikali mpya na kuwasili kwa vikosi vya MISCA, hali ya usalama imeanza kuimarika.

***Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyingine, tarehe 10 Aprili 2014, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilipitisha Azimio la kuunda Kikosi cha Kulinda Amani nchini humo *(UN Multilateral Integrated Stabilization Mission in Central African Republic – MINUSCA)* kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi 30 Aprili, 2015 kuchukua nafasi ya MISCA. MINUSCA ambayo itakuwa na idadi ya walinda amani 12,000 inatarajiwa kuanza kazi rasmi mwezi Septemba 2014.

***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ikiwa mjumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika itaendelea kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Umoja wa Afrika, Umoja wa Mataifa pamoja na wadau wengine ili kuhakikisha suluhu ya kudumu inapatikana nchini Jamhuri ya Afrika ya Kati.

**Misri**

***Mheshimiwa Spika,*** mgogoro nchini Misri umeendelea hasa baada ya Rais Mohamed Morsi kuondolewa madarakani mwezi Julai 2013 ambapo watu wengi wamepoteza maisha kutokana na mgogoro huo. Kwa mujibu wa sheria za Umoja wa Afrika, Serikali yoyote inayoingia madarakani kwa nguvu na kinyume na Katiba, inapoteza uanachama wake AU na kuwekewa vikwazo. Ni matumaini yetu kuwa baada ya uchaguzi kufanyika mwezi huu wa Mei, 2014 Misri itachukua tena nafasi yake kwenye Umoja wa Afrika, na kwamba hali ya usalama na kisiasa nchini Misri itakuwa na unafuu. Kama maoni ya magazeti na wanasiasa ni sahihi, basi Rais mpya wa Misri anategemewa kuwa Mheshimiwa Mohamed Fatah El Sisi.

**Libya**

***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama nchini Libya bado ni tete. Baada ya kuuawa kwa kiongozi wa Libya Kanali Muammar Gaddafi miaka mitatu iliyopita, na baada ya Balozi wa Marekani nchini Libya kuuawa, miaka miwili iliyopita mapigano ya wenyewe kwa wenyewe na mauaji ya wageni na raia yanazidi kushika kasi siku hadi siku. Hali imekuwa mbaya hadi kupelekea Waziri Mkuu kutekwa nyara na baadae kuachiliwa na Bunge kuvamiwa na kuchomwa moto. Mapigano na mauaji yanayoendelea, yanaifanya nchi ya Libya isitawalike na kusababisha ofisi nyingi za Ubalozi mjini Tripoli na Benghazi kufungwa. Tunashauri Watanzania wasiende Libya kwa sasa kutokana na hali iliyopo mpaka pale watakaposhauriwa vinginevyo.

**Burundi**

***Mheshimiwa Spika,*** hivi karibuni kumekuwa na taarifa za hali ya kisiasa na kiusalama nchini Burundi kuwa kuna mvutano wa Viongozi wa vyama vya siasa. Hali hii inatokana na hofu kwamba Serikali iliyopo madarakani ya Rais Pierre Nkurunziza inataka kubadilisha katiba ili kumpatia Rais Nkurunziza nafasi nyingine ya kugombea Urais kwa mara ya tatu. Wanasiasa, hasa kutoka kambi ya upinzani na Viongozi wastaafu wanasema kuwa kubadili katiba kutavunja makubaliano ya Arusha ya Amani na Maelewano kwa Burundi (*Arusha Peace and Reconcilliation Agreement for Burundi)* na hivyo kuhatarisha Amani na usalama wa nchi hiyo.

***Mheshimiwa Spika,*** sisi kama Tanzania tunalo jukumu la kuhakikisha kuwa ndugu zetu wa Burundi hawatumbukii kwenye matatizo ya kisiasa na usalama. Tunaamini kwamba, Mheshimiwa Pierre Nkurunziza hana nia wala sababu ya kubadili katiba ili kumwezesha kuendelea kubaki madarakani. Hivi sasa, mawasiliano ya kumaliza tatizo hili yanaendelea kati ya Serikali yetu, Umoja wa Afrika na viongozi mbalimbali wa Burundi. Tunashawishika kuamini kuwa wale wote wanaoitakia mema Burundi wataisaidia katika kulimaliza tatizo hili hasa nchi za jirani zinazoizunguka.

**Mapambano Dhidi ya Ugaidi**

***Mheshimiwa Spika,*** vitendo vya kigaidi vinavyofanywa na kikundi cha Boko Haram nchini Nigeria na pia kikundi cha Al-Shabaab nchini Kenya ni vitendo vya kulaaniwa na kukomeshwa na wapenda amani wote duniani. Mauaji ya hivi karibuni ya watu wasiopungua 400 na utekaji wa wanafunzi wasichana zaidi ya 200 nchini Nigeria na vilevile mauaji ya jumla ya watu zaidi ya 100 kwa jirani zetu Kenya ni ushaidi tosha wa kuitaka dunia kushirikiana kwa pamoja kupambana na vitendo vya kigaidi vya aina zote. Serikali yetu tayari imekwisha tuma salamu za pole tukilaani vitendo hivi na kutumia fursa hiyo kuwahakikishia wenzetu utayari wetu katika kushirikiana kwenye mapambano dhidi ya ugaidi.

***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ni nchi ya amani na yenye utulivu mkubwa. Pamoja na tofauti zetu, tusikubali wala kushawishika kuzimaliza tofauti zetu kwa njia za kigaidi. Tuendelee na tabia ya kukosoana na kumaliza tofauti zetu kwa mazungumzo na njia zinazokubalika kisheria. Tuwe macho na watu wote wasioitakia mema nchi yetu.

**MSIMAMO WA TANZANIA KATIKA MASUALA MUHIMU SADC NA UKANDA WA NCHI ZA MAZIWA MAKUU**

**Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC)**

***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imeendelea kuwa mstari wa mbele katika kushiriki kulinda amani, usalama na demokrasia kwenye nchi za Afrika. Kutokana na msimamo huo, Tanzania imechangia kikosi kimoja cha askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwenye *Force Intervention Brigade* (FIB) iliyoko chini ya kikosi cha Umoja wa Mataifa cha kulinda amani nchini DRC (MONUSCO). FIB inaongozwa na kamanda Mtanzania, Brig Gen. James Alois Mwakibolwa, kwa ajili ya kupambana na waasi ndani ya DRC. Ninafurahi kutamka kwamba askari wetu kwa kushirikiana na majeshi ya DRC na MONUSCO walifanya kazi nzuri na kukisambaratisha kabisa kikundi cha waasi wa M23 ambao wamekuwa wakivuruga amani kwa muda mrefu mashariki mwa DRC na kupelekea kupatikana kwa amani ambayo ilikuwa imepotea kwa muda mrefu.

***Mheshimiwa Spika,*** katika Mkutano wa dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika sanjari na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika jijini Addis Ababa, Ethiopia, tarehe 30 Januari, 2014, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) ilitoa taarifa kuhusu hali ya usalama inavyoendelea nchini humo baada ya kusainiwa kwa makubaliano ya kusitisha mapigano kati ya Serikali na kikundi cha M23.

***Mheshimiwa Spika,*** mwakilishi wa DRC alieleza kuwa baada ya kutiwa saini makubaliano hayo, hivi sasa Serikali yake imejielekeza katika kuvisambaratisha vikundi vya kijeshi vilivyosalia nchini humo ikianza na ADF-Nalu na baadaye FDLR. Mwakilishi huyo pia alieleza kuwa Bunge la nchi hiyo lilikuwa kwenye mchakato wa kutunga Sheria ya msamaha (amnesty law) ambayo itafafanua ni waasi gani watanufaika nayo na wale ambao hawataweza kunufaika na sheria hiyo. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, sheria hiyo imekwishapitishwa tangu tarehe 5 Februari 2014. Kwa mujibu wa sheria hiyo, walioshiriki katika makosa ya kimbari, makosa ya kivita na jinai dhidi ya ubinadamu *(genocide, war crimes and crimes against humanity)* hawatanufaika nayo.

**Malawi**

***Mheshimiwa Spika,*** mazungumzo ya usuluhishi wa mgogoro wa mpaka kati yetu na Malawi bado yanaendelea. Tarehe 20 na 21 Machi, 2014 tuliitwa Malawi kwenye jopo la usuluhishi lililopo chini ya uenyekiti wa Rais Mstaafu wa Msumbiji Joachim Chissano. Wengine ni Rais Mstaafu wa Afrika Kusini Thabo

Mbeki na Rais Mstaafu wa Botswana Festus Mogae. Pamoja nao kulikuwa na kikosi cha wanasheria sita waliobobea kwenye migogoro ya mipaka duniani.

Baada ya mjadala mkubwa uliotoa fursa kwa kila upande kuwasilisha hoja zake za kisheria mbele ya Jopo, Jopo lilishauri kuwa hoja za kisheria tuziweke pembeni kwa muda na badala yake kila upande uainishe hoja zisizo za kisheria. Tulitakiwa tujadili hoja zinazogusa maisha ya kila siku ya kijamii. Kwa mfano, Malawi wanatakiwa kueleza hasara watakazozipata endapo itaamriwa kuwa mpaka utapita katikati. Na Tanzania tunatakiwa kueleza hasara tutakazozipata endapo itaamriwa kuwa mpaka utapita kwenye ufukwe wa Ziwa.

**Mheshimiwa Spika,** timu ya Tanzania ambayo inajumuisha Wizara ya Ardhi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara yangu sasa inaandaa majibu. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Anna Tibaijuka (Mb.) na Mwanasheria Mkuu Jaji Fredrick Werema kwa kazi nzuri sana wanayoifanya katika kujenga hoja nzito na zenye ushawishi wa kuuweka mpaka katikati ya Ziwa na siyo ufukweni. Na huo ndio msimamo wa Tanzania. Aidha, kwa kuwa sasa Serikali mpya ya Malawi imechaguliwa na kuundwa, Jopo la usuluhishi litaitisha kikao cha pili ili kuendelea na shughuli za usuluhishi. Niwashukuru pia Mheshimiwa John Komba, Mbunge wa Mbinga na Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mbunge wa Ludewa ambapo waliambatana nasi na kutoa mchango wa hoja nzito kwa niaba ya wananchi wanaolizunguka Ziwa Nyasa.

**Zimbabwe**

***Mheshimiwa Spika,*** hali ya kisiasa nchini Zimbabwe kwa sasa ni shwari. Zimbabwe ilifanya Uchaguzi wake Mkuu wa Rais tarehe 31 Julai, 2013. Kabla ya uchaguzi huo, Zimbabwe ilifanya mchakato wa kutengeneza Katiba mpya kwa mafanikio makubwa. Tanzania ilishiriki katika uangalizi wa shughuli zote mbili kupitia timu ya uangalizi ya SADC ambayo niliiongoza mimi mwenyewe. Wananchi wa Zimbabwe walitumia nafasi yao ya kidemokrasia katika kuchagua viongozi wao na vyama walivyopenda kwa uhuru na haki. Katika uchaguzi huo, Mheshimiwa Robert G. Mugabe aliibuka mshindi wa Urais kwa kipindi cha miaka mitano kwa kupata asilimia 61.09 ya kura zote. Aidha, timu ya uangalizi ya SADC iliridhika na maandalizi yaliyofanywa na Tume ya Uchaguzi katika mchakato mzima wa uchaguzi nchini Zimbabwe kwa mwaka 2013 na kwamba ulikuwa huru na wa amani.

**Madagascar**

***Mheshimiwa Spika,*** baada ya jitihada za SADC za kuandaa mazingira ya uchaguzi kufanyika Madagascar, na baada ya kufanikisha zoezi la kuwaomba viongozi wa zamani; Ravanomanana, Rajoelina, Rasiraka na Mama Ravaromanana kutogombea kwa sababu za kiusalama, wananchi wa

Madagascar hatimaye walipiga kura tarehe 25 Oktoba, 2013 na kurudia Desemba 2013 ambapo Henry Martial Rakotoarimanana Rajaonarimampianina alichaguliwa kuwa Rais mpya wa Madagascar. Hali ya kisiasa nchini Madagascar kwa ujumla ni shwari ingawa kuna kutoelewana kati ya Rais aliyeondoka Rajoelina na Rais wa sasa baada ya Rais mpya kukataa pendekezo la Rais Rajoelina la kutaka ateuliwe kuwa Waziri Mkuu.

***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia ushindi huo, Wakuu wa Nchi wanachama wa SADC walikubaliana kwa kauli moja kuiondolea vikwazo nchi ya Madagascar na hivyo kuikaribisha rasmi kushiriki katika shughuli za SADC, ikiwemo kuhudhuria vikao vyote kama mwanachama halali. Kufuatia hatua hiyo Rais Rajaonarimampianina pia alikaribishwa rasmi kujumuika na kukalia kiti cha Madagascar katika mikutano ya Umoja wa Afrika (AU). Tuendelee kuwaombea amani ya kudumu wananchi wa Madagascar ili waweze kuijenga nchi yao.

## UTEKELEZAJI WA DIPLOMASIA YA UCHUMI

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara, Idara na Taasisi nyingine imeendelea kutekeleza Diplomasia ya Uchumi kwa kuvutia wawekezaji wenye vigezo na sifa kuja kuwekeza katika sekta mbalimbali hapa nchini. *Mikakati inayotumika ni pamoja na kujenga mazingira wezeshi ya ndani ya Kukuza Uchumi; Kuimarisha Ubia wa Kimataifa; Kuweka mbele Malengo ya Uchumi katika Ushirikiano Kati ya Nchi Mbili (Bilateral Cooperation); Kuimarisha Uhusiano wa Kimataifa (Multilateral Cooperation); kukuza ujirani mwema; na kukuza Ushirikiano wa Kikanda. Masuala haya yanatekelezwa kupitia ushiriki wetu kwenye Mikutano mbalimbali (Tume za Pamoja za Ushirikiano na mikutano mingine ya nchi na nchi na ile ya Kikanda na Kimataifa); Ziara za Viongozi wa Kitaifa Nje ya Nchi; ziara za Viongozi wa Mataifa ya Nje hapa nchini; na ofisi za uwakilishi nje ya nchi.*

***Mheshimiwa Spika,*** kwa ufupi kabisa napenda kuelezea baadhi ya mafanikio tuliyoyapata kwenye sekta mbalimbali ambayo yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa diplomasia ya uchumi:-

### Sekta ya Kilimo

***Mheshimiwa Spika,*** mwaka jana nililiarifu Bunge lako tukufu kuhusu mafanikio tuliyoyapata katika kutafuta masoko ya bidhaa zetu za kilimo kwenye soko kubwa la China. Mafanikio hayo ni pamoja na kuingia Mikataba, Makubaliano na Itifaki mbalimbali na Mamlaka pekee ya China inayoruhusu biashara za namna hiyo (***Administration of Quality Supervision, Inspection and Quarantine – AQSIQ***) ambayo imeruhusu Tanzania kuingiza zao la tumbaku nchini China. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, hivi sasa Mamlaka

hiyo imeruhusu pia mazao ya baharini kuingia nchini China. Makubaliano hayo yaliwekwa saini mbele ya Mawaziri Wakuu Mhe. Li Keqiang na Mhe. Mizengo Pinda wakati wa ziara ya Mhe. Waziri Mkuu nchini China mwezi Oktoba 2013. Hii ni fursa adhimu kwa wavuvi wetu kupata soko la uhakika la bidhaa zao.

***Mheshimiwa Spika,*** mchakato wa kuliwezesha zao la pamba kupata soko nchini China umefikia hatua nzuri, ambapo Mkoa wa Shinyanga na kampuni ya Dahong ya Jimbo la Jiangsu zimeingia Mkataba wa kuendeleza zao la pamba mkoani humo na kuuza katika viwanda vya Dahong, China. Mkataba huo unajulikana kwa jina la "***Agreement On China-Tanzania Modern Agro-Industrial Zone"*** na ni mmoja kati ya mikataba mitano (5) iliyowekwa saini Oktoba 17, 2013 mbele ya Mawaziri Wakuu Mizengo Pinda na Li Keqiang mjini Beijing.

***Mheshimiwa Spika,*** hivi sasa Wizara kupitia Ubalozi wa Tanzania Beijing, inafuatilia kwa karibu uingiaji wa Makubaliano na Serikali ya China yatakayoiwezesha Tanzania kuingiza China zao la muhogo kwa ajili ya matumizi ya viwandani ambako wanga wake unahitajika sana. Mchakato huo upo katika hatua nzuri baada ya *AQSIQ* kutoa taarifa kwamba imeridhika na hoja za mapendekezo yetu na hivyo, Wizara inaendelea kufuatilia ujio wa timu ya wataalam wa AQSIQ nchini kujiridhisha kuhusu utoshelevu na ubora wa viwango vya zao hilo ili kukidhi mahitaji ya soko la China.

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeziomba mamlaka za kilimo nchini kuanzisha michakato kama hiyo kwa mazao ya korosho, kahawa, ufuta, karanga, ngozi n.k, ili yaweze kuingia katika soko la China. Uzoefu unaonesha kwamba bila kuwa na mikataba au makubaliano ya namna hiyo mazao yetu yatakumbana na vikwazo kuingia katika soko hilo.

***Mheshimiwa Spika,*** katika Mkutano wa Tatu wa Ushirikiano kati ya Nchi za Afrika na nchi za Kiarabu uliofanyika nchini Kuwait mwezi Novemba 2013, Serikali ya Kuwait iliahidi kutoa kiasi cha Dola za Marekani bilioni moja kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano kwa ajili ya mikopo nafuu kwa nchi za Afrika, hususan katika sekta ya kilimo. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Tume za Mipango za Tanzania Bara na Zanzibar imekwishawasilisha miradi kadhaa ya umwagiliaji na maendeleo ya jamii.

***Mheshimiwa Spika,*** katika Mkutano huo, Serikali ya Saudi Arabia ilitenga kiasi cha dola za kimarekani bilioni nne kwa lengo la kukuza uzalishaji na usalama wa chakula. Ili kuchangamkia fursa hiyo, Wizara yangu imekamilisha majadiliano ya kuingia Mkataba wa Ushirikiano na Saudi Arabia utakaowezesha nchi yetu kunufaika na fursa hiyo. Ninatarajia kusaini Mkataba huo wakati wowote kabla ya mwisho wa Mwaka huu wa fedha.

***Mheshimiwa Spika,*** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ametoa mchango mkubwa kwenye sekta ya kilimo. Msisitizo umekuwa katika masuala yanayohusu usalama wa chakula na majaribio ya kuongeza matumizi ya teknolojia katika kilimo kwa lengo la kuwaongezea kipato wananchi na kukuza uchumi wa nchi. Kwa kutambua mchango wa Mheshimiwa Rais, mwezi Septemba 2013, Chuo Kikuu cha Guelph cha nchini Canada, kilimtunukia Shahada ya Heshima ya Uzamivu (*Honorary Doctorate*) ya Sheria. Mheshimiwa Rais amekuwa Mtanzania wa kwanza kutunukiwa shahada hiyo katika historia ya zaidi ya miaka 100 ya Chuo hicho maarufu kwa utafiti wa kilimo na magonjwa ya wanyama. Mchango huo wa Mheshimiwa Rais ambao umetambuliwa na Chuo cha Guelph unatoa fursa kwa taasisi na vyuo vyetu vinavyojihusisha na kilimo kuwa na ushirikiano wa karibu na chuo hicho katika kufanya tafiti mbalimbali na kuendeleza sekta ya kilimo.

***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua ukweli kwamba asilimia kubwa ya watanzania wanategemea kilimo na wanakabiliwa na changamoto ya umasikini wa kipato, serikali imefanya jitihada kuhakikisha kuwa nchi yetu inakuwa ni moja ya nchi za majaribio ya mpango wa kuwawezesha wananchi wengi zaidi kupata huduma za kifedha *(Inclusive Financing for Development)* hususan wasioweza kumudu masharti ya kibenki.

Katika kufanikisha juhudi hizo, Wizara yangu iliratibu kwa mafanikio makubwa ziara ya Malkia Maxima wa Uholanzi aliyetembelea Tanzania kuanzia tarehe 11 hadi 13 Desemba 2013 akiwa Mwakilishi Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika masuala ya *Inclusive Financing for Development*. Malkia Maxima alifuatana na wakuu wa Mashirika Matatu ya Umoja wa Mataifa yanayoshughulikia kilimo na chakula ambayo ni FAO, IFAD na WFP kuja kujionea maendeleo ya miradi iliyo chini ya mpango huo hapa nchini. Mpango huu umekuwa msaada mkubwa kwa wakulima wadogo katika kupunguza umasikini na kuongeza usalama wa chakula.

**Sekta ya Nishati**

***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha uliopita Wizara yangu ikitambua umuhimu wa nishati katika maendeleo ya Taifa letu, ilifanya juhudi katika kutafuta uwekezaji katika sekta hiyo. Mwaka huu tumeendelea kupata fursa mbalimbali ikiwa ni pamoja na mpango mpya wa ushirikiano na Serikali ya Marekani kwenye uzalishaji umeme barani Afrika uitwao *"Power Africa Initiative"* uliozinduliwa hapa nchini tarehe 2 Julai 2013 na Rais Barack Obama wa Marekani pamoja na Rais Jakaya Mrisho Kikwete wa Tanzania. Tanzania ni miongoni mwa nchi sita barani Afrika zinazonufaika na Mpango huo. Nchi nyingine ni Kenya, Ethiopia, Msumbiji, Ghana na Nigeria. Katika mpango huo,

Serikali ya Marekani imetenga kiasi cha Dola za Marekani bilioni saba wakati sekta binafsi nchini humo imeahidi kuwekeza kiasi cha Dola za Marekani bilioni tisa za kufanikisha utekelezaji wake.

***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa kuiandaa vyema nchi yetu kunufaika na nishati ya gesi iliyogundulika kwa wingi hivi karibuni, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini imeanza kutafuta fursa za kujifunza uzoefu wa wenzetu waliobahatika kuwa na nishati hiyo na kupata mafanikio makubwa ili nasi tuweze kuingia katika uchumi wa gesi na mafuta bila matatizo.

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu kupitia Balozi zake imeratibu ziara za mafunzo nchini India, Japan, Malaysia, Canada, Algeria, Oman, Australia na Qatar. Aidha, tumeendelea kutafuta fursa mbalimbali za masomo kwa ajili ya wataalam katika sekta ya mafuta na gesi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa matunda ya juhudi hizo yameshaanza kupatikana. Tayari nchi za Thailand, Australia, China na Canada zimetoa nafasi za masomo kwa wataalam wetu. Tunaendelea kutafuta fursa zaidi katika nchi zingine.

***Mheshimiwa Spika,*** juhudi zetu za kutafuta fursa za uwekezaji katika sekta ya Nishati zimewezesha nchi yetu kuingia makubaliano ya ushirikiano wa kiuchumi na nchi ya Algeria ambapo miradi mbalimbali katika masuala ya gesi na umeme itatekelezwa. Kwa kuanzia tumekubaliana kuanzisha kwa pamoja migodi ya Phosphate kwa ajili ya uzalishaji wa mbolea kwa matumizi ya ndani na kuuza nje. Pia tumekubaliana kuanzisha Kampuni ya pamoja ya kusambaza umeme na kujenga kiwanda cha kusindika gesi asilia kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Kutekelezwa kwa miradi hiyo sio tu kutatoa ajira kwa wananchi wengi katika sekta ya huduma, lakini pia kutalipatia taifa fedha za kigeni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kupunguza uharibifu wa mazingira.

***Mheshimiwa Spika,*** wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, aliyoifanya nchini Singapore mwezi Juni 2013, alikutana na viongozi wa Makampuni Makubwa ya Biashara. Kufuatia mkutano huo, Kampuni ya Pavillion Energy ya nchini Singapore imekubali kuwekeza katika sekta ya gesi nchini ambapo kwa kuanzia imenunua asilimia 20 ya hisa za Kampuni ya Ophir Gas kwa kiasi cha Dola za Marekani bilioni 1.3.

**Sekta ya Biashara**

***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa sekta ya biashara, Wizara yangu imeendelea kutafuta fursa mbalimbali za biashara kwa watanzania nje ya nchi

na pia masoko kwa bidhaa zetu nje ya nchi. Balozi zetu zote duniani zimeendelea kuwezesha upatikanaji wa taarifa juu ya maonesho ya biashara, masoko ya bidhaa na fursa za uwekezaji. Mwaka huu Kampuni ya Dragon Mart ya Dubai imeonesha nia ya kuwekeza nchini kwa kushirikiana na TANTRADE. Lengo la ushirikiano huo ni kujenga eneo la kisasa la maonesho ya kimataifa ya biashara nchini ambalo litakuwa linafanya maonesho ya biashara kwa kipindi cha mwaka mzima. Kwa wale waliobahatika kufika katika jiji la Dubai na kutembelea Dragon City, hivyo ndivyo itakavyokuwa hapa, pale mpango huo wa kuanzisha eneo hilo hapa Tanzania utakapofanikiwa.

***Mheshimiwa Spika,*** vilevile napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Shirika la Emirates, limekubali kuanzisha safari za ndege za Shirika lake lingine la FlyDubai kutoka Dubai kwenda Kilimanjaro, Dar es Salaam na Zanzibar. FlyDubai ni shirika lenye bei nafuu kwa wateja (*budget airline*), kwani mara nyingi nauli zake zinakuwa nusu ya nauli ya ndege nyingine ikiwamo Emirates. Huduma hii italeta unafuu mkubwa hasa kwa wafanyabiashara wetu wanaofanya shughuli zao kati ya Tanzania na Dubai au maeneo mengine kupitia Dubai.

**Sekta ya Utalii**

***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kukuza utalii Serikali kupitia Ubalozi wetu wa Washington Marekani imefungua Ofisi tisa za Uwakilishi wa Heshima (Honorary Consulates) sehemu mbalimbali nchini Marekani. Hatua hiyo inatarajiwa kuongeza idadi ya watalii kutoka Taifa hilo.

***Mheshimiwa Spika,*** ni dhahiri kwamba soko kubwa la utalii duniani lipo China. Wizara yangu kupitia Ubalozi wake nchini China imeanza mazungumzo na mamlaka za Utalii za China kuhusu utangazaji wa vivutio vya utalii vya Tanzania. Aidha, wakati wa Ziara ya Waziri Mkuu nchini China mwezi Oktoba 2013, kampuni kubwa ya Usafirishaji wa Watalii ya Hong Kong Travels iliahidi kusafirisha watalii wapatao 10,000 kila mwaka kutembelea Tanzania. Kampuni hiyo imekubali ombi la Mheshimiwa Waziri Mkuu kuja kuwekeza katika ujenzi wa hoteli zenye hadhi ya Nyota Tano katika maeneo ya karibu na Mbuga za Wanyama kwa ajili ya kulaza watalii.

***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2013/2014, Wizara katika juhudi zake za kukuza utalii iliratibu kwa ushirikiano na TANAPA kongamano la vijana wa Tanzania na Saudi Arabia kuhusu Bio-Anuai lililofanyika mkoani Arusha mwezi Januari, 2014. Kongamano hilo lilisaidia sana kukuza diplomasia ya uchumi hasa kwenye kuwavutia watalii kutoka Saudi Arabia na wananchi wengine wa Nchi za Ghuba kuijua Tanzania. Tayari misafara zaidi ya

mitatu inayowahusisha wanafamilia za kifalme wa Nchi za *Gulf Cooperation Council* imefanya ziara nchini Tanzania ikifuata mfano wa vijana hao wa Saudi Arabia.

***Mheshimiwa Spika,*** vilevile Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa katika ziara nchini China alifanya mazungumzo na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Ndege ya Hainan na South China Airlines ili kuwavutia waanzishe safari za moja kwa moja kutoka China kuja nchini ili kurahisisha usafiri wa watalii wanaotaka kuja nchini. Makampuni hayo yamekubali kutuma wataalam wake kuja nchini kufanya upembuzi yakinifu.

***Mheshimiwa Spika,*** halikadhalika, mnamo tarehe 25 Machi, 2014, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mhe. Frank-Walter-Steinmeier, Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani aliyewasili nchini na ujumbe wa watu 80 wakiwemo wafanyabiashara kutoka makampuni makubwa ya Ujerumani, Wabunge, watendaji wa Serikali na Waandishi wa Habari. Lengo la ziara yake lilikuwa kuimarisha ushirikiano wa kihistoria uliopo kati ya Tanzania na Ujerumani hususan katika nyanja za utalii, biashara na uwekezaji. Kama sehemu ya mafanikio ya ziara hiyo, Mhe Steinmeier alimkabidhi Waziri wa Maliasili na Utalii, ndege ndogo kwa ajili ya kukabiliana na uwindaji haramu wa wanyamapori.

**Sekta ya Miundombinu na Uchukuzi**

***Mheshimiwa Spika,*** Ubalozi wetu Abu Dhabi kupitia Ubalozi Mdogo wa Dubai kwa kushirikiana na Shirika la Taifa la Nyumba (NHC) ulifanya vikao kadhaa na wamiliki wa mashirika makubwa ya ujenzi wa majengo ya biashara na ya makazi ambapo walifanikiwa kuwapata wawekezaji wakubwa kwenye sekta hiyo. Mashirika yaliyokubali kuja kuwekeza Tanzania ni:- DAMAC, AL GHURAIR, SOBHA na NAKHIL. Mashirika hayo ndiyo yaliyojenga majengo makubwa na mashuhuri yanayoonekana katika Jiji la Dubai. Kampuni ya DAMAC ipo tayari kuwekeza kwenye eneo la ufukwe wa bahari, Kawe Dar es Salaam lisilopungua ukubwa wa ekari 1000, kwa kujenga Hoteli za Nyota 5, nyumba za kuishi (Villas) na uwanja wa kisasa wa Golf (golf course). Aidha, kwa kutambua fursa hiyo Ubalozi umeandaa mkutano wa wawekezaji wa Dubai na Tanzania tarehe 11 Juni, 2014, katika Hoteli ya Jumeirah Emirates Tower, Jijini Dubai. Shirika la NHC, ndio wanaoratibu ushiriki wa wawekezaji kutoka Tanzania. Tunawapongeza na kuwaahidi ushirikiano wetu.

**Sekta ya Ajira**

***Mheshimiwa Spika,*** baada ya mji wa Dubai kushinda kinyang'anyiro cha kuwa mwenyeji wa Maonesho ya Biashara ya Dunia ya 2020 (World Expo 2020),

ni wazi fursa nyingi zitapatikana kupitia maonesho hayo, hasa tukitilia maanani uhusiano mzuri wa kidiplomasia uliopo kati yetu na Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu (U.A.E). Kati ya fursa hizo, ni pamoja na nafasi za ajira milioni mbili na laki nane ambazo serikali ya UAE itahitaji kuzijaza kwa ajili hiyo. Kwa kutambua fursa hiyo, Wizara kwa kushirikiana na Ubalozi wetu wa U.A.E tumejipanga kikamilifu ili kuchangamkia fursa hizo.

***Mheshimiwa Spika,*** tayari Ubalozi umekutana na Shirika la Emirates (*Emirates Group*) ambalo ndio mmiliki wa Shirika la ndege la Emirates, Dnata, na FlyDubai, na kuweka mikakati ya kuongeza ajira kwa watanzania katika mashirika yote yaliyo chini ya Emirates. Shirika la Emirates limekubali kuajiri wafanyakazi kutoka Tanzania katika kada za wahudumu wa ndege (*cabin crews*), mafundi (*technicians*), maafisa mipango (*planning assistants*), watoa huduma kwa wateja na masuala ya tiketi (*customer care and ticketing*). Napenda kuwasihi watanzania wote wenye sifa zitakazotakiwa, waombe nafasi hizi kwa wingi mara zitakapotangazwa rasmi.

**Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano (JPC)**

***Mheshimiwa Spika,*** katika kuratibu shughuli za Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano (JPC), Wizara imeendelea kufanya vikao vya wadau wa ndani na nje ya nchi ili kutekeleza shughuli hizo. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na wadau kutoka Wizara nyingine, Taasisi za Umma na Sekta Binafsi iliandaa awamu ya nane ya Mkutano wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano kati ya Tanzania na India uliofanyika katika Hoteli ya Kilimanjaro, Hyatt tarehe 8 hadi 9 Julai, 2013. Maazimio ya Mkutano huo yalitiwa saini na mimi mwenyewe na Mhe. Prabeet Kaur, Waziri wa Nchi wa Mambo ya Nje wa India. Maazimio ya Mkutano huo yanalenga katika kuweka maeneo ya ushirikiano wa Tanzania na India kwa kipindi cha miaka mitatu. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu shughuli na utekelezaji wa makubaliano ya JPCs mbalimbali ambazo nchi yetu imefikia makubaliano, hususan Algeria, Botswana, Kenya, Msumbiji, Rwanda na Zambia.

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanikiwa kutekeleza sehemu ya majukumu yaliyotajwa hapo juu kwa ushirikiano na washirika wa maendeleo kutoka nchi na asasi mbalimbali za kitaifa, kikanda, kimataifa pamoja na sekta binafsi. Naomba nitumie fursa hii kuwashukuru washirika wetu wote wa maendeleo ikiwa ni pamoja na Australia, Brazil, Canada, China, Cuba, Finland, India, Italia, Ireland, Japan, Korea Kusini, Kuwait, Malaysia, Marekani, Norway, Oman, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uhispania, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu, Ureno, Urusi, Uswisi, Uturuki, Umoja wa Ulaya, FAO, IAEA, ILO, IMF, IOM, UNDP, UNEP, UN-HABITAT, UNWTO, UNHCR, UNICEF, UNFPA, UNESCO,

UNIDO, WHO World Bank na WWF kwa mchango wao mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa Diplomasia ya uchumi.

**Ziara za Viongozi wa Kitaifa Nje ya Nchi**

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ndiyo msimamizi mkuu wa masuala ya Itifaki ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo Wizara imeendelea kutoa huduma ya Itifaki kwenye sherehe zote na maadhimisho ya Kitaifa; kuratibu safari za Viongozi wa Kitaifa walipokwenda nje ya nchi; na kuratibu mapokezi ya Viongozi wa Nje waliotembelea Tanzania. Wizara imeandaa na kuratibu ziara za kikazi za Viongozi wa Kitaifa katika nchi za:- Nigeria, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Afrika Kusini, Malawi, Namibia, Kenya, Uganda, Oman, Marekani, Canada, Ethiopia, Uingereza, Sri Lanka, Poland, Kuwait, Ufaransa, Falme za Kiarabu, India, Uholanzi na China.

***Mheshimiwa Spika,*** ziara hizo zimefungua milango mipya ya ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi hizo, kati ya wananchi wa nchi zetu na kati ya sekta binafsi kutoka pande zote. Aidha, ziara hizo pia zimechochea na kukuza biashara na kuimarisha mahusiano. Nitapata muda baadae mchana wa kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu jambo hili ambalo kila mara limekuwa linazua maswali.

**Ziara za Viongozi wa Nchi na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa Nchini**

***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Viongozi wa Kimataifa kutoka nje ya nchi, Wizara iliandaa na kuratibu ziara za kikazi za Wakuu wa Nchi na Serikali kutoka nchi za; Marekani, Thailand, Burundi, Finland, Sweden, Uholanzi, Benin na Comoro.

***Mheshimiwa Spika,*** pia Wizara imehusika kikamilifu katika kuandaa na kuratibu ushiriki wa Viongozi Wakuu wa Nchi na Serikali na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa kutoka nchi mbalimbali katika sherehe za maadhimisho ya miaka 52 ya Uhuru wa Tanganyika, tarehe 09 Desemba, 2013, sherehe za maadhimisho miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar tarehe 12 Januari 2014 na maadhimisho ya Miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar sherehe ambazo zilizofanyika tarehe 26 Aprili, 2014.

**KUSIMAMIA MIKATABA NA MAKUBALIANO YA KIMATAIFA**

**Mikataba ya Kimataifa**

***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza jukumu la kusimamia Mikataba na Makubaliano baina ya Tanzania, nchi nyingine na Taasisi mbalimbali za

Kimataifa, Wizara iliratibu na kusimamia uwekwaji saini wa Mikataba kati ya Tanzania na Nchi Nyingine (Bilateral Agreements) kama ifuatavyo:-

i. Mkataba kati ya Serikali ya Tanzania na Thailand kuhusu kuanzisha mahusiano ya kibiashara na kiuchumi, 30 Julai 2013;

ii. Mkataba kati ya Serikali ya Tanzania na Thailand kuhusu Ushirikiano katika Utunzaji wa Wanyamapori, 31 Julai, 2013;

iii. Mkataba kati ya Tanzania na Thailand kuhusu kubadilishana wafungwa, 30 Julai, 2013;

iv. Mkataba kati ya Tanzania na Thailand kuhusu kulinda Uwekezaji, 30 Julai 2013;

v. Makubaliano (MoU) ya kuongeza muda wa matumizi ya Hati ya Makubaliano kati ya Wizara ya Nishati na Madini na Chuo cha Gem and Jewelery cha Thailand, 30 Julai 2013;

vi. Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ya Tanzania na Taasisi ya Clinton Foundation kuhusu ushirikiano katika masuala ya Kilimo, Agosti 2013;

vii. Mkataba wa Kimataifa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Nchi ya Kuwait kwa ajili ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji, 17 Novemba, 2013;

viii. Mkataba kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Nchi ya Kuwait wa kushirikiana katika Sekta ya Utalii, 17 Novemba, 2013;

ix. Mkataba wa Wenyeji wa Mahakama ya Kimataifa iliyorithi shughuli za iliyokuwa Mahakama ya Kimataifa ya Mauaji ya Kimbari ya Rwanda kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Umoja wa Mataifa, 26 Novemba, 2013;

x. Hati za Makubaliano (Memoranda of understanding) baina ya Tanzania na *Brazil, Iceland, Yemen, Seychelles, Swaziland, Zimbabwe, Qatar na Saudi Arabia* katika Sekta ya Usafiri wa Anga, Desemba 2013;

xi. Mkataba wa Nyongeza kwenye Mkataba wa Uenyeji baina ya Tanzania na Umoja wa Mataifa kuhusu ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Kimataifa (MICT), iliyorithi shughuli za

iliyokuwa Mahakama ya Mauaji ya Kimbari ya Rwanda (ICTR), Februari, 2014;

xii. Mkataba kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya kuhusu Mapambano dhidi ya Uharamia, Aprili 2014; na

xiii. Mkataba kati ya Tanzania na Kosovo kuhusu kuanzisha Mahusiano ya Kidiplomasia, Aprili 2014.

***Mheshimiwa Spika,*** mikataba hii itasimamiwa na kutekelezwa na kila sekta husika. Wizara yangu itaendelea na jukumu la kuratibu uwekaji saini na kufuatilia utekelezaji wa mikataba na makubaliano mbalimbali baina ya nchi yetu na nchi nyingine pamoja na mashirika ya kimataifa.

**USHIRIKI WA TANZANIA KATIKA JUMUIYA ZA KIMATAIFA, BARA LA AFRIKA NA KIKANDA**

**USHIRIKIANO WA KIMATAIFA**

***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu, japo kwa ufupi, mafanikio yaliyopatikana kutokana na ushiriki wetu kwenye mikutano ya kimataifa na katika jumuiya mbalimbali ambazo nchi yetu ni mwanachama.

**Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA);**

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ushiriki wa nchi yetu kwenye Mkutano wa 68 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA), uliofanyika New York, Marekani kuanzia mwezi Septemba hadi Desemba 2013. Katika Mkutano huo masuala mbalimbali yalijadiliwa ikiwa ni pamoja na suala la ajenda ya maendeleo baada ya mwaka 2015 ambapo Malengo ya Maendeleo ya Milenia tunayoyatekeleza sasa yatafikia ukomo. Katika kujadili ajenda hiyo, mjadala uligusa pia suala la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ambayo kimkakati ndiyo yanaandaliwa kuchukua nafasi ya Malengo ya Milenia ifikapo 2015.

***Mheshimiwa Spika,*** katika mkutano huo, Tanzania ilipata fursa ya kuelezea ulimwengu jitihada zake kwenye maeneo mbalimbali ya kukuza uchumi, kuendeleza kilimo, lishe na usalama wa chakula; utatuzi wa migogoro; na ushiriki wa nchi kwenye ulinzi wa amani kupitia Umoja wa Mataifa. Vilevile, Tanzania iliendeleza jitihada zake za kusimamia ukombozi duniani kuzitaka nchi zote zinazotawaliwa ikiwemo Palestina na Saharawi kupatiwa uhuru wake.

***Mheshimiwa Spika,*** zaidi ya hayo, Mheshimiwa Rais alishiriki kwenye Mikutano ya pembeni ya nchi na nchi na mingine ukiwemo Mkutano wa Kupambana na Ujangili kwenye mbuga za wanyama unaotishia kutoweka kwa baadhi ya wanyama kama vile tembo na faru. Mheshimiwa Rais alitumia mkutano huo kuelezea ulimwengu jitihada zinazotumiwa na Serikali kupambana na ujangili, pia alitumia fursa hiyo kuitaka Jumuiya ya Kimataifa kuweka nguvu za pamoja katika kupambana na ujangili. Matokeo ya mkutano huo ni kuanza kupatikana kwa misaada ya vifaa kwa ajili ya kupambana na ujangili kutoka Marekani, Ujerumani na Uingereza.

**Kikundi Kazi cha kuandaa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs)**

***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ni mjumbe wa kikundi kazi cha nchi 30 kilichoanzishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwa ajili ya kufanya majadiliano ya kuanzishwa kwa malengo ya maendeleo endelevu (SDGs) yanayotarajiwa kurithi malengo ya maendeleo ya milenia baada ya muda wake kumalizika mwaka 2015. Kuanzia Machi 2013 hadi sasa imeshafanyika mikutano 11 ya majadiliano hayo na Wizara imekuwa ikishiriki kikamilifu ili kuona kwamba taifa haliachwi nje ya mchakato na maslahi ya nchi yanapata nafasi katika malengo ya maendeleo endelevu.

***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha wadau wote wanashirikishwa kikamilifu kwenye mchakato huo zikiwemo taasisi za serikali na zisizo za serikali, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango tayari imeshafanya makongamano manne; mawili Zanzibar na mawili Tanzania Bara. Makongamano haya yameshirikisha Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu Zanzibar na Tanzania Bara; Wakurugenzi wa Sera na Mipango, Zanzibar na Tanzania Bara; na taasisi mbalimbali zisizo za serikali kwa pande zote mbili. Lengo la makongamano hayo ni kuelezea kwa kina maendeleo ya mchakato huo na kupokea maoni na ushauri wa taasisi hizo kuhusu majadiliano hayo.

**Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 19)**

***Mheshimiwa Spika,*** Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 19) ulifanyika Warsaw, Poland tarehe 11 - 22 Novemba 2013. Pamoja na ujumbe wa Tanzania kushiriki kama nchi, Mheshimwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwawakilisha Wakuu wa Nchi za Bara la Afrika kwa nafasi yake ya Mwenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (CAHOSCC). Akiwa Warsaw, Mheshimiwa Rais alifanya kikao na Mawaziri wa Mazingira na "negotiators" wa Afrika na kuweka msimamo wa pamoja wa namna ya kuhakikisha maslahi ya Afrika yanalindwa kwenye mkutano huo na mingine ya mabadiliko ya Tabianchi. Mheshimiwa Rais alisisitiza umuhimu wa kutoa kipaumbele kwenye

masuala ya upatikanaji wa fedha, teknolojia na kuijengea Afrika uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

***Mheshimiwa Spika,*** kwenye suala la upatikanaji wa fedha, nchi tajiri na zenye viwanda duniani ziliahidi kuchangia kiasi cha Dola za Marekani bilioni 100 kila mwaka hadi mwaka 2020. Kiasi hiki cha fedha kitasaidia nchi maskini kwenye masuala ya *adaptation na mitigation.*

**Mkutano wa Kimataifa kuhusu Biashara Haramu ya Wanyamapori**

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ushiriki wa nchi kwenye Mkutano wa Kimataifa kuhusu Biashara Haramu ya Wanyamapori (London Conference on illegal Wildlife Trade) uliofanyika London, Uingereza, tarehe 12 na 13 Februari 2014. Mkutano huu uliikutanisha Jumuiya ya Kimataifa kwa lengo la kujadili na kutafuta mbinu za kupambana na hatimaye kutokomeza kabisa biashara haramu ya pembe za Ndovu na Faru. Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zimeathirika sana na biashara hii na Serikali imeendelea kupambana vikali na vitendo vya kijangili vinavyosabisha biashara hiyo haramu.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huo, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipata fursa ya kuifahamisha Jumuiya ya Kimataifa kuhusu juhudi na hatua ambazo Serikali ya Tanzania inachukua kutokomeza tatizo hili. Aidha, Mheshimiwa Rais alitumia jukwaa hilo kusisitiza umuhimu wa jumuiya ya kimataifa kuhakikisha kuwa soko la bidhaa hizi linatokomezwa kabisa hasa kwenye nchi za Asia ambako ndiko kuna soko kubwa.

***Mheshimiwa Spika,*** mkutano ulikubaliana pamoja na masuala mengine, kuongeza ushirikiano kati ya mataifa katika kudhibiti biashara hiyo; kupiga marufuku biashara hiyo bila kutoa ahueni kama ilivyokuwa inafanyika awali; kuhakikisha kuwa nchi zinapitisha sheria kali dhidi ya ujangili na kuhakikisha kuwa meno yaliyohifadhiwa sasa hivi yanakosa soko.

**Mkutano wa Jukwaa la Uchumi la Dunia (WEF)**

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ushiriki wa nchi kwenye Mkutano wa Jukwaa la Uchumi la Dunia (WEF) uliofanyika Davos, Uswisi, kuanzia tarehe 22

hadi 25 Februari 2014. Kupitia Jukwaa hili, Tanzania imeendelea kuvutia wawekezaji hasa katika sekta ya kilimo kupitia mpango wa "*Grow African Partinership*". Aidha, katika mkutano huo, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Bodi ya Chai na *Tanzania Smallholder Tea Development Agency* ilisaini makubaliano na Kampuni ya Unilever. Makubaliano hayo ni baada ya Kampuni hiyo kuonesha nia ya kuwekeza kwenye kilimo cha Chai kupitia SAGCOT. Inatarajiwa kuwa uwekezaji huu utainua uzalishaji wa chai mara tatu zaidi ya kiwango kinachozalishwa sasa na kuingiza wastani wa Euro Milioni 110. Hatua hii itasaidia kuongeza mapato kutokana na bidhaa zitakazosafirishwa nje ya nchi.

***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeingia makubaliano (MoU) na WEF katika maeneo ya uendelezaji wa miundombinu na usimamizi wa Maji. Makubaliano hayo yamefanyika baina ya Serikali kupitia Wizara ya Maji na "*Water Resources Group Partnership*" ya WEF. Makubaliano hayo yatasaidia kuvutia uwekezaji kwenye sekta ya Maji na hivyo kuhakikisha usimamizi endelevu wa maji kwa maendeleo. Aidha, Makubaliano hayo yamejikita katika kuboresha huduma ya maji katika maeneo matatu ambayo ni upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi yote ya viwanda na majumbani; usimamizi wa maji taka; na umwagiliaji.

***Mheshimiwa Spika,*** eneo lingine ambalo Serikali imenufaika kupitia Mkutano huo ni kwenye sekta ya miundombinu. Serikali iliingia mkataba na WEF chini ya mpango wa "*Africa Strategic Infrastructure Initiative*" wenye madhumuni ya kuvutia wawekezaji kwenye miundombinu na hivyo kuleta manufaa kwa uchumi (*Infrastructure with larger multiplier effect*). Mpango huu ambao pia unahusisha Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) umeichagua Bandari ya Dar es salaam kuwa sehemu ya miradi yake ya awali. Tayari AfDB ilituma timu yake nchini kufanya tathmini ya awali ya mradi wa upanuzi wa Bandari hiyo.

**Jumuiya ya Madola**

***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ilichaguliwa tena na Wakuu wa nchi na Serikali wa Jumuiya ya Madola kuendelea kuwa mjumbe wa Kikundi Kazi cha Mawaziri wa Jumuiya ya Madola (CMAG). Mawaziri wanaounda CMAG walinipendekeza na kunichagua kwa nafasi yangu kama Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wa Tanzania kuwa Mwenyekiti wa CMAG kwa mwaka 2013 - 2015. Kuchaguliwa kwangu ni mafanikio kwa Diplomasia ya nchi na kumedhihirisha jinsi nchi inavyoheshimika kwenye Jumuiya ya Kimataifa, ikizingatiwa kuwa CMAG ni chombo maalum na chenye hadhi ya kipekee kwenye muundo wa

Jumuiya ya Madola kinachosimamia kanuni na taratibu za Jumuiya hiyo kwa nchi wanachama.

**Diplomasia ya Michezo**

***Mheshimiwa Spika,*** Jumuiya ya Madola itakuwa na mashindano ya Olimpiki huko Glasgow, Uingereza mwezi Julai mwaka huu. Katika mashindano hayo, vijana wanariadha wa Tanzania watashiriki katika maeneo ya mbio fupi na ndefu, pamoja na michezo ya mpira wa meza, ngumi, judo n.k vijana wasiopungua 50 wanatarajiwa kushiriki katika mashindano hayo.

Kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Wizara yangu, kwa kutumia diplomasia ya mahusiano katika michezo, tumeweza kupeleka vijana 50 pamoja na walimu wao kwenye makambi ya mafunzo Ethiopia, Uturuki, New Zealand na China. Vijana wapo huko na taarifa tulizonazo ni kwamba mazoezi yanakwenda vizuri sana. Ni matumaini yetu kuwa huko Glasgow, vijana wetu watafanya maajabu na kuijengea heshima nchi yetu.

**USHIRIKIANO WA KIKANDA**

**Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC)**

***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imeendelea kushiriki kikamilifu kwenye Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika. Mwezi Agosti, 2013, Wizara iliratibu na kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC uliofanyika Lilongwe, Malawi. Mkutano huo ulijadili na kufanya maamuzi mbalimbali yakiwemo yafuatayo:-

a) Kumteua Mheshimiwa Joyce Banda, Rais wa Malawi kuwa Mwenyekiti wa SADC hadi Agosti, 2014; Mhe. Banda alichukua nafasi hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Emilio Armando Guebuza, Rais wa Msumbiji;

b) Kumteua Mheshimiwa Hifikepunye Pohamba, Rais wa Namibia kuwa Mwenyekiti wa Asasi ya SADC inayoshughulikia masuala ya Siasa, Ulinzi na Usalama. Mheshimiwa Pohamba alichukua nafasi hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

c) Kumteua Dkt. Stergomena L. Tax kutoka Tanzania kuwa Katibu Mtendaji wa SADC kuchukua nafasi ya Dkt. Tomaz Agosto Salamao ambaye kipindi chake kilimalizika. Dkt. Tax amekuwa mwanamke wa kwanza kuteuliwa kuingoza Jumuiya hii katika miaka 33 ya uhai wake. Uteuzi huo ni uthibitisho mwingine wa kuzidi kushamiri kwa diplomasia ya Tanzania na umeendelea kuijengea heshima kubwa na kuitangaza nchi yetu katika medani ya Kimataifa.; na

d) Kuendelea kutoa ushauri juu ya utatuzi wa migogoro mbalimbali ya kisiasa inayoendelea ukanda wa SADC.

**Ukanda wa Nchi za Maziwa Makuu (ICGLR)**

***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imeendelea kushiriki kikamilifu katika Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu (The International Conference on the Great Lakes Region -ICGLR). Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi za ICGLR uliyofanyika tarehe 15 Januari 2014 Luanda, Angola na uliiomba Jumuiya ya Kimataifa kuendelea kutoa misaada ya kibinadamu Mashariki mwa DRC; na pia kuziomba nchi zote za jirani na DRC zilizosaini Mpango wa Amani, Usalama na Ushirikiano (The Peace, Security and Cooperation Framework for the DRC and the Region) kuendelea kutekeleza makubaliano yaliyoazimiwa katika Mpango huo ikiwemo kutohifadhi wala kusaidia makundi ya waasi. Aidha, mkutano huu uliiagiza Sekretarieti ya ICGLR kwa kushirikiana na Ofisi ya Mjumbe maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika nchi za Maziwa Makuu, Mhe. Mary Robinson kuandaa mkutano wa kwanza wa aina yake katika eneo letu utaokojadili suala la vijana na ukosefu wa ajira *(ICGLR's Special Summit on Youth and Unemployment)*. Mkutano huu unatarajiwa kufanyika mjini Nairobi, Kenya mwishoni mwa mwezi Juni 2014 na kuhudhuriwa na Wakuu wa Nchi na Serikali wa ICGLR na pia wadau mbalimbali katika suala la ajira za vijana.

***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa uwekezaji vitega uchumi na biashara katika kuleta maendeleo ya haraka na endelevu, unaandaliwa mkutano mwingine maalum wa uwekezaji (*the Private Sector Special Investment Forum)* utakaofanyika baadaye mwaka huu. Lengo la mkutano huu ni kuchochea uwekezaji katika nchi za Maziwa Makuu hususan zile ambazo zimekumbwa na machafuko.

**BARA LA AFRIKA**

**Umoja wa Afrika (AU)**

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Balozi zetu imeendelea kuratibu ushirikiano wa Tanzania na nchi nyingine Barani Afrika na kushiriki

kwenye shughuli za Umoja wa Afrika (AU). Mwezi Julai 2013, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano Maalum wa Wakuu wa Nchi wa Umoja wa Afrika kuhusu UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria uliofanyika Abuja, Nigeria. Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliongoza ujumbe wa Tanzania kwenye mkutano huo. Mkutano huu, pamoja na masuala mengine, ulipitisha Azimio linalozitaka nchi za Afrika kuchukua hatua za makusudi kutokomeza UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria Barani Afrika ifikapo mwaka 2030.

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano Maalum wa Wakuu wa Nchi wa Umoja wa Afrika kuhusu Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai (ICC) uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia, mwezi Oktoba 2013, ambapo Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliongoza ujumbe wa Tanzania. Mkutano huo, ulijadili suala la kesi inayowakabili Viongozi Wakuu wawili wa Serikali ya Kenya kwenye ICC. Mkutano huo, ulipitisha Azimio ambalo pamoja na masuala mengine, lilisisitiza umuhimu wa kuheshimu misingi ya haki na kukabiliana na ukiukwaji wa sheria, utawala bora, amani na usalama Barani Afrika pamoja na kuheshimu utu na mamlaka ya nchi.

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara vilevile iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 22 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, ambapo nilimuwakilisha Mheshimiwa Rais kuongoza ujumbe wa Tanzania. Mkutano huu ulijadili na kupitisha maamuzi mbalimbali yenye maslahi kwa Taifa letu, ikiwemo Msimamo wa pamoja wa Afrika kuhusu Agenda ya Maendeleo baada ya Mwaka 2015 *(Common African Position on Post – 2015 Development Agenda)* na kuanzisha Chombo cha Mpito cha Kukabiliana na Migogoro Barani Afrika *(African Capacity for Immediate Response to Crises – ACIRC)*. Tanzania ni miongoni mwa nchi waanzilishi wa chombo hicho. Aidha, wakati wa Mkutano huo, Tanzania ilichaguliwa kwa muhula wa pili kuwa mjumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kwa kipindi cha miaka miwili hadi mwezi Aprili 2016.

***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imeendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwenye Baraza hilo, ambapo mwezi Desemba 2013, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano Maalum wa Wakuu wa Nchi wa Baraza hilo uliofanyika mjini Banjul, Gambia, kwa ajili ya kujadili hali tete ya migogoro nchini Jamhuri ya Afrika ya Kati na Sudan Kusini. Mkutano huo ndiyo uliotoa pendekezo la kupelekwa kwa vikosi vya kulinda amani vya Umoja wa Afrika katika nchi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati.

## WATANZANIA WAISHIO UGHAIBUNI NA SWALA LA URAIA PACHA (DUAL CITIZENSHIP)

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza jukumu lake la kuwashirikisha Watanzania waishio ughaibuni *(Diaspora)* katika maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii ya nchi yetu. Wizara, kwa kutumia kurugenzi yake ya Diaspora inaendelea na utafiti kwa kushirikiana na Balozi zetu duniani pamoja na uongozi wa Jumuiya za Diaspora ili kubaini idadi kamili ya Watanzania waishio nje, ikiwa ni pamoja na kubaini taaluma zao.

Changamoto na kilio kikubwa cha wana-Diaspora cha kutaka Serikali yetu ikubali na kuipitisha sheria ya kuruhusu uraia wa nchi mbili (*dual citizenship*) inashughulikiwa kikamilifu na Wizara yangu. Wizara tayari imelifikisha suala la uraia pacha kwa Tume ya Jaji Warioba na tayari suala hili limewekwa kwenye Rasimu ya Katiba Mpya na tutajadili kwa nguvu za hoja na kwamba umefika wakati wa nchi yetu kuwa na sheria ya kuruhusu uraia pacha kwa maslahi na maendeleo ya Taifa letu. Ni matumaini yangu kuwa Bunge hili litaunga mkono pendekezo hilo.

## ULINZI NA UJENZI WA AMANI DUNIANI

***Mheshimiwa Spika,*** katika miaka ya hivi karibuni Jumuiya ya Kimataifa imeshuhudia Tanzania ikichukua majukumu kwa kushiriki moja kwa moja katika harakati za ukombozi na utatuzi wa migogoro Barani Afrika na duniani kote. Mpaka sasa, Tanzania imeendelea kushiriki katika utatuzi wa migogoro na ulinzi wa amani ambapo imekuwa ikichangia Vikosi vya kulinda amani katika nchi mbalimbali zinazokabiliwa na migogoro.

***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi 2014, Tanzania ilikuwa na jumla ya wanajeshi 2,259 kwenye maeneo manne (4) ya kulinda amani ya Umoja wa Mataifa. Maeneo hayo ni DRC (MONUSCO); Sudan (UNAMID); Lebanon (UNFIL); na Ivory Coast (UNOCI). Hii inaonesha jitihada za Tanzania za kuifanya dunia kuwa mahali salama pa kuishi.

***Mheshimiwa Spika,*** ushiriki wa Tanzania kwenye misheni za kulinda amani unazidi kuifanya nchi yetu iaminike na kuheshimiwa na Jumuiya ya Kimataifa. Hii imedhihirishwa na uteuzi wa Watanzania kwenye nafasi za juu kwenye misheni hizo ikiwemo "Force Intervention Brigade – FIB" chini ya MONUSCO nchini DRC na UNAMID ya Darfur, Sudan. Aidha, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa niaba ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ameiomba Serikali yetu ipeleke jeshi lake Sudani ya Kusini. Tumekubali.

***Mheshimiwa Spika,*** ushiriki wetu kwenye maeneo hayo umewawezesha wanajeshi wetu kuendelea kupata uzoefu. Pia, wanajeshi hao wanaendelea kuongeza maarifa na mbinu za kijeshi na kujifunza matumizi ya vifaa vya kisasa vya kijeshi. Ushiriki wetu pia huwa ni nafasi nzuri ya kuanzisha au kuimarisha mahusiano ya kijeshi na nchi nyingine zinazoshiriki kwenye maeneo hayo.

Watanzania tunayo kila sababu ya kujivunia jeshi letu ambalo ni dogo lakini kali kweli kweli. Mmeona wenyewe nguvu ya jeshi letu kwenye Maadhimisho ya miaka hamsini ya Muungano kwenye Uwanja wa Taifa.

**MAADHIMISHO YA MIAKA HAMSINI YA MUUNGANO**

***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 26 Aprili, 1964 Jamhuri ya Tanganyika iliungana na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Watanzania tunajivuna kwamba tarehe 26 Aprili, 2014 Muungano umetimiza miaka 50 tangu kuundwa kwake. Hatua tuliyoifikia ni ya kujivunia, kwani katika kipindi hicho zipo nchi nyingi zilizojaribu kuungana bila mafanikio.

***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka 50, Tanzania kupitia utekelezaji wa Sera yake madhubuti ya Mambo ya Nje tulikataa kufungamana na upande wowote; tukatetea haki za wanyonge; tukadai usawa; tukapambana dhidi ya ubaguzi wa rangi; tukapigania uhuru; na tukahimiza umoja na mshikamano wa Bara la Afrika. Msimamo wetu huu umetujengea heshima duniani na pengine tusingefanya hayo nje ya muungano.

***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa wito kwa Bunge lako Tukufu na na watanzania wote, tuendelee kuunganisha nguvu katika kutekeleza Sera yetu ya Mambo ya Nje ambayo inahimiza diplomasia ya uchumi. Tukumbuke kwamba nchi nyingi duniani sasa hivi zinaungana kwa malengo ya kukuza uchumi wao. Hivyo nasi tudumishe muungano wetu ili tuendelee kunufaika na kujenga uchumi wenye nguvu.

**UTAWALA NA MAENDELEO YA WATUMISHI WIZARANI NA BALOZINI**

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ina jumla ya Watumishi 401 ambao kati yao 152 wapo kwenye Balozi zetu, 234 wapo Makao Makuu na Watumishi 15 waliopo Idara ya Mambo ya Nje Zanzibar. Aidha, Watumishi wengine 12 wapo kwenye likizo bila malipo kwa kuwa wanafanya kazi katika mashirika mbalimbali ya Kimataifa.

***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwezesha kuwajengea uwezo na kukidhi vigezo vya muundo kwa Watumishi, Wizara imeandaa mpango wa mafunzo kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2013/2014 hadi 2015/2016. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wafadhili mbalimbali imeendelea

kugharamia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi ambapo Watumishi 13 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi na watumishi 14 wanahudhuria mafunzo ya muda mrefu katika mwaka huu wa fedha.

***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza uwakilishi wetu nje, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya uteuzi wa Mabalozi na Naibu Mabalozi kuiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali. Mabalozi walioteuliwa ni Mheshimiwa Naimi Switie Aziz (Addis Ababa), Mheshimiwa Anthony Ngereza Cheche (Kinshasa), Mheshimiwa Daniel Ole Njoolay (Abuja), Mheshimiwa Wilson Masilingi (The Hague), Mheshimiwa Chabaka Kilumanga (Moroni), Mheshimiwa Lt. Gen. Abdulrahaman Amiri Shimbo Rtd. (Beijing), Mheshimiwa Modest Mero (Geneva), Mheshimiwa Mbaruk Nasoro Mbaruk (Abu Dhabi), Mheshimiwa Liberata Rutageruka Mulamula (Washington D.C), Mheshimiwa Dkt. Azizi Ponaly Mlima (Kuala Lumpur), Mheshimiwa Dora Mmari Msechu (Stockholm), Mheshimiwa Lt. Gen. Wynjones Mathew Kisamba (Moscow) na Mheshimiwa Joseph Edward Sokoine (Idara ya Ulaya na Amerika). Aidha, Naibu Mabalozi ni; Bwana Mohamed Hija Mohamed (New Delhi), Bwana Juma Othman Juma (Muscat) na Bwana Omary Mjenga (Dubai).

***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara imewateua Wakurugenzi Wasaidizi 16 kuziba nafasi zilizokuwa wazi katika Idara za; Diaspora (2), Itifaki (2), Ushirikiano wa Kimataifa (1), Ushirikiano wa Kikanda (2), Asia na Australasia (2), Ulaya na Amerika (1), Mashariki ya Kati (1), Afrika (1) Nje Zanzibar (1) na Sera na Mipango (3).

## TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

### Chuo Cha Diplomasia

***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/2014, Chuo cha Diplomasia kimeendelea kufanya maboresho ili kukidhi masharti ya Baraza la Ithibati ya Elimu ya Ufundi (National Council for Technical Education – NACTE). Chuo kimezidi kutambulika na kuimarika katika utoaji taaluma, ushauri na kufanya tafiti katika masuala ya utatuzi wa migogoro, itifaki, diplomasia ya uchumi, stratejia na menejimenti ya mahusiano ya kidiplomasia. Aidha, Chuo kimeendelea kuishauri Wizara yangu katika masuala ya kidiplomasia na kutoa mafunzo maalum kwa watumishi wa Wizara, Mabalozi na wenza wao.

***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na kuongeza udahili kutoka wanafunzi 590 katika mwaka wa masomo wa 2012/2013 na kufikia wanafunzi 881 katika mwaka huu wa masomo 2013/2014. Chuo kipo katika hatua za mwisho za mchakato wa kutoa shahada na kufundisha lugha za kichina kwa watanzania na kiswahili kwa wageni kuanzia mwaka ujao wa masomo.

***Mheshimiwa Spika,*** katika kujiimarisha zaidi, Chuo kimejikita katika kutekeleza Mpango Mkakati wa Miaka Mitano 2012/2013 – 2016/2017 kwa kuboresha miundombinu kama ilivyoainishwa katika *Master Plan* ya Chuo, kuongeza ufanisi katika utoaji taaluma, kuajiri wataalam wenye sifa ili kufanya Chuo kiwe kituo bora cha kikanda kilichobobea katika taaluma, tafiti na utoaji ushauri wa kitaaluma katika fani za mahusiano ya kimataifa, diplomasia ya uchumi na stratejia. Mipango hii ina lengo la kukifanya Chuo kiwe na uwezo wa kujitegemea katika utekelezaji wa majukumu yake.

**Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC)**

***Mheshimiwa Spika***, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kimeendelea kutuwakilisha vyema katika diplomasia ya mikutano na kuvutia utalii nchini kwa njia ya mikutano. Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, Kituo kimeweza kukaribisha wastani wa mikutano 61 kwa mwaka. Kati ya mikutano hii, asilimia 30 ya mikutano ni ya kimataifa na asilimia 70 ni ya kitaifa. Idadi hiyo ya mikutano imeweza kuleta Arusha wageni wanaokadiriwa kufikia 17,680 kila mwaka. Kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2013, Kituo kiliweza kuwa wenyeji wa mikutano ya kimataifa 29 na ya kitaifa 33 iliyoingiza nchini wageni wanaokadiriwa kufikia 15,040.

***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa mara nyingine tena, Kituo kimeendelea kupata hati safi ya hesabu zake zilizoandaliwa na kukaguliwa kwa wakati kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2013. Katika kipindi hicho, kituo kilipata faida ghafi ya shilingi milioni mia moja tisini na moja, mia tatu thelathini na moja elfu na mia tatu themanini na tano (191,331,385.00) na kinaendelea kufanya shughuli zake kwa ufanisi na bila kuwa tegemezi kwa Serikali Kuu.

***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2014/2015, Kituo kimepanga kuingiza mapato ya shilingi bilioni kumi na tatu, mia nane themanini na tano milioni, mia saba na saba elfu, mia nane thelathini na mbili (13,885,707,832.00) kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato ikiwemo ya Kituo kipya cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), ambacho kilikabidhiwa kwa AICC Agosti, 2013 na AICC inategemea kukopa shilingi bilioni 5.4 kwa ajili ya miradi ya maendeleo na mali za kudumu zenye thamani ya shilingi bilioni tano, mia tisa sitini na tatu milioni, mia nne thelathini na sita elfu (5,963,436,000.00).

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu itaendelea kuhakikisha Kituo kinatimiza moja ya jukumu lake la kupangisha asasi za kimataifa. Taasisi mbili za Umoja wa Afrika (*AU Advisory Board on Corruption* na *African Institute of International Law)* zilizoanzishwa hivi karibuni, makao makuu yake ni katika kituo cha AICC. Kwa kuzingatia upatikanaji wa nafasi baada ya Mahakama ya Mauaji ya Kimbari ya

Rwanda (*UN-ICTR*) kupunguza shughuli zake na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (*EAC*) kurudisha baadhi ya ofisi zake na kuhamia kwenye jengo lao jipya, Kituo kitaendelea kupokea taasisi zingine za kitaifa na kimataifa zitakazopenda kuweka makao yake jijini Arusha.

***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha Mpango Mkakati wa Kituo unatekelezeka, Wizara yangu inaendelea kufuatilia ujenzi wa Kituo kipya cha mikutano mjini Arusha kitakachoitwa *Mount Kilimanjaro International Convention Centre (MK-ICC)*. Mradi huo ni moja ya miradi itakayofadhiliwa na Serikali ya Watu wa China kupitia benki yao ya Exim.

***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara yangu baada ya kupata kibali cha Hazina iliidhinisha Kituo kukopa ili kiweze kujenga majengo matatu ya kisasa (condominium) katika viwanja vyake vilivyoko Arusha kwa ajili ya kupangisha. Aidha, kituo kina mpango wa kujenga maduka ya kisasa (*shopping malls*) kwa ubia na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Serikali za Mitaa (LAPF) katika viwanja vyake vilivyoko Kaloleni, Arusha na kina mpango wa kupanua Hospitali yake iliyoko Arusha, kwa mkopo toka taasisi za fedha.

**Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika (APRM- Tanzania)**

***Mheshimiwa Spika,*** kulingana na Mpangokazi wa APRM kwa mwaka wa fedha 2013/2014 baadhi ya shughuli zilizotekelezwa:

- Kufanya uchambuzi wa masuala yaliyojitokeza katika Ripoti ya APRM na kuoanisha masuala hayo na Mipango ya Maendeleo ya Taifa ambayo ni pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16), MKUKUTA II, MKUZA II na mipango mingine;

- Kutafsiri Ripoti ya Nchi ya Utawala Bora katika lugha ya Kiswahili kwa lengo la kuifanya Ripoti hiyo ieleweke kwa watu wengi zaidi ukizingitia kuwa lugha ya Kiingereza ambayo Ripoti hii imeandikwa inafahamika na Watanzania wachache;

- Kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa APRM Tanzania toka mwaka 2007 (ulipoanza) hadi Aprili 2014 kwenye kikao cha Makatibu Wakuu kwa lengo la kuwafahamisha hatua zilizofikiwa. Pia kuwaomba Makatibu Wakuu waingize changamoto zilizobainishwa katika Ripoti ya Nchi ya Utawala Bora kwenye Mipango yao ya Wizara ya Muda Mfupi na wa Kati. Hatua hii ni mwanzo wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kuondoa Changamoto za

Utawala Bora zilizobainishwa na Ripoti ya APRM na kuzitolea Taarifa itakayowasilishwa kwenye vikao vya AU kila mwaka;

- Kutayarisha mfumo wa tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kuondoa Mapungufu yaliyojitokeza ya Utawala Bora;

- Kutayarisha makala zitakazotumika wakati wa uwasilishaji wa matokeo ya Ripoti ya Nchi ya Tathmini ya Utawala Bora kwa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Makatibu Wakuu Tanzania Bara na Zanzibar, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Baraza la Wawakilishi Zanzibar, taasisi za kiraia na sekta binafsi.

***Mheshimiwa Spika***, mipango ya baadae ya APRM ni kufanya uzinduzi wa Ripoti ya Nchi ya Utawala Bora ambao utafanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kuendelea kuwafahamisha wananchi kuhusu matokeo ya Ripoti ya Nchi ya Utawala Bora (CRR); kufuatilia utekelezaji wa Mpango kazi wa Taifa wa kuondoa changamoto za utawala bora zilizobainishwa na kutayarisha Ripoti za utekelezaji za kila mwaka; na kuendelea kushirikiana na taasisi zinazoshughulikia masuala mbalimbali ya Utawala Bora ambazo APRM Tanzania imeanzisha ushirikiano kama vile CHRAGG na PDB kwa lengo la kubadilishana uzoefu kwa manufaa ya nchi yetu.

**MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014**

***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara yangu iliidhinishiwa kutumia kiasi cha Shilingi bilioni mia moja na thelathini na nane, mia tatu hamsini na tisa milioni, mia tisa arobaini na nne elfu na mia mbili ishirini na moja **(138,359,944,221.00)**. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni mia moja na kumi, mia tatu hamsini na tisa milioni, mia tisa arobaini na nne elfu na mia mbili ishirini na moja **(110,359,944,221.00)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni ishirini na nane (**28,000,000,000.00**) ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Katika fedha zilizotengwa kwa Matumizi ya Kawaida (Recurrent Budget), Shilingi bilioni mia moja na nne, mia tisa na sita milioni, mia mbili themanini na nne elfu na mia saba kumi na tisa **(104,906,284,719.00)** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi bilioni tano, mia nne hamsini na tatu milioni, mia sita hamsini na tisa elfu na mia tano na mbili **(5,453,659,502.00)** ni kwa ajili ya Mishahara.

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Balozi zake ilitarajia kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni kumi na sita, milioni mia tisa sitini na sita, mia saba ishirini na tisa elfu na mia tatu (**16,966,729,300.00**) kama maduhuli ya Serikali. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2014, Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 12,909,470,376.00**

ikiwa ni makusanyo ya maduhuli Balozini. Kiasi hicho cha makusanyo ya maduhuli ni sawa na **asilimia 76** ya makisio ya makusanyo yote ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia **tarehe 31 Machi 2014, Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha Shili**ngi bilioni mia moja kumi na saba, milioni mia tatu ishirini na saba na mia tisa sitini na mbili **(117,327,353,962.00)**. Kati ya kiasi hicho, Shilingi bilioni mia moja na sita, milioni mia nne tisini na mbili, mia nane arobaini na nane na arobaini na mbili **(106,492,848,042.00)** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, Shilingi bilioni nne, milioni mia tatu sitini na nane, mia saba na tano elfu na mia tisa ishirini **(4,368,705,920.00)** ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi bilioni sita, mia nne sitini na tano milioni na mia nane elfu **(6,465,800,000.00)** ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

**CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KATIKA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014**

***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara yangu imekabiliwa na changamoto mbalimbali za kiutawala na kibajeti katika utekelezaji wa majukumu yake. Baadhi ya changamoto hizo ni upungufu wa Watumishi Makao Makuu ya Wizara na Balozini; upungufu wa vitendea kazi; uchakavu wa majengo ya ofisi na makazi Balozini; na uchakavu wa magari ya uwakilishi na huduma Balozini.

***Mheshimiwa Spika,*** Katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuomba kibali Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma cha kuajiri Watumishi wapya. Vilevile, Wizara imeendelea kununua vitendea kazi vya Watumishi kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, Wizara itaendelea kutumia fedha za bajeti ya Maendeleo zinazopangwa katika bajeti kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kuzingatia vipaumbele na kuishirikisha mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika kuingia ubia wa kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopo Balozini. Halikadhalika, Wizara imepanga kutumia utaratibu wa *higher purchase* katika kufanikisha ununuzi wa magari Balozini. Utaratibu huu ni mzuri kwa kuwa utapunguza gharama za ununuzi wa magari hayo.

**MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, pamoja na mambo mengine, Wizara yangu imepanga kutekeleza malengo makuu muhimu kulingana na majukumu yake kama ifuatavyo:-

i. Kuitangaza nchi yetu kama moja ya nchi duniani yenye mazingira mazuri kwa ajili ya uwekezaji;

ii. Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa kwa nchi yetu na nchi mbalimbali wahisani na mashirika ya kikanda na ya kimataifa katika kusaidia utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo;

iii. Kuendelea kuratibu Wizara, Idara na Taasisi nyingine za Serikali kikanda na kimataifa kwa lengo la kuvutia wawekezaji na watalii; kutafuta nafasi za masomo, ajira na nafasi za kubadilishana uzoefu; na kutafuta masoko;

iv. Kusimamia, kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa mikataba mbalimbali iliyosainiwa kati ya nchi yetu na nchi nyingine na ile ya mashirika ya kikanda na kimataifa;

v. Kuendelea kufuatilia kwa karibu mageuzi kwenye taasisi za Umoja wa Mataifa kama vile Baraza la Kiuchumi na Kijamii (ECOSOC); Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA); kuanzishwa kwa Malengo Endelevu ya Maendeleo – Sustainable Development Goals – SDGs na agenda ya maendeleo baada ya kumalizika kwa kipindi cha Malengo ya Milenia 2015. Tutaendelea kufuatilia kwa karibu masuala yote yanayogusa maslahi yetu;

vi. Kuendelea kusimamia na kupigania maslahi ya nchi maskini kwenye mikutano yote mikubwa na hasa ile ya Umoja wa Mataifa na taasisi zake. Vilevile, tutaendelea kufanya mazungumzo na nchi tajiri duniani ili kuhakikisha zinatekeleza ahadi mbalimbali zilizozitoa ili kuharakisha maendeleo ya nchi maskini;

vii. Kuongeza uwakilishi wetu nje kwa kufungua Balozi mpya na Balozi ndogo na kuongeza umiliki wa nyumba za makazi na ofisi za Ubalozi katika Balozi zetu nje kwa kadri hali ya fedha itakavyoruhusu;

viii. Kutekeleza maelekezo ya Viongozi wa kitaifa pamoja na kuzingatia ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

ix. Kujenga mahusiano ya kirafiki na ushirikiano wa kiuchumi kati ya vyombo vya Kikanda na Kimataifa, unaozingatia maslahi muhimu ya Taifa letu;

x. Kuendelea kusimamia na kuzihimiza Balozi zetu nje kutafuta wawekezaji, fursa za ajira, nafasi za masomo na masoko kwa bidhaa zetu;

xi. Kuendelea kuitambua Jumuiya ya Watanzania wanaoishi ughaibuni na kuweka utaratibu utakaowawezesha kuchangia maendeleo ya Taifa lao; na

xii. Kuendeleza Ujirani Mwema.

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

***Mheshimiwa Spika,*** ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu yaliyotajwa hapo juu, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara yangu imepangiwa bajeti ya kiasi cha Shilingi bilioni mia moja tisini na moja, mia tisa kumi na tisa milioni na mia saba arobaini na nane elfu **(191,919,748,000.00)**. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni mia moja sitini na moja, mia tisa kumi na tisa milioni na mia saba arobaini na nane elfu **(161,919,748,000.00)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni thelathini (**30,000,000,000.00**) ni kwa ajili ya bajeti ya Maendeleo. Aidha, katika bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara, Shilingi bilioni mia moja hamsini na sita, mia moja hamsini na nane milioni na sabini na nane elfu **(156,158,078,000.00)** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi bilioni tano, mia saba sitini na moja milioni na mia sita sabini elfu **(5,761,670,000.00)** ni kwa ajili ya Mishahara.

***Mheshimiwa Spika,*** katika bajeti ya Matumizi Mengineyo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Shilingi bilioni moja, mia saba sitini na nne milioni **(1,764,000,000.00)** ni kwa ajili ya Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Tanzania (APRM), Shilingi bilioni moja, mia tano na nne milioni, mia tano sabini na nne elfu, mia nne sabini na nane **(1,504,574,478.00)** ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na Shilingi bilioni nne, tisini na nne milioni na mia tisa na mbili elfu **(4,094,902,000.00)** ni kwa ajili ya fedha za Mishahara na Matumizi Mengineyo ya Chuo cha Diplomasia.

***Mheshimiwa Spika,*** katika fedha za bajeti ya maendeleo za kiasi cha Shillingi bilioni thelathini (**30,000,000,000.00**) zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015, kiasi cha Shilingi bilioni kumi na nne, mia moja sitini na saba milioni, mia tano na nne elfu **(14,167,504,000.00)** ni kwa ajili ya kukamilisha ununuzi wa jengo la ofisi na makazi ya balozi jijini Paris, kiasi cha Shilingi bilioni saba, mia nne ishirini na tano milioni (**7,425,000,000.00)** ni kwa ajili ya ujenzi wa makazi ya Balozi *Mount Vernon*-New York, kiasi cha Shilingi bilioni moja, mia tatu na tisa milioni, mia sita sitini na saba elfu na tisini na sita **(1,309,667,096.00)** ni kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Serikali yaliyopo jijini Khartoum, Sudan, kiasi cha Shilingi bilioni nne, mia tisa hamsini milioni (**4,950,000,000.00)** ni kwa ajili ya

ukarabati wa Ofisi ya Ubalozi jijini New York, kiasi cha shilingi milioni mia moja arobaini na mbili, mia mbili ishirini na saba elfu (**142,227,000.00)** ni kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya Balozi jijini Geneva na kiasi cha shilingi bilioni mbili na milioni tano, mia sita na mbili elfu (**2,005,602,000.00)** ni kwa ajili ya ukarabati wa jengo la Makao Makuu ya Wizara.

***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Wizara yangu kupitia Balozi zake, inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni kumi na nane, mia tano sitini na nane milioni, ishirini na mbili elfu, mia nne sabini na nane (**18,568,022,478.00**) kama maduhuli ya Serikali. Kwa maana ya utekelezaji wa Bajeti, kiasi hiki cha maduhuli tayari kimejumuishwa kama sehemu ya bajeti ya Matumizi Mengineyo ya Wizara.

**HITIMISHO**

***Mheshimiwa Spika,*** ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu yaliyotajwa hapo juu, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi bilioni mia moja tisini na moja, mia tisa kumi na tisa milioni na mia saba arobaini na nane elfu **(191,919,748,000.00).** Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni mia moja sitini na moja, mia tisa kumi na tisa milioni na mia saba arobaini na nane elfu **(161,919,748,000.00)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni thelathini (**30,000,000,000.00**) ni kwa ajili ya bajeti ya Maendeleo.

***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa kutoa hoja na hoja imeugnwa mkono. Ahsante sana kwa kusoma Hotuba yako vizuri na kwa wakati.

Ninaomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje; badala yake anakuja Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, kusoma maoni ya Kamati kuhusu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

**Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kama ilivyosomwa Bungeni**

**MHE. BETTY E. MACHANGU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na 117 (11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara

ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, kwa niaba ya Kamati yangu, tunapebda kutoa salamu za pole kwa Wananchi wa Jamhuri ya Malawi, kwa kifo cha mpendwa wao, aliyekuwa Balozi wa nchi hiyo nchini Tanzania, Marehemu Balozi Flossie Gomile Chidyaonga, aliyefariki tarehe 9 Mei, 2014. Bara la Afrika limempoteza mmoja kati ya Wanadiplomasia aliyepigania amani na umoja wakati wote. Mwenyeizi Mungu, alilaze roho yake mahali pema peponi; amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri utakaotolewa na Kamati hii unatokana na kazi ya Bunge kupitia Kamati zake na kushauri na kusimamia Serikali kama ilivyo katika Ibara ya 63 (iii) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifuatlia kazi mbalimbali za Wizara katika nyakati tofauti kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014 na kukagua Miradi ya Wizara ili kuweza kuwa na usimamizi na ushauri mzuri kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni na lengo la maoni ushauri huu pamoja na mambo mengine ni kuisaidia Serikali katika kukamilisha kwa ufanisi, dira, dhamira na kaulimbiu ya Wizara hii, ambazo zinalenga kuimarisha Diplomasia ya Kiuchumi, kupitia uhusiano na ushirikiano wa Kimataifa ili kuleta maisha bora kwa Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwenendo wa Ushirikiano wa Kimataifa wa nchi ili iweze kukubalika na kuthaminiwa na nchi nyingine Duniani, ni lazima ijipange vyema na kila mara kujitathmini kama inavyo vigezo vya aina hiyo katika nyanja mbalimbali hususan za kushirikiana kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika dhana hiyo, kamati yangu ilitumia ujuzi na uzoefu wake kuishauri Wizara hii, ili hadhi na heshima ya Tanzania mbele ya Jumuiya ya Kimataifa izidi kupanda na kukubalika, kwani kuna dalili zinazoonesha kuwa, baadhi ya nchi hazifurahii hata kidogo kuiona nchi yetu inazidi kubalika Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara iliidhinishiwa Shilingi 138,356,944,221, ambapo kati ya

fedha hizo, Shilingi 110,359,944,22 ni kwa ajli ya Matumizi ya Kawadia na Shilingi 28,000,000,000 ni kwa ajli ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, Wizara kupitia Balozi zake, ilitarajia kukusanya maduhuli ya Shilingi 16,969,729,300.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014, Wizara hii ilikuwa imepatiwa Shilingi 117,327,353,962; kati ya fedha hizo, Shilingi 106.492,848,042 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi 4,368,705,920 ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi 6,465,800,000 ni kwa ajili ya fedha za Miradi ya Maendeleo. Aidha, Wizara imefanikwia kukusanya Shilingi 12,909,470,376 ikiwa ni makusanyo ya maduluhi Balozini, ambayo ni asilimia 76 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na fedha hizo na matumizi ya kawaida, Wizara imeweza kutekeleza kazi zifutazo: Kubuni na kusimamia uekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ya Nchi. Kamati ilielezwa kuwa jukumu hili limekuwa likitekelezwa kwa kushirikiana na Balozi za Tanzania, Wizara mbalimbali za Serikali, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali pamoja na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Niabu Spika, kwa kipindi cha 2013/2014, Wizara iliendelea kuvuvutia uwekezaji katika sekta mbalimbali nchini, zikiwemo kilimo, afya, viwanda, utalii na nishati na kutafuta masoko ya nje kwa bidhaa zinazozalishwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inachukua nafasi hii, kuipogeza Serikali kupitia Wizara hii, kwa kupokea tuzo maalum ya *CEO Round Table,* kwa nchi yetu kufungua fursa kwa sekta binafsi. Kamati vilevile inapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutunukiwa Shahada ya Heshima ya Uzamivu *(Ph.D.)* ya Sheria ya Julai, 2013 katika Chuo Kikuu cha Guelph cha nchini Canada, kutokana na mchango wake mkubwa kwenye sekta ya kilimo hususan katika masuala yanahohusu usalama wa chakula na majaribio makuwba ya kuongeza matumizi ya teknolojia katika kilimo cha Tanzania, kwa lengo la kuwaongezea kipato Wananchi na kukuza uchumi wa nchi.

Mhehimiwa Naibu Spika, Kamati vilevile inampongeza kwa dhati, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutunukiwa tuzo ya Kiongozi Bora wa Bara la Afrika, mwenye mchango mkubwa zaidi wa kuleta maendeleo kwa mwaka 2013, iliyopokelewa kwa niaba yake na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mshimiwa Bernard Membe, mwezi Aprili, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika kutekeleza jukumu la kusimamia Mikataba baina ya Tanzania na nchi nyingine na Taasisi

mbalimbali za Kimataifa, Wizara iliratibu na kusimamia uwekaji sahihi kwa mikataba kati ya Tanzania na nchi nyingine *(Bilateral Agreements)* ipatayo 13 katika kipindi hiki hadi tarehe 31 Machi, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya Mikataba hiyo 13, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara hii, kuchukua hatua za haraka katika utekelezaji wa Mikataba miwili muhimu, ambayo ni:-

Wa kwanza ni Mkataba kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzana na ya Thailand kuhusu ushirikiano katika utunzaji wa Wanyamapori ya Julai, 2013. Kamati inatoa msisitizo na utekelezaji wa Mkataba huu, kutokana na umuhimu wa sekta hii katika mchango wa Pato la Taifa ambapo taarifa zinaonesha kuwa, sekta hii imekumbwa na dhoruba ya uwindaji haramu wa wanyama aina ya tembo. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara inayohusika, kuchukua hatua madhubuti, ili kuwapa matumaini wale wanaokusudia kushirikiana nasi katika kuiimarisha sekta hii.

Mkataba wa pili ni Hati ya Makubaliano kati ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ya Tanzania na Taasisi ya *Clinton Foundation* kuhusu ushirikiano katika masuala ya Kilimo ya mwezi Agosti, 2013. Mkataba huu ni muhimu kwa maendeleo ya Wananchi wa Tanzania. Kwa kutambua kuwa Sekta ya Kilimo inachangia kwa kiasi kikubwa, pato la Watanzania walio wengi, hivyo, Serikali ione umuhimu katika utekelezaji wake pamoja na mikataba mingine ya kimataifa ya aina hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uratibu, ushirikiano wa Kimataifa, Kikanda na Bara la Afrika, Wizara iliratibu na kutekeleza mambo mbalimbali ambayo yamechangia kuleta miundombinu na njia ya kuimarisha diplomasia ya kiuchumi, ikiwa ni pamoja na ustawi wa Wananchi kwa ujumla wake. Mambo hayo ni pamoja na Mkutano wa Baraza la Uchumi na Jamii la Umoja wa Mataifa *(EOCOC)* Julai, 2013; Mkutano wa 68 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa *(UNGA);* Mkutano wa 37 wa *UNESCO;* Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Madola *(CHOGM);* Mkutano wa Jukwaa la Uhumi la Dunia *(WEF);* Mkutano wa Kimataifa kuhusu biashara haramu ya wanyamapori; Mikutano ya kikundi kazi kuhusu mapendekezo ya Ajenda za Malengo mapya ya Maendeo endelevu baada lya mwaka 2015; na mikutano wa Kikundi kazi cha Mawaziri wa Jumuiya ya Madola *(CMAG).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ushirikiano wa kikanda, Wizara iliweza kuratibu na kushiriki mamboyafuatayo: Mikutano na Chaguzi mbalimbali katika nchi za *SADC;* Mikutano ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki; Mikutano ya Nchi za Maziwa Makuu *(CGLR);* Kuratibu mambo yanayohusu Jumuiya ya Nchi za

Mwambao wa Bahari ya Hindi *(IORA);* na Kuratibu shughuli mbalimbali zinazohusu ushirikiano wa Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa, Wizara ikishirikiana na Balozi zake, imeendelea kulinda masilahi ya Taifa na Watanzania wote kwa ujumla, katika nyanja za kiuchumi na nyinginezo nje ya nchi kwa kuratibu na kushirki, kwenye mikutano mbalimbali, kama vile Mkutano wa Mabadiliko ya tabianchi uliofanyika Warsaw Poland, Novemba, 2013 na mengineyo.

Kusimamia masuala yanayohusu kinga na haki za Mabalozi waliopo nchini kulingana na Mkataba wa Vienna wa mwaka 1961 na 1963. Kamati ilielezwa kuwa Wizara inashirikiana na Mamlaka mbalimbali nchinil ili kuhakisha kuwa jamii za Kibalozi zinazowakilisha nchi zao hapa nchini, zinapata haki zao kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Kimataifa hususan Mkataba wa Vienna kuhusu Mahusiano ya Kidiplomasia wa Mwaka 1961 (*Vienna Convention on Diplomatic Relations of 1961.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kusimaia na kuratibu masuala ya itifaki *(Protocal)* na uwakilishi *(Credentials)*. Kamati ilielezwa kuwa Wizara ilisimamia kazi ya Itifaki za Kitaifa hususan katika mapokezi na ziara mbalimbali za Viongozi wa Kitaifa wanaotembea nchi yetu. Kati ya ziara zilizoratibiwa na Wizara hii, ni ziara ya Rais wa Marekani, Barrack Obama ya Julai, 2013 na Rais wa China, Mheshimiwa Xi Jiping, tarehe 25 Machi, 2013. Kamati inachukua fursa hii kuipongeza Serikali kupitia Wizara hii, kwa kuratibu vyema ziara za Viongozi hao na kuliletea Taifa letu heshima kubwa mbele ya Jumuiya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliarifiwa kuwa, Wizara kwa kupitia Balozi zake, zimeendelea kutoa *visa* kwa raia wa nje wanaotembelea Tanzania, kushirikiana na mamlaka nyingine kutafuta ufumbuzi wa matatizo mbalimbali yanayowakabili Watanzania waishio nje ya nchi. Vilevile Wizara hii insaidia kuratibu upatikanaji wa vibali vya kutumia ukumbi wa watu mashuhuri *(VIP Lounge)* wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa, katika kuratibu shughuli za Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano, Wizara imeendelea kufanya vikao vya wadau wa ndani ya nchi ili kutekeleza shughuli hiyo. Katika utekelezaji wa jambo hii, Wizara iliandaa mkutano wa pamoja kati ya India na Tanzania wa Julai, 2013 hapa nchini, ambapo maazimio yaliyofikiwa yanalenga katika kuweka maeneo ya ushirikiano wa Tanzania na India, kwa kipindi cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilielezwa kuwa Wizara inaendelea na kushughulikia mambo yote ya utumishi yanayohusiana na ajira, mafunzo, upelekaji na upangaji wa Mabalozi nchi za nje, pamoja kusimamia shughuli zote za uendeshaji katika Wizara hii na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa Wizara inaendelea na juhudi za kuratibu juhudi ya kuandaa mazingira wezeshi kwa lengo la kuwatumia Watanzania waishio ughaibuni, kuwekeza na kuwavutia wawekezaji nchini. Kamati inaishauri Serikali kubuni njia bora zaidi zitakazowapa motisha Watanzania walioko nje kuwekeza hapa nyumbani, kwani inaonekana mwamko wa Watanzania walioko ughaibuni kufanya hivyo bado ni mdogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza ushauri huu, Kamati inapendekeza Serikaki kwenda kujifunza na kubadilishana uzoefu na nchi ya Ethiopia, ambayo imepiga hatua kubwa katika masuala ya Diaspora; ambayo inasemekana raia wake walioko nje wanachangia karibu Dola za Kimarekani bilioni tatu kwa mwaka na kuiwezesha nchi hiyo kuwekeza katika Mradi mkubwa wa kujenga bwawa la kuzalisha umeme kutoka Mto Nile.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi hizo, Kamati ilipokea na kujadili Bajeti ya Mwaka 2013/2014 na ilitoa ushauri na maoni 15, ili yaende sambamba na utekelezaji wa kazi za Wizara kwa mwaka 2013/2014. Kamati inaipongeza Wizara, kwa juhudi kubwa inayofanya ya kutekeleza maoni na ushauri wake kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 pamoja na changamoto ilizozipata kutokana na ufinyu wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ndiyo kioo cha Watanzania nje ya nchi; hivyo, ni vyema Serikali ihakikishe inaitengea Bajeti ya kutosha ili kukabiliana na changamoto ya Wizara zikiwemo zinazowakabili Watanzania wanaoishi nje ya nchi. Wizara hii kama haitapewa fedha za kutosha kwa wakati, itaathiri shughuli zetu za mambo ya nje na ushirikiano wetu wa Kimataifa, pamoja na heshima iliyokwisha kujengeka kwa nchi yetu kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2013, Wizara ilikuwa imepatiwa Shilingi 6,465,800,000; kati ya Shilingi 28,000,000,000, ambapo ni asilimia 23 tu kwa ajili ya Miradi miwili ya Maendeleo iliyopo Paris Ufaransa na Maputo Msumbiji. Lengo la Miradi hii ni ukarabati wa jengo la ghorofa tisa kule Maputo Msumbiji na ununuzi wa Jengo la Ubalozi kule Paris Ufaransa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilitembelea na kukagua Miradi hiyo katika mwezi wa Februari, 2014 na kubaini changamoto mbalimbali zilizojitokeza kutokana na fedha hizo kutopatikana kwa wakati. Kati ya changamoto zilizojitokeza ambazo zitaigharimu nchi yetu ni ile ya Mkandarasi na Msimamizi wa Ujenzi kutoa tozo, yaani *penaties,* kutokana na ucheleweshaji wa malipo. Mradi wa ukarabati wa ghorofa tisa kule Maputo Msumbiji, unadaiwa tozo ya Dola za Kimarekani 26,583 hadi kufikia Machi, 2013. Kamati imebaini kuwa, Serikali inapoteza Dola za Kimarekani 1,000,000 kila mwaka kutokana na kutokamilika kwa Mradi wa Ukarabati wa Jengo hili la Maputo Msumbiji, fedha ambazo zingepatikana kwa kulikodisha. Fedha hizi ni nyingi sana na zingeliweza kugharimia uendeshaji wa Ofisi zote za Kibalozi ziizoko katika nchi za *SADC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaishauri Serikali kufanya kila liwezekanalo, kukamilisha utoaji wa fedha za Miradi hii kabla ya kumalizika Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mradi wa ununuzi wa jengo lililopo Paris Ufaransa, Tanzania inaweza kupoteza fursa ya kupata jengo hilo ambalo lipo sehemu nzuri kama fedha hizo hazitatolewa na Serikali kabla ya kumalizika mwaka huu wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya shilingi bilioni 40.5 zilizopangwa kutolewa kwa ununuzi wa jengo hili ni shilingi bilioni 10.6 tu ndiyo zilikuwa zimetolewa wakati Kamati yangu ilipokuwa ikikagua mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa inatoa fedha za miradi hii kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili kuepuka changamoto zinazotokana na mikataba ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi za Ubalozi na Diplomasia ya kiuchumi, fedha za kuendesha ofisi za Kibalozi: Kamati ilieleza kuwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014 zipo ofisi 34 za Kibalozi katika dunia nzima ambazo hadi mwezi Machi, 2014 zilikuwa zimepatiwa shilingi bilioni 39.3 kati ya fedha zote shilingi bilioni 74.3 zilizoidhinishwa na Bunge mwaka wa fedha 2013/2014 kwa ajili ya matumizi mengineyo ya uendeshaji wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa ofisi hizo za Ubalozi kwa mwaka ujao wa fedha zinaombewa shilingi bilioni 78,278,523,900/= kwa ajili ya mishahara na matumizi ya kawaida ya uendeshaji wa ofisi hizo. Kiasi hiki ni kutokana na ufinyu wa bajeti ambao umesababisha Wizara hii kupewa mgawo

mdogo sana wa shilingi bilioni 75.2 kwa matumizi ya gharama za uendeshaji, lakini mahitaji halisi ni shilingi bilioni 92.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Serikali kuzingatia upya makisio ya fedha zilizopangwa kutolewa kwa Ofisi za Kibalozi katika kukidhi mahitaji ya kuendesha uhusiano na ushirikiano wa kimataifa katika nchi wanazotuwakilisha duniani kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo ya Ofisi za Kibalozi: Kamati yangu ilijadili na kuchambua kwa kina suala zima la umuhimu wa ofisi za kibalozi katika uwakilishi wa diplomasia ya kiuchumi. Jambo la kusikitisha ni kwamba majengo ya ofisi hizo na vifaa vingine vya kuendesha kazi kama vile magari kwa ujumla viko katika hali duni. Aidha, hata watendaji wa ofisi hizo nao wamejikuta mara nyingi katika hali isiyoridhisha kwa kile kinachoelezwa ufinyu wa bajeti kwa miaka mingi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa zipo dalili za kutia moyo wa kupatikana suluhisho la tatizo hili sugu kwa ujenzi wa ofisi hizo kwa njia ya *mortgage financing* katika nchi ziliko Balozi hizo kama maoni na ushauri wa Kamati yangu ulivyotolewa wakati wa kupokea na kujadili bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2013/2014 mwezi Mei, 2013.

Kamati yangu imefarijika sana kuona ushauri wake huu umetekelezwa na kuanza kuzaa matunda kwa kiwango hiki. Kamati yangu inaendelea kuishauri Serikali kulipa kipaumbele jambo hili ili juhudi hizi zisije zikafia njiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikiano wa Kimataifa wa Diplomasia ya Kiuchumi. Bila ya uhusiano na ushirikiano wa Kimataifa madhubuti na imara nchi yetu itajifunga yenyewe nai naweza kutengwa katika kujenga na kuimarisha Diplomasia ya Kiuchumi. Kamati ilielezwa kuwa uhusiano na ushirikiano wa nchi yetu nan chi nyingine duniani kwa mwaka 20123/2014 katika mambo ya kiuchumi kwa ujumla wake ni mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizopangwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015: Baada ya Kamati kupokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2013/2014 pamoja na fedha zilizotengwa na kutolewa hadi Machi, 2014 Wizara iliwasilisha kazi ambazo inakusudia kutelekeza kwa kipindi cha mwaka 2014/2015 kama ifuatavyo:-

Kazi ya kwanza ni kutangaza nchi yetu kama moja ya nchi duniani yenye mazingira mazuri kwa ajili ya uwekezaji kutokana historia yake ya miaka mingi ya amani, umoja, utulivu na mshikamano wa kitaifa.

Kazi ya pili ni kuendela kufuatilia utekelezaji wa ahadi mbalimbali zilizotolewa kwa nchi yetu na nchi mbalimbali wahisani na mashirika ya kikanda na ya kimataifa katika kusaidia utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo.

Kazi ya tatu ni kuendelea kuratibu Wizara, Idara na taasisi nyingine za Serikali katika masuala yote ya kikanda na yale ya kimataifa kwa lengo la kuvutia wawekezaji na watalii, kutafuta nafasi za masomo, ajira na nafasi za kubadilisha uzoefu na kutafuta masoko.

Kazi ya nne ni kusimamia, kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa mikataba mbalimbali iliyosainiwa kati ya nchi yetu na nyingine na ile ya mashirika ya kikanda na kimataifa.

Kazi ya tano ni kuendelea kufuatilia kwa karibu mageuzi kwenye Taasisi za Umoja wa Mataifa kama vile Baraza la Kiuchumi la Kijamii, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, kuanzishwa kwa malengo endelevu ya maendeleo yaani *Sustainable Development Goals* na *agenda* ya maendeleo badaa ya kumalizika kwa kipindi cha Malengo ya Milenia 2015.

Kazi ya sita ni kuendelea kusimama na kupigania maslahi ya nchi maskini kwenye mikutano yote mikubwa na hasa ile ya Umoja wa Mataifa na taasisi zake. Vilevile itaendelea kufanya mazungumzo na nchi tajiri duniani ili kuharakisha maendeleo ya nchi maskini.

Kazi ya saba ni kuongeza uwakilishi wetu nje kwa kufungua Balozi mpya na Balozi ndogo na kuongeza umiliki wa nyumba za makazi na ofisi za Ubalozi katika Balozi zetu nje kwa kadri ya hali ya fedha itakavyoruhusu.

Kazi ya nane ni kujenga mahusiano ya kirafiki na ushirikiano wa kiuchumi kati ya vyombo mbalimbali vya kikanda na kimataifa unaozingatia maslahi muhimu ya taifa letu.

Kazi ya tisa ni kuendelea kusimamia na kuhimiza Balozi zetu nje kutafuta wawekezaji, fursa za ajira, nafasi za masomo na masoko kwa bidhaa zetu.

Kazi ya kumi ni kukamilisha mchakato wa kuitambua Jumuiya ya Watanzania wanaoishi Ughaibuni na kuweka utaratibu utakaowezesha kuchangia maendeleo ya Taifa lao.

Kazi ya kumi na moja na ya mwisho ni kuendeleza ujirani mwema na nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati katika utekelezaji wa kazi za Wizara zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015: Baada ya Kamati kupokea na kujadili taarifa ya mipango ya Wizara kwa kazi ilizopanga kutekelezwa kwa mwaka 2014/2015 ilitoa maoni na ushauri ili uendane na utekelezaji huo kama ifuatavyo:-

Ushauri wa kwanza ni Wizara ione umuhimu wa kununua vitendeakazi vipya kama vile magari katika ofisi za Balozi zetu ambavyo vinakwenda na wakati na kwa kuanzia zigawiwe zile Balozi ambazo hali zao ni mbaya sana kiasi cha kuitia aibu nchi yetu.

Ushauri wa pili; Serikali ione umuhimu wa kuiwezesha Wizara hii kutekeleza mipango yake ya *Mortgage Financing* pamoja na kutumia mifuko ya hifadhi ya jamii itakayowezesha Balozi zetu kujengewa ofisi zake na nyumba za wafanyakazi katika zile nchi ambazo zinaonyesha nia ya kukubaliana na mipango hii.

Ushauri wa tatu; Serikali itafute fedha hata kama ni za mkopo ili kujenga ofisi na nyumba za watumishi katika viwanja vyake vilivyopewa katika nchi mbalimbali kama vile Msumbiji, Uingereza na kwingineko.

Nne; Serikali iangalie namna bora ya kumiliki eneo linalokusudia kulichukua katika Wilaya ya Bagamoyo kwa ajili ya kujenga Chuo cha Diplomasia ili iweze kutumika kiuchumi na kuepusha migongano ya jamii inayoweza kuzuka.

Tano; Wizara itafute utaratibu ambao utawezesha kutoa elimu kuhusu dhana na madhumuni ya *African Peer Review Mechanism* kwa wananchi na wadau wengine na taswira ya taasisi hiyo na faida zake kwa taifa.

Sita; Kutokana na umuhimu wa mpango huu wa *APRM,* Kamati inaishauri Serikali kuipatia fungu lake la matumizi yaani *Vote* badala ya fedha hizo kupitia katika fungu la 34 la Wizara.

Saba; Serikali ihakikishe inatoa fedha zote zinazobakia za mradi wa ukarabati wa ujenzi wa jengo la ofisi ya Msumbiji na ununuzi wa jengo la Ubalozi wa Ufaransa zilizotengwa katika fungu 34, mradi namba 6391 kabla ya kumalizika mwaka wa fedha 2013/2014 ili kukamilisha mambo yaliyobakia kama ilivyopangwa.

Nane; Kamati inaendelea kusisitiza ofisi zote za Ubalozi duniani zipewe mafungu yao yaani *Votes* na fedha zao ziende moja kwa moja kwenye mafungu hayo badala ya kupitia fungu 34 la Wizara.

Tisa; Ili kuondoa dhana kuwa Wizara hii inatengewa na kupatiwa fedha nyingi, Serikali iweke utaratibu wa malipo ya itifaki *(protocol)* ya viongozi wa kitaifa fungu la Wizara ya Fedha na kuwalipia moja kwa moja badala ya kuziweka fedha hizo katika fungu la 34.

Kumi; Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, iweke utaratibu wa uhakika wa kukusanya mapato katika Balozi za Heshima *(Honorary Consulate)* zote duniani na fedha hizo ziweze kukaguliwa kama zilivyo fedha nyingine za umma. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa ufunguzi wa Ubalozi wetu nchini Uholanzi na inashauri Ubalozi kusimamia ukusanyaji wa mapato yake na *Visa* na kuachana na utaratibu uliokuwepo awali wa fedha kukusanywa na *Honorary Consulate*.

Serikali iweke utaratibu wa kuwajulisha wananchi hali halisi ya uhusiano na ushirikiano wa nchi yetu na nchi mbalimbali duniani kuondoa wasiwasi ambapo hujengeka mara kwa mara hususani kwa nchi ambazo uhusiano wetu unaingia dosari.

Serikali ifanye kila jitihada kuhakikisha kuwa mwaka ujao wa fedha inaandaa mkutano wa Mabalozi wote ambao ulishindikana katika mwaka uliopita 2013/2014 ili kuwa na Diplomasia ya Uchumi inayoeleweka.

Juhudi za ununuzi wa majengo mapya ya Ubalozi na mengineyo ndani na nje ya nchi lisimamiwe na Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Majengo yaani TBA kama sheria na taratibu zinavyoelekeza. Wizara iweke utaratibu mzuri wa ufuatiliaji na utekelezaji wa mikataba mbalimbali ya kimataifa pamoja na kuunga mkono na kumpongeza kwa dhati Rais wetu kwa safari zake za nchi za nje ambazo zimeleta mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali, Kamati inashauri kupunguza ukubwa wa misafara hiyo na kuwepo wale watu ambao ni muhimu sana kufuatana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefurahishwa na hatua ya Serikali ya kutafuta ajira kwa Watanzania kutoka shirika la Emirates.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2014/2015: Ili Wizara iweze kutekeleza kazi zilizopangwa 2014/2015 zikiambatana na maoni na ushauri wa Kamati, imekasmiwa kupatiwa shilingi bilioni 191,919,744,000 na kati ya fedha hizo bilioni 161,919,748 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi milioni 30 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Wizara imetengewa shilingi milioni 200 tu kati ya shilingi bilioni 1.5 zinazohitajika kwa ajili ya mkutano huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho: Kamati kwa kiwango kikubwa imeridhishwa na utekelezaji na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara hii na taasisi zake ambazo zinakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu itaendelea kusimama na kuishauri Wizara hii ili iweze kuendelea na kutoa huduma nzuri zilizo bora na kwa wakati kwa wananchi na wadau wengine wote kama ilivyo katika kaulimbiu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhitimisha naomba kukushukuru tena wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili niwasilishe taarifa hii pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Benard Membe, Waziri na Naibu Waziri Mheshimiwa Mahadhi Maalim kwa ushirikiano mzuri walioipatia Kamati yangu katika utekelezaji wa kazi yake. Aidha, tunawashukuru watendaji wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu, John Haule na Ndugu Balozi Rajab Gamau. Kipekee nawashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa ushirikiano wao wakati wa kupitia, kujadili na kuchambua makadirio ya matumizi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Thomas Kashillila kwa kuhakikisha kuwa Kamati inatekeleza majukumu yake na Katibu wa Kamati Ndugu Ramadhani Issa kwa kufanikisha kazi za Kamati na kuandaa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa naliomba Bunge lako tukufu lipokee taarifa hii na kujadili pamoja na kuyakubali makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii Fungu 34 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja kwa kuzingatia maoni ya Kamati kuhusu kuongeza bajeti ya Wizara hii kwa shilingi bilioni 1 na milioni 300 ili kuandaa mkutano wa Mabalozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Betty Machangu kwa kusoma hotuba hiyo ya Kamati ya Mambo ya Nje. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Betty.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014;**

**PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HII KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI.**

## 1.0 UTANGULIZI:

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na 117 (11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, nomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2013/2014; pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kwa niaba ya Kamati yangu tunapenda kutoa salamu za pole kwa wananchi wa Jamhuri ya Malawi kwa kifo cha mpendwa wao, aliyekuwa Balozi wa Nchi hiyo nchini Tanzania Marehemu Balozi Flossie Gomile Chidyaonga aliyefariki tarehe 9 Mei, 2014. Bara la Afrika limepoteza mmoja kati ya Wanadiplomasia aliyepigania amani na umoja wakati wote. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi, Amen.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri utakaotolewa na Kamati hii unatokana na kazi za Bunge kupitia Kamati zake za kuishauri na kuisimamia Serikali kama ilivyo katika Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifuatilia kazi mbalimbali za Wizara hii katika nyakati tofauti kwa mwaka huu wa fedha wa 2013/2014 na kukagua miradi ya Wizara ili kuweza kuwa na usimamizi na ushauri mzuri kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, madhumuni na lengo la maoni na ushauri huu pamoja na mambo mengine ni kuisadia Serikali katika kukamilisha kwa ufanisi, dira, dhamira na kaulimbiu ya Wizara hii ambazo zinalenga kuimarisha Diplomasia ya kiuchumi kupitia uhusiano na ushirikiano wa Kimataifa ili kuleta maisha bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utandawazi uliopo duniani, inaonyesha wazi kwamba huwezi kujifungia ndani ya nchi yako na kutegemea kuimarisha uchumi wake na kuwaletea maisha bora wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwenendo wa ushirikiano wa Kimataifa ili nchi iweze kukubalika na kuthaminiwa na nchi nyingine duniani ni lazima ijipange vyema na kila mara kujitathmini kama inavyo vigezo vya aina hiyo katika Nyanja mbali mbali hususan za kushirikiana kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, katika dhana hiyo, Kamati yangu ilitumia ujuzi na uzoefu wake kuishauri Wizara hii ili hadhi na heshima ya Tanzania mbele ya Jumuiya ya Kimataifa izidi kupanda na kukubalika, kwani kuna dalili zinazoonyesha kuwa, baadhi ya nchi hazifurahii hata kidogo kuiona nchi yetu inazidi kukubalika duniani.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2013/2014

### 2.1 Fedha zilizoidhinishwa na zilizotolewa

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 Wizara iliidhinishiwa Shs, 138,359,944,221/= ambapo kati ya fedha hizo Shs.110,359,944,221/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shs. 28,000,000,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo. Aidha Wizara kupitia Balozi zake ilitarajia kukusanya maduhuli ya Shs. 16,966,729,300/=.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014 Wizara hii ilikuwa imepatiwa shilingi 117,327,353,962/= kati ya fedha hizo shilingi 106,492,848,042/= kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 4,368,705,920/= ni kwa ajili ya Mishahara na shilingi 6,465,800,000/= Kwa ajili ya fedha za miradi ya maendeleo. Aidha Wizara imefanikiwa kukusanya Shs. 12,909,470,376/= ikiwa ni makusanyo ya maduhuli Balozini ambayo ni asilimia 76 tu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na fedha hizo za matumizi ya kawaida, Wizara imeweza kutekeleza kazi zifuatazo:-

**i) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje:**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, jukumu hili limekuwa likitekelezwa kwa kushirikiana na Balozi za Tanzania, Wizara mbalimbali za Serikali, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali pamoja na Sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha 2013/2014 Wizara iliendelea kuvutia uwekezaji katika sekta mbalimbali nchini zikiwemo Kilimo, Afya, Viwanda, Utalii na Nishati na kutafuta masoko ya nje kwa bidhaa zinazozalishwa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa kupokea Tuzo Maalum ya *C.E.O Roundtable* kwa nchi yetu kufungua fursa kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kamati vile vile inampongeza Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutunukiwa Shahada ya Heshima ya Uzamivu (PhD) ya Sheria mwezi Julai, 2013 kutoka Chuo Kikuu cha Guelph cha nchini Canada kutokana na mchango wake mkubwa kwenye sekta ya Kilimo hususan katika masuala yanayohusu usalama wa chakula na majaribio makubwa ya kuongeza matumizi ya teknolojia katika kilimo cha Tanzania kwa lengo la kuwaongezea kipato wananchi na kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati vile vile inampongeza kwa dhati Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kutunukiwa tunzo ya Kiongozi bora wa Bara la Afrika mwenye mchango mkubwa zaidi wa kuleta Maendeleo kwa mwaka 2013 iliyopokelewa kwa niaba yake na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernad C. Membe (Mb) tarehe 9 Aprili, 2014.

**ii) Kusimamia Mikataba na Makubaliano ya Kimataifa;**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, katika kutekeleza jukumu la kusimamia Mikataba na Makubaliano baina ya Tanzania na nchi nyingine na Taasisi mbalimbali za Kimataifa, Wizara iliratibu na kusimamia uwekwaji saini wa Mikataba kati ya Tanzania na nchi nyingine *(Bilateral Agreements)* ipatayo kumi na tatu (13) katika kipindi hiki hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2013.
Mheshimiwa Spika, kati ya Mikataba hiyo kumi na tatu (13), Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara hii, kuchukua hatua za haraka katika utekelezaji wa Mikataba miwili (2) muhimu ambayo ni:-

(a) Mkataba kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Thailand kuhusu ushirikiano katika utunzaji wa wanyamapori wa tarehe 31 Julai, 2013.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa msisitizo wa utekelezaji wa mkataba huu kutokana na umuhimu wa sekta hii katika mchango wa pato la Taifa

ambapo, taarifa zianonyesha kuwa, sekta hii imekumbwa na dhoruba kubwa ya uwindaji haramu wa wanyama aina ya Tembo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara zinazohusika kuchukua hatua madhubuti ili kuwapa matumaini wale wanaokusudia kushirikiana na sisi katika kuimalisha sekta hii.

(b) Hati ya Makubaliano (MOU) kati ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ya Tanzania na Taasisi ya *Clinton Foundation* kuhusu ushirikiano katika masuala ya kilimo wa mwezi Agosti, 2013.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi wa Tanzania kwa kutambua kuwa, sekta ya Kilimo inachangia kwa kiasi kikubwa pato la Watanzania walio wengi, hivyo Serikali ione umuhimu katika utekelezaji wake pamoja na mikataba mingine ya kimataifa ya aina hii.

**iii) Kuratibu Ushirikiano wa Kimataifa, Kikanda na Bara la Afrika:**

Mheshimiwa Spika, katika kipengele hiki, Wizara hii iliratibu na kutekeleza mambo mbalimbali ambayo yamechangia kuleta miundombinu na njia za kuimarisha Diplomasia ya Kiuchumi pamoja na Ustawi wa wananchi kwa ujumla wake. Mambo hayo ni pamoja na:-

(a) Mkutano wa Baraza la Uchumi na Jamii la Umoja wa Mataifa (ECOSOC) Julai, 2013
(b) Mkutano wa 68 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA)
(c) Mkutano wa 37 wa UNESCO.
(d) Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Madola (CHOGM).
(e) Mkutano wa Jukwaa la Uchumi la Dunia (WEF).
(f) Mkutano wa Kimataifa kuhusu biashara haramu ya Wanyamapori.
(g) Mikutano ya kikundi kazi kuhusu mapendekezo ya Ajenda za Malengo mpya ya Maendeleo endelevu baada ya mwaka 2015.
(h) Mkutano wa kikundi kazi cha Mawaziri wa Jumuiya ya Madola (CMAG).

Mheshimiwa Spika, katika Ushirikiano wa Kikanda, Wizara iliweza kuratibu na kushiriki mambo yafuatayo:-

(a) Mikutano na Chaguzi mbalimbali katika nchi za SADC.

(b) Mikutano ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.
(c) Mikutano ya Nchi za Maziwa Makuu (ICGLR).
(d) Kuratibu mambo yanayohusu Jumuiya ya Nchi za mwambao wa Bahari ya Hindi (IORA).
(e) Kuratibu shughuli mbalimbali zinazohusu ushirikiano na Bara la Afrika.

**iv) Kulinda na kuendeleza maslahi ya kitaifa ya kiuchumi na mengineyo nje ya nchi:**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, Wizara ikishirikiana na Balozi zake imeendelea kulinda maslahi ya Taifa na Watanzania wote kwa ujumla katika Nyanja za kiuchumi na nyinginezo nje ya nchi kwa kuratibu na kushiriki kwenye mikutano mbalimbali kama vile mkutano wa Mabadiliko ya Tabia Nchi (COPIA) uliofanyika *Warsaw Poland* tarehe 11-22 Novemba, 2013 na mingineyo.

**v) Kusimamia masuala yanayohusu kinga na haki za Mabalozi waliopo nchini kulingana na mkataba wa Vienna wa mwaka 1961 na 1963:**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa, Wizara inashirikiana na Mamlaka mbalimbali nchini ili kuhakikisha kuwa, Jamii za Kibalozi zinazowakilisha nchi zao hapa nchini zinapata haki zao kama ilivyoainishwa katika sheria za Kimataifa hususan Mkataba wa Vienna kuhusu mahusiano ya Kidiplomasia wa mwaka 1961 *(Vienna Convention on Diplomatic Relations of 1961).*

**vi) Kusimamia na kuratibu masuala ya itifaki (Protocal) na uwakilishi (Credentials):**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, Wizara ilisimamia kazi za Itifaki za Kitaifa hususan katika mapokezi na ziara mbalimbali za viongozi wa Kimataifa wanapotembelea nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kati ya ziara zilizoraitbiwa na Wizara hii ni ziara ya Rais wa Marekani, Barrack Obama tarehe 01-02 Julai, 2013 na Rais wa China Mheshimiwa Xi Jinping tarehe 24 – 25 Machi, 2013.

Mheshimiwa Spika, Kamati inachukua fursa hii kuipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa kuratibu vyema ziara za viongozi hao na kuliletea Taifa letu heshima kubwa mbele ya Jumuiya ya Kimataifa.

**vii) Kuanzisha na kusimamia Huduma za Kikonseli:**

Mheshimiwa Spika, Kamati iliarifiwa kuwa, Wizara kwa kupitia Balozi zake zimeendelea kutoa VISA kwa raia wa nje wanoitembelea Tanzania, kushirikiana na Mamlaka nyingie kutafuta ufumbuzi wa matatizo mbalimbali yanayowakabili Watanzania waishio nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, vile vile Wizara hii inasaidia kuratibu upatikanaji wa vibali vya kutumia ukumbi wa watu mashuhuri (VIP Lounge) wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam.

**viii) Kuratibu shughuli za Tume za Kudumu za pamoja za ushirikiano:**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, katika kuratibu shughuli za Tume za pamoja za Kudumu za Ushirikiano (JPC), Wizara imeendelea kufanya vikao vya wadau wa ndani na nje ya nchi ili kutekeleza shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, katika utekelzaji wa jambo hili Wizara iliandaa mkutano wa pamoja kati ya India na Tanzania tarehe 8-9 Julai, 2013 hapa nchini ambapo maazimio yaliyoafikiwa yanalenga katika kuweka maeneo ya ushirikiano wa Tanzania na India kwa kipindi cha miaka mitatu.

**ix) Utawala na maendelo ya utumishi Wizarani na kwenye Balozi zetu:**

Mheshimiwa Spika, ilielezwa kuwa, Wizara imeendelea na kushughulikia mambo yote ya kiutumishi yanayohusiana na ajira, mafunzo, upelekaji na upangaji wa Mabalozi nchi za nje pamoja na kuimamia shughuli zote za uendeshaji katika Wizara hii na taasisi zilizo chini yake.

**x) Ushirikishwaji wa Diaspora katika maendeleo ya Taifa:**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, Wizara iliendelea na juhudi za kuratibu juhudi za kuandaa mazingira wezeshi, kwa lengo la kuwatumia watanzania waishio ughaibuni kuwekeza na kuwavutia wawekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri serikali kubuni njia bora zaidi zitakazowapa motisha Watanzania walioko nje kuwekeza hapa nyumbani kwani inaonekana mwamko wa Watanzania waliko ughaibuni kufanya hivyo bado ni mdogo sana.

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza ushauri huu, Kamati inapendekeza Serikali kwenda kujifunza na kubadilishana uzoefu na nchi ya Ethiopia

ambayo imepiga hatua kubwa katika masuala ya Diaspora, ambayo inasemekana raia wake walioko nje wanachangia karibu dola za kimarekani bilioni tatu kwa mwaka na kuiwezesha nchi hiyo kuwekeza katika Mradi Mkubwa wa kujenga Bwawa la kuzalisha Umeme kutoka mto Nile.

**2.1 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Bajeti ya mwaka 2013/2014:**

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi hizo, Kamati ilipokea na kujadili bajeti ya mwaka 2013/2014 na ilitoa ushauri na maoni kumi na tatu (13) ili yaende sambamba na utekelezaji wa kazi za Wizara kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa juhudi kubwa iliyofanya ya kutekeleza maoni na ushauri wake kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 pamoja na changamoto iliyozipata kutokana na ufinyu wa Bajeti.

Mheshimwa Spika, Wizara hii ndiyo kioo cha Watanzania nje ya nchi yetu, hivyo ni vyema Serikali ikahakikisha inaitengea Bajeti ya kutosha ili kukabiliana na changamoto za Wizara zikiwemo zinazowakabili Watanzania wanaoishi nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii kama haitapewa fedha za kutosha kwa wakati, itaathiri shughuli zetu za Mambo ya Nje na Ushirikiano wetu wa Kimataifa pamoja na heshima iliyokwisha jengeka kwa nchi yetu kwa miaka mingi.

**2.2 Miradi ya Maendeleo**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2013 Wizara ilikuwa ilipatiwa Shs. 6,465,800,000/= kati ya Shs. 28,000,000,000/= ambapo ni asilimia ishirini na tatu tu (23%), kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi miwili ya maendeleo iliyopo Paris – Ufaransa na Maputo – Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, miradi hii lengo lake ni "Ukarabati wa Jengo la Ghorofa tisa kule Maputo – Msumbiji" na "Ununuzi wa Jengo la Ubalozi kule Paris- Ufaransa" Kamati yangu ilitembelea na kukagua miradi hiyo katika mwezi wa Febuari, 2014, na kubaini changamoto mbali mbali zilizojitokeza kutokana na fedha hizo kutopatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kati ya changamoto zilizojitokeza na ambayo itaigharimu nchi yetu ni ile ya mkandarasi na msimamizi wa ujenzi kutoa tozo *(Penalties)* kutokana na ucheleweshaji wa malipo. Mradi huu wa ukarabati wa jengo la ghorofa tisa kule Maputo – Msumbiji unadaiwa tozo ya usd 26,583.33 hadi mwezi Machi 2013.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa serikali inapoteza dola za kimarekani milioni moja (usd 1,000,000/=) kila mwaka kutokana na kutokamilika kwa mradi wa Ukarabati wa jengo hili la Maputo – Msumbiji, fedha ambazo zingepatikana kwa kulikodisha.
Mheshimiwa Spika, fedha hizi ni nyingi sana na zingeweza kugharimia uendeshaji wa Ofisi zote za Kibalozi zilizoko katika nchi za SADC.

Mheshimiwa Spika, kamati inaishauri Serikali kufanya kila liwezekanalo kukamilisha utoaji wa fedha za miradi hii kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mradi wa ununuzi wa jengo liliopo Paris – Ufaransa, Tanzania inaweza kupoteza fursa ya kupata jengo hilo ambalo lipo sehemu nzuri kama fedha hizo hazikutolewa na Serikali kabla ya kumalizika mwaka huu wa fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kati ya Shilingi Bilioni 40.536 zilizopangwa kutolewa kwa ununuzi wa jengo hili ni shilingi Bilioni 10.609 tu ndio zilikuwa zimetolewa wakati kamati yangu ilipokuwa ikikagua Mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa inatoa fedha za Miradi hii kama zinavyoidhinishwa na Bunge ili kuepuka changamoto zinazotokana na Mikataba ya Utekelezaji wa Miradi hiyo.

## 2.4 OFISI ZA UBALOZI NA DIPLOMASIA YA KIUCHUMI

### 2.4.1 Fedha za Kuendeshea Ofisi za Kibalozi

Mheshimiwa Spika, kamati ilielezwa kuwa kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 zipo Ofisi 34 za Kibalozi katika Dunia nzima ambazo hadi mwezi Machi 2014 zilikuwa zimepatiwa Shs. Bilioni 39.315 kati ya fedha zote Shs.

Bilioni 74.333 zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 kwa ajili matumizi mengineyo ya uendeshaji kazi.
Mheshimiwa Spika, kamati pia ilielezwa kuwa Ofisi hizo za Ubalozi kwa mwaka ujao wa fedha zinaombewa shs. 78,278,523,900/= kwa ajili ya mishahara na matumizi ya kawaida ya uendeshaji wa ofisi hizo.

Mheshimiwa Spika, kiasi hicho ni kutokana na ufinyu wa bajeti ambao umesababisha Wizara hii kupewa mgao mdogo sana wa Shs. Bilioni 75.22 kwa matumizi ya gharama za uendeshaji, lakini mahitaji halisi ya Ofisi hizo fedha zisizopungua Shs. Bilioni 92.40

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali, kuzingatia upya makisio ya fedha zilizopangwa kutolewa kwa Ofisi za Kibalozi katika kukidhi mahitaji ya kuendesha uhusiano na ushirikiano wa kimataifa katika nchi wanazotuwakilisha duniani kote.

**2.4.2 Majengo ya Ofisi za Kibalozi**

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilijadili na kuchambua kwa kina suala zima la umuhimu wa majengo ya Ofisi za Kibalozi katika uwakilishi wa Diplomasia ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha ni kuwa majengo ya Ofisi hizo na vifaa vingine vya kuendeshea kazi kama vile magari kwa ujumla viko katika hali duni. Aidha, hata watendaji wa Ofisi hizi nao wamejikuta mara nyingi wakiwa katika hali isiyoridhisha kwa kile kinachoelezwa ufinyu wa bajeti kwa miaka mingi sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa zipo dalili za kutia moyo wa kupatikana suluhisho la tatizo hili sugu kwa ujenzi wa Ofisi hizo kwa njia ya "Mortgage Financing" katika nchi ziliko Balozi hizo, kama maoni na ushauri wa kamati yangu ulivyotolewa wakati wa kupokea na kujadili Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2013/14 mwezi Mei 2013.
Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imefarajika sana kuona ushauri wake huu umetekelezwa na kuanza kuzaa matunda kwa kiwango hiki.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaendelea kuishauri Serikali kulipa kipaumbele jambo hili ili juhudi hizi zisije zikafia njiani.

**2.4.3 Ushirikiano wa Kimataifa wa Diplomasia ya Kiuchumi**

Mheshimiwa Spika, bila ya uhusiano na ushirikiano wa kimataifa madhubuti na imara nchi yetu itajifunga yenyewe na inaweza kutengwa katika kujenga na kuimarisha diplomasia ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, hata ukichukulia uchumi wa mtu mmoja mmoja hapa hapa nchini, utagundua kuwa ni lazima uwe na uhusiano na ushirikiano na watu wengine mbali mbali wa nje na unapoishi au kufanyia biashara zako.

Mheshimiwa Spika, taaswira na maudhui haya ndio yanayoipelekea nchi yetu kulazimika kuwa na uhusiano na ushirikiano na nchi nyengine nyingi duniani katika Nyanja za kiuchumi. Kamati ilielezwa kuwa uhusiano na ushirikiano wa nchi yetu na nchi nyingine duniani kwa mwaka 2013/2014 katika mambo ya kiuchumi kwa ujumla wake ni mzuri.

## 3.0 KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2014/2015:

Mheshimiwa Spika, Baada ya Kamati kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2013/2014 pamoja na fedha zilizotengwa na kutolewa hadi tarehe 31 Machi, 2014 Wizara iliwasilisha kazi ambazo inakusudia kutekeleza kwa kipindi cha mwaka 2014/2015, kama ifuatavyo:-

i) Kuitangaza nchi yetu kama moja ya nchi duniani yenye mazingira mazuri kwa ajili ya uwekezaji kutokana na historia yake ya miaka mingi ya amani, umoja, utulivu na mshikamano wa kitaifa;

ii) Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa ahadi mbalimbali zilizotolewa kwa nchi yetu na nchi mbalimbali wahisani na mashirika ya kikanda na ya kimataifa katika kusaidia utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo;

iii) Kuendelea kuratibu wizara, idara na taasisi nyingine za serikali katika masuala yote ya kikanda na yale ya kimataifa kwa lengo la kuvutia wawekezaji na watalii; kutafuta nafasi za masomo, ajira na nafasi za kubadilishana uzoefu na kutafuta masoko.

iv) Kusimamia, kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa mikataba mbalimbali iliyosaniwa kati ya nchi yetu na nchi nyingine na ile ya mashirika ya kikanda na kimataifa;

v) Kuendelea kufuatilia kwa karibu mageuzi kwenye taasisi za Umoja wa Mataifa kama vile Baraza la Kiuchumi na Kijamii (ECOSOC);

Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA); kuanzishwa kwa malengo endelevu ya maendeleo – *Sustainable Development Goals (SDGs)* na agenda ya maendeleo baada ya kumalizika kwa kipindi cha malengo ya milenia 2015.

vi) Kuendelea kusimamia na kupigania maslahi ya nchi maskini kwenye mikutano yote mikubwa na hasa ile ya Umoja wa Mataifa na Taasisi zake. Vile vile, itaendelea kufanya mazungumzo na nchi tajiri duniani ili kuharakisha maendeleo ya nchi maskini.

vii) Kuongeza uwakilishi wetu nje kwa kufungua Balozi mpya na Balozi ndogo na kuongeza umiliki wa nyumba za makazi na ofisi za Ubalozi katika Balozi zetu nje kwa kadri hali ya fedha itakavyoruhusu;

viii) Kujenga mahusiano ya kirafiki na ushirikiano wa kiuchumi kati ya vyombo mbalimbali vya kikanda na kimataifa, unaozingatia maslahi muhimu ya Taifa letu;

ix) Kuendelea kusimamia na kuzihimiza balozi zetu nje kutafuata wawekezaji, fursa za ajira, nafasi za masomo na masoko kwa bidaa zetu;

x) Kukamilisha mchakato wa kuitambua Jumuiya ya Watanzania wanaoishi ughaibuni na kuweka utaratibu utakaowawezesha kuchangia maendeleo ya Taifa lao; na

xi) Kuendeleza ujirani mwema na nchi jirani.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI KATIKA UTEKELEAZAJI WA KAZI ZA WIZARA ZILIZOPANGWA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2014/2015:

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kupokea na kujadili taarifa ya mipango ya Wizara kwa kazi zilizopanga kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ilitoa maoni na ushauri ili uendane na utekelezaji huo kama ifuatavyo:-

i) Wizara ione umuhimu wa kununua vitendea kazi vipya (kama vile magari) katika Ofisi za Balozi zetu ambavyo vinakwenda na wakati na kwa kuanzia ziangaliwe zile Balozi ambazo hali zao ni mbaya sana kiasi cha kuitia aibu nchi yetu.

ii) Serikali ione umuhimu wa kuiwezesha Wizara hii kutekeleza mipango yake ya *"Mortgage Financing"* pamoja na kutumia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ikayowezesha Balozi zetu kujengewa majengo ya Ofisi zake na nyumba za wafanyakazi katika zile nchi ambazo zimeonyesha nia ya kukubaliana na mipango hii.

iii) Serikali itafute fedha hata kama za mkopo ili kujenga Ofisi na Nyumba za Watumishi katika viwanja vyake vyote ilivyopewa katika nchi mbalimbali kama vile Msumbiji, Uingereza na kwingineko.

iv) Serikali iangalie namna bora ya kulimiliki eneo inalokusudia kulichukuwa katika Wilaya ya Bagamoyo kwa ajili ya kujenga Chuo Cha Diplomasia ili liweze kutumika kiuchumi na kuepusha mgongano na jamii inalolizunguka.

v) Wizara itafute utaratibu ambao utawezesha kutoa elimu kuhusu dhana na madhumuni ya "African Peer Review Mechanism (APRM)" kwa wananchi na wadau wengine na taswira ya taasisi hiyo na faida zake kwa taifa.

vi) Kutokana na umuhimu wa mpango huu wa APRM kamati inaishauri Serikali kuipatia Fungu lake la matumizi (Vote), badala ya fedha hizo kupitia katika fungu 34 la Wizara.

vii) Serikali ihakikishe inatoa fedha zote zilizobakia za mradi wa ukarabati wa ujenzi wa jengo la ofisi ya Msumbiji na ununuzi wa jengo la Ubalozi wa Ufaransa zilizotengwa katika Fungu 34 Mradi namba 6391 kabla ya kumalizika mwaka wa fedha wa 2013/2014 ili kukamilisha mambo yaliyobakia kama ilivyopangwa.

viii) Kamati inaendelea kusisitiza Ofisi zote za Ubalozi duniani zipewe Mafungu yao (Votes), na fedha zao ziende moja kwa moja kwenye mafungu hayo badala ya kupitia fungu 34 la Wizara.

ix) Ili kuondoa dhana kuwa Wizara hii inatengewa na kupatiwa fedha nyingi, Serikali iweke utaratibu wa malipo ya itifaki *(Protocal)* kwa viongozi wa Kitaifa katika Fungu la Wizara ya Fedha (Hazina) na kuwalipia moja kwa moja badala ya kuziweka fedha hizo katika fungu 34 la Wizara hii.

x) Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iweke utaratibu wa uhakika wa kukusanya mapato katika balozi za heshima "Honourable Cousel" zote Duniani

na fedha hizo ziweze kukaguliwa kama zilivyo fedha nyingie za umma. Aidha Kamati inapongeza Serikali kwa ufunguzi wa Ubalozi mpya wa Uholanzi na inashauri kusimamia ukusanyaji wa mapato yake ya Visa na kuachana na utaratibu uliokuwepo awali, wa fedha ya VISA kukusanywa na Honorable Counsel.

xi) Serikali iweke utaratibu wa kuwajulisha wananchi hali halisi ya uhusiano na ushirikiano wa nchi yetu na nchi mbalimbali duniani ili kuondoa wasiwasi ambao hujengeka mara kwa mara hususan kwa zile nchi ambazo uhusiano wetu unaingia dosari.

xii) Serikali ifanye kila jitihada kuhakikisha kuwa, mwaka ujao wa fedha wa 2014/2015 inaandaa mkutano wa Mabalozi wote ambao ulishindikana katika mwaka uliopita wa 2013/2014, ili kuwa na Diplomasia ya kiuchumi inayoeleweka na siyo ya kufikirika.

xiii) Jukumu la Ununuzi na Ujenzi wa Majengo mapya ya Ubalozi na mengineyo ndani na nje ya nchi lisimamiwe na Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Majengo (Tanzania Building Agency –TBA) kama sheria na taratibu zinavyoelekeza.

xiv) Wizara iweke utaratibu mzuri wa ufuatiliaji na utekelezaji wa mikataba mbalimbali ya kimataifa inayosainiwa na nchi yetu.

xv) Pamoja na kuunga mkono na kumpongeza kwa dhati Rais wetu kwa safari zake za nje ya nchi ambazo zimeleta mafanikio makubwa katika Sekta mbali mbali, Kamati inashauri kupunguza ukubwa wa misafara hiyo na kuwepo wale watu ambao ni muhimu sana kufuatana nao.

xvi) Kamati inaishauri Wizara kufuatilia kuhusu ajira kaika mashirika ya ndege ambayo ndege zake zinatua na kufanya biashara na nchi yetu kama vile Shirika la Ndege la Emirates, ambalo limewanufaisha sana majirani wetu.

**5.0 MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA KWA MWAKA 2014/2015 ILI KUTEKELEZA KAZI ZA WIZARA ZIKIAMBATANA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

Mheshimiwa Spika, ili Wizara hii iweze kutekeleza kazi zilizopangwa kwa mwaka 2014/2015 zikiambatana na maoni na ushauri wa Kamati, imekasimiwa kupatiwa shilingi 191,919,748,000/=. Kati ya fedha hizo shs. 161,919,748,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 30,000,000,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.
Mheshimiwa Spika, kama inavyoonekana, fedha hizi ni kidogo sana ambazo zinaipa changamoto Wizara hii kutokana na majukumu yake.
Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia ukweli huo, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu kwa kupitia Kamati yake ya Bajeti kufanya kila liwezekanalo kuipatia fedha za ziada Wizara hii ili kuweza kuratibu Mkutano wa Mabalozi wa Tanzania katika mwaka wa fedha wa 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Wizara imetengewa shilingi 200,000,000/= tu kati ya shilingi 1,500,000,000/= zinazohitajika kwa ajili ya mkutano huo.

**6.0 HITIMISHO:**

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa kiwango kikubwa imeridhishwa na utekelezaji na ufuatiliaji wa shughuli mbali mbali za Wizara hii na taasisi zake, ambao unakabiliwa na changamoto za ufinyu wa Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu itaendelea kuisimamia na kuishauri Wizara hii ili iweze kuendelea kutoa huduma nzuri zaidi, zilizo bora na kwa wakati kwa wananchi na wadau wengine wote kama ilivyo katika kauli mbiu yake.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha, naomba kukushukuru tena wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu ili niwasilishe taarifa hii pamoja na maoni na ushauri wa kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.
Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati kabisa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Bernad Camilius Membe (Mb) na Mheshimiwa Mahadhi Juma Maalim (Mb) kwa ushirikiano mzuri wanaoipatia Kamati yangu katika utekelezaji wa kazi zake.

Aidha tunawashukuru watendaji wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wao Ndugu John Haule na Ndugu Balozi Rajabu Gamaha.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Ushirikiano wao wakati wa kupitia, kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

Kwa kuthamini michango yao naomba kuawatambua kwa majina kama ifuatavyo;-

1. Mhe. Edward N. Lowassa(Mb)-Mwenyekiti
2. Mhe. Mussa Zungu Azzan (Mb)-M/Mwenyekiti
3. Mhe. Suleiman Said Jaffo (Mb)-Mjumbe
4. Mhe. Khalifa Suleiman Khalifa (Mb)-Mjumbe
5. Mhe. Susan A. Jarome Lyimo (Mb)-Mjumbe
6. Mhe. Betty Eliezer Machangu (Mb)-Mjumbe
7. Mhe. Eng. Yussuf H.Masauni (Mb)-Mjumbe
8. Mhe. Faith Mohammed Mitambo (Mb)-Mjumbe
9. Mhe. Thuwaiba Idrissa Muhamed (Mb)Mjumbe
10. Mhe. Leticia Mageni Nyerere (Mb)-Mjumbe
11. Mhe. Muhammad Ibrahim Sanya (Mb)Mjumbe
12. Mhe. John Magale Shibuda (Mb)-Mjumbe
13. Mhe. Anastanzia James Wambura (Mb) Mjumbe
14. Mhe. Khamis Sued Kagasheki (Mb)-Mjumbe

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu namshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashililah, kwa kuhakikisha kuwa kamati inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha nawashukuru Katibu wa Kamati hii Ndugu Ramadhan Issa kwa kufanikisha kazi za Kamati na kuandaa Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa naliomba Bunge lako tukufu lipokee Taarifa hii na kujadili pamoja na kuyakubali Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Fungu 34 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja kwa kuzingatia maoni ya Kamati kuhusu kuongezwa Bajeti ya

Wizara hii kwa Shilingi Bilioni Moja na Milioni Mia Tatu (1,300,000,000/=) ili Kuandaa Mkutano wa Mabalozi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Edward N. Lowassa, Mb

**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YAMAMBO YA NJE**
**NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA**
MEI, 2014

**NAIBU SPIKA:** Sasa naomba nimuite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Mheshimiwa Wenje.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**MHE. EZEKIA D. WENJE – MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya sijaanza, naomba nifanye masahihisho madogo kwenye ukurasa wa 16 katika hotuba yangu, *paragraph* ya 3 ukurasa wa 3. Naomba isomeke kwamba baada ya kustaafu kwa aliyekuwa Balozi wetu nchini Sweden, Mohamed Mwinyi Mzale, kutoa hilo neno Marehemu, ni makosa ya uchapaji. Kwa hiyo, naomba hayo marekebisho yazingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha

2013/2014 na makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pia shukrani na pongezi kwa viongozi wakuu wa vyama vya *NCCR - Mageuzi,* Chama cha Wananchi - CUF na CHADEMA kwa busara zao za kuona umuhimu wa kuunganisha vyama hivi katika kuunda Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na katika kuunda Umoja wa Katiba ya Wananchi *(UKAWA)* ndani na nje ya Bunge ili kuharakisha ukombozi wa taifa hili katika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba nimshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mbunge, kwa kuendelea kuniamini na kuniacha katika nafasi ya Msemaji Mkuu na Waziri Kivuli katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Naibu wangu Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis Mbunge wa Chonga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa pamoja mimi na Mheshimiwa Haroub tunamuahidi Kiongozi wa Kambi ya Upinzani utendaji uliotukuka katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2013/2014 inayoisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na udhaifu mwingi wa kiutendaji na kiuwajibikaji na upungufu sugu katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa miaka mitatu mfululizo imekuwa ikitoa ushauri kwa Serikali kufanya mambo kadhaa ili kuboresha utendaji na ufanisi katika Wizara hii. Baadhi ya masuala tuliyoitaka Serikali kufanya ni pamoja na yafuatayo:-

Moja, tulitaka Serikali kutoa taarifa ya namna kila Balozi inavyotakeleza Sera ya Diplomasia ya Uchumi kwa kuzingatia kwamba Balozi nyingi ziko hoi kifedha kiasi cha kwamba waambata wa kiuchumi wanakosa hata fedha za kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa ajili ya upepelezi wa masuala ya kiuchumi.

Pili, tulitaka Serikali kuziwezesha Balozi zetu nje kwa kuzitengea fedha za kutosha ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Tatu, tuliitaka Serikali kufanya uchunguzi kuhusu tuhuma za Balozi zetu nchini China na Uingereza kutoa hati za kusafiria kwa mataifa mengine hasa ya Afrika Maghariki ili kubaini ukweli na kuliondolea taifa aibu kutokana na tuhuma hizi.

Nne, tulitaka Serikali kupeleka Mwambata wa Kiuchumi *(Economic Attachè)* nchini China ili kufuatilia fursa mbalimbali za kiuchumi katika kutekeleza Diplomasia ya Uchumi kutokana na mahusiano makubwa ya kibiashara kati ya nchi yetu na nchi ya China.

Tano, tuliitaka Serikali kuwawekea zuio wahusika wa kashfa ya rada kuwa viongozi wa shughuli za Kiserikali ili walau kuonyesha uwajibikaji wa kimaadili *(moral accountability)* baada ya kushindwa kuwawajibisha kisheria ili kuondoa dhana iliyojengeka miongoni mwa jamii kwamba dola imetekewa na mafisadi.

Sita, tuliitaka Serikali kueleza bayana faida za kiuchumi tunazopata kama Taifa kwa kushirikiana na Jumuiya mbalimbali za Kimataifa ili kuthibitisha kwamba mashirikiano hayo hayatumiki kupora rasilimali za nchi yetu kwa hila ya uwekezaji.

Saba, tuliitaka Serikali kutoa idadi ya majengo ya Balozi zetu, nyumba za Mabalozi, nyumba za Maafisa wa Mabalozi na ofisi za Ubalozi kwa mchanganuo wa idadi ya nyumba katika nchi na kama nyumba hizo zina hati miliki au la!

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwa Wizara. Katika bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2013/2014 zilitengwa shilingi bilioni 30 kwa ajili hiyo. Hata hivyo, kiasi cha fedha kilichotolewa na Hazina hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2014 ni shilingi bilioni 6.5 tu sawa na 21.6% tu. Hii ina maana kwamba bajeti ya maendeleo kwa Wizara hii haikutekelezwa kwa 78.3%.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo kiasi hiki cha fedha ambazo hazikutolewa kingekuwa kimetolewa kwa wakati, malalamiko ya muda mrefu ya uchakavu wa Balozi zetu na ukosefu wa magari kwa Mabalozi wetu ungekuwa umepungua sana au kumalizika kabisa. Jambo la kushangaza ni kwamba kwa mwaka huu wa fedha 2014/2015 zimetengwa shilingi bilioni 30 kwa ajili ya bajeti ya maendeleo kwa Wizara ya Mambo ya Nje kiwango kilekile kilichotengwa mwaka jana na kwa miradi ileile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama fedha ya maendeleo inatolewa kwa asilimia kidogo namna hiyo licha ya Serikali kuwa na taarifa za uduni wa Balozi zetu nje ya nchi, ni kwa namna gani Mabalozi wetu wanaweza kutekeleza diplomasia ya uchumi ambayo inategemea fedha za maendeleo na ambayo

tumekuwa tukipigania kwa miaka mingi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwa makini inapofanya makisio ya bajeti na pia Hazina itoe fedha kama zilizopitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya utengamano *(Intergration Policy)* na ushiriki wa Tanzania katika mahusiano ya Kikanda. Tanzania ni nchi mwanachama wa Jumuiya mbalimbali za kikanda katika Bara la Afrika Mathalani SADC na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, mpaka sasa kama nchi hatuna mwongozo wa kisera na kisheria ambao unatuongoza katika mahusiano hayo, kwa maneno mengine nchi haina sera ya utengamano *(Intergration Policy)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumuiya za kikanda pamoja na mahusiano mazuri ya kidiplomasia ni fursa muhimu za kiuchumi katika nchi yetu. Katika mchango wake katika bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Mbowe alibainisha upungufu huu mkubwa wa kisera ambao unaligharimu taifa kwa kuwa nchi yetu inajiunga na Jumuiya mbalimbali za kikanda bila kuwa na ajenda maalum ya kisera juu ya nini tunachokitahiji na nini tutapata kama taifa tunapojiunga na Jumuiya hizo. Katika mchango wake huo Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni aliitaka Serikali kuwa na sera na mipango katika uhusiano wa kikanda ili kujua namna ya kutumia fursa za kiuchumi katika mahusiano ya nchi washirika hasa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati akifanya majumuisho ya hoja yake hapa Bungeni, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, alisema kuwa sera ya Afrika Mashariki au sera ya kikanda ipo katika mchakato wa kukamilika chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, imeshangazwa na Serikali kukosa sera mahsusi inayoratibu mahusiano yetu kama nchi katika jumuiya ambazo sisi ni wanachama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya haraka kukamilisha sera hiyo na inashauri kuwa Wabunge kama wadau wahusishwe mapema na pia baadaye sera hiyo itungiwe sheria, Bunge liweze kuisimamia Serikali katika kutekeleza sera hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Balozi za Tanzania nje ya nchi: Kutokana na changamoto za kiuchumi na kiusalama, mataifa mbalimbali duniani yanatafuta kushirikiana ili kukabiliana na changamoto hizo. Licha ya ushirikiano katika masuala ya siasa na huduma za jamii, msingi mkubwa wa msukumo wa ushirikiano wa mataifa mbalimbali kupitia balozi zao umekuwa na malengo ya kiuchumi zaidi. Hivyo, kwa msingi huo huo, Tanzania inatakiwa kutumia balozi zake kimkakati ili ziweze kutumia fursa mbalmbali za kiuchumi katika nchi

inazotuwakilisha katika kuleta mageuzi ya kiuchumi katika sekta za biashara, uwekezaji, utalii na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kwamba Tanzania iondokane na fikra za kutegemea misaada pekee kupitia balozi zetu, *begging diplomacy* (hii diplomasia ya ombaomba). Ikiwa tunapata misaada, iwe ni sehemu ndogo tu kati ya mapato makubwa tutakayokuwa tunapata kutokana na biashara, utalii, uwekezaji katika sekta mbalimbali na fursa nyingine ambazo balozi zetu zitakuwa zimetafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuzaji na uendelezaji wa Diplomasia ya Uchumi: Balozi zetu nyingi za Tanzania nje ya nchi zilianzishwa kabla dhana ya diplomasia ya uchumi haijaenea duniani. Dhana ya diplomasia ya uchumi, ilianza kusambaa kwa kasi kutokana na msukumo wa utandawazi ulioambatana na mageuzi ya kiuchumi duniani. Hivyo, kabla ya kuanza kwa harakati za diplomasia ya uchumi, balozi nyingi zilianzishwa kwa misukumo au malengo ya kisiasa zaidi *(political diplomacy)* kuliko masuala ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kumalizika kwa vita baridi baina ya kambi mbili kuu duniani zenye milengo ya siasa za kijamaa na kibepari, na kutokana na Ujamaa kushindwa katika vita hiyo, mahusiano katika ya nchi zilizokuwa na siasa za kijamaa ambayo yalikuwa ni ya kisiasa zaidi, yalianza kubadilika taratibu na kuanza kuwa ya kiuchumi zaidi. Hii ni kwa sababu mfumo wa kiuchumi na kisiasa uliokuwa unatawala dunia ulikuwa ni Ubepari *(Capitalism)* baada ya Ujamaa *(Socialism)* kusambaratika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtanzamo kwamba, Serikali inapoteua mabalozi kwenda nchi mbalimbali duniani, ifanye hivyo kimkakati. Mkakati namba moja uwe ni mkakati wa kukuza na kuedeleza diplomasia ya uchumi ndipo mambo mengine yafuate.

Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kwamba ikiwa hakuna fursa za kiuchumi tutakazopata kama taifa kwa kuwa na ubalozi katika nchi fulani, ni bora ubalozi huo usianzishwe. Hivyo tunaitaka Serikali kufanya tathmini upya juu ya faida halisi za kiuchumi tunazopata kutoka kila nchi tuliyoweka Ubalozi. Taarifa ya tathmini hiyo itumike kama dira ya kufanya uamuzi kama bado kuna haja ya kuendelea na ubalozi huo au kuufunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo pia kwamba, kama mkakati wetu katika balozi utakuwa ni wa kiuchumi zaidi, basi uteuzi wa mabalozi ulenge kupunguza gharama za uendeshaji wa balozi (*administrative costs*) na kuchuma kwa wingi iwezekanavyo matunda ya kiuchumi (*maximization of opportunities*) katika balozi zetu. Hii ni pamoja na

kupunguza idadi ya mabalozi ili watakaobaki wawe wanahudumu katika nchi zaidi ya moja zinazopakana. Mathalani katika nchi za Rwanda na Burundi, Tanzania ina balozi katika nchi zote hizo. Kijiografia, nchi hizi ni ndogo na zinapakana, hivyo ingekuwa nafuu zaidi, kwa maana ya gharama za uendeshaji kuwa na balozi mmoja katika nchi mojawapo atakayehudumia nchi zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni katika muktadha huohuo Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji ni kwa nini tuwe na mrundikano wa mabalozi katika ukanda mmoja kama ilivyo sasa kwa balozi zetu za Maputo, Harare, Lusaka, Kinshasa, Lilongwe na Pretoria? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba, badala ya kuwa na mabalozi sita katika ukanda huu, tungekua na mabalozi wawili tu ambao wangeweza kuhudumia hizi nchi zote kwa sababu ziko kwenye ukanda mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kutumia mfano wa wa ubalozi wetu nchini Sweden ambao unahudumia nchi nyingine za Scandinavia kama vile Denmark, Norway na Finland. Ushauri huu unatokana na ukweli kwamba, tunapata faida za kiuchumi zaidi kutoka katika nchi hizo kupitia fursa mbalimbali ikiwemo misaada licha ya kuwa na ubalozi mmoja tu katika ukanda huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imeshawishika kwamba hii itakua ni njia nzuri zaidi ya kupunguza utitiri wa diplomasia za kisiasa (*political diplomacy*) ambazo kwa sasa hazina nguvu tena kama zamani wakati wa vita baridi na badala yake tuweke balozi zetu kimkakati kwenye maeneo yenye tija kubwa zaidi kwetu kiuchumi ili tuweze kuwa na ushindani katika dunia hii ya leo ambapo uchumi imara na endelevu ndiyo kigezo kikubwa cha taifa lenye nguvu duniani.

Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitika kwamba licha ya wazo hili la diplomasia ya uchumi kuwa muhimu na lenye tija kubwa kwa taifa, bado Serikali haijaona umuhimu wa kutenga fedha maalum kwa ajili ya utekelezaji wa diplomasia ya uchumi. Nasema hivi kwa sababu katika bajeti ya maendeleo ya Wizara hii, shilingi bilioni 30 iliyotengwa mwaka huu wa fedha 2014/2014 haijaonesha mchanganuo wa fedha iliyotengwa kwa ajili ya diplomasia ya uchumi. Hivyo Waziri alieleze Bunge kuwa Serikali ina mpango gani na diplomasia ya uchumi ikiwa haijatenga bajeti ya kushughulikia suala hilo hata kidogo!

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi mabaya ya fedha katika balozi. Kuna mwenendo mbaya wa matumizi ya fedha za umma katika balozi zetu. Licha ya malalamiko ya kila mwaka kwamba bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje ni

kidogo kiasi kwamba, balozi nyingi za Tanzania nje ya nchi ziko hoi kifedha, bado kumekuwa hakuna nidhamu ya matumizi na utunzaji wa fedha katika balozi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2013 inaonesha kwamba, walau balozi tatu za Tanzania nje zilipata hati chafu na hati zenye mashaka katika matumizi na utunzaji wa fedha. Ubalozi uliopata hati chafu ni ubalozi wa Tanzania Muscat, hii ni kwa sababu taarifa za fedha za ubalozi huo zilionesha kuwa bakaa ya mwisho ya fedha ilikuwa ni shilingi milioni 150 badala ya shilingi milioni 639 kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha.

Kwa mujibu wa CAG, hitilafu hii ilitokana na kutoonesha mapokezi ya fedha shilingi milioni 97 na kujumuisha hasara ambayo haikuwa na mchanganuo wa kuthibitisa uhalali wake ya shilingi milioni 392 iliyotokana na kubadili fedha za kigeni na hivyo kupelekea kiasi hicho cha fedha kuonesha pungufu kwa shilingi milioni 489.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhaifu mwingine wa ubalozi huo wa Muscat katika utunzaji wa fedha ni makusanyo ya mapato ya ubalozi ya shilingi milioni 108 kutopelekwa benki. Kwa mujibu wa CAG, ubalozi huo ulikusanya kiasi cha shilingi milioni 564 ambapo kati ya kiasi hicho ni shilingi milioni 456 tu ndizo zilizopelekwa benki na shilingi milioni 108 hazikupelekwa benki. Aidha, ubalozi wa Muscat haukuandaa taarifa za usuluhusho wa benki *(bank reconciliation)* jambo ambalo ni kinyume na Kanuni ya 162 ya Fedha za Umma ya mwaka 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, balozi nyingine zilizopata hati zenye mashaka ni balozi za Tanzania Kinshasa (Congo DRC) na Kampala (Uganda). Katika ubalozi wa Tanzania katika nchi ya Kidemokrasia ya Congo kulikuwa na matumizi ya shilingi milioni 31 ikiwa ni malipo ya kabla ya kupata huduma ya pango kama bakaa iliyokuwepo mwanzoni mwa mwaka. Hata hivyo, hakukuwa na nyaraka zozote za uthibitisho juu ya uhalali na usahihi wa matumizi hayo. Hali kadhalika katika ubalozi wetu nchini Uganda, kulikuwa na tofauti ya shilingi milioni 48 katika bakaa ya mwisho wa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili imechukua hatua gani kwa balozi zilizopata hati chafu na hati zenye mashaka katika masuala ya matumizi na utunzaji fedha? Serikali pia ieleze imeweka mikakati gani ya kudhibiti matumizi mabaya ya fedha katika balozi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukarabati wa Jengo la Ubalozi wa Tanzania Washington – Marekani: Katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu bajeti ya Wizara hii mwaka jana 2013/2014, tuliishauri Serikali kulifanyia ukarabati jengo letu la Ubalozi la zamani lilipo Washington nchi Marekani kuliko kuliacha hivi hivi kuendelea kuchakaa. Ukarabati huo ungekua na tija ya kiuchumi maana hilo jengo linaweza kupangishwa na likawa mojawapo ya vyanzo vya mapato. Gharama ya jumla ya ukarabati wa jengo hilo inakadiriwa kuwa dola za kimarekani millioni 1.5. Lakini jambo la ajabu ni kwamba Serikali imelitelekeza jengo hilo na kuhamia kwenye jengo jipya. Hivi ni kweli Serikali imekosa kabisa dola za kimarekani milioni 1.5 kukarabati jengo hilo ili liwe chanzo cha mapato? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takriban miaka mitatu mfululizo Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikiikumbusha Serikali kuhusu jengo hili lakini Serikali haifanyi chochote. Hivi hii ni Serikali gani inayojiita sikivu lakini haitekelezi ushauri mzuri inayopewa hapa Bungeni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Uwiano wa Mabalozi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar: Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ni Wizara inayoshughulika na mambo ya Muungano. Hivyo ni matarajio ya Watanzania wa pande zote mbili za Muungano kuwa uteuzi wa mabalozi utazingatia uwiano wa nchi hizi mbili. Ila jambo la kusikitisha ni kwamba, kati ya balozi 34 za Tanzania nje ya nchi kwa sasa, ni mabalozi wanne tu sawa na asilimia 1.2 ndiyo wanatoka Tanzania Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashangazwa na kushitushwa zaidi kwamba, hata baada ya kustaafu kwa aliyekuwa balozi wetu nchini Sweden, Balozi Mohamed Mwinyi Mzale aliyekuwa anatokea Zanzibar, nafasi yake ilizibwa na balozi mpya kutoka Tanzania Bara badala ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua kama alikosekana mtu kutoka Zanzibar mwenye sifa na uzoefu wa kitaaluma ambaye angeweza kujaza nafasi hiyo. Ukiachilia mbali uteuzi wa kibaguzi wa mabalozi, bado kuna malalamiko mengi kutoka Zanzibar kuhusu wafanyakazi wa Wizara ambapo inadaiwa kwamba wengi wa waajiriwa wa Wizara na mabalozi mbalimbali wanatoka upande mmoja wa Muungano.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kutoa kauli juu ya uwiano wa uteuzi wa mabalozi kutoka katika pande zote mbili za Muungano na juu ya uwiano wa wafanyakazi wa Wizara na Balozi mbalimbali nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa matumizi mabaya ya fedha kwa ajili ya safari za viongozi Wakuu wa Serikali nje ya nchi: Katika hotuba yangu mwaka jana kuhusu bajeti ya Wizara hii, nilionesha jinsi ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikihoji suala la misafara ya viongozi wa kitaifa kuwa mikubwa kutokana na kuambatana na watu wengi ambao wengine wanakuwa hawana hata majukumu ya msingi ya kufanya kwenye ziara hizo.

Aidha, nilionyesha jinsi safari hizo zilivyogharimu taifa na kuwaongezea mzigo walipa kodi wa taifa hili kwa kuwa mwisho wa siku wananchi ndiyo wanaowajibika kulipia malazi na starehe za viongozi hao kupitia kodi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hali hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani ilipendekeza kuwa Rais wa nchi awe anatuma wasaidizi wake kwenye baadhi ya ziara za nje kama wanavyofanya viongozi wengine wa nchi jirani ili yeye awe na jukumu la kushiriki kwenye ziara rasmi za kiserikali *(state visits)* na mikutano maalum ya Kimataifa kama UN na AU.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma hasa safari za nje zenye misafara mikubwa ya maafisa wa Serikali, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarudia tena kuitaka Serikali kutengeneza kanuni za kuthibiti idadi ya maafisa na watu ambao watakuwa wakiambatana na Rais kwenye ziara za nje. Idadi ya wajumbe kwenye misafara iwe wazi na ijulikane. Aidha, kanuni hizo ziweke ukomo *(ceiling)* wa bajeti ya safari za Rais nje ya nchi.

Mheshimwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kuanzishwa kwa kanuni zitakazoweka utaratibu wa safari za viongozi ikiwa ni pamoja na kuweka ukomo wa bajeti wa safari za viongozi kwa sababu safari za viongozi zimekuwa ndiyo kichaka cha wizi wa fedha za umma. *(Makofi)*

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, imekuwa ikipewa fedha zaidi ya bajeti iliyopangwa kwa ajili ya safari za viongozi. Kwa mfano, taarifa ya Waziri iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum (Mb.) kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2013/14 Julai, 2013 mpaka Aprili, 2014) inasema kwamba; baadhi ya mafungu yalipokea mgao zaidi ya asilimia 100 ya bajeti iliyopitishwa na Bunge kutokana na mahitaji muhimu yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa bajeti. Miongoni mwa mafungu hayo ni pamoja na Fungu 34, *Ministry of Foreign Affairs and International Cooperation* ambayo iliongezewa 116% kugharimia safari za viongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Waziri wa Fedha, matumizi yaliyozidi kiwango *(over expenditure)* yalikuwa ni kwa ajili ya kugharimia safari za viongozi nje ya nchi. Hatuongezi fedha katika Wizara nyingine zenye athari

ya moja kwa moja kwa wananchi kama vile Maji, Kilimo, Nishati na kadhalika, lakini tunaongeza fedha kwa viongozi kusafiri. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua kama safari za viongozi nje ya nchi ndiyo vipaumbele vya bajeti katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahusiano ya Tanzania na Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu: Mnamo tarehe 4/9/2013 mwandishi wa BBC katika kipindi cha Mtazamo wa Afrika *(Focus on Africa)* Bwana, Paul Bakibinga, alitangaza mahojiano yaliyofanyika kati ya mwandishi wa BBC Bi. Catherine Byaruhanga ambaye ni Mganda na Mheshimiwa Bernard Membe, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Mahojiano yalikuwa yanahusu migogoro na vita inayoendelea nchini Kongo *(DRC)*.

Katika mahojiano hayo, Mheshimiwa Membe alikaririwa akijibu swali la mwandishi wa BBC lililouliza nanukuu:- Sasa naanza na swali; "*Some people say that the rude tension between your two countries is the DRC, the fact that now you have troops there and Rwanda is accused of supporting M23 something that Rwanda denies but many people belive that, that is real at the heart of tensions between your countries, are you on opposing sides now?*"Hilo swali.

Kwa kifupi mwandishi wa BBC alimuuliza Mheshimiwa Membe kwamba, tatizo lililopo kati yetu na nchi ya Rwanda ni migogoro ya kiusalama na kimaslahi iliyopo nchini Kongo *(DRC)*. Katika majibu yake Mheshimiwa Membe alisema yafuatayo:- Nanukuu: "*Because what is happening in DRC is that you have two protagonists in Rwanda fighting in the DRC. If you use the economic jargon, you export a civil war in another country. You have exported the civil war because there are two main groups of Rwanda fighting in the DRC*"

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tafsiri ya kawaida Mheshimiwa Membe anasema kwamba, nchi ya Rwanda imesafirisha vita nchini Kongo *(DRC)* kwa maana ya makundi mawili hasimu ya chini ya Rwanda yanapigana ndani ya ardhi ya Kongo yaani Kundi la Waasi wa Kongo M23 na Kundi la Waasi wa Rwanda *FDLR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa majibu haya ni wazi Mheshimiwa Membe siyo tu kwamba, anaendelea kuchochea vita inayoendelea nchini Kongo lakini ndiyo chanzo kikubwa cha kudorora kwa mahusiano mazuri yaliyokuwepo kati yetu na nchi jirani ya Rwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka waziri Membe alieleze Bunge hili ni kwanini anaamini kuwa Waasi wa Kundi la M23 wa Kongo ni Wanyarwanda wakati nchi ya Kongo pamoja na Umoja wa Mataifa hawajawahi kusema kwamba, Kundi la Waasi wa M23 ni Wanyarwanda bali muda wote wameamini kuwa ni Waasi wa Kongo yenyewe. Kama hiyo haitoshi, kungekuwa na haja gani ya kuwa na mazungumzo ya upatanishi ya

Kampala kati ya Serikali ya Kongo na Waasi wa M23 kama wangekuwa ni Wanyarwanda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mawazo potofu ya Waziri na inadhihirisha wazi kuwa uwezo wake ni mdogo katika mambo ya kidiplomasia na Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji Serikali kwa kutambua uchochezi huu kwa nini huyu Waziri mzigo hajawabishwa hadi sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kundi la Waasi wa FDLR baada ya kusababisha mauaji ya Kimbari ya mwaka 1994 nchini Rwanda walikimbilia Kongo. Kiongozi wao wa kisiasa Bwana Murwanashyaka yuko gerezani nchini Ujerumani, na kuna hati ya kukamatwa kwa kiongozi wao wa kijeshi *(Arrest Warrant of INTERPOL and ICC)* kwa kuongoza kundi la wauaji. Kundi la Waasi wa FDLR siyo chama cha kisiasa bali ni kundi la wauaji *(Criminal Organization)* ambalo linatakiwa lilaaniwe na kila binadamu.

Hivi karibuni kuna taarifa kwamba Waziri Mkuu wa zamani wa Rwanda ambaye kwa sasa amepewa hifadhi nchini Ubeligiji kwa kukimbia nchini kwake bwana Faustine Twagiramungu ambaye ameungana rasmi na kundi la wauaji wa FDLR lililosababisha mauaji nchini Rwanda alikuja Tanzania akiongozana na viongozi wawili wa kundi hilo haramu ambao ni Kanali Hamad na Luteni Kanali Wilson, kwa mwaliko wa Serikali na kuna taarifa kuwa walikutana na viongozi waandamizi wa Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku chache baada ya ugeni huu wa Serikali kuondoka, Bwana Faustine Twagiramungu alikaririwa akiwa nchini Ufaransa mji wa Leone, kwenye mkutano wa chama chake akisema kwamba ametoka nchini Tanzania na amefanya mazungumzo ya kimkakati *(Strategic Negotiations)* na Serikali ya Tanzania na kwamba sasa wako tayari kuchukua dola nchini Rwanda hata kwa kutumia mtutu wa bunduki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya taarifa hizi kuenea katika vyombo vya habari vya kimataifa, kama Waziri Kivuli wa Wizara hii nilitoa taarifa kwa vyombo vya Habari nikiitaka Serikali kumtaka Faustine Twagiramungu kukanusha taarifa yake ya kukutana na viongozi waandamizi wa Serikali ya Tanzania na kufanya nao kikao cha kimkakati. Badala yake Serikali ilikanusha taarifa hiyo ya kukutana na Twagiramungu bila ya kumtaka afute kauli hiyo na kuomba radhi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu haya yanadhihirisha wazi kuwa kigugumizi hiki cha Serikali kutomtaka Twagiramungu kukanusha taarifa hizi za uchochezi ambao una athari kubwa katika mahusiano yetu na nchi jirani ya Rwanda kama Serikali haikushiriki katika mipango hiyo na wauaji wa *FDLR* kwa kuwa na kikao cha kimkakati kwa mujibu wa Twagiramungu, ni kwa nini Serikali haikutaka kumtaka akanushe taarifa hizo zilizosambaa duniani kote?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kwa nini Serikali ilimkaribisha Twagiramungu nchini, mtu ambaye ameungana na waasisi wa *FDLR* ambao walisababisha mauaji nchini Rwanda?

Pili, kambi Rasmi ya upinzani inataka kujua, wakati dunia ikijua kuwa Serikali ya Tanzania ilimkaribisha Twagiramungu nchini na kukutana na viongozi waandamizi wa Serikali, kwa nini Serikali mpaka leo iko kimya na wala haijatamka Twagiramungu kukanusha maneno aliyotoa akiwa Ufaransa ambayo yameendelea kuchochea kuwepo kwa mahusiano mabovu kati ya nchi yetu na Rwanda.

Tatu, baada ya Tanzania kupeleka majeshi yetu Kongo kwa lengo la kurudisha amani na kupambana na kundi la Waasi wa M23, moja ya Maazimio ya Addis *(The Addis Declaration)* ni kuwa baada ya kutokomeza M23 kinachofuata ni kutokomeza wauaji wa *FDLR*. Je, jitihada zitafanikiwa vipi ikiwa Tanzania imetengeneza urafiki na wauaji na kushiriki kuwasaidia katika mikakati yao ya kuitawala Rwanda kwa mtutu wa Bunduki?

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri Serikali kuwa ni vyema ikaheshimu mamlaka ya nchi zingine iliyowekwa na mikataba ya Kimataifa kama *Vienna Convention* na kwa maana hiyo Serikali yetu iache kushirikiana kwa namna yoyote ile na makundi haramu kama *FDLR* yenye nia ovu ya kupindua Serikali iliyochaguliwa kwa demokrasia na wananchi wa Rwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa mataifa mbalimbali wanaoishi na kufanya kazi nje ya nchi zao huwa wanakuwa na mchango hususani wa kiuchumi katika nchi zao za asili. Kwa kuthamini michango hii ya wananchi wanaoishi nje, Balozi za nchi hizo zinashirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje ya nchi hizo kufanya sensa ya watu wanaoishi ughaibuni na kuainisha vipato vyao na kwa maana hiyo kuweza kuanzisha kanzidata yaani *data base* ya mchango wa kiuchumi katika nchi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uzoefu wangu sijawahi kusikia Waziri wa Mambo ya Nje akitoa taarifa ya mchango wa kiuchumi unaofanywa na Watanzania waoishi na kufanya kazi nje ya nchi. Kwa sababu hiyo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ningependa kujua kama Serikali ina

utaratibu wa kushughulika na Watanzania walioko nje kwa maana ya idadi yao, kazi wanazofanya, vipato vyao ili kuweza kujua mchango wao katika kujenga uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho: Kama ilivyoelezwa awali ushirikiano wa Kimataifa katika zama hizi za sayansi na teknolojia unajengwa zaidi katika msingi wa diplomasia ya uchumi kuliko diplomasia ya kisiasa ambayo ilikuwa na nguvu zaidi katika enzi za vita baridi. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza na kushauri kwamba Serikali kuanzia sasa iwe inatenga bajeti maalumu kwa ajili ya kukuza na kuendeleza diplomasia ya uchumi. Katika mukhtadha huo wa kukuza na kuendeleza uchumi ni lazima uteuzi wa Mabalozi uzingatie weledi na uzoefu wa kutafuta fursa za kiuchumi katika nchi wanazotuwakilisha.

Aidha ili kutimiza azma hiyo ni lazima pia Balozi zijenge utamaduni wa kutathimini fedha za umma kwa kuzitunza na kuzitumia vyema katika kufikia malengo hayo. Kitendo cha Balozi zetu kupata hati chafu na zenye mashaka kunatupa wasiwasi kama Mabalozi hao wanaweza kuleta tija katika uwakilishi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba ushirikiano na mataifa mengine katika nyanja mbalimbali utafanikiwa tu iwapo kuna mahusiano mazuri kati ya viongozi na wananchi wa mataifa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua pia kwamba kauli za viongozi nyakati nyingine zinaweza kuchochea uvunjifu wa amani kwa mataifa husika kutokana na…

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani naomba kuwasilisha na naomba taarifa hii kama ilivyo iingie kwenye Hansard. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wenje, tunakushukuru sana kwa hotuba yako kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. Hotuba hii imetetea sana Rwanda sijui ni kwa nini! *(Kicheko)*

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013)*

## 1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili, kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzania kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka 2013/2014 na makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, natoa pia shukrani na pongezi kwa viongozi wakuu wa vyama vya NCCR-Mageuzi, CUF na CHADEMA kwa busara zao kuona umuhimu wa kuunganisha vyama hivi katika kuunda Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na katika kuunda Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) ndani na nje ya Bunge ili kuharakisha ukombozi wa Taifa hili katika nyanja mbalimbali. Kwa namna ya pekee, namshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mhe. Freeman Aikaeli Mbowe (Mb) kwa kuendelea kuniamini na kuniacha katika nafasi ya Msemaji Mkuu na Waziri Kivuli katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Ninamwahidi utendaji uliotukuka katika utekelezaji wa majukumu yangu.

## 2. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA KWA MWAKA 2013/2014

Mheshimiwa Spika, kutokana na udhaifu mwingi wa kiutendaji na kiuwajibikaji na mapugufu sugu katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kwa miaka mitatu mfululizo, imekuwa ikitoa ushauri kwa Serikali kufanya mambo kadhaa ili kuboresha utendaji na ufanisi katika Wizara hii. Baadhi ya masuala tuliyoitaka Serikali kufanya ni pamoja na yafuatayo:-

1. Kutoa taarifa ya namna kila ubalozi ulivyotekeleza sera ya Diplomasia ya uchumi kwa kuzingatia kwamba balozi nyingi ziko hoi kifedha kiasi cha kwamba waambata wa kiuchumi wanakosa hata fedha za kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa ajili ya upelelezi wa masuala ya kiuchumi.

2. Kuziwezesha balozi zetu nje kwa kuzitengea fedha za kutosha ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi

3. Kufanya uchunguzi kuhusu tuhuma za balozi zetu nchini China, na Uingereza kutoa hati za kusafiria kwa mataifa mengine hasa ya Afrika Magharibi ili kubaini ukweli na kuliondolea taifa aibu kutokana na tuhuma hizi.

4. Kupeleka mwambata wa kiuchumi (economic attaché) nchini China ili kufuatilia fursa mbalimbali za kiuchumi katika kutekeleza diplomasia ya uchumi kutokana na mahusiano makubwa ya kibiashara kati ya nchi yetu na China.

5. Kuwawekea zuio wahusika wa kashfa ya rada kuwa viongozi wa shughuli za kiserekali ili walau kuonesha uwajibikaji wa kimaadili (moral accountability) baada ya kushindwa kuwawajibisha kisheria, ili kuondoa dhana iliyojengeka miongoni mwa jamii kwamba dola imetekwa na mafisadi.

6. Kueleza bayana faida za kiuchumi tunazopata kama taifa kwa kushirikiana na jumuiya mbalimbali za kimataifa ili kuthibitisha kwamba mashirikiano hayo hayatumiki kupora rasilimali za nchi yetu kwa hila ya "uwekezaji"

7. Kutoa idadi ya majengo ya balozi zetu nje (nyumba za mabalozi, nyumba za maafisa wa balozi na ofisi za balozi) kwa mchanganuo wa idadi ya nyumba katika nchi na kama nyumba hizo zina hati miliki au la.

### 2.1. Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2013/2014, zilitengwa shilingi bilioni 30 kwa ajili hiyo. Hata hivyo kiasi cha fedha kilichotolewa na hazina hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2014 ni shilingi bilioni 6.5 tu sawa na asilimia 21.6 tu. Hii ina maana kwamba bajeti ya maendeleo kwa Wizara hii haikutekelezwa kwa asilimia 78.3.

Mheshimiwa Spika, endapo kiasi hiki cha fedha ambazo hazikutolewa kingekuwa kimetolewa kwa wakati, malalamiko ya muda mrefu ya uchakavu wa balozi zetu na ukosefu wa magari kwa mabalozi wetu ungekuwa umepungua sana au kumalizika kabisa. Jambo la kushangaza ni kwamba mwaka huu wa fedha 2014/2015 zimetengwa shilingi bilioni 30 kwa ajili ya bajeti ya Maendeleo kwa Wizara ya Mambo ya Nje kiwango kilekile kilichotengwa mwaka jana na kwa miradi ile ile.

Mheshimiwa Spika, kama fedha ya maendeleo inatolewa kwa asilimia kidogo namna hiyo licha ya Serikali kuwa na taarifa za uduni wa balozi zetu nje ya nchi ni kwa namna gani mabalozi wetu wanaweza kutekeleza dipolamasia ya uchumi ambayo inategemea fedha za maendeleo na ambayo tumekuwa tukiipigania kwa miaka mingi? Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa makini inapofanya makisio ya bajeti na pia hazina itoe fedha kama zilivyopitishwa na Bunge.

## 3. SERA YA UTANGAMANO (INTERGRATION POLICY) NA USHIRIKI WA TANZANIA KATIKA MAHUSIANO YA KIKANDA

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi mwanachama wa Jumuiya mbalimbali za kikanda katika bara la Afrika, mathalani SADC na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Hata hivyo mpaka sasa kama nchi hatuna mwongozo wa kisera na kisheria ambao unatuongoza katika mahusiano hayo. Kwa maneno mengine nchi haina Sera ya Utangamano (Intergration Policy)

Mheshimiwa Spika, Jumuiya za kikanda pamoja na mahusiano mazuri ya kidiplomasia ni fursa muhimu za kiuchumi katika nchi yetu. Katika Mchango wake katika bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mhe. Freeman Aikaeli Mbowe, alibainisha upungufu huu mkubwa wa kisera ambao unaligharimu taifa kwa kuwa nchi yetu inajiunga na jumuiya mbalimbali za kikanda bila kuwa na ajenda maalumu ya kisera juu ya nini tunachokihitaji na nini tutapata kama taifa tunapojiunga na Jumuiya hizo. Katika mchango wake huo, KUB aliitaka serikali kuwa na sera na mipango katika uhusiano wa kikanda ili kujua namna ya kutumia vizuri fursa za kiuchumi katika mahusiano ya nchi washirika hasa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, wakati akifanya majumuisho ya hoja yake hapa Bungeni Waziri wa Afrika Mashariki alisema kuwa sera ya Afrika Mashariki au sera ya kikanda ipo katika mchakato wa kukamilika chini ya Wizara ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshangazwa na Serikali kukosa sera mahsusi inayoratibu mahusiano yetu kama nchi katika Jumuiya ambazo sisi ni wanachama.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya haraka kukamilisha sera hiyo na inashauri kuwa wabunge kama wadau wahusishwe mapema na pia baadaye sera hiyo itungiwe sheria Bunge liweze kuisimamia Serikali katika kutekeleza sera hiyo.

## 4. BALAOZI ZA TANZANIA NJE YA NCHI

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto za kiuchumi na kiusalama, mataifa mbalimbali duniani yanatafuta kushirikiana ili kukabiliana na changamoto hizo. Licha ya ushirikiano katika masuala ya siasa na huduma za jamii, msingi mkubwa wa msukumo wa ushirikiano wa mataifa mbalimbali kupitia balozi zao umekuwa na malengo ya kiuchumi zaidi. Hivyo, kwa msingi huo huo, Tanzania inatakiwa kutumia balozi zake kimkakati ili ziweze kutumia fursa mbalmbali za kiuchumi katika nchi inazotuwakilisha katika kuleta mageuzi ya kiuchumi katika sekta za biashara, uwekezaji, utalii n.k.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kwamba; Kamwe Tanzania iondokane na fikra za kutegemea misaada pekee kupitia balozi zetu. Ikiwa tunapata misaada, iwe ni sehemu ndogo tu kati ya mapato makubwa tutakayokuwa tunapata kutokana na biasahara, utalii, uwekezaji katika sekta mbalimbali na fursa nyingine ambazo balozi zetu zitakuwa zimetafuta.

### 1.1. Ukuzaji na Uendelezaji wa Diplomasia ya Uchumi

Mheshimiwa Spika, balozi zetu nyingi za Tanzania nje ya nchi zilianzishwa kabla dhana ya diplomasia ya uchumi haijaenea duniani. Dhana ya diplomasia ya uchumi ilianza kusambaa kwa kasi kutokana na msukumo wa utandawazi ulioambatana na mageuzi ya kiuchumi duniani. Hivyo, kabla ya kuanza kwa harakati za diplomasia ya uchumi, balozi nyingi zilianzishwa kwa misukumo au malengo ya kisiasa zaidi (political diplomacy) kuliko masuala ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kumalizika kwa vita baridi baina ya Kambi Mbili Kuu duniani zenye milengo ya siasa za Kijamaa na Kibepari, na kutokana na Ujamaa kushindwa katika vita hiyo, mahusiano katika ya nchi zilizokuwa na siasa za kijamaa ambayo yalikuwa ni ya kisiasa zaidi, yalianza kubadilika taratibu na kuanza kuwa ya kiuchumi zaidi. Hii ni kwa sababu mfumo wa kiuchumi na kisiasa uliokuwa unatawala dunia ulikuwa ni ubepari (Capitalism) baada ya ujamaa (Socialism) kusambaratika.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtanzamo kwamba Serikali inapoteua mabalozi kwenda nchi mbalimbali duniani, ifanye hivyo kimkakati. Na mkakati namba moja, uwe ni mkakati wa kukuza na kuedeleza diplomasia ya uchumi ndipo mambo mengine yafuate. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kwamba ikiwa hakuna fursa za kiuchumi tutakazopata kama taifa kwa kuwa na ubalozi katika nchi fulani, ni bora ubalozi huo usianzishwe. Hivyo tunaitaka Serikali kufanya tathmini juu ya faida halisi za kiuchumi tunazopata kutoka kila nchi tuliyoweka Ubalozi. Taarifa ya tathmini hiyo itumike kama dira ya kufanya uamuzi kama bado kuna haja ya kuendelea na ubalozi huo au kuufunga.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo pia kwamba, kama mkakati wetu katika balozi utakuwa ni wa kiuchumi zaidi, basi uteuzi wa mabalozi ulenge kupunguza gharama za uendeshaji wa balozi (administrative costs) na kuchuma kwa wingi iwezekanavyo matunda ya kiuchumi (maximization of opportunities) katika balozi zetu. Hii ni pamoja na kupunguza idadi ya mabalozi ili watakaobaki wawe wanahudumu katika nchi zaidi ya moja zinazopakana. Mathalani katika nchi za Rwanda na Burundi, Tanzania ina balozi katika nchi zote hizo. Kijiografia, nchi hizi ni ndogo na zinapakana. Hivyo

ingekuwa nafuu zaidi, kwa maana ya gharama za uendeshaji kuwa na balozi mmoja katika nchi mojawapo atakayehudumia nchi zote mbili.

Mheshimiwa Spika, ni katika muktadha huohuo Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji ni kwa nini tuwe na mrundikano wa mabalozi katika ukanda mmoja kama ilivyo sasa kwa balozi zetu za Maputo, Harare, Lusaka, Kinshasa, Lilongwe na Pretoria? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba; badala ya kuwa na mabalozi sita katika ukanda huu, tungekua na mabalozi wawili tu ambao wangeweza kuhudumia hizi nchi zote kwa sababu ziko kwenye ukanda mmoja.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kutumia mfano wa wa ubalozi wetu nchini sweden ambao unahudumia nchi nyingine za Scandinavia kama vile Denmark, Norway na Finland. Ushauri huu unatokana na ukweli kwamba tunapata faida za kiuchumi zaidi kutoka katika nchi hizo kupitia fursa mbalimbali ikiwemo misaada licha ya kuwa na ubalozi mmoja tu katika ukanda huo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imeshawishika kwamba hii itakua ni njia nzuri zaidi ya kupunguza utitiri wa diplomasia za kisiasa (political diplomacy) ambazo kwa sasa hazina nguvu tena kama zamani wakati wa vita baridi na badala yake tuweke balozi zetu kimkakati kwenye maeneo yenye tija kubwa zaidi kwetu kiuchumi ili tuweze kuwa na ushindani katika dunia hii ya leo ambapo uchumi imara na endelevu ndio kigezo kikubwa cha taifa lenye nguvu duniani.

Lakini Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitika kwamba licha ya wazo hili la diplomasia ya uchumi kuwa muhimu na lenye tija kubwa kwa taifa bado Serikali haijaona umuhimu wa kutenga fedha maalum kwa ajili ya utekelezaji wa diplomasia ya uchumi. Nasema hivi kwa sababu katika bajeti ya maendeleo ya Wizara hii shilingi bilioni 30 iliyotengwa mwaka huu wa fedha 2014/2014 haijaonyesha mchanganuo wa fedha iliyotengwa kwa ajili ya diplomasia ya uchumi. Hivyo Waziri alieleze Bunge kuwa Serikali ina mpango gani na Diplomasia ya uchumi ikiwa haijatenga bajeti ya kushughulikia suala hilo.

### 1.2. Uteuzi wa Mabalozi Usiozingatia Sifa

Mheshimiwa Spika, uteuzi wa mabalozi unatakiwa kuzingatia sifa za anayeteuliwa sambamba na malengo au maslahi Taifa letu katika nchi ambayo anatumwa kuiwakilisha nchi yetu. Lakini jambo la ajabu ni kwamba hapa kwetu uteuzi wa mabalozi wetu unafanywa kisiasa na kirafiki mara nyingi kwa kutafutiana fursa tu baada ya wateuliwa kuwa wameshindwa chaguzi mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu au udhaifu huo, mabalozi wetu wamejikuta hawajui ipasavyo wajibu wao. Licha ya ukweli kwamba mabalozi wetu wanatakiwa kulisaidia taifa kutoa taarifa muhimu kuhusu wawekezaji na wageni mbalimbali wanaokuja kuwekeza hapa nchini, jambo hili limekuwa halifanyiki kwa weledi ndio maana tunashuhudia makampuni mbalimbali yakija kuwekeza nchini bila mitaji ya kutosha wala teknolojia lakini yamepewa fursa za kuwekeza kwenye sekta nyeti nchini. Laiti mabalozi wangekuwa wanafanya kazi kwa ufanisi, kitendo cha wawekezaji wababaishaji kuja bila mitaji, na kupewa ardhi ambayo wanaitumia ardhi hiyo kama dhamana benki ili kupata mitaji ya uwekezaji kisingekuwepo kabisa.

Mheshimiwa Spika, balozi nyingi zimeshindwa hata kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo katika nchi yetu na kwa maana hiyo tunapoteza fursa nyingi za kupata watalii kutoka katika nchi mbalimbali. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kubadili mfumo wa ubalozi kwa kuainisha fursa za kiuchumi ambazo taifa linataka kutoka katika nchi inayopeleka balozi, na balozi huyo atakiwe kuwa na sifa za kitaaluma na uzoefu wa kuweza kufuatilia na kuhakikisha kuwa fursa hizo zinapatikana na zinatoa faida zilizokusudiwa.

**1.3. Matumizi Mabaya ya Fedha katika Balozi**

Mheshimiwa Spika, kuna mwenendo mbaya wa matumizi ya fedha za umma katika balozi zetu. Licha ya malalamiko ya kila mwaka kwamba bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje ni kidogo kiasi kwamba balozi nyingi za Tanzania nje ya nchi ziko hoi kifedha, bado kumekuwa hakuna nidhamu ya matumizi na utunzaji wa fedha katika balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2013 inaonesha kwamba walau balozi tatu za Tanzania nje, zilipata hati chafu na hati zenye mashaka katika matumizi na utunzaji wa fedha. Ubalozi uliopata hati chafu ni ubalozi wa Tanzania Muscat. Hii ni kwa sababu taarifa za fedha za ubalozi huo zilionesha kuwa bakaa ya mwisho ya fedha ilikuwa ni shilingi 150,681,699 badala ya shilingi 639,874,314 kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha. Kwa mujibu wa CAG, hitilafu hii ilitokana na kutoonyesha mapokezi ya fedha shilingi 97,065,176 na kujumuisha hasara ya ambayo haikuwa na mchanganuo wa kuthibitisa uhalali wake ya shilingi 392,127,439 iliyotokana na kubadili fedha za kigeni na hivyo kupelekea kiasi hicho cha fedha kuonyeshwa pungufu kwa shilingi 489,192,615.

Mheshimiwa Spika, udhaifu mwingine wa ubalozi huo wa Muscat katika utunzaji wa fedha ni makusanyo ya mapato ya ubalozi ya shilingi 108,108,753 kutopelekwa benki. Kwa mujibu wa CAG, ubalozi huo ulikusanya kiasi cha

shilingi 564,194,173 ambapo kati ya kiasi hicho ni shilingi 456,085,421tu ndizo zilizopelekwa benki na shilingi 108,108,753 hazikupelekwa benki. Aidha ubalozi wa Muscat haikuandaa taarifa za usuluhusho wa benki jambo ambalo ni kinyume na kanuni ya 162 ya fedha za umma ya mwaka 200.

Mheshimiwa Spika, balozi nyingine zilizopata hati zenye mashaka ni balozi za Tanzania za Kinshasa (Congo DRC) na Kampala (Uganda). Katika ubalozi wa wa Tanzania katika nchi ya kidemokrasia ya Congo kulikuwa na matumizi ya shilingi 31,817,025 ikiwa ni malipo ya kabla ya kupata huduma ya pango kama bakaa iliyokuwepo mwanzoni mwa mwaka. Hata hivyo, hakukuwa na nyaraka zozote za uthibitisho juu ya uhalali na usahihi wa matumizi hayo. Hali kadhalika katika ubalozi wetu nchini Unganda, kulikuwa na tofauti ya shilingi 48,893,168 katika bakaa ya mwisho wa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili kuwa imechukua hatua gani kwa balozi zilizopata hati chafu na hati zenye mashaka katika masuala ya matumizi na utunzaji fedha? Seirikali pia ieleze imeweka mikakati gani ya kudhibiti matumizi mabaya ya fedha katika balozi zetu.

**1.4. Ukarabati wa Jengo la Ubalozi wa Tanzania Washington – Marekani**

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu bajeti ya Wizara hii mwaka jana 2013/2014, tuliishauri serikali kulifanyia ukarabati jengo letu la Ubalozi la zamani lilipo Washington nchi Marekani kuliko kuliacha hivi hivi kuendelea kuchakaa. Ukarabati huo ungekua na tija ya kiuchumi maana hilo jengo linaweza kupangishwa na likawa moja wapo ya vyanzo vya mapato. Gharama ya jumla ya ukarabati wa jengo hilo inakadiriwa kuwa dola za kimerekani millioni 1.5. Lakini jambo la ajabu ni kwamba Serikali imelitelekeza jengo hilo na kuhamia kwenye jengo jipya. Hivi ni kweli Serikali imekosa kabiasa dola za kimarekani milioni 1.5 kukarabati jengo hilo ili liwe chanzo cha mapato?

Mheshimiwa Spika, kwa takriban miaka mitatu mfululizo Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikiikumbusha Serikali kuhusu jengo hili lakini Serikali haifanyi chochote. Hivi hii ni Serikali gani inayojiita sikivu lakini haitekelezi ushauri mzuri inayopewa?

**1.5. Uwiano wa Mabalozi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar**

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni Wizara inayoshughulika na mambo ya Muungano. Hivyo ni matarajio ya

watanzania wa pande zote mbili za Muungano kuwa uteuzi wa mabalozi utazingatia uwiano katika ya nchi hizi mbili. Ila jambo la kusikitisha ni kwamba kati ya balozi 34 za Tananzania nje ya nchi kwa sasa, ni mabalozi wanne (4) tu sawa na asilikia 1.2 ndio wanatoka Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilishangazwa na kushtushwa zaidi kwamba hata baada ya kifo cha aliyekuwa balozi wetu nchini Sweden, marehemu Mohamed Mwinyi Mzali aliyekuwa anatokea Zanzibar, nafasi yake ilizibwa na balozi mpya kutoka Tanzania bara badala ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua kama alikosekana mtu kutoka Zanzibar mwenye sifa na uzoefu wa kitaaluma ambae angeweza kujaza nafasi hiyo. Ukiachilia mbali uteuzi wa mabalozi wa kibaguzi, bado kuna malalamiko mengi kutoka zanzibar kuhusu wafanya kazi wa wizara ambapo inadaiwa kwamba wengi wa waajiriwa wa wizara na balozi mbalimbali wanatoka upande mmoja wa Muungano. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kauli juu ya uwiano wa uteuzi wa mabalozi kutoka katika pande zote mbili za Muungano na juu ya uwiano wa wafanyakazi wa wizara na balozi mbalimbali nje ya nchi.

## 2. UDHIBITI WA MATUMIZI MABAYA YA FEDHA KWA AJILI YA SAFARI ZA VIONGOZI WAKUU WA SERIKALI NJE YA NCHI

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu mwaka jana kuhusu bajeti ya wizara hii, nilionyesha jinsi ambayo Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikihoji suala la misafara ya Viongozi wa kitaifa kuwa mikubwa kutokana na kuambatana na watu wengi ambao wengine wanakuwa hawana hata majukumu ya msingi ya kufanya kwenye ziara hizo. Aidha, nilionyesha jinsi safari hizo zinavyoligharimu taifa na kuwaongezea mzigo walipakodi wa taifa hili kwa kuwa mwisho wa siku wananchi ndio wanaowajibika kulipia malazi na starehe za viongozi hao kupitia kodi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani ilipendekeza kuwa Rais wa nchi awe anatuma wasaidizi wake kwenye baadhi ya ziara za nje kama wanavyofanya viongozi wengine wa nchi jirani ili yeye awe na jukumu la kushiriki kwenye ziara rasmi za kiserikali '*State Visits*' na mikutano maalum ya Kimataifa kama UN na AU.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma hasa safari za nje zenye misafara mikubwa ya maafisa wa Serikali, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarudia tena kuitaka Serikali kutengeneza kanuni za kuthibiti idadi ya maafisa na watu ambao watakuwa wakiambatana na Rais kwenye ziara za nje (idadi ya wajumbe kwenye misafara iwe wazi na ijulikane. Aidha, kanuni hizo ziweke ukomo (ceiling) wa bajeti ya safari za Rais Nje ya Nchi.

Mheshimwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kuanzishwa kwa kanuni zitakazoweka utaratibu wa safari za viongozi ikiwa ni pamoja na kuweka ukomo wa bajeti wa safari za viongozi kwa sababu safari za viongozi zimekuwa ndio kichaka cha wizi wa fedha za umma. Wizara ya mambo ya nje imekuwa ikipewa fedha zaidi ya bajeti iliyopangwa kwa ajili ya safari za viongozi. Kwa mfano taarifa ya waziri iliyowasilishwa na waziri wa fedha Mhe Saada Mkuya Salum(Mb) kwa kamati ya bunge ya bajeti kuhusu utekelezaji wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2013/14 (Julai 2013-April 2014) inasema kwamba "… *baadhi ya mafungu yalipokea mgao zaidi ya asilimia 100 ya bajeti iliyopitishwa na bunge kutokana na mahitaji muhimu yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa bajeti, Miongoni mwa mafungu hayo ni pamoja na fungu 34 Ministry of Foregn Affairs and International Cooperation (116%) kugharimia safari za viongozi*".

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa waziri wa Fedha, matumizi yaliyozidi kiwango (over expenditure) yalikuwa ni kwa ajili ya kugharimia safari za viongozi nje ya nchi. Hatuongezi fedha katika wizara nyingine zenye athari ya moja kwa moja kwa wananchi kama vile maji, kilimo, nishati nk. Lakini tunaongeza fedha kwa viongozi kusafiri. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua kama Safari za Viongozi nje ya nchi ndio vipaumbele vya bajeti katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

**3. MAHUSIANO YA TANZANIA NA NCHI ZA UKANDA WA MAZIWA MAKUU.**

Mheshimiwa Spika, Mnamo tarehe 4/9/2013 mwandishi wa BBC katika kipindi cha Mtazamo wa Afrika (Focus on Afrika) bwana Paul Bakibinga alitangaza mahojiano yaliyofanyika kati ya mwandishi wa BBC Bi Catherine Byaruhanga na Mheshimiwa Bernard Membe Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, mahojiano yakiwa yanahusu migogoro na vita inayoendelea nchini Kongo (DRC), Katika mahojiano hayo Mheshimiwa Membe alikaririwa akijibu swali la mwandishi wa BBC lililouliza nanukuu "*Some people say that the rude tension between your two countries is the DRC, the fact that now you have troops there and Rwanda is accused of supporting M23 something that Rwanda denies but many people belive that, that is real at the heart of tensions between your countries, are you on opposing sides now?*" kwa kifupi mwandishi wa BBC alimuuliza Mheshimiwa Membe kwamba tatizo lililopo kati yetu na Nchi ya Rwanda ni migogoro ya kiusalama na kimaslahi iliyopo nchini Kongo (DRC) katika majibu yake Mheshimiwa Membe alisema yafuatayo nanukuu "*Because what is happening in DRC is that you have two protagonist in Rwanda fighting in the DRC. If you use the economic jargon, you export a civil war in another country. You have exported the civil war because there are two main groups of Rwanda fighting in the DRC*"

Mheshimiwa Spika, kwa tafsiri ya kawaida Mheshimiwa Membe anasema kwamba nchi ya Rwanda imesafirisha vita nchini Kongo (DRC) kwa maana ya makundi mawili hasimu ya nchini Rwanda yanapigana ndani ya ardhi ya Kongo (DRC) yaani kundi la waasi wa Kongo M23 na Kundi la waasi wa Rwanda FDLR.

Mheshimiwa Spika, Kwa majibu haya ni wazi kwamba Mheshimiwa Membe si tu kwamba anaendelea kuchochea vita inayoendelea nchini Kongo lakini ndio chanzo kikubwa cha kudorora kwa mahusiano mazuri yaliyokuwepo kati yetu na nchi jirani ya Rwanda.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka waziri Membe alieleze bunge hili ni kwa nini anaamini kuwa waasi wa kundi la M23 wa Kongo (DRC) ni wanya- Rwanda wakati Nchi ya Kongo pamoja na umoja wa mataifa hawajawahi kusema kwamba kundi la waasi wa M23 ni wanya-Rwanda bali muda wote wameamini kuwa ni waasi wa Kongo yenyewe, Kama hiyo haitoshi kungekuwa na haja gani ya kuwa na mazungumzo ya upatanishi ya Kampala kati ya serikali ya Kongo na waasi wa M23 kama wangekuwa ni wanya- Rwanda? Haya ni mawazo potofu ya waziri na inadhihirisha wazi kuwa uwezo wake ni mdogo katika mambo ya kidiplomasia na Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji serikali kwa kutambua uchochezi huu kwa nini huyu waziri mzigo hajawabishwa hadi sasa?

Mheshimiwa Spika, Kundi la waasi wa FDLR baada ya kusababisha mauaji ya Kimbari ya mwaka 1994 nchini Rwanda walikimbilia Kongo, kiongozi wao wa kisiasa Bwana Murwanashyaka yuko gerezani nchini Ujerumani, na kuna hati ya kukamatwa kwa kiongozi wao wa kijeshi (Arrest Warrant of INTERPOL and ICC) kwa kuongoza kundi la wauaji.

Kundi la waasi wa FDLR sio chama cha kisiasa bali ni kundi la wauaji(Criminal Organization) ambayo inatakiwa ilaaniwe na kila binadamu, hivi karibuni kuna taarifa kwamba Waziri Mkuu wa zamani wa Rwanda ambaye kwa sasa amepewa hifadhi nchini Ubeligiji kwa kukimbia nchini kwake bwana Faustin Twagiramungu ambaye ameungana rasmi na kundi la wauaji wa FDLR lililosababisha mauaji nchini Rwanda alikuja Tanzania akiongozana na viongozi wawili wa kundi hilo haramu ambao ni Kanali Hamad na Luteni Kanali Wilson, kwa mwaliko wa serikali na kuna taarifa kuwa walikutana na viongozi waandamizi wa serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Siku chache baada ya ugeni huu wa serikali kuondoka Bwana Faustin Twagiramungu alikaririwa akiwa nchini Ufaransa mji wa Leone Kwenye mkutano wa chama chake akisema kwamba ametoka nchini Tanzania na amefanya mazungumzo ya kimkakati (Strategic

negotiations) na serikali ya Tanzania na kwamba sasa wako tayari kuchukua dola nchini Rwanda hata kwa mtutu wa bunduki.

Mheshimiwa Spika, baada ya taarifa hizi kuenea katika vyombo vya habari vya kimataifa kama waziri kivuli wa wizara hii nilitoa taarifa kwa vyombo vya habari nikiitaka serikali kumtaka Bwana Faustini Twagiramungu kukanusha taarifa yake ya kukutana na viongozi waandamizi wa serikali ya Tanzania na kufanya nao kikao cha kimkakati, badala yake serikali ilikanusha taarifa hiyo ya kukutana na Twagiramungu bila kumtaka afute kauli hiyo na kuomba radhi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Majibu haya yanadhihirisha wazi kuwa kigugumizi hiki cha serikali kutomtaka Twagiramungu kukanusha taarifa hizi za uchochezi ambao unaathari kubwa katika mahusiano yetu na nchi jirani, Kama serikali haikushiriki katika mipango hiyo na wauaji wa FDLR kwa kuwa na kikao cha kimkakati kwa mujibu wa Twagiramungu ni kwa nini serikali haikutaka kumtaka akanushe taarifa hizo zilizosambaa duniani?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kwa nini serikali ilimkaribisha Twagiramungu nchini, mtu ambae ameungana na waasi wa FDLR ambao walisababisha mauaji nchini Rwanda?

Pili, Kambi rasmi ya Upinzani inataka kujua wakati dunia ikijua kuwa serikali ya Tanzania ilimkaribisha Twagiramungu nchini na kukutana na viongozi waandamizi wa serikali kwa nini serikali mpaka leo ipo kimya na wala haijamtaka Twagiramungu kukanusha maneno aliyotoa akiwa Ufaransa ambayo yameendelea kuchochea kuwepo kwa mahusiano mabovu kati ya nchi yetu na Rwanda?

Tatu, baada ya Tanzania kupeleka majeshi yetu Kongo kwa lengo la kurudisha amani na kupambana na kundi la waasi wa M23 moja ya maazimio ya Addis (Addis Declaration) ni kuwa baada ya kutokomeza M23 kinachofuata ni kutokomeza wauaji wa FDLR je jitihada zitafanikiwa vipi ikiwa Tanzania imetengeneza urafiki na wauaji na kushiriki kuwasaidia katika mikakati yao ya kuitawala Rwanda kwa mtutu wa bunduki?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri serikali kuwa ni vyema ikaheshimu mamlaka za nchi zingine iliyowekwa na mikataba ya kimataifa kama Vienna Convention na kwa maana hiyo serikali yetu iache kushirikiana kwa namna yeyote ile na makundi haramu kama FDLR yenye nia ovu ya kupindua serikali iliyochaguliwa kidemokrasia na wananchi wa Rwanda.

## 4. MANUFAA YA KIUCHUMI TANZANIA INAYOPATA KUTOKA KWA WATANZANIA WANAOISHI NA KUFANYA KAZI NJE YA NCHI (DIASPORA REMTTANCE)

Mheshimiwa Spika, wananchi wa mataifa mbalimbali wanaoishi na kufanya kazi nje ya nchi zao huwa wanakuwa na mchango hususan wa kiuchumi katika nchi zao za asili. Kwa kuthamini michango hii ya wananchi wanaoishi nje, balozi za nchi hizo, zikishirikiana na wizara za mambo ya nje ya nchi hizo hufanya sensa ya watu wao wanaoishi ughaibuni na kuainisha vipato vyao na kwa maana hiyo kuweza kuanzisha kanzidata (database) ya mchango wao wa kiuchumi katika nchi zao.

Mheshimiwa Spika, kwa uzoefu wangu, sijawahi kusikia Waziri wa Mambo ya Nje akitoa taarifa ya Mchango wa Kiuchumi unaofanywa na watanzania wanaoishi na kufanya kazi nje ya nchi. Kwa sababu hiyo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ningependa kujua kama Serikali ina utaratibu wa kushughulika na watanzania waliopo nje kwa maana ya idadi yao, kazi wanazozifanya, vipato vyao ili kuweza kujua mchango wao wa katika kujenga uchumi wa Tanzania.

## 5. HITIMISHO:

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa awali, Ushirikiano wa Kimataifa katika zama hizi za sayansi na teknolojia unajengwa zaidi katika msingi wa diplomasia ya Uchumi kuliko diplomasia ya Kisiasa ambayo ilikuwa na nguvu zaidi katika enzi za vita baridi. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza na kushauri kwamba Seriakali kuanzia sasa iwe inatenga bajeti maalum kwa ajili ya kukuza na kuendeleza diplomasia ya Uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika muktadha huo wa kukuza na kuendeleza diplomasia ya uchumi, ni lazima uteuzi wa mabalozi uzingatie weledi na uzoefu wa kutafuta fursa za kiuchumi katika nchi wanazotuwakilisha. Aidha, ili kutimiza azma hiyo, ni lazima pia balozi zijenge utamaduni wa kuthamini fedha za umma kwa kuzitunza na kuzitumia vyema katika kufikia malengo hayo. Kitendo cha balozi zetu kupata hati chafu na zenye mashaka, kunatupa wasiwasi kama mabalozi hao wanaweza kuleta tija katika uwakilishi wao.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba ushirikiano na mataifa mengine katika nyanja mbalimbali utafanikiwa tu iwapo kuna mahusiano mazuri kati ya viongozi na wananchi wa mataifa hayo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua pia kwamba kauli za viongozi nyakati nyingine zinaweza kuchochea uvunjifu wa amani kwa

mataifa husika. Kutokana na kauli ya Faustin Twagiramungu, Tanzania inaonekana kama vile imeungana na kundi la waasi la FDLR jambo ambalo linaweza na tayari kuna viashiria vya mgogoro kati ya Tanzania na Rwanda. Hivyo tunaitaka Serikali imtake huyo Faustin Twagiramungu kuiomba radhi Serikali ya Tanzania na pia Serikali itoe kauli hapa ilimkaribishaje mtu ambaye ni muasi katika nchi yake? Kwa kufanya hivyo, Serikali inaweza kuwaondoa hofu watu wa Rwanda kwamba haihusiki na waasi na pia itawaondoa hofu watanzania kwamba hutuendi kuingia kwenye vita kutokana na sintofahamu hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

Ezekiah Dibogo Wenje (Mb)
**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI NAWAZIRI KIVULI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA**
27 Mei, 2014

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, nina tangazo, naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote ya kwamba kama tulivyokubaliana kwenye *Briefing* kule katika Ukumbi wa Msekwa kuhusiana na tofauti ya Kadi za Bima ya Afya za *Silver, Platinum* na *Gold,* kwamba zile kadi za *Gold* sasa zipo tayari eneo la mapokezi, jengo la utawala. Kwa hiyo kila mmoja wetu akachukue, na wale waliopata *Platinum* na Silver warudishe. Sasa tunaendelea na uchangiaji. Wachangiaji wetu wakaozungumza asubuhi ya leo, ataanza Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Mwanjelwa na Mheshimiwa Suzan Lyimo. Mheshimiwa Kombo!

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kupata nafasi hii ya kuchangia Wizara hii ya Mambo ya Nchi za Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni Wizara ya Muungano. Kama ni Wizara ya Muungano baina ya nchi mbili, ilitarajiwa sana kuzingatia Muungano uliopo kati ya Tanganyika na Zanzibar na kwa hivyo kulitakiwa kuwe na mizania katika kuteua Mabalozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Tanzania ina Mabalozi 34, ndani ya Mabalozi 34 Zanzibar ilikuwa na Mabalozi watano. Lakini baada ya kustaafu Balozi Mohammed Mwinyi Mzale aliyekuweko nchini Sweden kuiwakilisha Tanzania, Balozi mwingine aliyeteuliwa aliteuliwa kutoka Bara na kwa hivyo Zanzibar tumebakia na Mabalozi wane. Kubakiwa na

Mabalozi wanne Zanzibar nchi ambayo inasemwa kwamba ni Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na kuwa na 1.3% ya Mabalozi, nchi ambayo ni ya Muungano. Suala hili ni maonevu, ni kuonewa kwa Zanzibar ndani ya Muungano huu. Na ndipo mara nyingi tunaposema kwamba Tanganyika imeifanya Zanzibar kama Koloni lake, halikuifanya kama nchi Washirika wa Muungano huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba baada ya kustaafu Mohammed Mwinyi Mzale, hakuonekana Mzanzibar mwingine ambaye anafaa kuchukua nafasi ya kuwa Balozi nchini Sweden kuiwakilisha Tanzania? Hivyo, si kutufanya kama Wazanzibar siku zote labda ni mambumbu, tunaburuzwa na Muungano huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niseme katika nafasi za ajira kwenye Balozi: Nafasi za ajira katika Balozi zetu mpaka wapishi asilimia 98 nukta, wanatoka Tanganyika. Hivi huu ni Muungano kweli? Huuni Muungano kweli wa Tanganyika na Zazibar? Bado tukisema kwamba Tanganyika mmevaa koti la Muungano kuinyanyasa Zanzibar msikatae, kubalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, ni kuhusiana na fedha ambazo zilitengwa mwaka jana kwa ajili ya ukarabati wa majengo mbalimbali ya kibalozi. Kulitengwa bilioni thelathini 2003/2014. Lakini kilichotolewa ni bilioni 6.5. Tujiulize bilioni 24.5 zilizotengwa kwa ajili ya kukarabati majengo zitatolewa lini? Na bado mwezi mmoja tu, zitatolewa lini hizi? Hapa hapakuwa na nia ya dhati katika kuyakarabati majengo. Hapakuwa na nia ya dhati katika kukarabati majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kama mwaka jana mpaka leo kumetolewa bilioni 6.5, bilioni 24.5 hazijatolewa na leo hatujaambiwa na Waziri kwamba kumetengwa kiasi gani ili kushughulikia majengo hayo, hatujaambiwa! Na ndipo aliposema Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na jengo lile ambalo liko Washington. Jengo lile lingekuwa ni sehemu ya kitega uchumi kwa Tanzania. Lakini kwa sababu limeshindwa kushughulikiwa, limebaki kama gofu. Hatujui kuna namna gani juu ya jengo lile kushughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo watu wanakodi majengo mengine badala ya kushughulikia jengo ambalo lingekuwa ni miliki yao au ni miliki ya Tanzania, kupunguza gharama, lakini tunakodi majengo mengine. Jengo lipo limebakia kuwa gofu halishughulikiwi wala fedha hazitolewi kwa wakati. Tanzania Bado tutaendelea kusota, tunashindwa na nchi ndogo ndogo za jirani wana Balozi ambazo zinatazamika.

**NAIBU SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Kombo. Nakushukuru sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Mary Mwanjelwa!

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hakika ninashukuru sana Yehova.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mimi kila mwaka nimekuwa nikichagia sana hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, lakini cha kushangaza sana *nothing happens***.**

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi dunia inabadilika, uchumi unabadilika na siasa zinabadilika na ndiyo maana hata Serikali iliweza kuanzisha Sera ya *economic diplomacy* mwaka 2004, lengo kuu lilikuwa ni kuwezesha nchi kiuchumi katika ushirikiano pamoja na nchi zingine, na hili bado halijafanikiwa hadi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nashindwa kuelewa *Commercial Attaché* wetu kule nchi za nje sijui wanafanya nini, *are they proactive and innovative enough?* Mimi ningeshauri tu kwamba ifike wakati sasa Watanzania ambao wanatoka kwenye *private sector* washirikishwe, maana kule kwenye *private sector* hakuna bla bla! Kule ni *deliverables with marbles!*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri pia kuwe na kitengo kabisa cha *economic diplomacy* katika Wizara hii ya Mambo ya Nchi za Nje. Vilevile *Diplomats* wetu ambao wanakuwa *appointed* katika nchi za nje waweze kuwa *appointed* kulingana na vigezo vyao na ni nchi za aina gani ambazo wanakwenda na vilevile kuwe na *quarterly reports at least.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninavyoelewa Sera hii ya *economic diplomacy* huwa inatakiwa ipitiwe kila baada ya miaka mitano. Sasa sielewi kama imeishapitiwa na kama bado ni kwa nini, Mheshimiwa Waziri husika atueleze hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni *Sovereign State,* lakini cha kushangaza na nashangaa sana inakuwaje Balozi nyingi ziko *based* Nairobi na hadi sasa *visa* inabidi kuchukulia Nairobi. Watanzania wanapata shida sana linapokuja suala zima la *visa.* Wizara inatakiwa kutumia kila aina ya *lobbying* inayotakiwa kuhakikisha kwamba na sisi hatupati matatizo linapokuja suala zima la Watanzania kupata *visa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala linguine, Mheshimiwa Waziri hapa kwenye hotuba yake ametueleza sana masuala ya migogoro katika Afrika na nchi zinginezo. Na vilevile amesema msimamo wa Tanzania ni kutofungamana na

upande wowote. Hilo ni jambo jema, ni vema sana na Tanzania ni *expert* sana katika masuala mazima ya *conflict resolution*. Sasa nilikuwa ninataka Mheshimiwa Waziri hapa atueleze pamoja na kwamba Tanzania ni *expert* katika masuala ya *conflict resolution* atuambie imefanikiwa vipi na imeshiriki vipi katika migongano ambayo inaendelea katika Afrika na duniani kote na mafanikio yake. Maana yake ametueleza tu ilivyoshiriki, lakini mafanikio hajatuambia, atueleze hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ametueleza suala la mpaka wa Malawi na jinsi ambapo *shuttle diplomacy* inatumika kwa Mzee wetu Chissano pamoja na Thabo Mbeki kule South Africa. Lakini nilitaka kujua ni kwa kiwango gani hili jambo limeweza kufanikiwa na ni kwa nini limekuwa likichukua muda mrefu sana. Sasa sijui hii *shuttle diplomacy* haifanikiwi au ni namna gani? Ningependa vilevile Mheshimiwa Waziri aweze kutueleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kabla sijagongewa kengele, sauti yangu imekauka, nilikuwa kule Kyela kwa ndugu zangu kwenye mafuriko. Sitaki kugongewa kengele, yangu yalikuwa ni machache sana. Nilikuwa nataka kusema gharama za Balozi zetu ni kubwa sana, basi ingefika mahala kwa sababu sisi bado tuko kwenye *LDC,* ifike mahala kwamba katika hizi nchi za Afrika ambazo ni wenzetu, mila na desturi mara nyingi zinafanana, hebu tujaribu kuangalia utaratibu, zile nchi ambazo tunaweza tuka-*gain something,* basi tuwe na Balozi karibu katika kila nchi kuliko Mabalozi wote kulundamana huku katika nchi hizi za Afrika ambako na sisi tunatoka na vitu vingi katika *norms and values* tunafanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina mengi sana kwa leo. Lakini naomba na nimesema mara nyingi nachangia Wizara hii na nimekuwa nikishauri, lakini hayafuatwi. Ifike mahala ushauri ambao Wabunge wanautoa hapa Bungeni, ushauri ambao ni *very much valuable,* uwe unatekelezwa, tusiwe tunapiga tu *business as usual. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mary Mwanjelwa. Naomba sasa nimuite Mheshimiwa Susan Lyimo, atafuatiwa na Mheshimkiwa Ally Keissy.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu sana katika masuala ya Mahusiano na Ushirikiano wa Kimataifa. Ninaomba na-*declare* kwamba mimi ni Mjumbe katika Kamati hii inayoshughulikia masuala haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwa kweli Kamati imetoa ushauri mzuri sana na vilevile Kambi ya Upinzani imetoa ushauri mzuri sana na ninaamini na ninajua Waziri ni msikivu, lakini kama atachukua ushauri ambao umetolewa na Kamati pamoja na Wabunge ambao watakuwa wanachagia katika Wizara hii, ninaamini kabisa Wizara hii itaendelea kufanya vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitachangia kwenye mambo makubwa matatu na moja ni la *dual citizenship* au wengine wanaita ni uraia pacha kwa Kiswahili. Jambo hili limezungumzwa kwa muda mrefu sana na ninakumbuka kabisa Mheshimiwa Waziri alisema ataleta Muswada, nadhani miaka mitatu au minne imepita. Lakini sasa hivi naona anasema litaingizwa kwenye Katiba Mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaamini kabisa pamoja na nia njema bado, ninamini tunaweza bado Wizara ikaleta Muswada, Serikali ikaleta Muswada wakati suala la Katiba linaendelea kwa sababu suala hili ni la muda mrefu sana na wote tunajua umuhimu na naamini sasa hivi Serikali, siku za nyuma ilikuwa kuna matatizo kwamba walikuwa wanaona kuna matatizo lakini sasa hivi wanakubali kwamba ni muhimu na wote tunaelewa kwamba kuna umuhimu mkubwa sana wa Watanzania kuwa na uraia pacha au *dual citizenship* kwa sababu kuu mbili; kwanza watasaidia sana kuongeza pato la taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuambie tu, nimefanya utafiti kidogo, nimeangalia nchi mbalimbali na nilimsikia Waziri akisema kwamba ni kwa kiasi gani wenzetu wanaweza kuingiza pato la taifa kuongeza uchumi wao. Kwa mfano nchi ya Nigeria peke yake wale *diaspora* wanaoishi nchi za nje, wanaingizia shilingi za Kitanzania trilioni 34 au dola bilioni 22 kwa mwaka. Sasa *imagine* kama Tanzania tungeweza kwa hawa walioko nje, lakini hata hatujui Mpaka leo Waziri anasema bado anaendelea kufanya utafiti kujua ni Watanzania wangapi wanafanya kazi nje au wanaishi nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuna tizo kubwa sana, tunajiuliza hawa mabalozi wetu katika nchi wanazotuwakilisha hawajui idadi ya Watanzania wanaoishi huko, sasa tutapataje hizi *remittance*? Kwa hiyo, nadhani bado kuna tatizo kubwa sana kwenye balozi zetu, lakini vilevile katika Wizara tuna matatizo makubwa, hawawezi kutuambia kwa miaka yote hiyo bado wanafanya utafiti kujua ni Watanzania wangapi?

Je, ni fedha kiasi gani ambazo zinapotea, ambazo wenzetu nchi nyingine kama Kenya peke yake wanaingiza zaidi ya trillioni tano kwa hawa wanaoishi nje. Lakini Tanzania hatujui ni kiasi gani kinaingizwa. Fedha hizi *actually* zinasaidia *direct* kwenye maendeleo kwa sababu wanapeleka moja kwa moja

kwenye familia zao. Kwa hiyo, unaona ni jinsi gani fedha hizi zingeweza kubadilisha maisha ya Watanzania tukaondokana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bado Serikali haijafanya jukumu lake la msingi kuhakikisha ni Watanzania wangapi wanafanya kazi nje, lakini vilevile naendelea kuisukuma Serikali ihakikishe kwamba *dual citizenship* inakuwepo ili Watanzania waweze kufaidika na fursa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niendelee kwenye suala zima la sera au diplomasia ya kiuchumi. Jambo hili ni miaka kumi sasa, toka mwaka 2004 sera hii au hii *policy* imekuwepo! Lakini hebu tumuulize Mheshimiwa Waziri toka sera hii imeanzishwa mpaka leo kumekuwa na mabadiliko gani? Kumekuwa na manufaa gani? Bado tunaona ni diplomasia ya kisiasa ndiyo inayoendelea. Je, mabalozi tulionao wana sifa zipi za kuhakikisha kwamba tunabadilisha nchi hii kutoka kwenye diplomasia ya kisiasa kwenda kwenye diplomasia ya kiuchumi? Tunajua kwamba moja ya sifa za mabalozi ni kutetea maslahi ya nchi yao na kujenga marafiki, lakini kuvutia uwekezaji. Unawezaje kuleta wawekezaji wakati balozi zetu nchi za nje ni choka mbaya? Balozi hana gari, gari iliyopo ni chakavu, watu tunatembelea nchi mbalimbali ni aibu. Nilikuwa nasema kwamba kama balozi ndiyo kioo cha nchi, balozi wa nchi husika anawakilisha nchi, halafu hana gari, gari iliyoko ni ya ajabu yaani haiwezekaniki!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba kwanza tuweze kuboresha balozi zetu, tuweze kuboresha vifaa vilivyopo kwa mfano vya usafirishaji ndipo tutaweza kuongelea suala zima la kutangaza fursa za nchi yetu. Tunajua kwamba nchi yetu ina fursa nyingi za kitalii, lakini yule balozi aliyepo ni kiasi gani anatangaza? Kwa hiyo, nilikuwa nadhani ni vyema sana suala hilo likaweza kushughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la lugha. Ni wazi kwamba Tanzania imekuwa ikiwakilishwa katika mikutano mbalimbali, lakini ni kwa kiasi gani Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya elimu wanatusaidiaje katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na wakalimani katika mikutano mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze ni jinsi gani Tanzania tunatia aibu katika mikutano mbalimbali na tumeona Mawaziri, Wabunge, lakini nitazungumza moja tu ambalo kwa kweli linatia aibu sana kwamba Mtanzania tunajua Kiswahili ni lugha yetu, lakini tunapoenda nchi za nje tunaongea Kiingereza kwa sababu hatuna wakalimani na tunajua kuna watu wana matatizo makubwa ya lugha. Haiwezekani Waziri au Naibu Waziri anaenda nje ya nchi anaongea Kiingereza ambacho hakieleweki kabisa na hamna mkalimani. Huwezi ukasema, Tanzania *is the unification of the Island of* Pemba *and* Zimbwabwe. Unaongea katika mikutano ya kimataifa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama tungekuwa na wakalimani wazuri, huyu mtu kwa vyovyote vile anaelewa, lakini kwa sababu ya tatizo la lugha inakuwa tatizo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara hii kwa kweli ihakikishe kwamba tunakuwa na wakalimani wazuri ili Mtanzania anapoenda nje aongee lugha yake anayoielewa? Aongee Kiswahili lakini kitafsiriwe, Kwanini Kiswahili ni lugha ya saba duniani, lakini haipo katika lugha ambazo zinapata wakalimani? Hii ni kwa sababu hatujawekeza vizuri katika lugha ya Kiswahili na kwa maana hiyo mtu anaenda nje ya nchi anaongea Kiingereza ambacho hakieleweki. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Wizara ihakikishe kwamba Watanzania wanapoenda nje wanaongea Kiswahili, lakini kunakuwa na wakalimani na kama anaongea Kiingereza, aongee KKiingereza kinachoeleweka, maana wakati mwingine unaweza ukaongea lugha ukaleta mtafaruku mkubwa kwa sababu Zimbabwe wangeweza kuja kudai, hivi ni lini Zimbabwe ilikuwa Kisiwa na ni lini…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan *clarification* ilitolewa kwamba ilikuwa *a slip of the tongue,* kwa hiyo…

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana hivyo, lakini mimi sikubaliani na hilo kwa sababu hata ukisikiliza unaona kabisa ni tatizo. Kwa hiyo, nilichokuwa nasema naomba sana Wizara hii kwa kweli ihakikishe kwamba inashirikiana na Wizara nyingine kuweza kupata wakalimani ili mtu anapoenda nje aweze kuongea lugha ambayo ameizoea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Susan Lyimo. Sasa Mheshimiwa Ally Keissy.

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nataka kuzumzia habari ya *DRC* Congo na wapiganaji M23. Nadhani msemaji wa Kambi ya Upinzani, Waziri Kivuli haielewi *DRC* Congo, mimi ndiyo nakaa mpakani. Moja kwa moja M23 ni majeshi kutoka Rwanda, hamna kuficha. *DRC* Congo tangu mgogoro umeanza wameshakufa raia zaidi ya milioni saba, hana uchungu nao. Ni sisi tunapata shida, wananchi tunaokaa mipakani kupokea wakimbizi, kuwalisha na kuwahudumia. Kwanza ingekuwa mimi ndiyo *President* wa nchi hii ningepeleka wanajeshi zaidi ya elfu kumi au kumi na tano kwenda kuzuia. Rwanda imekaa ni kuiba moja kwa moja Congo, inaiba mpaka inafumua mabati ya majumba, imeiba ngombe, wanyama, mbao na madini. Leo unasema habari ya DRC Congo, Tanzania isipeleke jeshi kule kusaidia ndugu zetu wa Congo ili Rwanda iendelee kuipora na kuiba mali ya *DRC* Congo.

Leo Rwanda inafanywa kuwa ndiyo tajiri katika Afrika kwa wizi wa mali ya DRC Congo. Haina chochote inechimba mashimo, imefukia madini ya Congo na baadaye inasema ni madini yake. Wameiba kila kitu Congo, wameua kila kitu. Leo unakwenda kusema kwamba sisi ni wachokozi kwenda kuweka majeshi? Yote ni ubaya wako unataka wananchi wa Congo wazidi kufa! Sisi tunakaa mpakani tunaona uchungu wananchi wakuja, wanaacha watoto wao wadogo, wanafia njiani!

Kwa hiyo, naomba Serikali iendelee, kama jeshi halitoshi, iepeleke jeshi zaidi kukabili wizi wa Rwanda kuiba madini ya Congo. Chokochoko zote ni wizi wa Rwanda, hamna kitu kingine. Naiomba Serikali yangu ipeleke jeshi kubwa zaidi, sisi ndiyo tunaomba uchungu, wanachi wanakuja wakimbizi uchi uchi kwenye mpaka wetu. Wameshakufa watu milioni saba, acha elfu saba, DRC Congo. Rwanda inaingia mchana na usiku kupora kila kitu.

Tuzungumzie habari ya ndugu zangu wa Zanzibar. Ndugu zangu hii kusema ubalozi sijui asilimia, kila mara nazungumza mimi hapa kwamba ninyi mko 2.8% na wala hamchangii gharama ya Muungano miaka 20 leo. Hizo balozi ziko kule nje ni kodi ya Nkasi, Kahama, Biharamulo na Dar es Salaam. Na sisi mtueleze Waziri unapokuja hapa, Zanzibar imechangia kiasi gani katika Muungano huu?

Maana isiwe upande mmoja tumevaa koti sisi, wakati koti limeishaanza kutubana. Sisi *population* yetu Tanzania wala siyo milioni 45, wengine hawakuhesabiwa! Wengine hatujahesabiwa. Bado mnadai asilimia 21 ya ajira, ndugu zangu wengine Watanganyika wakafanye kazi wapi?

Kama koti limekuvaa uamue moja. Mimi napendekeza Serikali moja kama mnashindwa barabara nyeupe! Lakini siyo chokochoko kila siku tukija hapa mnaonewa, kila mkija mnaonewa, wakati hamchangii! Kuna mfuko wa Jimbo tunawapa wala hamchangii kodi ya Nkasi, Kahama, Biharamulo kwenye machimbo ya Nzega tunawapa mfuko wa Jimbo, Jimbo lenyewe ukipiga filimbi wananchi wote wanakusanyika pamoja. *(Kicheko)*

Jimbo la Nkasi, Kata yangu moja ya Mtenga sawa na Majimbo mawili ya Zanzibar, lakini mnapeleka mfuko wa Jimbo sawa, bado na kule kwenu mnapewa mfuko wa Jimbo. Elimu ya Juu mna mfuko wenu wa Elimu ya Juu na huku Mfuko wa Elimu ya Juu, mnapata kotekote. Umeme hamlipi miaka mingapi leo? Tutawadai na riba ya umeme. Kwa hiyo, ndugu zangu usimpige mtu wala usimchokoze mwehu halafu unakimbia kwenye nyumba ya vioo! *(Kicheko)*

Kwa hiyo, nawaomba kama mnaona koti limewabana amueni moja, kuliko kila siku kelele kelele kelele, hapana. Sisi vilevile tuna uchungu na nchi yetu. Hamchangii Muungano miaka 20, sisi hatuna maji, nyie mnasema kila mtu ana maji, kila mtu ana umeme, wakati sisi kwetu hatuna umeme wala maji.

**TAARIFA**

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**MHE. ALLY KEISSY. MOHAMED:** Taarifa, nitakujibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kombo, taarifa! *(Kicheko)*

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, natumia kifungu 68(7). Nchi hii haiwi na wendawazimu namna hii. Hii ni nchi yenye heshima watu wanaoheshimiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakubaliana na wewe…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kombo, tafadhali samahani sana.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Naam!

**NAIBU SPIKA:** Lugha uliyoitumia kidogo sijaielewa, mwendawazimu ni nani?

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa nitakupa ufafanuzi nini mwendawazimu. Mwendawazimu ni yule anayepiga mawe, mwendawazimu mwingine akipita anaweza akawa anacheka tu, hehe hehe hehe! Wendawazimu wengine ni wale wanaosema maneno ambayo watu wenye heshima zao na busara wamefikiria kama hili jambo ni la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wazanzibari siyo watu maskini. Wazanzibar Wameingia katika Muungano huu kwa masikitiko makubwa, kwenye 45 kwa milioni 1.3. Sasa hata kama mkawa mnatusaidia kama sadaka, basi hakuna chochote mnachotusaidia. Ni aibu sana Mbunge wa Chama Cha Mapinduzi ambacho kiliingia saini na Zanzibar akazungumza maneno kama hayo. Naomba muongozo wako, umwambie asivuke kuja Zanzibar.

**NAIBU SPIKA:** Ulisimama kwa maana ya taarifa, kwa hiyo, iishie kuwa taarifa. Mheshimiwa Wenje hebu twende kwa utaratibu! Mheshimiwa Keissy umepewa taarifa!

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo taarifa siikubali na kama anasema mimi mwendawazimu, yeye ndiye mwendawazimu zaidi.

**TAARIFA**

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Wenje, muda haupo upande wetu sana.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu *very sensitive*.

**NAIBU SPIKA:** Unampa taarifa Mheshimiwa Keissy?

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, *yeah, very sensitive.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye taarifa ya Kambi ya Upinzani ni makosa makubwa sana, hatujazungumzia suala la majeshi yetu Congo kwamba tunapinga kupelekwa. Kwa hiyo, naomba Keissy apate hiyo taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ni aibu kubwa sana kwa taifa letu, Keissy kusema hapa ndani ya Bunge kwamba M23 ni ya Wanyarwanda na wanaiba huko Congo na Waziri wa Mambo ya Nje anapiga makofi. Ni fedheha na ni aibu sana kwa taifa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Keissy, umepewa taarifa hiyo!

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo taarifa taarifa siikubali. Mimi naijua Congo kuliko anavyoijua yeye, mimi nishakwenda Congo zaidi ya mara kumi ama kumi na tano na nakwambia ukweli M23 ni Wanyarwanda, hiyo hakuna ubishi, hakuna kubabaisha, wala sibabaiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naendelea, dakika zangu zilinde.

Nazungumzia kuhusu mambo ya Muungano mkija hapa mnasema tunawadhalilisha, tunawagandamiza, tunafanya nini! Haiwezekani! Nyie mko 2.8% na kila kitu mnachotaka tunawapa, sasa inafikia mwisho. Tunakaa humu Bungeni kwa heshima na adabu, hatukubali na sisi nchi yetu kutoa kodi huku kwetu kwenda kwenu. Lazima mchangie Muungano kama mnataka ubalozi sawa, watumishi na nyie mchangie. Miaka 20 hamjachangia Muungano!

**TAARIFA**

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. ALLY KEISSY. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu nilinde. Wewe ulizungumza, tuliwaacha mkazungumza mpaka mwisho, na nyie mtachangia. Taarifa, taarifa namna gani? Wacha nimalize kuchangia. Mwiba unatokea ulipoingilia. Vumilieni muwe na moyo mkubwa, msibabaike. Mimi nasema ukweli!

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani, anatukashifu huyu sasa!

**MHE. ALLY KEISSY. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, siwakashifu ondokeni nje kama nina wakashifu.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na sisi hatukai kitako, tutasema!

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, wewe sema na mimi nitasema. Hatukubali sisi…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba wote mkae chini.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Hatukai kama hajakaa! Anatudhalilisha huyu!

**NAIBU SPIKA:** Naomba wote make chini, tusikilizane Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Hana adabu!

**NAIBU SPIKA:** Nawaombeni wote tukae chini, tuzime mic. Tutasikilizana tu, sisi wote Watanzania. Tatizo lilotokea ninyi wenyewe mmeamua kuleta mada za Bunge la Mheshimiwa Samuel Sitta kwenye hili Bunge lingine. *(Kicheko)*

Leo tupo kwenye Wizara ya Mambo ya Nje ya Nchi, sasa mmehamisha mada mmeleta mada zile zingine, matokeo yake ndiyo haya. Haya mkiyataka, tusubiri mwezi Agosti si keshokutwa tu jamani, tutakutana uwanja huu huu. Hoja ni kwamba mrudi tu jamani ili tuje tuonge na yeye angojee vilevile wakati huo. Ahsante sana. Nashukuru. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda mkiangalia saa yetu, muda hauruhusu kabisa, mjadala huu ni mzuri unaendelea tu vizuri msiwe na wasiwasi. Tutaendelea na uchangaji jioni ambapo Mheshimiwa Shibuda, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Mushashu, Mheshimiwa Fakharia, Mheshimiwa Shomari na wengine mtapata nafasi ya kuchangia na tutahitimisha hoja yetu jioni ya leo.

Basi kwa nafasi hii naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 10.00 jioni ya leo.

*(Saa 6.56 Mchana Bunge liliahirishwa hadi saa 10.00 jioni)*
*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Wakati tunaendelea kujipanga, basi Mheshimiwa Anastazia Wambura awe mchangiaji wa kwanza jioni ya leo. Mheshimiwa Anastazia!

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikiifanya na imejionesha wazi kabisa katika hotuba nzuri ambayo imetolewa na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kukuomba unipelekee salamu zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Spika kwa kututeua mimi na Mheshimiwa Khalifa mwaka jana 2013 kuhudhuria mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa kule New York Marekani, nasema ahsante sana Spika kwa uteuzi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Kabla sijaendelea nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kupata tuzo ya kuwa Kiongozi Bora Barani Afrika, hongera sana Mheshimiwa Rais. Vile vile labda nichukue nafasi hii pia kueleza kidogo kuhusiana na masuala yaliyotokea kule Umoja wa Mataifa mwaka jana mwezi wa Tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na ajenda nyingi, lakini moja ya ajenda ilikuwa ni malengo ya milenia na katika hili Wakuu wa Nchi za Afrika, Carribean, Pacific walitakiwa waelezee ni jinsi gani nchi zao zimepata mafanikio katika malengo ya Milenia. Katika hili naomba nichukue nafasi hii kumpongeza

sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa sababu alituwakilisha vizuri sana katika hotuba yake aliyoitoa akielezea ni jinsi gani nchi yetu imepata mafanikio katika kutekeleza malengo ya milenia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msisitizo katika eneo la afya aliweza kuonesha ni jinsi gani tumepata mafanikio katika kupunguza vifo vya watoto wachanga na walio chini ya umri wa miaka mitano na vilevile tumepunguza vifo vya akinamama wajawazito, tumepunguza *incidence* za *malaria* na UKIMWI pamoja na magonjwa mengine ya kuambukiza. Vile vile alionesha tulivyoongeza idadi ya Madaktari, tulivyoongeza zahanati zetu na pia tuliongeza bajeti ya mwaka 2013/2014 katika Wizara ya Afya mpaka kufikia asilimia 11 ili kusudi kuondoa utofauti katika maeneo ya vijijini na mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Rais aliweza kutambua mchango mkubwa wa Wabunge katika kupambana na lishe duni hasa ya watoto kupitia Kikundi cha Lishe cha Bunge. Kikundi hiki kinaongozwa na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o. Kwa hiyo, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ombi moja kwa Serikali, naomba Serikali yetu iwe na tabia ya kuzingatia, pamoja na kwamba inazingatia kwa kiasi kikubwa, lakini naomba katika maeneo fulani fulani iwe na tabia ya kuzingatia hii mikataba ya Kimataifa. Malengo ya Milenia ni Mkataba wa Kimataifa, ambapo nchi za Afrika, Caribbean na Pacific pamoja na *European Union* ziliweka mkataba unaoitwa Cotonou *Agreement* wa mwaka 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mkataba huu au malengo haya ya milenia ni zaidi ya asilimia 30 yanahusiana na afya, utakuta Lengo la Nne ni kupunguza vifo vya watoto, Lengo namba Tano ni kupunguza vifo vya akina mama wajawaziti na Lengo namba Sita ni kupambana na maradhi yakiwemo *Malaria* na UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu nimekuwa nikiangalia hizi *documents* za bajeti, bajeti ya Wizara ya Afya imepungua hailingani na ya mwaka jana, sijui sababu ni nini. Vile vile ukija kuangalia tena katika maeneo ya *Big Result Now*, Wizara ya Afya haipo katika *Big Results Now,* sijui ni kwanini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijiuliza je, ni kwamba matatizo yamekwisha? Nichukue nafasi hii kuwaomba Wabunge tusikubaliane na hii hali, tuiombe Wizara ya Afya iongeze bajeti ili kusudi mwakani tuweze kufikia malengo yetu ya milenia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malengo mengine ya milenia kama lengo namba tatu halihitaji hela za mtu ni utashi tu wa kisiasa na hili lengo ni usawa

wa kijinsia. Hili lengo lipo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2010/2015 kwamba ikifika mwaka 2015 nafasi za uongozi kwa ngazi zote tufikie asilimia hamsini kwa hamsini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuiomba Serikali ijiandae vizuri ikiwezekana ilete Muswada wa Sheria ili tuweze kuupitisha hapa Bungeni tuone tunatimizaje lengo hili kwa sababu tunapokuwa tumefanikiwa, tuone tunatimizaje lengo hili, kwa sababu tunapokuwa tumefanikiwa katika malengo ya Milenia yupo mtu ambaye anapeleka sifa zetu kwenye Umoja wa Mataifa ambaye ni Rais, lakini tunapokuwa tumekwama kwa makusudi au tumefeli kwa makusudi tujue kwamba ni yeye atakayebeba aibu zetu. Hivyo, naomba tusimwangushe Mheshimiwa Rais kwa mambo madogo kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara sasa iboreshe hali za Balozi zetu nchi za nje, magari ni chakavu, katika maeneo mengi nyumba watumishi wanatimuliwa kutokana na kutokulipa kodi ya nyumba, lakini hata posho zao wakati mwingine zinachelewa na pia inakuwa ni aibu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja ambalo ningependa nimalizie, ambalo ni kuhusiana na matumizi ya fedha zetu ya fedha za ndani na fedha za nje ambazo tunapata kutoka kwa Wabia wa Maendeleo. Naomba sana Serikali na Watendaji wa Serikali Kuu pamoja na Serikali za Mitaa tuwe na tabia na tujifunze kuwa na matumizi mazuri katika eneo hili kwa sababu hii siyo siri tumeharibu shilingi trilioni 1.6, wenzetu wamelalamika, vilevile wanalalamika sana wanasema kuanzia mwaka huu sasa watabadilisha mfumo wa uwajibikaji na hasa kwa upande wa afya, itabidi wahesabu idadi ya watu ambao maisha yao yameokolewa *in terms of thousands*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona niishie hapo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anastazia Wambura. Anayefuata ni Mheshimiwa Mtutura Abdalla Mtutura na Mheshimiwa Bernardetha Mushashu ajiandae.

*(Hapa Waheshimiwa wote wawili walioitwa kwanza hawakuwepo Ukumbini)*

**NAIBU SPIKA:** Kama wote wawili hawapo Mheshimiwa Fhakharia Shomar Khamis, tafadhali!

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza sina budi kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa na imetoa elimu kwa Watanzania wote. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumwomba Mheshimiwa Waziri, mwaka jana alituambia kwamba Zanzibar ana kiwanja na huenda wakajenga, lakini hali halisi ninayoiona kiwanja hicho bado hana nia ya kujenga. Ningemwomba, najua kwa bajeti hii hatoweza kujenga, lakini afikirie na aweke maanani kwamba naombwa na Wazanzibari niwajengee ofisi kama walivyojenga Bunge, walivyojenga Ofisi ya Makamu ya Rais, walivyojenga Mambo ya Ndani na Taasisi zingine za Muungano, kwa sababu kujenga kule kutamsaidia badala ya kukaa kwenye jengo la nyumba ya makazi itabidi akae ndani ya ofisi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatutaki ofisi lazima iwe kubwa ya ghorofa hapana! Iwe ya kiasi, lakini ya kupendeza, ya kileo, ili wale wafanyakazi wa Zanzibar nao wajisikie kwamba wapo katika jengo lao na watakapofika ile waliyokuwa wameifanya ofisi wataifanya *rest house* kwa kuweza kufikia kwa makazi wakati atakapokuwa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba tena, najua kuna Katibu Mkuu ni kiongozi pale katika Wizara kiutendaji, lakini yeye simpi majukumu hayo, naomba majukumu hayo nimpe *DAP,* aweze kutembelea Zanzibar, aweze kuja kukaa na Watendaji wa Zanzibar, asikie kilio cha wafanyakazi wa pale. Hata wakati mwingine wanapofanya Mabaraza ya Wafanyakazi wakaamua kuja kufanya Zanzibar angalau na wale wafanyakazi wa Zanzibar wakapata kujumuika na wafanyakazi wenzao kutoka Tanzania Bara ili kuwa na msimamo na lengo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie uraia wa nchi mbili (*Diasporas)*. Ni jambo la siku nyingi na tunasema tunapoteza mapato na fursa za kuinua uchumi wa Tanzania, kwa sababu Watanzania hawa wakipata uraia wataweza kuja kuwekeza nyumbani, wataweza kuitangaza Tanzania, wataweza kuwatafuta marafiki wao wa karibu wenye uwezo kuja Zanzibar kuwekeza. Hili nimeona Mheshimiwa Waziri ameliandika kidogo katika ukurasa wake wa 34, lakini ningeomba alipanue ingawa amesema kwamba ameshalipeleka kwenye rasimu ya Katiba limo, lakini bado naomba alipe haiba ya nguvu ili hili jambo liweze kusimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunazungumzia uchumi wa nchi, hayo mengine yote lakini uchumi wetu ukue, tunataka waje wawekeze, tunataka waitangaze Tanzania, kwa sababu kuwa mbali na sisi ndiyo kama chombo kikuu kinachoifanya wao kuichukia Tanzania. Tutakapokuwa nao karibu tunataka waitangaze Tanzania kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba hayo uyazingatie kwa sababu wenzetu Kenya hivi karibuni walipata *USD* milioni 100 na wamefikia kwa kiwango cha asilimia 14 ya kuongeza mapato yao kutokana na *Diaspora*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia kuhusu Diplomasia ya Kiuchumi, Tanzania tunatangaza na leo Waziri umezungumza kwamba sera ya nje inasimama katika Diplomasia ya kiuchumi, mimi ninakubali na haina matatizo. Siku hizi sera za nje kuzungumza Mabalozi siasa haziwezi kutufaidisha kitu, tunataka Mabalozi wazungumze uchumi, wautangaze uchumi wa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani, watangaze utalii; vivutio vya utalii tunavyo, wanyama wapo, fukwe za bahari tunazo ni nzuri tu, milima tunayo na vitu vingi vya kuvutia Tanzania vipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa Mabalozi wetu watakuwa wanafanya kazi ya kutangaza uchumi wetu, itatufanya watuunganishe na wawekezaji wa kila aina, waweze kutoa kila mbinu ya wawekezaji kufika Zanzibar, wengine kuja kufanya utalii, wengine kuja kuwekeza. Hilo ndiyo liwe kubwa la kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la msingi litakalosaidia kwa Wizara ni Mabalozi watakaowachagua kuwapeleka nje wajue kwamba wana elimu ya uchumi, wanaweza kufanya *publicity* ya nchi yetu ambao wanakwenda kule wanaielewa nchi yetu na wana uchungu na nchi yetu ili wakifika kule waweze kufanya kazi ya kuieleza Tanzania kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia uchakavu wa majengo yetu ya Balozi. Najua tunayo Mifuko ya Hifadhi, kuna *LAPF, NSSF, GEPF* na kadhalika. Mifuko hii inashindwa kusaidia kwa sababu kuna sheria inayowakwaza. Hii sheria inayowakwaza mngeitafutia tafsiri kwa sababu Mifuko hii tungeipa jukumu la kutengeneza Balozi zetu wangetusaidia. Kwa sababu wanajenga majumba hapa, lakini wanashindwa kufanya nje kwa sababu wataonekana kama wanajenga makampuni ya nje au wanajenga vitu ambavyo vipo nje ya Tanzania, lakini nyumba zile ni za Watanzania, jasho la Watanzania na wanaofanya kazi humo ni Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningemwomba Mheshimiwa Waziri kama kuna sheria inakwaza au tafsiri yake haileti maana ambayo wao waweze kufanya kazi hii, basi iletwe Bungeni, tuje tuiangalie, tuifanyiekazi ili iweze kufaidisha Watanzania kwa sababu majumba yale yakibomoka, yakiharibika, jasho la Watanzania linapotea wakati haya yetu ni kujenga na siyo kubomoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana katika bajeti yake ukurasa wa 36 alisema…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nimemwona Mheshimiwa Benardetha Mushashu yupo, atafuatiwa na Mheshimiwa Magalle John Shibuda.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza kabisa napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji Wakuu wote kwa hotuba nzuri na kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mheshimiwa Membe una chapa kazi, nje na ndani ya nchi, Watanzania wote wanakuona wewe siyo mzigo, wewe ni Waziri wa kutegemewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii waliyopangiwa Wizara hii ni finyu na Wabunge miaka mingi wamepiga kelele juu ya ufinyu wa bajeti ya Wizara hii, lakini Serikali imezidi kufumba macho au masikio. Lazima tutambue umuhimu wa Wizara hii. Napendekeza kwamba bajeti hii irudishwe kwenye Kamati ya Bajeti, ifumuliwe ili kusudi waweze kuongeza na siku ya mwisho Waziri wa Fedha atakapokuwa anawasilisha bajeti ya Serikali aweze kutuambia ameongeza kiasi gani cha bajeti kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Diaspora*, wapo Watanzania wengi ambao wanakaa nje, wengine mababu wa mababu zao walikwenda kule wakati wa enzi za utumwa, wengine wamekwenda huko kutafuta *green pastures* wapate kazi, lakini wangependa kuchangia maendeleo ndani ya nchi zao. Hawa wanasaidia sana katika nchi nyingine kama takwimu zinavyoonesha na wanaweza vilevile kuwekeza nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua je, kuna mipango gani ya kukuza ushirikiano huu kati ya nchi yetu na *Diaspora* (Watanzania waliopo huko nje) na je, kuna kitu *structured* ambacho labda kuna namna tunavyowasiliana nao, tunavyokutana nao kila mwaka labda mara moja au mara mbili ili kusudi tuwape nafasi waweze kuchangia uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia juu ya uchakavu wa Ofisi za Mabalozi. Sababu ya ufinyu wa bajeti unakuta kwamba Wizara hii imeshindwa kukarabati ofisi za Balozi nyingi, lakini tukumbuke kwamba ofisi za Balozi kati ya Tanzania nchi za nje, vilevile ni kioo cha Tanzania kwenye uso wa dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya ofisi ni chakavu sana. Nilikwenda pale Ubelgiji, nikaenda Brussels kwa kweli ni aibu tupu, zile kuta mvua ikinyesha maji yanavuja mle ndani. Kwa hiyo, walichofanya wamechukua zile *posters* kubwa za wanyama, akina twiga na nini wameegeshea kwenye ukuta kuficha zile alama za maji yanayovuja. Hata ile *door bell* na yenyewe haifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hii ni aibu, you *can imagine* huyu Balozi amemwita Mwekezaji ndani ya ofisi, anajaribu kuiuza Tanzania, anaanza kusema unajua Tanzania ni nchi ya amani, sekta ya miundombinu inakua kwa haraka, *we are strategically placed* tuna nchi nyingi zinatuzunguka, uchumi unakua kati ya asilimia sita na saba, lakini huyu Mwekezaji akiangalia paa, akiangalia alama ya maji yanayovuja anaanza kutudharau hata kabla hajafika Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napendekeza kwamba ofisi hizi ziangaliwe upya *especially* hiyo ya Brussels pamoja na ofisi za Addis Ababa mahali ambapo kuna shughuli nyingi za kidiplomasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Balozi zinafanya *economic Diplomacy* (Diplomasia ya Kiuchumi), wanaangalia sera za uchumi za nchi hizo, wanaangalia fursa zilizopo, mazingira ya kuweza kupata mikopo, mazingira ya kuweza kupata misaada, fursa za *export* na *import*, wanavutia wawekezaji. *On that note,* nipende kuwapongeza Mabalozi wengi, wamefanya kazi kubwa, wameweza kuwa-*attract* wafanyabiashara wakaweza kufanya biashara kati ya Watanzania na watu wa nje, lakini vile vile mnaona kwamba tumeweza kupata wawekezaji wengi. Hivyo, nawapongeza Mabalozi wetu wanaofanya kazi hiyo vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, humu Bungeni tumechagua Wabunge ambao wanatuwakilisha kwenye vyombo mbalimbali au kwenye mikutano mbalimbali, kwenye Taasisi mbalimbali. Kuna wanaokwenda kwenye Bunge la Afrika Mashariki, kuna wanaokwenda *SADC,* kuna wanaokwenda Bunge la Afrika, kuna wanaokwenda *APU,* kuna wanaokwenda kwenye ushirikiano wa *Caribbean Pacific,* kuna wanaokwenda kwenye ushirikiano wa *European Union* na kadhalika. Kuna wanaokwenda *CPA* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Nje inasimamia Sera na misimamo ya Tanzania katika mambo mbalimbali. Ningependa kujua Wizara hii inawaandaaje hawa tunaowatuma nje kama wawakilishi wetu wakaenda na msimamo mmoja wa Tanzania. Napendekeza basi kwamba Wizara hii iandae utaratibu wa kuwa inakutana na hawa wawakilishi wetu angalau mara moja au mbili kwa mwaka, kusudi waweze kuipata misimamo ya Tanzania na wakienda kule waweze kutetea misimamo ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge la Afrika ni chombo kimojawapo cha vyombo kumi vya Umoja wa Afrika. Bunge hili lilianzishwa mwaka 2004 likiwa na makusudi kwamba liendelee baada ya miaka mitano liweze kufikia hatua ya kutunga Sheria ambayo ndiyo kazi muhimu ya Bunge lolote, lakini hadi leo Bunge hili halijaanza kutunga Sheria, wanakutana, wanashauri, lakini hawawezi kutunga Sheria. Wao wameweza kuandika na kupeleka marekebisho yao ya Itifaki ambayo imeanzisha Bunge la Afrika, tangu mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kwamba Umoja wa Mawaziri wa Mambo ya Nje ni kiungo kikubwa kati ya Bunge la Afrika na Umoja wa *Heads of States and Governments,* Wakuu wa Nchi na Serikali. Ni tatizo gani hasa linalofanya Wakuu hao wa nchi wakatae kuridhia kwamba Bunge la Afrika lianze kutunga Sheria. Labda hata haya matatizo mengine tunayoyaona kwenye Bara la Afrika yangeweza kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningependa Mheshimiwa Waziri aniambie kwamba kuna tatizo gani na labda ni lini wataweza kuridhia ili Bunge la Afrika lianze kufanya kazi yake ya msingi ya kutunga Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, wakati Wizara yake inabainisha wafanyakazi mbalimbali walio kwenye Balozi mbalimbali kuwatambua ili kusudi waweze kuchangia na kusudi waweze kuingia kwenye Mifuko ya Pensheni, kuna watu walisahaulika, tumewakuta watu wamestaafu...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Shibuda John Magalle!

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru kupata fursa hii ili niweze kuchangia Wizara hii. Awali ya yote, natoa pongezi za dhati kwa mema yote yanayotekelezwa na Wizara hii kwa maslahi na umoja na mshikamano wa nchi yetu na Mataifa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kwamba Wizara hii ndiyo kiungo kati ya Tanzania na diplomasia za Kimataifa na kwa kutambua kwamba ina majukumu mtambuka na unganifu kwa Wizara nyingine kama Wizara ya Biashara na Viwanda, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Wizara hii isaidie kuwaambia Watanzania faida za Wizara hii za diplomasia ya uchumi. Je, Wizara hii ina viarifu gani vya kupitia mchango wa mashirikiano ya Kimataifa ya kupitia *Cabinet*, Baraza la Mawaziri ambapo wameweza kuinua Wizara ya Viwanda na Biashara na Masoko na vile vile Wizara ya Mifugo, wakasaidia kupitia mashirikiano ya Kimataifa, Wizara ya Viwanda ikaanza kufikiria kuwa mkombozi na kuwa na uokovu kwa masuala ya pamba, Viwanda vya Pamba? Vile vile je, Wizara hii imesaidia vipi kupitia mashirikiano ya Kimataifa kuielimisha Wizara ya Mifugo iwe na Viwanda vya Nyama, Viwanda vya Ngozi na Maziwa ili na wananchi waweze kufaidika na hicho kitu kinachoitwa diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema nika-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje na haya ninayoyasema ni kwa faida kwamba Wizara hii ijitambulishe na itoe taarifu ambazo ni maelimisho kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, diplomasia ya uchumi inahitajika katika masuala ya kukuza masoko, kukuza biashara. Natambua kwamba masuala ya wanaoitwa *Commercial Attachees* wanapashwa kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, lakini Mratibu Mkuu na Mjenga Hoja na mtu anayepaswa kuwa mbunifu wa mawazo na fikra ya kuibua hoja hizo, ni Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa watutambulishe ubunifu wao wakitambua kwamba dunia hii iko katika vita ya utandawazi dhidi ya tabia zembe na uvivu wa kufikiri. Tanzania kama tutakuwa na uvuvi wa kufikiri, tutaachwa nyuma na tutaendelea kuwa watu ambao ni tegemezi kwa misaada ya kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba yetu inazungumzia juu ya ujamaa na kujitegemea. Watanzania ni vema sasa wakatambua kwamba Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa mnatekeleza Siasa na Sera na Itikadi ya mwegemeo wa msukumo wa siasa zipi ili Watanzania wajitambue baada ya kuwa kwamba dunia iko katika utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendelea vile vile Wizara hii itekeleze mawazo huisho kwa Wizara mbalimbali ambazo zinahusiana na mambo ya kustawisha hayo niliyoyasema masuala ya viwanda, biashara na masoko. Nina masikitiko makubwa sana, ni muda mrefu nimekuwa nikiiasa Wizara hii ikutanishe Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo, pamoja na Wizara ya Mifugo waweze kutatua matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo na-*declare* kabisa kwamba, nitashika shilingi pamoja na kwamba Mheshimiwa Bernard Membe ni mdogo wangu,

ndugu yangu, swahiba wangu, lakini kwa maslahi ya Watanzania tuweke pembeni udugu wetu kwa sababu wenyewe hauna kasoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile Wizara hii iseme itatengua kasoro *dhulumat* kwa makutano ya fikira ya kwamba Watanzania hawajafaidika na mikataba mibovu na vile vile ningependa kuelewa hivi nufaiko kubwa kwa wafugaji, nufaiko kubwa kwa wakulima na wavuvi kutokana na Ziara za Mheshimiwa Rais anatuachia urithi baada ya miaka yake 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeyasema hayo nikitambua ya kwamba sitopata majibu ya sarakasi ya tabia ya kifuniko kwa yale ambayo hayajapata majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema haya kwa dhamira njema. Vile vile napenda kusema kwamba, Wizara hii inaepusha vipi CCM isipewe hati chafu na hivyo kuwekwa katika tuhuma na hapo hapo kuwekwa katika shutuma ya kwamba imepatikana na hatua ya kunyimwa kura iwapo yenyewe itakuwa haisimamii masuala ya kukuza masoko, kukuza biashara za masuala ya wakulima wa pamba na korosho na kuhakikisha kwamba hizi Wizara zinajituma kutengua vitendawili na kukunjua dhuluma zilizopo kwenye suala la bei ya mazao yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu Wizara hii ina wajibu mtambuka wa kuzaa lindo la usalama kwa utulivu wa fikra, lakini hadi sasa haijazaa lindo la utulivu wa fikra kwa wakulima wa pamba, haijawa lindo la usalama kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba kwa upekee na umuhimu mkubwa, niseme mie ni Mjumbe wa *APRM*. Ni ghali sana kutunza uongo kuliko kutunza ukweli. Tanzania tulifanya jukumu la kujitathmini kuhusu uongozi na utawala bora, lakini hadi leo mrejesho wa taarifa haujarejeshwa kwa wananchi, hata Bunge hili halijashirikishwa likatambua kasoro zilizotokea, tujisahihishe nini na tujiimarishe nini, lakini tatizo naambiwa ni fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara hii ieleze, je, iko tayari sasa kukutana na Kamati ya Bajeti baada ya kuagizwa na Mheshimiwa Spika au Naibu Spika, ili kutatua kitendawili cha kwa nini *APRM* ambao ndiyo nyenzo kuu ya kujenga utulivu wa fikra kama tutajijua tuna kasoro gani? Kwa sababu viaga uaminifu kwa fikra za Watanzania ni pale panapokuwa na fikra hasi za kuhusu kupata haki, kupata usawa na kuhusu kuwa na kasoro za uongozi bora na utawala bora katika masuala ya uchumi.

Je, Wizara hii itakuwa tayari baada ya pesa ndogo walizokuwa wametenga, sasa wawe tayari kupitia upya wakitambua kwamba

pasipokuwepo na uongozi bora na utawala bora hakuna siasa bora na athari yake ni mparaganyiko wa Kitaifa na kasoro hiyo inazaa jinamizi na kasoro hiyo italeta mparaganyiko ambapo watu watasambaratika amani na utulivu kupotea?

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile itambulike kwamba Mheshimiwa Rais Kikwete anapaswa kukabidhi taarifa tukufu aliyoisimamia katika uongozi na utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri na kupitia kwako uhakikishe Wizara hii inakutana na Kamati ya Bajeti nakuomba sana sana ili tukamilishe zoezi la kurejesha taarifa yenye viarifu vya kasoro vinavyozaa hila dhidi ya uongozi na utawala bora. Nitashukuru sana kama hilo tutaweza kulitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuwatakia kila la kheri lakini na kusema ya kwamba narejea tena, ni ghali sana kutunza uongo kuliko kutunza ukweli na kama tutaendelea kuwa na tabia ya kifuniko Tanzania tutaparaganyika. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa John Magalle Shibuda. Mheshimiwa Moses Machali!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa nami nichangie kwenye Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ukurasa wa 24 wa hotuba ya Waziri ni kwamba nchi yetu inatajwa kuweza kuingia mikataba mbalimbali ambayo imetajwa ni takriban mikataba 13.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako kwa nyakati tofauti limekuwa na mjadala mpana wa kutaka kuona kwamba Serikali haiendelezi suala la kusaini mikataba mbalimbali, mikataba mikubwa pasipo kulishirikisha, Serikali haiingii mikataba ya Kimataifa pasipo kuishirikisha nchi yetu na pasipo kulishirikisha Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba pengine baadaye wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind up* atusaidie hii mikataba ambayo pengine imeridhiwa, halafu pia hata kuletwa Bungeni na Bunge lako na wakati mwingine likaridhia mikataba hiyo. Kumekuwa na suala la ucheleweshaji na mingi imesainiwa mwaka 2013. Itakuja kujitokeza kama ambavyo tumeona kwenye mikataba mingine ilisainiwa toka miaka ya 1980, miaka ya 1990 halafu

imekuja kuletwa kwenye miaka ya 2010 na kuendelea. Kwa hiyo, bado kwanza kuna tatizo. Mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo nchi yetu imekuwa inaingia, kumekuwa kuna suala la ucheleweshaji wa kuletwa hapa Bungeni ili kusudi Bunge letu likaweza kuiridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa na hii mikataba utaona kwamba mikataba 13 ambayo pamoja na sauti za Waheshimiwa Wabunge kwa nyakati tofauti kusema kwamba tunaitaka mikataba hiyo hata kabla ya kuingiwa iwe imeletwa, lakini kwa sababu masuala mengine ni matakwa ya kisheria, lakini hata suala la kuridhiwa kwa mikataba hii, bado tunaendelea kuchelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mmeingia mkataba na mkataba mnaamini kwamba mkataba huo ni safi, mnapata kigugumizi gani cha kutuletea mikataba hiyo ndani ya Bunge na ikaweza kuridhiwa mapema ili wananchi wakajua kwamba, huu mkataba umeingiwa na Serikali una maslahi mapana kiasi gani na kama kuna maslahi ambayo kidogo ni finyu, basi tutawaambieni kwamba huu mkataba nendeni mkauvunje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunahitaji *transparency,* huu usiri wa mikataba nadhani Serikali ijitafakari. Imekuwa ni tatizo la miaka mingi na bado linaendelea. Kwa hiyo, nitaomba ufafanuzi wa kina ni kwa nini mikataba hii 13 imechelewa. Hata ile mikataba ambayo mlisaini na Rais wa China nafikiri itakuwa humu ndani. Wananchi wamekuwa wanahoji ni mikataba saba kama sijasahau. Tutaomba pengine muweze kutumegea kidogo, tujue kwamba ni kitu gani, lakini mharakishe kuleta mikataba hiyo hapa ndani tujue mikataba hiyo ilikuwa ina maslahi mapana kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo nijielekeze kwenye suala la uraia pacha *(dual citizenship)*. Katika hili naomba ku-*declare interest* tu kwamba, niseme ni jambo ambalo kimsingi ni zuri na nakubaliana na wale wote ambao wamekuwa na mtazamo wa kuona kwamba tunakuwa na uraia pacha na sababu za msingi za kutaka pengine tuweze kuwa na uraia pacha zimekuwa zinaelezwa hasa ni katika ule mtazamo au mlengo wa kuangalia kwamba kiuchumi tunaweza tuka-*benefit* namna gani sisi kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mataifa mengine yameweza kuona kwamba jambo hili ni jema. Tanzania tunasitasita au tunasuasua nini kuweza kuridhia suala hili wakati wa Bunge maalum na Katiba tulimsikia Amosi Wako alikuwa *Attorney General* wa Kenya kwamba Kenya wao wamekwenda mbali na kwa kweli wananchi wananufaika kutokana na raia wa Kenya ambao wanaishi katika nchi nyingine kwa sababu wanatumia mapato yao kuweza kuja kujenga makazi safi na pengine kuweza kuanzisha makampuni ya kibiashara na

hatimaye wameweza kuanzisha makampuni ya kibiashara na hatimaye wameweza kusaidia nchi ya Kenya kuweza kutoa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Watanzania tuache uongo, tuache uongo wakati mwingine katika mambo fulani fulani na kuanza kufikiria kwamba labda kutakuwa na matatizo. Kama kutakuwa na matatizo watu hawa nafikiri kama tutakuwa tumeruhusu kuwa raia wa nchi mbili, tutawanyang'anya tutawaambia pengine wachague, je, wanapenda ku-*value* nchi ya Tanzania au wanapenda ku-*value* nchi nyingine ambayo pia wana haki za kiraia kwa sababu watakuwa na uraia ambao ni wa aina mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mtu yoyote ambaye pengine ana mawazo tofauti, binafsi namchukulia ni kama ni mchawi juu ya suala hili. Niombe kabisa kwamba suala hili tulione kwamba ni suala ambalo ni jema na hii hofu hii inaweza ikaondolewa na Sheria ambayo tunaweza tukawa tumejitungia kupitia Bunge itungwe Sheria kama mtu ataonekana kwamba ana *misbehave* kwa mujibu wa masharti ambayo tutakuwa tumeyaweka kwenye Sheria na Kanuni na hata kwenye Katiba. Nafikiri watu hao watashughulikiwa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hakuna sababu ya kuwa na hofu. Ni sawasawa hata katika masuala mengine ya *East Africa* bado tumekuwa tunasua sua, tumekuwa tunasuasua pengine kuweza kukubaliana katika mambo fulani fulani kwamba tunasema ngoja sisi twende taratibu. Hebu ifike mahali, hivi hatuna *think tanks?* Watu wakae waangalie faida na hasara juu ya mambo haya kuliko kuendelea kuchelewa chelewa namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, nijielekeze kwenye suala la Mabalozi wetu ambao wanafanya kazi kwenye Balozi mbalimbali. Ukienda kwenye Balozi mbalimballi huko duniani, wengi wa Mabalozi wetu ni watu ambao walifanya kazi Serikalini na wakastaafu. Sasa najiuliza watu wamefanya kazi wamestaafu, halafu tena tunaendelea kwenda kuwakabidhi majukumu makubwa, nafasi za Kibalozi. Akina Abrahamani Shimbo, wametumikia Taifa kwa miaka mingi. Hawa vijana ambao wamemaliza Vyuo Vikuu na wengine wako Vyuo Vikuu tunategemea wakapate ajira wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ambao wana jukumu la kumshauri Mheshimiwa Rais, kuna haja ya kuweza ku-*review* juu ya mwenendo huu. Hawa vijana ambao wako wengi leo tunasema kwamba tumeweza kuanzisha Vyuo Vikuu vingi, watu wanasoma na hapa naona kuna wanafunzi hapa kutoka Chuo cha Diplomasia, hawa vijana

mnawapeleka wapi? Watakwenda wapi hawa watu ambao wanasoma diplomasia?

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine nasikia naambiwa kwamba wanasiasa walioshindwa, wanawataja tena kwa majina, mimi sitaki kuyataja, lakini naomba niseme suala hili siyo jema. Ni lazima kama mtu ameweza amefikia umri wa kustaafu basi ni bora hata waje kwenye siasa huku, waende wakagombee Ubunge, waje humu ndani, watumie uzoefu wao walioupata katika kuhakikisha kwamba tunafanya mambo ambayo yanakuwa na tija. Hizo nafasi tuwapatie vijana waende wakafanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Machali. Mheshimiwa Rajab Mbarouk atafuatiwa na Mheshimiwa Mtutura Mtutura.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii inayohusiana na Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Awali kabisa, kwa kweli lazima nikiri kwamba, Wizara hii ni nyeti na Wizara ambayo kwa kweli ndiyo kiunganishi chetu baina ya nchi yetu na Mataifa mengine katika dunia hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la *economic diplomacy*. Kwa kweli juu ya maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyaeleza, nimejaribu kupitia katika taarifa zake za mwaka juzi, mwaka jana na mwaka huu. Kwa kweli bado lugha ni ile ile katika suala zima la *economic diplomacy*. Bado inaonekana Wizara haijachukua hatua madhubuti katika kuhakikisha kwamba, Mabalozi wetu sasa wanajishughulisha zaidi katika kutafuta hawa wawekezaji. Bado inaonekana kwamba Waziri hajaweka mkazo ama Wizara yenyewe haijaweka mkazo katika kuwashawishi Mabalozi wetu kuhakikisha sasa hivi tunawapata wawekezaji ambao wanaweza kutupeleka mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hivyo, ni kwamba Mheshimiwa Waziri karibu kipindi cha maiaka mitatu aliahidi kufanya mkutano wa Mabalozi wetu wote hapa nchini, ili Mabalozi hawa kuweza kuangalia fursa ambazo tunazo hapa nchini, fursa ambazo wao wanatakiwa kuondoka nazo na kwenda kuzitangaza kule nje. Sasa hivi ni miaka mitatu, bado hili limegeuka kuwa hadithi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachokiona leo katika Taarifa yake Mheshimiwa Waziri, anatueleza habari ya kwenda kuuza mihogo China. Nchi hii ina rasilimali nyingi, nchi hii ni tajiri, yako mambo mengi tu, leo tunazungumzia mambo ya muhogo kupeleka China?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wachina wako Dar-es-Salaam sasa hivi wataanza kuuza mihogo ya kuchoma na wao. Hebu tutafute kitu ambacho kwa kweli, kitakuwa na tija, lakini anazungumzia habari ya kwenda kupeleka bidhaa za baharini huko China, lakini sasa Mheshimiwa Waziri ni kwa namna gani sasa; yeye kama Wizara ya Mambo ya Nje ameweza kuisaidia Serikali katika kupata wavuvi walio bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Uvuvi juzi katueleza hapa kwamba, sasa hivi Tanzania ina kilometa karibu laki mbili na za Bahari Kuu, lakini hatujazitumia. Sasa leo tunaingia Mikataba na China na nchi nyingine, wakati sisi wenyewe bado tunajiweka sawa katika kutafuta hizo bidhaa za baharini? *Is it true* Mheshimiwa Waziri? Nafikiri tuache kuandika lugha ambazo kwa kweli, sioni kama zinajenga, lakini tuangalie kiti ambacho kina ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la *travelling expenditures.* Safari za Viongozi pamoja na safari za Maofisa wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje; ukiangalia katika vitabu vya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu kwa kweli, ni aibu na ni hatari kuona namna ambavyo wenzetu wanatumia fursa za ununuaji wa tiketi kwa ajili ya safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Wizara inafika hadi inanunua tiketi kwa shilingi milioni 40, tiketi ambayo ilikuwa inunuliwe kwa milioni 18; huu ni ufisadi mkubwa. Au nyingine katika sampuli ya tiketi 22 ambayo *CAG* alikagua ya safari 239 Wizara inatumia milioni 44 badala ya milioni 23 kwa ajili ya kununua tiketi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani Maofisa wa Wizara wanafanya ufisadi wa hali ya juu katika kununua tiketi. Kwa hiyo, tunaomba hili Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi; kiko Kitengo cha *GPSA* ambacho kinaweka ukomo wa manunuzi, kwa nini hatumii hii Mheshimiwa Waziri, anaachia Maofisa wake wananunua tiketi tu katika Mawakala mbalimbali? Au kama kweli, hii nchi anaipenda kwa nini sasa hivi asianze mpango wa kununua tiketi kupitia *ATCL?*

Mheshimiwa Naibu Spika, watakaponunua tiketi *ATCL* ile kamisheni itabaki pale katika Shirika letu la Ndege, lakini leo wanatumia Mawakala, tiketi ya milioni 20 wananunua kwa milioni 40 na. Si hiyo tu, iko na nyingine hapa, tiketi ambazo wamenunua milioni 70.8, tiketi ambazo thamani yake ilikuwa ni milioni 18.4; hawa ndio Maafisa wa Wizara wanavyofanya katika suala zima la safari hizi za Viongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile suala la safari za Viongozi Wakuu, kwa maana ya Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu, Makamu wa Rais. Ni vyema sasa hivi Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho yake akatupa maelezo juu ya safari hizi ambazo zinatumiwa na Viongozi wetu hawa Wakuu. Kuna Taarifa ambazo zina ukweli kwamba, ndani ya robo moja tu ya kwanza ya mwaka tayari Rais alishamaliza Bajeti yake ya safari; sasa bajeti ni ya mwaka mzima, katika robo ya kwanza tu tayari ameshamaliza, inaonekana kwamba, hizi safari Mheshimiwa Waziri, hazina mpangilio.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, tunakubali kwamba, Rais wetu anakwenda nje kwa ajili ya kutafuta manufaa ya nchi, lakini ziwe na mpangilio, bajeti yake iwe inaeleweka. Au kingine Mheshimiwa Waziri ambacho naweza kumshauri ni kwamba, hebu hii Bajeti ya Safari za Rais na Viongozi isiwe katika Fungu lake la Wizara. Ikae mbali na Fungu lake la Wizara, ijulikane kwamba, hii ni Bajeti ya Safari za Mheshimiwa Rais, hapo nafikiri atakuwa anakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla kengele haijanililia, nataka vile vile Mheshimiwa Waziri anipe maelezo juu ya wanafunzi 17 ambao tayari walishamaliza mafunzo katika Chuo cha Diplomasia, Dar-es-Salaam wa Zanzibar, ambao sasa hivi wameshakaa nje kwa muda wa mwaka mmoja na nusu bila ya kuajiriwa. Tunataka tupate maelezo ni kwa nini vijana hawa mpaka leo hawajaweza kupata ajira?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Mtutura Mtutura, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, ajiandae. Mheshimiwa Mtutura!

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuwa Mchangiaji wa Mwisho katika Wizara hii. Kwanza nitoe pongezi sana kwa uongozi wa Wizara hii kwa maana ya Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote kwa kazi nzuri sana wanayoifanya kwa bajeti ndogo. Kwa kweli, kitu kinachoitwa *value for money* inaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, napenda katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amethibitisha kwamba, nchi ya China ndiyo ambayo sasa hivi inayoongoza kwa kuzalisha Watalii wengi duniani, lakini vile vile amekiri kwamba, uchumi wa China sasa hivi ni mkubwa. Sasa kutokana na maelezo hayo nitafarijika zaidi kama Serikali itaamua kuhakikisha kwamba,

katika nchi hii ya China ambayo tuna Ubalozi wetu katika Mji wa Beijing tunapeleka wafanyakazi wengi pamoja na rasilimali fedha za kutosha, ili tuweze kutumia fursa hii ya watalii wengi ambao wanazalishwa China sasa hivi kuweza kuingia katika nchi yetu. Hii ni mwendelezo wa ule utekelezaji wa *economic diplomacy* ambayo sasa hivi ndio ambayo tunayoikamatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile katika nchi hii ya China kuna Mji mmoja maarufu sana wa viwanda pamoja na biashara unaitwa Guangzhou. Katika mji huu Watanzania wengi wanafanya biashara katika mji ule. Sasa Guangzhou mpaka Beijing pana hatua kubwa kidogo, sasa ni bora zaidi kama Wizara yetu itaamua kufungua Ofisi Ndogo katika Mji ule wa Guangzhou itawarahisishia Watanzania wengi kuhakikisha kwamba, wanafanya biashara kwa ufanisi mkubwa na biola matatizo yoyote na pale wanapopata matatizo basi inakuwa rahisi Ofisi ya Ubalozi kuweza kuwasaidia kutatua matatizo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile pamoja na hilo itakuwa vizuri zaidi kama Wizara itafungua Ofisi, wanaita *Trade Centre,* Ofisi za kibiashara katika Balozi mbalimbali katika nchi yetu kama vile walivyofanya katika nchi ya Uingereza, Mji ule wa London. Itakuwa ni vizuri sana kwa sababu, itarahisisha kutafuta masoko ya bidhaa zetu na kuwasaidia Watanzania ambao wameamua kujikita katika masuala ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile Wizara ituambie hivi ni kwa nini sasa hivi mtu anapotaka kwenda Canada, anapotaka kwenda Uingereza, pamoja na kwamba, una-*lodge* maombi yako ya *Visa* hapa hapa Tanzania, lakini *Visa* ile lazima ikachukuliwe Nairobi. Inaleta usumbufu kwa kweli, kwa wananchi wetu ambao wanapenda kusafiri katika nchi hizi. Sasa hebu tuambieni sababu ni zipi na sababu hizo kweli, haziwezi kutatulika? Ili wananchi wetu waweze kusafiri kwa urahisi katika nchi hizo bila vikwazo vyovyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirejea Hotuba ya wenzetu, watani zetu, yaani bila hata kusitasita wanasema Waziri huyu ni mzigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa kisa kimoja ambacho ni cha kweli kabisa. Siku moja tulipokea mgeni kule nyumbani kwetu, Tunduru kwa baba yangu mzazi. Baba akampokea vizuri sana mgeni yule, siku ya kwanza kabisa kwa sababu, alikuja jioni akachinja kuku, kesho yake akachinjiwa mbuzi. Akafanyiwa takrima zote zinazostahili kufanyiwa mgeni; siku anaondoka yule mgeni akasema, baba yetu katika kumuaga yule mgeni, anasema mgeni tunashukuru umetutembelea, lakini utuwie radhi kwa makosa yote tuliyoyafanya kwako wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya mgeni alisema, kama Mzee Mtutura kunichinjia kuku ni makosa, kunichinjia mbuzi ni kosa, kunipa malazi mazuri sikuumwa hata na mbu ni kosa, mazungumzo ya bashasha ni kosa, basi naomba makosa hayo yaendelee. Alisema makosa yale yaendelee, nikifika ufanye kosa hilo hilo tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifungua ukurasa wa kuanzia wa 11 wa Hotuba ya Rais, ninachotaka kumwambia Mheshimiwa Waziri, kama…

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Rais au Mheshimiwa Waziri.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Eeh Waziri, daah, nakuombea dua Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kutafuta masoko ya biashara ya kilimo ni kosa, ni mzigo, basi naomba mzigo huu uendelee. Kama kutafuta wawekezaji, kutafuta misaada ya nishati katika nchi yetu, mpaka sasahivi tunapata umeme karibu kila Kijiji ni mzigo, naomba mzigo huo Mheshimiwa Waziri uendelee nao. Kama kutafuta fursa mbalimbali za biashara nje ya nchi yetu, kutafuta vyanzo mbalimbali na fursa mbalimbali za biashara nje ya nchi yetu ni mzigo, naomba mzigo huo uendelee nao na kama kutuongezea fursa za watalii wanaokuja nchini mwetu ili kutuletea fedha za kigeni nyingi ni mzigo, naomba mzigo huo uendelee nao. *(Makofi)*

Vile vile kama kutafuta ajira mbalimbali kwa ajili ya Watanzania wapate kazi nje ya nchi ni mzigo, Mheshimiwa Waziri endelea kuwa mzigo. Kama kutupelekea vijana wetu zaidi ya 50 nje ya nchi, ili wakachukue mazoezi mbalimbali, ili nchi yetu ipate medali za dhahabu, ni mzigo, Mheshimiwa Waziri naomba uendelee kuwa mzigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtutura kwa hotuba yako nzuri sana.

Kabla sijamuita Mheshimiwa Naibu Waziri Mahadhi, kuna Wageni tuliwatambulisha asubuhi, lakini hawakuwepo; naomba nitambue uwepo wa Dkt. Stagomena *Tax*, *Executive Secretary* wa *SADC*. *(Makofi)*

Karibu sana Katibu Mkuu *SADC*. Tangu upate mamlaka hayo hatujakuona hapa Bungeni, ulikuwa ukija mara kwa mara wakati ule ukiwa Katibu Mkuu.

Karibu sana na sisi kama Wabunge tunakutakia kila la heri na tunajivunia sana uwepo wako kwa nafasi hiyo kule *SADC*. Ahsante na karibu sana. *(Makofi)*

Pia yuko ndugu Kwacha Chisiza, ni Kaimu au Naibu Balozi wa Malawi hapa nchini. Karibu sana. *(Makofi)*

Pia yupo Mheshimiwa Waziri Rajabu Salum, Mjumbe wa Bunge Maalum la Katiba. Karibu sana pale ulipo. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hongera kwa Waziri wa Mambo ya Nje ya Nchi, Mheshimiwa Membe kwa kusoma hotuba yake kwa utulivu sana na kila mtu ameielewa. Hongera sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie mambo haya:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mpango gani wa kupata *percent* ya dinosaur (mjusi) aliyeko Ujerumani? Watu wa Mipingo Lindi Vijijini ambako mjusi huyo ametoka, hawana shule, wala maji: Je, haiwezekani kusaidiwa na Wajerumani hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, taarifa ya mjusi huyo sasa ikoje? Atarudi au harudi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1997 katika Mkutano wa *SADC*, ukizungumzia masuala mbalimbali pamoja na maendeleo Kusini mwa Afrika wakilenga Mikoa ya Lindi – Mtwara Rukwa, Iringa Mbeya, Ruvuma, Pwani, Morogoro (Mikoa ya pembezoni) katika Mkutano huo nchi zilizohudhuria ni nchi za Afrika Kusini, Malawi, Zambia, Mozambique, Zimbabwe na Tanzania. Kulikupwepo maazimio kadhaa lakini leo nataka niongelee Azimio la *Mtwara Corridor,* tarehe 15/12/2004.

Azimio hilo la Mtwara *Corridor* lilitiwa saini na maazimio kadhaa yaliyokuwepo ili *Mtwara Corridor* litekelezwe kwa madhumuni ya kuendeleza mawasiliano, ujirani mwema, biashara, kilimo, uchimbaji madini, utalii, umeme, uchukuzi na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba: Je, maazimio hayo yametelekezwaje? Je, mfuko wa *SADC* peke yake utaweza? Kwanini Serikali isitunge sheria inayohusu uwekezaji katika maeneo ya *Mtwara Corridor* ili kusaidia kutekeleza maazimio hayo?

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwasilisha mchango wangu kwa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kuwa na Wizara hii ni pamoja na kudumisha ushirikiano baina ya nchi na nchi kwa kufuata diplomasia ya ushirikiano na maridhiano. Lakini kwa jinsi mjadala unavyoendelea, inashangaza kuona Waheshimiwa Wabunge wanachangia kwa kuweka misimamo binafsi kwenye mambo ambayo yanaweza kuhatarisha uhusiano baina yetu na nchi ambazo tunajenganazo mahusiano ya Kimataifa hasa kwa nchi zetu jirani.

Kwanza kitendo cha Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kutumia nyadhifa zake na badala ya kutengeneza mahusiano mazuri ya kidiplomasia, anatoa kauli za kuchonganisha nchi na nchi ni kibaya na kinatakiwa kipingwe. Leo hii katika vita ya waasi kati ya *DRC* na kikundi cha *M23* hatujapata hata kusikia Mawaziri wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Nchi za Afrika Mashariki wakitoa maoni yao kuhusu mgogoro huo. Siyo kwa kuwa wananufaika nao ila wana *safeguard interests* za nchi zao kwa gharama kubwa ya kuwajibika.

Leo, Waheshimiwa Wabunge wanaposimama na kuishambulia Rwanda hadharani, huku Waziri mwenye dhamana akishangilia, ni ishara kuwa Wizara hii haiwezi! Waswahili husema, usitukane wakunga uzazi ungalipo! Hatuwezi jua *DRC* na Rwanda nani atatufaa zaidi katika siku za usoni. Pia Waswahili husema, punguza maadui, usiongeze maadui. Lakini ni dhahiri kuwa sera mpya ya Wizara hii ni punguza marafiki, ongeza maadui. Itatufikisha pabaya!

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kejeli kuwa sisi kama Wazanzibar tu wachache na hatuna mchango katika Serikali ya Muungano, ni lazima ikumbukwe kuwa tulipoungana na Tanganyika, kila nchi ilikuwa na hadhi yake. Ndiyo maana leo hii tupo hapa, siyo kwa udogo wetu bali kwa hadhi ya nchi zetu. Hivyo ni haki yetu ya msingi kuweza kuhoji uhalali na misingi ya ugawaji wa nafasi za uwakilishi katika masuala ya Kibalozi na Kidiplomasia. Kila kitu kina gharama yake, na gharama ya Muungano wetu ni pamoja na kupewa nafasi za uwakilishi kwa kadri itakavyopendeza machoni petu kwa manufaa ya Muungano wetu ila siyo kwa hoja za kuwa hatuna msaada kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nafasi za Uwakilishi wa Kibalozi na Kidiplomasia siyo tu kwa ngazi za juu, bali katika ngazi za Maafisa Ubalozi. Ingawa inaonekana kama hoja ya kupuuzwa, ni dhahiri kuwa kuna Wazanzibar wana uwezo, weledi na taaluma zinazostahiki katika kuhakikisha wanapata nafasi hizo za Afisa za Balozi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuthibitishwa wizi wa zaidi ya Shilingi bilioni 3.5 za Kitengo cha Itifaki katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na waliohusika na wizi huo kujulikana, Serikali ilijibu kuwa watu hao hawajafunguliwa mashtaka kutokana na kutokuwapo ushahidi wa kutosha. Sasa Waziri atuambie, kama watu hawajafunguliwa mashtaka, pesa hizo zimekwenda wapi? Inashangaza kuona tunapewa majibu mepesi!

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taasisi muhimu ya kuisimamia Serikali, Bunge lako Tukufu tunaweza kuwapa nafasi Wizara hii kuleta maombi yake ya makadirio ya matumizi huku mianya ya wizi, ufisadi na ubadhirifu wa fedha za walipa kodi ukifanyika kwa staili ya "funika kombe," Naliomba Bunge lako, lisipitishe bajeti hii ikiwa Wizara itakosa majibu ya kuweza kujibu hoja hii ya msingi, kwani sasa Serikali inaonekana kuitunishia Bunge misuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu kuwa uchunguzi wa TAKUKURU ulibaini kwamba kweli fedha hizo zilichotwa Hazina kwa uzembe au kwa nia ya kuiba, Wizara imetoa majibu mepesi kuwa watu hao hawatafunguliwa mashtaka zaidi ya kuchukua hatua za kiutawala kwa kuwa ushahidi hamna. Niweke wazi kuwa, sasa nchi itaingia katika *Guiness World's Records* kwa kushindwa kuwachukulia hatua za kisheria Maafisa wa Wizara kwa wizi wa mchana mweupe huku Mahakama zetu leo zikiwa zinaendelea na usikilizaji wa kesi za wezi wa kuku ambao ushahidi haujakamilika, Watanzania masikini wanaozea mahabusu kwa wizi wa mbao, kwa kufungua biashara maeneo yaliyokatazwa, ila wezi wa Shilingi billion 3.5 za kodi za wananchi inaachwa ipotee hivi hivi. Haiwezekani! Haiwezekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili, siungi mkono hoja ya Serikali mpaka hapo Wizara litakapoeleza Shilingi bilioni 3.5 zinarudije?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni ya Muungano baina ya Tanganyika na Zanzibar. Hivyo basi, katika ugawaji wa nafasi katika nchi mbalimbali ilikuwa uzingatiwe Muungano uliopo. Balozi zote ambazo zinaiwakilisha Tanzania nchi za nje ni 34. Zanzibar ilikuwa na Mabalozi watano na sasa ina Mabalozi wanne tu, sawa na asilimia 1.3 ya Mabalozi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 1.3 siyo dalili za kuenzi Muungano wa Tanganyika na Zanzibar bali kuna fikra zile na mawazo yale yale ya kuifanya Zanzibar kuwa ni Koloni la Tanganyika katika kila hali. Ushahidi wa kauli hii unathibitishwa na uteuzi wenyewe wa Mabalozi ulivyofanyika na mambo mengine yatokanayo na hayo. Kwa mfano, baada ya kustaafu Mohamed

Mwinyi Mzale aliyekuwa Balozi wa Tanzania nchini Sweeden, kwanini hakuteuliwa Balozi mwingine kutoka Zanzibar?

Mheshimiwa Naibu Spika, Hivyo ni kweli kwamba hakuna mtu mwingine kutoka Zanzibar ambaye angeweza kuiwakilisha Tanzania katika Ubalozi huo? Siyo hivyo tu, hata nafasi za Mabalozi wadogo ni asilimia 1.3 jambo ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa kuonekana Muungano huu kuwa na kasoro siku hadi siku. Asilimia 90.3 ya wafanyakazi katika Balozi hizo ni wa upande mmoja wa Muungano, yaani Tanganyika. Hivyo ni kwa kiasi gani Zanzibar inakosa haki na fursa zitokanazo na Wizara hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa dhana inayodhihirika miongoni mwa Watanzania na hasa upande mmoja wa Muungano, yaani Zanzibar kuna haja ya kuangaliwa upya uteuzi na Uwakilishi wa Mabalozi katika nchi za nje baina ya Tanganyika na Zanzibar. Hivyo hivyo, ikiwa ni pamoja na ajira za wafanyakazi wa pande mbili za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2013/2014 katika Wizara hii zilitengwa Shilingi bilioni 30 kwa ajili ya ukarabati wa majengo katika fedha za maendeleo. Cha kusikitisha, Shilingi bilioni 30 zilizotengwa kwa ajili hiyo, fedha iliyopelekwa kwa ajili hiyo ni Shilingi bilioni 6.5 tu. Hivi ni kweli kwamba Serikali hii iko makini na kinachoamuliwa, ikiwa kilichotengwa mwaka jana, 2013/2014 ni Shilingi bilioni 30, zilizotolewa ni Shilingi bilioni 6.5? Shilingi bilioni 24.5 zitatolewa lini? Je, mwaka 2014/2015 zimetengwa kiasi gani kwa ajili hiyo? Maana katika hilo Waziri hakulisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo la Ubalozi lililoko Washington nchini Marekeni limetelekezwa kabisa na limezidi kuchakaa. Kama Serikali ilikuwa na nia ya dhati kwa kiasi ambacho kilitengwa mwaka 2013/2014, jengo lile lingeshughulikiwa na kuwa kitega uchumi ambacho kingeingiza mapato kwa nchi, lakini kinyume chake ni janga ambalo litakuja kuikabili Serikali ijayo katika kulishughulikia jengo hilo kwa gharama kubwa zaidi kinyume na sasa. Malalamiko ya Watendaji na wafanyakazi katika Balozi mbalimbali kuhusu makazi na kutopatiwa mishahara yao kwa wakati ni jambo ambalo limetawala Ofisi mbalimbali za Kibalozi za Tanzania katika nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanini Serikali haiangalii uwezo katika kutoa ajira katika Ofisi na majengo ya Kibalozi ikijua kwamba wanaowaajiri ni wageni wa nchi wanazokwenda kuitumikia Tanzania? Hivi hawaelewi kwamba wafanyakazi hao ni watu wanaotegemewa na familia zao? Hivi hawaoni pia kuwakosesha mishahara yao kwa wakati ni jambo la kuwadhalilisha na kuwafanya wasiishi kwa amani katika nchi walizopangiwa kufanya kazi? Ni kinyume na sheria ya kazi na ni kinyume na haki za binadamu!

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pia nawapongeza viongozi wa Wizara hii kwa kufanya kazi zao kwa bidii na juhudi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara hii kwamba ni vyema ikawa na utaratibu mzuri wa kugawa wafanyakazi katika nchi za nje katika Balozi zetu, ikizingatia pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ushirikiano na nchi nyingine; naipongeza Serikali kuwa na uhusiano mzuri na baadhi ya nchi nyingi duniani na tuendelee hivyo. Lakini napenda kutoa tahadhari, nchi yetu ya Tanzania isipendelee kuifuatafuata nchi ya Somalia, maana hawa wanatafuta pa kuanzia tu ili wavamie watu wetu na kufanya hujuma. Kwa hiyo, kama hakuna sababu za msingi, tuachane nao.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, namwomba Mheshimiwa Waziri aje Zanzibar kwa kufanya ziara ya kikazi na atuarifu Wabunge tumpokee kwa wingi. Asiogope, kwani yeye ni kiongozi mpenda watu na kazi, na kule Zanzibar kuna Ofisi yake.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 14 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, Wizara imeendelea kutekeleza Diplomasia ya uchumi kwa kuvutia wawekezaji wenye sifa na vigezo kuja kuwekeza katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuitangaza nchi yetu, nchi za nje, Maafisa wa Wizara hii wanaopelekwa kufanya kazi nchi za nje, ihakikishwe kwamba ni wale wenye ufahamu wa Diplomasia ya Uchumi. Hii itasaidia sana, nchi yetu kutangazwa vizuri nchi za nje na hivyo kupata wawekezaji wenye sifa, vigezo na wanaomaanisha kuwekeza hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha ambacho miaka ya nyuma kimekuwa kikijitangaza sana katika *media* zetu na huenda ndio sababu kimeweza kufanya vizuri katika kukusanya mapato mazuri ya kuridhisha, Aidha, napendekeza kituo hicho kiendelee kujitangaza ndani ya nchi na nje ili wageni wengi zaidi waweze kukifahamu kituo hicho na hivyo kukitumia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jukumu mojawapo la Wizara ya Mambo ya Nje kukitangaza Kiswahili katika mikutano mbalimbali nje ya nchi. Tunaamini

kwamba Wizara haitasita kuandika ripoti/taarifa zake kwa Kiswahili ili kukiendeleza. Lakini je, Wizara hii huwasilisha taarifa zake katika mikutano mbalimbali nje ya nchi kwa lugha gani? Aidha, napendekeza, endapo taarifa/ripoti za Wizara haziandikwi kwa Kiswahili, basi ni vema ikafanyika hivyo, ili Kiswahili kiendelee kupanuka kwa kupata wateja wengi zaidi kuja nchini kuona mila na tamaduni zetu ambazo huunganishwa na Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje ukurasa wa 15, inaelezea kupatikana kwa soko huko China kwa mazao yetu, kwa mfano tumbaku, mazao ya baharini na mchakato unaendelea kwa mazao mengine kama korosho, kahawa, ufuta, karanga, ngozi na kadhalika ni taarifa nzuri kwa wakulima wengi ambao baada ya kuvuna mazao yao, mara nyingi wamepata changamoto ya kupata soko la uhakika ili kupata maendeleo na kumudu maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupatikana soko la mazao hayo, ni vema wananchi wengi zaidi wakafahamishwa kupitia *media* kuhusu fursa hizo kuliko kuwaachia watu wachache tu kunufaika na fursa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi waishio Ulaya na Amerika, huwa na mawasiliano finyu sana katika Balozi zetu. Hali ya kifedha ya Maafisa wa Balozi zetu huwa hairidhishi na hivyo kushindwa kuwasiliana na Watanzania waishio nje kwa kuwa na vikao nao vya kutosha. Wengi wangeweza kuwekeza hapa nchini endapo wangepata taarifa za kutosha na zilizo sahihi kuhusu uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo suala la uraia wa nchi mbili ambalo wana *Diaspora* wamelizungumzia kwa muda mrefu, Serikali itilie maanani suala hilo kwa kuanza mchakato wa kuwezesha jambo hilo hata bila ya kusubiri vikao vya Bunge maalum. Uraia wa nchi mbili utasaidia sana kwa wana *Diaspora* kuwekeza hapa nchini katika maeneo mbalimbali na hivyo kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kwanza kabisa kumshukuru Mungu kwa uwezo wake na kuniwezesha nami nitumie nafasi hii kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwa nafasi ya kipekee nimpongezee Mheshimiwa Waziri pamoja na jopo lake la wataalam kwa kuandaa bajeti nzuri

yenye kutekelezeka na kuhakikisha mahusiano yetu na nchi nyingine yanazidi kukua. Nipongeze Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa utawala wake bora na ufanisi mkubwa katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imezidi kuwa na mahusiano mazuri na Mataifa mbalimbali kote duniani, ni jambo zuri na la kujivunia kwani mahusiano hayo yanaonesha ni kiasi gani Taifa letu linavyokubalika Kimataifa. Hivyo basi, nasi hatuna budi kudumisha uhusiano huo na pia kama nchi kujifunza yale mazuri kutoka kwa wenzetu waliopiga hatua kimaendeleo na kupata fursa ya kupeleka wataalam wetu katika nchi hizo ili kujifunza zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana Watanzania walipokea ugeni mkubwa wa kiongozi wa Taifa la Marekani, Rais Barack Obama aliyeambatana na mamia ya wafanyabiashara kupitia ziara hiyo, Marekani ilizindua Mpango wa Umeme Afrika *(Power Africa)*, ambao utaongeza kwa mara mbili upatikanaji wa umeme katika Bara la Afrika. Tanzania ni miongoni mwa nchi zitakazonufaika na mpango huo unaolenga kuzalisha zaidi ya Megawati 8,000 za umeme katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Marekani imeahidi kutoa zaidi ya dola za Marekani bilioni saba. Kampuni za Marekani, Ulaya, Asia na Afrika ziliahidi kutoa zaidi ya Dola za Marekani bilioni tisa kwa ajili ya mradi huo kwa miaka mitano ijayo. Nchi yetu pia kupitia ziara hiyo ilipata fursa ya kujitangaza na kujiweka katika nafasi nzuri ya kukuza uchumi, biashara, utalii na uwekezaji, ni hatua nzuri kwa nchi kwani kama tusingekuwa na mahusiano mazuri na nchi hizi, basi tusingeweza kupata mradi mkubwa kama huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu iliingia katika mgogoro na nchi ya Rwanda, palitokea maneno na vyombo vya habari vikaandika mambo mengi sana kuhusu kiongozi wetu kusemwa vibaya na majirani zetu na mara nyingine kuliandikwa habari za upotoshaji, lakini napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa uvumilivu wake iliouonesha kipindi hicho kwa kutumia busara kubwa katika kutoa ufafanuzi wake, kutumia maneno ya kiungwana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ilionesha ni kiasi gani nchi yetu imekomaa kidemokrasia kwani ingawa kulikuwa na chokochoko za maneno ya kuudhi, lakini viongozi wetu walitulia na hawakukurupuka katika hilo. Hiyo ndio Tanzania, nchi yetu yenye viongozi safi na wazuri, hatuna budi kujivunia hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara iendelee na ushirikiano mzuri kama uliokuwepo hapo awali ila Serikali isikubali tena kwa mara nyingine

viongozi wetu kuambiwa maneno ya kejeli, inapaswa kukemea kama nchi kwa kutumia lugha yenye utashi mkubwa ili jambo hilo lisiweze kutokea kwa mara nyingine tena. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa uwezo wake mkubwa katika shughuli za Kimataifa kwa kutuletea sifa kubwa kwenye Taifa letu katika nyanja mbalimbali za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kupitia Bunge lako Tukufu nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa tuzo aliyoipata ya kiongozi bora wa Afrika, ni alama tosha kuwa tunaye kiongozi shupavu, mwenye kuleta maendeleo katika nchi yake na Afrika kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu hivi sasa imepata sifa mbaya katika baadhi ya nchi kama China, nchi yetu imeonekana kama njia ya kuvushia biashara haramu, hivi sasa Mtanzania akionekana anakwenda nchini China, kuanzia uwanja wa Ndege wa kwetu hapa mpaka huko anakokwenda ugenini, wenyeji wanakuwa makini sana kwa kumkagua wakihofia atakuwa amebeba madawa ya kulevya ama kitu chochote ambacho hakiruhusiwi kwa mujibu wa Sheria za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka kesi za madawa ya kulevya zimekuwa zikiongezeka na baadhi ya watuhumiwa wamekuwa wakihukumiwa kunyongwa, vifungo, lakini ushirikiano wa kidiplomasia uliokuwepo tangu awali baina ya China na Tanzania ndio unaopelekea kwa baadhi ya watuhumiwa wa Kitanzania wanaokutwa na hatia kuhukumiwa kunyongwa, lakini wanabadilishiwa adhabu hiyo na kufungwa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna haja sasa ofisi za Ubalozi wetu nchini China kuweka utaratibu wa kukutana na Watanzania wanaoishi huko na kuzungumza nao ili kuwaelimisha juu ya kufuata sheria na taratibu na kuwakumbusha kuwa biashara hiyo haikubaliki na ni hatari, pia inadhalilisha Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hii ya madawa ya kulevya imekuwa ikikithiri sana kwa Watanzania nchini China bila woga. Balozi zetu naziomba kuweka utaratibu wa kuwa karibu na Watanzania wanaoishi katika nchi hizo kwani kumekuwa na malalamiko mengi sana kuhusu Balozi zetu kutokuwa karibu na Watanzania mpaka pale yanapotokea matatizo ndipo hujitokeza, lakini kungekuwa na utaratibu wa Balozi kuwa karibu na watu wake basi ushirikiano huu ungesaidia sana hata kuwatambua mapema watu wanaofanya biashara hizo haramu na kuwadhibiti kabla hawajaingia katika nchi hizo, kwani ugenini watu wanajuana vizuri na kwa kuwatumia wenyewe itakuwa rahisi hata kudhibiti kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie kidogo kuhusu Balozi zetu, lakini hususani Ubalozi wetu nchini Marekani *New York*. Ofisi ile inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa rasilimali watu na ufinyu wa bajeti wa kuendeshea shughuli za ofisi hiyo. Ila napenda kuipongeza Serikali kwa kuchukua hatua za kukabiliana na changamoto hizo mbili kwa kununua jengo la Ubalozi wetu *New York*, kwani Serikali ilinunua jengo la Ubalozi kwa thamani ya dola za Marekani milioni 24.5 lenye urefu wa ghorofa sita ambalo lipo Mtaa wa 53 Na. 307E, ambalo kwa taarifa ghorofa mbili zitatumika kama ofisi za Ubalozi huo na ghorofa zitakazokuwa zimesalia zitatumika kama kitega uchumi kwa ajili ya kupangisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni uhaba wa rasilimali watu, ipo haja sasa ya Serikali kupitia Wizara kuajiri watu wenye taaluma ya mahusiano ya Kimataifa na kuwapeleka katika Balozi zetu kwani kuna Balozi nyingi zinakabiliwa na changamoto ya rasilimali watu, mfano kama ofisi hii nayoizungumzia hapa ya Ubalozi Nchini Marekani *New York*. Ofisi hiyo imeomba Wizara kuiongezea rasilimali watu, ili waweze kwenda na kutuongezea nguvu katika kazi mbalimbali kwa sababu uwakilishi wa Tanzania unaushawishi mkubwa *UN* baadhi ya nchi nyingi na Mashirika ya *UN* yanapenda kuishirikisha Tanzania katika kupata maoni na miongozo kuhusu masuala mbalimbali ya Kimataifa katika Nyanja ya Siasa, Uchumi, Amani na Usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukipata faida nyingi sana kwa uwakilishi wetu *UN*, faida ya kwanza ni kuisaidia *UN* kutekeleza majukumu yake likiwemo jukumu la kusaidia Umoja wa Mataifa kutekeleza jukumu lake na kusimamia amani, usalama na maendeleo duniani kwa mujibu wa Katiba ya *UN* ya mwaka 1945.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida ya pili ni kutoa ushawishi kwa nchi zilizoendelea na nchi za Kiafrika. Faida ya tatu, ni kuendeleza diplomasia ya kiuchumi kwa kushawishi wawekezaji na watalii kuja Tanzania kuwekeza na watalii wa nje kuja ndani kuleta mapato. Faida ya nne ni kusimamia uendelezaji wa Sera ya Tanzania ya uhusiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba kati ya Balozi zetu mbalimbali, ila Ubalozi wa *New York* umeweka ushawishi mkubwa duniani toka tumepata uhuru. Kwa hiyo, kila ofisa wetu anayekwenda kufanya kazi pale anatakiwa adumishe heshima hiyo kwa Taifa letu, kwa sababu Tanzania imeongoza kushawishi Jumuiya za Kimataifa katika masuala ya maendeleo na masuala ya amani duniani na pia imeshiriki kikamilifu kuziletea uhuru baadhi ya nchi za Afrika ikiwemo Msumbiji, Zimbambwe na nyingine nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuendelea kuhakikisha Kituo cha *New York* kinadumisha heshima hiyo ya muda mrefu inayotuletea sifa kama Taifa, namwomba Waziri atueleze changamoto hizi za upungufu wa rasilimali watu wanakabiliana nazo vipi? Je, kwenye Ubalozi huu wa Tanzania nchini Marekani *New York* walishatatua tatizo hilo? Pia ni Balozi ngapi zina changamoto kama hiyo na mpaka sasa wamechukua hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uamuzi wa Serikali kununua jengo la ghorofa sita nchini Marekani kwa ajili ya shughuli za Ubalozi wetu ni jambo la kupongezwa kwani ofisi hizo zitatumia ghorofa mbili tu na hizo zilizobaki watapangisha na kusaidia kupata kipato, fedha hizo zitapunguza mzigo kwa Serikali kwani Balozi zetu zimekuwa ni tegemezi kwa asilimia kubwa hutegemea matumizi yake kutoka Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuendelea na mpango huo katika Balozi zetu za nchi nyingine kununua majengo yenye tija na kuwekeza ili kupata faida ambayo itasaidia sana kuipunguzia Serikali matumizi katika bajeti zake kila mwaka na hivyo kutumia fedha hizo katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ila napenda kutoa angalizo kuwa Serikali, iweke usimamizi mkubwa wa mapato yatokanayo katika majengo yetu yote tunayomiliki na kuyapangisha, kwani watu wachache wanaweza kufanya ubadhirifu kwa kupitia mwanya huo mdogo wa Serikali kutofanya ukaguzi wa mara kwa mara. Kuna changamoto ya rasilimali watu katika Balozi zetu imejitokeza, najiuliza ni kwa nini changamoto hiyo ijitokeze wakati tunao vijana wetu wengi waliosomea mambo ya mahusiano ya Kimataifa na hawana kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Wizara ichukue hatua za haraka kwa kushirikiana na sekta husika ya ajira na kazi kuweza kutatua changamoto hiyo kwani ni aibu kusikia kuna upungufu wa wafanyakazi katika Balozi zetu ilihali vijana wetu kila siku wanamaliza vyuo vikuu na hawana ajira, kuna nini hapo? Ni lazima Wizara itatue changamoto hii haraka iwezekanavyo ili kuleta tija katika Balozi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza tena suala zima la utalii wetu kuanza kutangazwa kwanza kupitia balozi zetu katika nchi mbalimbali, naishauri Serikali kuwa hii pia ni njia nzuri ya kuwavutia wageni kwa kuandaa maonyesho ambayo yataonesha vitu mbalimbali vya kitalii vinavyopatikana hapa nchini kwetu, ushauri huu niliutoa katika Bunge lililopita ila kwa umuhimu wake kwa manufaa ya Taifa letu katika kukuza uchumi wetu kupitia sekta hii nimeona nirudie tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila kitu ni lazima kitangazwe, huwezi kujua jambo lolote lililopo katika nchi nyingine kama si kwa kusikia kupitia matangazo, ama kutembelea Balozi zao. Nchi yetu kama tujuavyo imebarikiwa sana na historia nzuri katika mambo ya kitalii, hivyo Balozi zetu zitumie fursa hiyo kutangaza utalii wetu kwa kushirikiana na sekta husika, kufanya hivyo kutafanya idadi ya watalii kuongezeka na kuliingizia Taifa pato.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kuishauri Wizara kupenda kutumia samani za ndani za asili ya Tanzania katika Balozi zetu, kama picha mbalimbali za vivutio vyetu, pia kuonesha video mbalimbali za mbuga zetu za wanyama, historia iliyopo katika Miji ya Bagamoyo, Tanga, Mtwara na kadhalika. Hali hiyo itawafanya wageni pindi wanapotembelea Balozi zetu kujionea na kutaka kujua zaidi kuhusu vitu hivyo asilia na hatimaye kuja kutembelea na kujionea vivutio mbalimbali hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Kamati ya Mambo ya Nje kutoa masikitiko yangu kuhusu bajeti finyu iliyopangiwa Wizara hii ya shilingi bilioni 191.92 hasa ukitilia maanani mazingira ya ofisi za Balozi zetu sehemu mbalimbali. Pamoja na hayo, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Mabalozi wote pamoja na watumishi wetu kwa kutekeleza majukumu yao licha ya hali mbaya ya kifedha walinayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijadili maeneo yafuatayo japo kwa ufupi. Kwanza, ni utekelezaji wa diplomasia ya kiuchumi. Mimi nashangaa iwapo Serikali iliyopitisha Sera hii, ikatunga Sheria ya *Tanzania Investment Centre*, Ibara ya 38 imeweka mpango wa kupunguza kodi mbalimbali ili wawekezaji wenye mitaji kutoka nje ya nchi wawekeze Tanzania, Wabunge leo wanataka vivutio hivyo *(tax incentives)*vifutwe. Kwa hali hii, Serikali yetu itakosa uaminifu nawawekezaji wataondoka. Nashauri Wizara ya Fedha *(TRA),* Waziri Mkuu (Uwekezaji) na Wizara ya Mambo ya Nje ziwe na Sera na kauli moja ili diploma ya kiuchumi iwe na maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili napenda kuzungumzia kuhusu biashara ya utalii. Wizara hiina Wizara ya Utalii ishirikiane kuleta wawekezaji katika sekta hii na kuuza biashara hii. Maofisa wa Bodi ya Utalii wapelekwe nchi zenye kuleta watalii Tanzania siyo kutumia Maafisa wa Ubalozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni*career diplomat*. Mheshimiwa Rais ashauriwe afute utaratibu wa kuwachagua wanasiasa kuwa Mabalozi badala ya Maafisa waliosomea kazi hii. Kwa mfano, kuwachaguaWabunge waliokosa nafasi au Wakuu wa Mikoa waliostaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika majumuisho ya mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naomba maelezo ya Waziri juu ya masuala yafuatayo: Ni kwanini mpaka kufikia tarehe 31 Machi, 2014, fedha ambazo Wizara imepata kwa ajili ya miradi ya maendelo ni shilingi bilioni sita, mia nne sitini na tano milioni na mia nane elfu tu wakati bajeti iliyopitishwa ni shilingi bilioni 28? Ni lini fedha zilizobaki zitatolewa na nini athari za hali hiyo kwa kuzingatia kwamba kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi ya ujenzi kunaongeza mzigo wa gharama kwa nchi na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nini sababu za Wizara kutokamilisha kwa wakati ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yaliyokadiriwa kuwa shilingi bilioni 16.9. Kama kiwango hicho hakikuweza kupatikana chote kwa kukusanya shilingi bilioni 12.9 kwa mwaka 2013/2014, ni mkakati gani mmeandaa wa kukusanya shilingi bilioni 18.5 katika mwaka wa fedha 2014/2015? Aidha, Wizara imeshughulikiaje madai ya udhaifu na ufisadi katika baadhi ya Balozi yaliyoelezwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* juu ya maduhuli na matumizi katika mwaka ulioishia tarehe 30Juni 2013?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango waKujitathimini Kiutawala Bora Tanzania *(APRM)* unapaswa kuweka kipaumbele katika mapendekezo ya ripoti zake. Hivyo wakati makala za uwasilishaji wamatokeo ya ripoti za tathmini zikiandaliwa, kwa sasa *APRM* itoe nakala za ripoti zake zilizotayari kwa Wabunge tunaohitaji. Naomba kabla ya kupitishwa kwa bajeti ya Wizara hii, nipatiwe nakala ya ripoti zote zinazoweza kupatikana kwa ajili ya kuzitumia kwenye kazi za Kibunge za kuishauri na kuisimamia Serikali katika mkutano huu wa Bunge unaondelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Diplomasia kinapaswa kupewa kipaumbele katika mgawo wa fedha za maendeleo na kuongezewa kwa kadiri ya mahitaji katika mwaka wa fedha 2014/2015 kutoka vyanzo vya Wizara na vyanzo vingine katika Serikali. Chuo hiki pamoja na utoaji huduma kinapaswa kuwa Kituvu cha Fikra kwa Serikali, nchi na taasisi za wananchi katika masuala ya utatuzi wa migogoro, itifaki, diplomasia ya uchumi,stratejia na menejimenti ya mahusiano ya kidiplomasia. Hivyo, Chuo kitoe nakala ya Mpango Mkakati waMiaka Mitano 2012/2013, 2016/2017 kwa Wabunge tunaohitaji kufuatilia utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu kwa kuwa na makao yake Tanzania, Wizara ya Mambo ya Nje ya Nchi yetu inapaswa kuwa mstari wa mbele kuitetea katika Umoja wa Afrika. Ni mkakati

gani Wizara inao kufanya Watanzania waitumie Mahakama hii na pia ipate mamlaka ya kutosha kusimamia haki za wananchi wa Afrika?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mapitio ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2013/2014, ningeomba majibu na marejesho kutoka kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa niliyoyahoji kwa nyakati mbalimbali kati ya mwaka 2011 na 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Diplomasia ya Uchumi: Sekta ya Viwanda – kuhusu kiwanda cha Nguo cha Urafiki chenye ubia kati ya China (51%) na Tanzania (49%), ni nini matokeo ya majadiliano niliyoomba yafanyike kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya China kuongeza msukumo wa Kiserikali kwa ajili ya ufumbuzi wa matatizo katika kiwanda hicho? Yapo masuala yenye kuhitaji mjadala wa ndani kitaifa lakini ambayo yanaweza kupatiwa ufumbuzi kimataifa nchini China kupitia diplomasia ya kiuchumi kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikano wa Kimataifa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekta ya ajira, pamoja na maelezo ya fursa zinazotarajiwa kupatikana katika nchi ya Dubai kuelekea *World Expo* 2020, naomba mrejesho juu ya namna Wizara ya Mambo ya Nje ilivyotumia diplomasia ya uchumi katika kuwezesha mipango maalum ya ajira kwa vijana unatekelezwa nchini kwa ushirikiano na washirika mbalimbali wa maendeleo. Katika mwaka za fedha 2014/2015, fursa za ajira zitakazopatikana, naomba Wizara ya Mambo ya Nje iliweke Jimbo la Ubungo kati ya maeneo vijana wa kike na wa kiume watahamasishwa kuzitumia fursa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa mikataba na makubaliano ya Kimataifa unahitaji ushauri na usimamizi wa karibu wa Kibunge. Hivyo, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa iwezeshe Kamati za Kisekta za Kudumu za Bunge kupewa mkataba kati ya Tanzania na nchi nyingine (*Bilateral Agreements*) iliyotajwa kwenye aya ya 73 (ukurasa wa 24 na 25) wa kitabu cha hotuba. Pamoja na kuwa sio mikataba yote ya kimataifa inahitaji kuridhiwa na Bunge, mikataba yote inahitaji ushauri na usimamizi wa Kibunge. Kazi hii haiwezi kufanywa na Kamati ya Kisekta ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa kimataifa pekee bali Kamati zote zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha *(AICC)* kwa kupewa kazi ya kuendesha kituo kipya cha mikutano cha Julius Nyerere (*JNICC*) Dar es Salaam na kwa miradi ya mingine ya ujenzi inayopangwa kutekelezwa kinapaswa kufanyiwa mabadiliko ya kimuundo na kimsukumo kukidhi matakwa na mahitaji ya kukua huko na kuongeza ufanisi.

Aidha, inapaswa kutekeleza pia miradi yenye kugusa jamii (*Corporate Social Responsibility*) kwa kutoa baadhi ya kumbi na ofisi zake kwa asasi za ndani za kiraia zinazohusisha masuala ya mahusiano ya kimataifa, diplomasia ya uchumi na stratejia kwa vipindi na kazi maalum.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu kwa utendaji mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika,nimpongeze kwa pekee Mheshimiwa Waziri kwa jinsi anavyotumia muda wake mwingi kupigania Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukiona juhudi zake za kutuletea viongozi wakubwa wa Kimataifa katika nchi yetu. Ni jambo jema na lenye tija kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika,changamoto kubwa, Serikali iangalie jinsi gani itasaidia Watanzania wanaosoma nje ya nchi pale kunapotokea tatizo. Ni vyema Wizara ikakaa pamoja na Wizara ya Elimu kuangalia jinsi ya kusaidia wanafunzi wanaoenda nje kusoma na haswa Madaktari na fani za *gas* na nyingine ambazo hatuna wataalam kuwapa angalau mkopo japokuwa ni kidogo unaolingana na ule wanaopewa wenzao wanaosoma Tanzania. Hiyo itaonesha jinsi gani Serikali yao imewajali kwa kuwachangia pindi watakapomaliza masomo wataipenda nchi yao na Serikali yao kwa msaada waliopewa. Pia wao ni watoto wa Tanzania kama wengine, kama waliopo hapa wanapewa mkopo mpaka wanaoenda vyuo binafsi kwa nini wanaosoma nje tusiwasaidie?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja 100%, ushauri wangu uzingatiwe.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia uraia wan chi mbili *(dual citizenship)*. Ni muda mrefu sasa toka suala hili kujadiliwa lakini bila ya kupata jibu la moja kwa moja kuhusiana na kigugumizi cha Serikali juu ya suala hili. Tumetolewa mfano na mgeni kutoka Bunge la Kenya Mr. Wako faida za *dual citizenship* walizopata Kenya baada ya wao kupitisha Muswada huo lakini mpaka sasa Serikali yetu imekuwa kama kipofu juu ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, naiomba Serikali kuliharakisha suala hilikwa kuwa faida zake ni kubwa katika kujenga nchi yetu mfano, viwanda vidogo vidogo, nyumbaza biashara *(malls)* na hata nyumba ya kuishi katika sehemu zenye hadhi, ajira nyingi kwa vijana wetu, hivyo itapunguza idadi ya vijana wasio na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Balozi za Tanzania nchi za Nje. Katika kuitangaza Tanzania na vivutio vyake vya utalii, suala hili linafanywa na Balozi zetu lakini sio kwa kasi inayotakiwa kama wafanyavyo majirani zetu Kenya. Hivyo, inatakiwa Mabalozi wetu wote waelimishwe na sio suala la vivutio tu hata nyanja nyingine kama biashara vilevile, tuna bidhaa nyingi kwa ajili ya kuuza nje lakini zinaozea hapahapa kwetu kwa ajili ya kukosa soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko kuhusu nafasi za Mabalozi kwa upande wa Zanzibar. Mabalozi wengi waKizanzibari wanapelekwa nchi za Kiarabu tofauti na Mabalozi wa Bara wanaopelekwa nchi za Ulaya. Kwa maana kumekuwa hakuna uwiano au kuna ubaguzi.Ni lini Serikali itahakikisha suala hili linapatiwa ufumbuzi wa kudumu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Watanzania ambao wapo nje nao wawe na uhuru au washirikishwe katika upigaji wa kura kama Kenya, raia wao ambao wanaishi nje wanashirikishwa katika kupiga kura. Vile vile Watanzania ambao wapo nje baadhi yao wana uwezo kwa maana hiyo naiomba Serikali iwashirikishe waje kuwekeza nchini na watatusaidia kutangaza utalii, kupitia Mabalozi wetu tutangaze utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania ambao wako nje wamekuwa wakinyanyaswa na wengine hulazimishwa kuuza dawa za kulevya. Naomba Mabalozi ambao wako nje ya nchi wanaoiwakilisha Tanzania walishughulikie suala hili kwani Watanzania wanapata tabu hasa wanawake ambao wanafanya kazi za ndani wanateswa, Pasipoti zao zinafichwa.Vilevile baadhi yaowamekamatwa na dawa za kulevya nchi za nje na hukumu zao hatujui zinaendelea vipi. Je,ni Watanzania wangapi ambao wamekamatwa na dawa za kulevya nchi za nje?Je,ni Watanzania wangapi ambao wanatumikia kifungo nchi za nje? Je,ni Watanzania wangapi ambao wamenyongwa nje ya nchi?

**MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nashauri yafuatayo yafanyike kama yanatufaa:- Tunayo majengo na viwanja katika nchi nyingi, iwapo Serikali haina fedha za kuweza kujenga au kukarabati majengo yake ni muhimu sana Wizara ikafanya mazungumzo ya kina na mifuko ya hifadhi, mfano *NSSF, PPF* na kadhalika, waweze kuingia ubia na kujenga au kukarabati majengo hayo, yakodishwe. Kwa maana hii mifuko hiyo itarudisha fedha zake, lakini pia faida itakayopatikana itasaidia kupunguza gharama zingine ubalozini.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Wizara ya Mambo ya Nje ishirikiane na Wizara ya Utalii iweze kusaidia kutangaza utalii katika balozi chache. Lakini pia Wizara ya Mambo ya Nje kila inapotokea Mabalozi wetu walio nje wakija, ni

muhimu wakatembelea katika hifadhi zetu na pia kufahamu fursa zilizopo nchini na kutafuta wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo katika hotuba ya bajeti ya upinzani ukurasa wa 10 ni muhimu Wizara ya Mambo ya Nje ikazingatia kuangalia balozi ambazo zipo ukanda mmoja zikaamua ni wapi kuwepo na balozi mmoja kuliko kuwa na balozi 6.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa siYo kwa umuhimu, napongeza mipango mizuri ya Wizara, nawapongeza Mawaziri, Naibu Waziri na Watendaji wote.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, nataka kujua yafuatayo:-

(1) Watanzania wangapi wanaishi nchi za nje ambao wameukana uraia wa Tanzania?

(2) Watanzania wangapi wanaishi nje kwa *VISA*?

(3) Watanzania wangapi wanashikiliwa nje kwa makosa ya jinai?

(4) Watanzania wangapi wamekuwa *deported* kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita?

**MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Bernard Membe, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa jinsi alivyowasilisha hoja ya bajeti ya Wizara kwa ufasaha na umakini wa hali ya juu. Ni kielelezo cha ushirikiano kati yake na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mahadhi, Katibu Mkuu Haule, Naibu Katibu Mkuu Balozi Gemaha na wafanyakazi wa Wizara. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wangu unahusu ushirikiano katika au baina ya nchi za Bonde la Mto Nile. Taarifa za habari (vyombo vya habari) leo tumeelezwa majibu ya Wizara kupitia Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Mkataba wa *Cooperative Framework (CTA)* uangaliwe upya kwa sababu ya kutetea maslahi ya Misri. Naamini waandishi wamekosea. Kwani Tanzania imekuwa mstari wa mbele kupinga *hegemony* ya Misri kuhusu suala la Nile. Tumeongozwa na *Nyerere doctrine on state succession* na tamko la mwalimu Nyerere la mwaka 1962 kuhusu Tanzania kutotambua mkataba ya Mistri na Uingereza kuhusu Nile wa 1929.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *CFA*, Tanzania ndiyo iliyoongoza mazungumzo na majadiliano ya *CFA* kwa niaba ya nchi 7 za juu za Bonde la Nile. Tumeheshimika sana kwa mchango wetu wa kufanikisha *CFA*. Maslahi ya Misri yamezingatiwa kikamilifu katika *CFA*. *CFA* haizungumzii matumizi sawa, inazungumzia matumizi ya uwiano *(equitable)*. Maana yake Misri kwa vyovyote vile itaendelea kutumia maji mengi kuliko nchi nyingine. Vile vile CFA inazungumzia umuhimu wa kutoathiri nchi nyingine katika matumizi ya Nile, kipengere muhimu sana katika matumizi ya maji shirikishi. Daima tunaongozwa na falsafa ya Mwalimu Nyerere kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, ziko nchi nyingi duniani zina uhusiano wa kibalozi na Tanzania. Raia wa nchi hizi wanapotaka kuja Tanzania hupewa Visa kwenye ofisi za ubalozi wetu nchini kwao. Nasi pia Watanzania tunapokwenda huko tunachukua Visa kwenye ubalozi wa nchi hizo hapa kwetu.

Mheshimiwa Spika, zipo nchi ambazo zimeondoa huduma za Visa kwenye Balozi zao hapa nchini na kupeleka huduma hiyo nchini Kenya. Naiomba Serikali iondoe huduma hiyo kwenye Balozi zetu nchini kwao na kupeleka nchi jirani. Mfano wa nchi hizo ni Uingereza na Canada.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli sina budi kuchukua nafasi hii kumpongeza Balozi wetu wa Tanzania nchini Ufaransa kwa vile Balozi huyu ameonesha mwamko mzuri katika uwakilishi wake nchini Ufaransa. Kwa nini nikasema hivi? Huyu Balozi ambaye ni mwana mama anaitumia nafasi yake vizuri sana kuiwakilisha nchi yetu siyo kisiasa tu ila zaidi anakwenda mbali kwa kuiwakilisha nchi yetu kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa lililopo ni vyombo vyetu vya utalii kutokuwa na uwakilishi mzuri nchini Ufaransa wakati wa maonesho mbalimbali ya utalii yanapofanyika nchini Ufaransa. Hakuna asiyeelewa ni vipi nchi ya Ufaransa inavyoeleweka katika jinsi inavyotoa watalii wengi kutembelea nje ya nchi yao. Hivyo basi tunaomba Wizara hii iendelee kuwezesha kifedha balozi zetu zilizopo nchi za nje, lakini zaidi katika nchi hii ya Ufaransa ambapo mwanamana huyu yuko *commited* kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ni wakati mzuri sasa kwa nchi yetu kujenga mazingira mazuri zaidi ili balozi zetu zitumike kiuchumi katika uchumi wetu hasa katika

sekta ya utalii na vilevile kutafuta wawekezaji kwa kuitangaza Tanzania. Sekta muhimu ni utalii, kilimo na hata miundombinu.

Mheshimiwa Spika, vilevile nachukua nafasi hii kumpongeza balozi huyu na watendaji wake wote kwa kusimamia hadi Serikali kuweza kununua jengo lake zuri la kisasa mjini Paris.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kumpongeza balozi huyu yeye pamoja na watendaji au wasaidizi wake katika ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo fedha huwa ni tatizo kwa ofisi hii, na maonesho ya Kilimo au Utalii mjini Paris, basi Balozi huyu halali kucha ili kuhakikisha na nchi yetu inashiriki. Hivyo hutafuta njia mbalimbali za kutafuta fedha ili na yeye apate banda la uwakilishi, na hatimaye anafuzu kupata fedha na nchi yetu kuwepo katika maonesho hayo.

Mheshimiwa Spika, haya ninayoyasema nina ushahidi nayo na ni Balozi mwana mama ngangari asiyepoteza muda wala kungoja fedha za ofisi ambazo ni finyu kwa bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba Wizara itoe fedha hasa za mishahara na posho nyingine kwa wafanyakazi wote wa Balozi zote ili Watanzania wasiadhirike wakati wako nje ya nchi, sehemu ambayo hakuna mjomba wala kaka wa kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazotengwa zitolewe na ziwafikie walengwa kwa wakati la sivyo Balozi zetu zitaadhirika na kupata usumbufu kwa maisha yao ya kila siku.

**MHE. MOSHI S. KASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa wanayoifanya hasa kwa kukuza mahusiano na mataifa ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali kupitia Wizara hii kutafuta masoko ya mazao yetu ya kahawa, tumbaku, pamba na mazao mengine kama ya mbogamboga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ikishirikiana na Wizara ya Kilimo na Viwanda wanaweza kabisa kutatua tatizo kubwa lililopo kwa sasa. Mazao mengi ni ya kusuasua sana, hivyo tukijenga hoja nzuri na maandalizi mazuri tutakuwa tumewasaidia sana jamii ambayo inategemea sana kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependea kuishauri Serikali ni juu ya jirani zetu wa nchi ya Burundi kwenye Ziwa Tanganyika. Wavuvi wa kutoka nchi ya Burundi wamekuwa wakivua sehemu ya nchi yetu na kuleta

uharibifu mkubwa sana, uvuvi wa nyavu zenye sumu ambazo zinahatarisha sana viumbe hai vilivyomo ndani ya Ziwa Tanganyika. Wavuvi wetu wanalalamikia sana jambo hili ambalo kama Serikali kupitia ubalozi tukawaeleza mazara yanayofanywa na raia wasio wema katika Ziwa Tanganyika. Mheshimiwa Waziri naomba sana ulifuatilie jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mpaka wa Ziwa Tanganyika ambalo ndilo linatenganisha mpaka kati ya Congo *DRC* na Zambia na Burundi, ni vema Wizara iangalie umuhimu wa kuweka mpaka huu wa maji kuliko ilivyo sasa haijulikani ni wapi tunapopakana.

Mheshmiwa Naibu Spika, ulinzi wa mpaka huu siyo madhubuti licha ya kuwa kuna vituo vidogo vidogo, ninaomba viimarishwe vituo hivi na kuwa na vifaa vya ulinzi vilivyo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni muhimu naomba Serikali iongeze bajeti ili iweze kwenda na uhalisia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri. Karibu sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje ya Nchi na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Mahadhi, una dakika 20!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya njema kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru kipekee Mheshimiwa Bernard Kamilius Membe, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa uongozi makini na kuhakikisha tunapata ufanisi mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara anayoiongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uongozi wake mahiri ndani ya Bunge hili. Aidha, napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Spika pamoja na wewe Naibu Spika, kwa namna wanavyoliongoza Bunge hili. Pia nawashukuru Wabunge wenzangu wote kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa. Nawaombea kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao hapa Bungeni na kwenye Majimbo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kwa namna ya pekee kuwashukuru wananchi wenzangu na wapiga kura wa Jimbo la Muyuni. Nawashukuru kwa imani kubwa wanayoendelea kuonesha kwangu, nitaendelea kuwa nao karibu na kushirikiana nao kuliletea Jimbo letu la Muyuni maendeleo makubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru sana familia yangu kwa uvumilivu wao kwangu na kwa namna inavyonisaidia na kuniunga mkono katika majukumu yangu ya kila siku. Aidha, shukrani za dhati ziende kwa Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje. Shukrani pia ziende kwa Watendaji na Wasaidizi wangu katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa ushirikiano, ushauri na msaada wao katika utekelezaji wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba nianze kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwanza niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Ni dhahiri kwamba, michango yao itaendelea kutusaidia katika kufanikisha shughuli za Wizara na kuimarisha ufanisi wa Watendaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kwa kuzungumzia hoja ya kutoa Taarifa ya namna kila Ubalozi ulivyotekeleza Sera ya Diplomasia ya Uchumi. Katika hotuba yetu tumeona sio mahali ambapo tungeweza kuzungumzia utekelezaji wa kila Balozi, ila kwa jumla tumegusia mafanikio ya Diplomasia ya Uchumi yaliyopatikana na ambayo tumesisitiza kwamba, Diplomasia ya Kiuchumi ni juhudi ambazo zinachangiwa na Sekta mbalimbali. Kwa hiyo, ndani ya Ubalozi, Balozi anakuwa Kiongozi, lakini ndani ya nchi yetu Wizara inaratibu jitihada za Wizara na Sekta Nyingine katika kuleta mafanikio ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia Diplomasia ya Kiuchumi tunasisitiza kwamba, katika mahusiano yetu na nchi nyingine na pia katika mahusiano yetu na Mashirika ya Kimataifa, tuwe tunalinda na kutetea maslahi ya kiuchumi ya Tanzania na ya Watanzania. Iwapo kama ilivyotokea katika Taarifa ya Kambi ya Upinzani, wakitaka Taarifa hiyo Wizarani sisi huwa tunapokea Taarifa za *quarter* kutoka katika kila Balozi na tutakuwa tayari kuwapatia taarifa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utekelezaji wa Diplomasia ya Kiuchumi, limechangiwa na Wabunge mbalimbali. Miongoni mwao ni pamoja na Mheshimiwa Shafin A. Sumar, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mheshimiwa Mariam Msabaha, Mheshimiwa Rebecca Mgondo na Mheshimiwa Susan Lyimo na wengineo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wako ambao wamekuwa pia wakieleza kwamba, hatuwezi kutekeleza Diplomasia ya Uchumi katika hali ambayo kuna ukosefu mkubwa wa fedha, lakini wapo pia waliotambua kwamba, tumekuwa tukipiga hatua kubwa katika kutekeleza Diplomasia hiyo, licha ya kwamba, bajeti yetu haitoshi. Kusema ukweli, kwa yeyote ambaye anatambua mafaniko yetu ambayo baadhi tumeyataja katika hotuba yetu, hataacha kuwapongeza Mabalozi wetu ambao wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu kidogo, lakini pia wamefanikisha mambo mengi ambayo yana maslahi ya kiuchumi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo ningeomba kuigusia ni hoja ya kutenga fedha za kutosha, ili kuwezesha Balozi zetu kufanya kazi kwa ufanisi. Hoja ambayo ilitolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, lakini pia imegusiwa na Mheshimiwa Rukia Kassim, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Kombo, Mheshimiwa Mustaph Akunaay na Mheshimiwa John Mnyika, miongoni mwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakiri kwamba, licha ya ufinyu wa bajeti ya Wizara, lakini katika Mwaka wa Fedha huu 2014/2015 bajeti yetu imeongezeka kidogo na tumetenga jumla ya shilingi bilioni 78.2 kwa ajili ya Balozi, ukilinganisha na bilioni 69.08 ambazo zilitengwa katika mwaka ambao tunaumaliza. Hii ni sawa na ongezeko la 13%. Ni nia ya Wizara kuziongezea uwezo Balozi zetu ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi kadiri hali inavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja nyingine ambayo ilizungumzwa ni kuhusu kufanya uchunguzi wa tuhuma dhidi ya balozi zetu nchini China na Uingereza kuhusiana na shutuma kwamba, zinztoa Hati za Kusafiria kwa raia wasio wa Tanzania, hususan raia wan chi za Afrika Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hati za Kusafiria ni Nyaraka muhimu za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hatua yoyote ya kutumika isivyo sahihi, ni jambo lisilokubalika. Baada ya kuzisikia taarifa hizi mwaka jana, Serikali ilifanya uchunguzi na kubaini kwamba, sio kweli, kwamba, Balozi hizo zinatoa Hati. Kwanza ieleweke kuwa Hati za Kusafiria hutolewa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi chini ya Idara ya Uhamiaji. Balozi inaweza tu kutoa Hati ya Dharura pale ambapo mtu amepoteza au kuibiwa *Passport* akiwa huko nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la hoja ya kupelekwa Muambata wa Kiuchumi nchini China ili kufuatilia fursa mbalimbali za kiuchumi hoja hii ilikuwemo katika maelezo ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, lakini pia Mheshimiwa Mtutura Mtutura naye pia aligusia hoja hii. Wizara inaye Afisa

anayeshughulikia masuala ya uchumi na uwekezaji katika ubalozi wa Beijing na anafanya kazi nzuri ya kutafuta fursa za uwekezaji na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa China katika biashara na uwekezaji na ukubwa wa nchi hiyo Wizara yangu ikishirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara inaangalia uwezekano wa kuanzisha kituo cha biashara China kama ilivyo Dubai na London.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuhusu lile suala ambalo liligusiwa na ndugu Mtutura la kuweza kufungua Ubalozi Mdogo Guangzhou tulieleza katika bajeti yetu iliyopita na kuweza kuripoti kwamba tupo katika hatua za mwisho za kuweza kufungua Ubalozi mdogo Guangzhou. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo lilizungumzwa pia kuhusiana na faida za kiuchumi tunazozipata kwa kujiunga na Jumuiya mbalimbali za Kimataifa na za Kikanda na hoja ya kwamba hakuna sera ya utangamana hadi hivi sasa. Faida za ushirikiano katika Jumuiya ya Kimataifa ni nyingi, lakini kwa kifupi ni kwamba lengo au sera ya mambo ya nchi za nje utekelezaji wake mkubwa ni kuzidi kujenga mahusiano mazuri na nchi mbalimbali na Mashirika ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi mnapokuwa katika Jumuiya za Kikanda au hata za Kimataifa inawezesha kuwa na mahusiano ya karibu zaidi katika biashara, katika siasa na ulinzi. Kwa hiyo, faida ambazo tumekuwa tukizipata katika Jumuiya hizo ni pamoja na hizo kukuza biashara baina yetu, kuvutia watalii, kufanya utafiti wa pamoja na pia kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi wanachama na nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kukosekana kwa Sera ya Utengamano hoja hiyo siyo sahihi kabisa, kwa sababu chini ya Sera ya Mambo ya Nchi za Nje, utengamano ni kipengele kimojawapo. Kwa hiyo, kinachokosekana ni Sera Mahususi au Sera Maalum ya Utengamano, lakini tayari suala la utengamano lipo ndani ya Sera ya Mambo ya Nchi za Nje na kwa hiyo muda wote ambao tumekuwa tukishirikiana na nchi nyingine katika masuala ya Regional *Integration* au utengamano, tumekuwa tukifuata Sera yetu ya Mambo ya Nchi za Nje ambayo yametuongoza hadi hivi sasa. Kinachofanyika hivi sasa ni kuweza kuandaa Sera Maalum ya Utengamano lakini siyo kwamba kuna ukosefu au *vacuum* katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani alitaka kujua idadi ya nyumba za Balozi na makazi na kiasi gani ya nyumba hizo tuna hati miliki na zipi hatuna. Serikali inamiliki jumla ya nyumba tisini na tatu zilizopo katika Balozi zetu 26. Miongoni mwa hizo ni makazi ya

Mabalozi, Ofisi za Ubalozi na nyumba za Maafisa. Kati ya nyumba hizo, nyumba 68 zina hati miliki na Balozi zinaendelea kuwasiliana na mamlaka za nchi husika kukamilisha upatikanaji wa hati miliki za nyumba 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ambayo ilizungumzwa na Wabunge mbalimbali, uteuzi wa Mabalozi ufanyike kimkakati. Chini ya hoja hii pia kulikuwa na maelezo, wengine wakisema kwamba Mabalozi wasitokane na wanasiasa, wengine walieleza wasitokane na wastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliozungumzia hoja hii ni pamoja na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mustafa Akunaay na Mheshimiwa Moses Machali. Kwanza niseme kwamba uteuzi wa Mabalozi siku zote tumekuwa tukiufanya kimkakati na umekuwa ukizingatia weledi wa watu wetu na Mabalozi wetu walioko nchi mbalimbali ni miongoni mwa Mabalozi weledi na mahiri kulinganisha na nchi nyingi tu.

Kwa hiyo, tutaendelea na utaratibu wa kuhakikisha kwamba tunafanya uteuzi wa Mabalozi kimkakati na kwa kuzingatia weledi wa wahusika. Si vyema kusema kwamba na kwa kiasi fulani inapingana na maelekezo ya kuchagua Mabalozi kimkakati tunaposema kwamba tusichague wanasiasa au tusichague wastaafu. Hawa wastaafu siyo wafu na siyo kwamba kila unapostaafu umechoka na hufai. Kwa hiyo, ni watu bado wana busara, wana taaluma, wana uzoefu na bado wanaweza kulisaidia Taifa hili katika mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni utaratibu wa nchi nyingi kuchanganya watu wenye taaluma na uzoefu tofauti na katika utaratibu huo Mabalozi wamekuwa wakiteuliwa wale ambao wanatokana na kufanya kazi katika Wizara za Mambo ya Nchi za Nje, *carrier Diplomats* , lakini pia wamekuwa wakichaguliwa Mabalozi ambao ni wanasiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo utaratibu ambao ni pekee kwa Tanzania na ukilinganisha na nchi nyingi, utaratibu wetu umekuwa ukija na uwiano mzuri wa kuzingatia *carrier diplomats* na hao ambao siyo *carrier diplomats*. Kwa hiyo, utaratibu huu utaendelea na tutaendelea kuufanya kwa kuzingatia mahitaji maalum na kwa hiyo utakuwa ni utaratibu wa kimkakati kama ulivyotakiwa na wasemaji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa pia na suala lililokuwa karibu na hilo lilitolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ni kwa nini tuwe na mlundikano wa Mabalozi katika ukanda mmoja kama ilivyo sasa kwa Balozi zetu Maputo, Harare, Kinshasa, Lilongwe na Pretoria, hili lilitolewa katika muktadha wa kuimarisha Diplomasia ya uchumi. Kwanza tuzingatie kwamba diplomasia ya Uchumi ni kipengele kimojawapo tu katika diplomasia ambayo tunaitekeleza na

kuwa na Balozi katika nchi fulani la mwanzo ni kulinda maslahi ya nchi husika na ya wananchi. Hapa tayari imeelezwa na wengine mfano, tuwe na Balozi mdogo Guangzhou, lengo na lilielezwa hapo, kwamba ni kulinda na kuwasaidia Watanzania watakaopata matatizo wakiwepo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuwa na Mabalozi katika nchi hasa hizi za jirani tunazingatia maslahi ya nchi yetu yakiwepo maslahi ya kiulinzi na kiusalama, lakini pia kwa nia ya kujenga ujirani mwema. Katika Historia ya nchi yetu na nchi nyingi nyingine za Kiafrika mahusiano ya kiuchumi zaidi yalikuwa ni baina ya nchi zetu za Kiafrika na waliokuwa watawala wetu kwa sababu ya mifumo iliyowekwa huko kabla, lakini lengo hivi sasa ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na mahusiano makubwa zaidi ya kiuchumi na nchi jirani zetu na kuwepo kwa Balozi kunatusaidia kufungua milango ya mahusiano ya kiuchumi ukiachilia yale ambayo nimetaja ya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Naibu spika, kwa hiyo, sidhani kama ni ushauri mzuri kusema kwamba tuondoe Mabalozi ambao wapo jirani na kusema kweli ndiyo utaratibu unaotumika duniani kote. Nchi nyingi kwanza huanza kufungua Balozi na majirani zake kabla ya kuangalia mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la ujenzi wa Ofisi Zanzibar. Suala hili lilitolewa na Mheshimiwa Fakharia Shomar. Ni kweli tayari tuna kiwanja na lengo la kujenga tunalo na tunaendelea kuchukua hatua mbalimbali tuweze kulitekeleza hilo, lakini kama ilivyoelezwa na wajumbe mbalimbali kuna ukosefu au ufinyu wa bajeti. Kwa hiyo, tunaangalia vyanzo vingine vitakavyoweza kutusaidia tuweze kukamilisha nia yetu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la Wizara ya Mambo ya Nje inawaandaje Wabunge wa Tanzania ambao wanawakilisha Bunge katika Mabunge mbalimbali duniani. Kwanza Wizara yetu itakuwa tayari wakati wowote kushauriana na Wabunge hao na kutoa ushauri pale inapohitajika, lakini wanapokwenda katika nchi ambazo tuna Balozi wasisite kukaa na Balozi zetu na kutafuta ushauri kuhusiana na masuala yote juu ya misimamo ambayo Tanzania tunayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba pia kupokea pongezi mbalimbali zilizotolewa katika kutambua utendaji kazi wa Balozi zetu lakini pia wa Wizara. Pongezi hizo zilitolewa na Wabunge kama vile Mheshimiwa Sanya, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Mtutura. Tunawashukuru sana kwa kutambua kazi ambayo Mabalozi na Watendaji mbalimbali katika Wizara hii wamekuwa wakitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Mahadhi kwa ufafanuzi wako mzuri tunakushukuru sana.

Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Bernard Membe, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ili aweze kupitia hoja za Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa. Waziri Membe karibu, una dakika arobaini!

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kukushukuru wewe kwa dhati kabisa kwa namna unavyoendesha vikao hivi hasa hiki cha leo, kuna muda nilidhani kitawaka moto, lakini uliuzima ule moto kidiplomasia, nakupongeza sana. Pia nipende kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kuzungumza na wale waliochangia kwa maandishi. Nianze moja kwa moja na wale waliochangia kwa kuzungumza.

**NAIBU SPIKA:** Hawa waruke tu Mheshimiwa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, niwaruke wote hawa. Basi nawashukuru sana wale wote waliochangia kwa kuzungumza na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu spika, naomba nianze kwa suala ambalo niliahidi asubuhi la safari za viongozi. Kwanza nianze tu kwamba, Rais yoyote makini duniani lazima asafiri, ukiona Rais hasafiri amekaa hapo hapo ama ni mgonjwa ama Kimataifa hajulikani sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata bahati kwamba, Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa Mbunge na Waziri wa Mambo ya Nje kwa muda wa miaka kumi na aliijua dunia na kuweka mtandao mkubwa, lakini kutokana na umahiri wake amekuwa kiongozi duniani ambaye anajulikana kwamba ni kiongozi mmoja mkubwa katika bara la Afrika dunia kuanzia *Security Council, The* G20.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika yote ya Kimataifa yanapofanya mikutano yao wakitaka kumualika Rais yoyote Afrika ambaye siyo tu kwamba anahudumia nchi yake, lakini anaweza pia kuhudumia nchi nyingine za majirani katika kujihusisha na masuala ya *peace keeping, conflict management* wakimulika katika bara la Afrika hawakuti kiongozi mwingine isipokuwa, Rais Jakaya Mrisho Kikwete, hajipeleki tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niseme la kwanza anasafiri kwa sababu anajulikana duniani na mchango wake wa mawazo katika masuala ya dunia ni mkubwa mno na ndiyo maana ndugu Watanzania mlishuhudia kwamba hata wale viongozi wakubwa, vingunge wa dunia, wanaposema waende Afrika watakuja Dar es Salaam. Kwa hiyo ni jambo la kujivunia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lipo suala la idadi, wengi wanalalamika, wanasema idadi ni kubwa mno, ukilinganisha na nini? Tukilinganisha na Nigeria ambayo Rais wa Nigeria anasafiri wakati wote na ujumbe wa watu mia sita. Tukilinganisha na Kenya ambaye Rais anasafiri wakati wote, *average* katika kipindi cha miaka kumi na watu 102. Tukilinganisha na wapi Afrika ya Kusini ambako Rais anasafiri wakati wote pamoja na *advanced party* yake na watu 92. Tukilinganisha na wapi na Uganda labda ambapo Mheshimiwa Rais Museveni akisafiri kwenda kwenye Umoja wa Mataifa, watu 180. Tukilinganisha na nani kwa sababu katika Diplomasia ya safari, lazima tujilinganishe na mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi *average* ya watu wanaosafiri ni hamsini na tunapoambiwa nasoma taarifa hapa kwamba Mheshimiwa Membe watu wengine wakienda huko wanakaa tu, wanakula tu, wanakula ndiyo, wanakaa ndiyo, lakini wanafanya kazi, sasa wafanye kazi bila kula na kinachotokea ni nini ndugu zangu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais anaposafiri kwanza lazima asafiri na vyombo vya usalama, anaposafiri na ndege yake kwa mfano, huwezi kwenda kuiacha ndege katika nchi za watu, ukaicha tu pale Rais muda wa siku mbili yuko kule, ukaiacha ndege bila kuwa na walinzi wanaoitunza ndege ile. Huwezi ukamuacha Rais katika ulimwengu wa leo ambako kuna Boko Haram, kuna *Al-Shabab*, *Al-Qaida*, usiongeze nguvu ya watu wanaokwenda kumlinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi ukamuacha Rais anaposafiri asisafiri na watu ambao wako katika sekta za kiuchumi za kutega uchumi ili wanapokwenda kule hata ukimkuta anakula ana mwenzake wa upande ule anazungumza masuala ya maendeleo, masuala ya biashara na masuala ya utalii na masuala kama hayo. Hiyo ndiyo inaitwa *team spirit* kwamba Rais anaposafiri anatembea na kundi.

Sasa wenzangu kama unadhani kwenye msafara wa Rais, kuna mtu anasafiri ambaye hana kazi kabisa na hatakiwi kwenda niandikie, halafu nione kama kweli hastahili, lakini katika Wizara, tunasema watu wote wanaokwenda kila mtu ana kipande chake cha kazi na ndicho kinachomfanya Mheshimiwa Rais afanikiwe katika safari.

Mheshimiwa naibu Spika, watu wangu wamenitayarishia hapa muhtasari ambao ningependa kwa kweli niusome kwa dakika tatu tu, kuonesha faida zinazotokana na ziara za Mheshimiwa Rais kwa sababu hatuwezi kusema tu idadi na gharama bila kuonesha tija na faida zinazoweza kutokana. Sasa nina mifano michache tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais amefanya ziara nchini Singapore katika kipindi cha mwaka 2012/2013, nini kilichopatikana? Kule akaikuta kampuni ya *Pavilion Energy* ya nchini Singapore ambayo ikakubali kuwekeza kwenye sekta ya gesi nchini na katika kufanya hivyo wamekuja wakanunua *share* 20 kutoka kampuni ya *OFIL Gas* ya Uingereza kwa dola za Marekani bilioni moja na milioni mia tatu na hapo Tanzania tukapata kodi yetu ya dola milioni mia mbili, si haba, ndiyo tunataka kuvutia wawekezaji wa aina hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ipo ziara ya Mheshimiwa Rais Davos, Uswiss alipohudhuria mkutano wa jukwaa la uchumi la dunia Davos Februari mwaka 2014, katika kupitia jukwaa hili Tanzania iliweza kuvutia wawekezaji hasa katika sekta ya kilimo na tulipata kampuni ya *Unilever*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Unilever* ilikubali kuwekeza kwenye kilimo cha chai kupitia *SAGCOT,* inatarajiwa kuwa uwekezaji huu utainua uzalishaji wa chai mara tatu zaidi ya kiwango kinachozalishwa sasa na kuingiza wastani wa *Euro* milioni 110, hatua hii itatusaidia kuongeza mapato kutokana na bidhaa zitakazosafirishwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziara ya Mheshimiwa Rais Marekani. Vile vile katika ziara hii Mheshimiwa Rais nchini Marekani, tulitia sahihi kati ya Serikali ya Marekani na Tanzania za makubaliano ya kutekeleza mpango wa *Millennium Challenge Account*. Kwenye *Millennium Challenge Account* tulipata karibu milioni mia saba na tukawekeza katika barabara kuu saba kukarabati uwanja wa ndege wa Mafia, kuweka waya wa kusafirisha umeme kutoka Tanzania Bara hadi Zanzibar, kukarabati mifumo ya usambazaji umeme kwenye Mikoa saba ambayo ni Tanga-Horohoro kilomita 65, Songea- Namtumbo kilomita 71, Tunduru-Ikana kilomita 63, Ikana -Laela kilomita 64, Laela- Sumbawanga kilomita 95 na Pemba *rural roads* kilomita 35; kukarabati na kupanua mifumo miwili ya maji ya Morogoro na Ruvu Chini kwa kipindi cha miaka mitano toka mwaka 2008. Mpango unakadiriwa kugharimu dola za Marekani milioni 698, huu ulikuwa ndiyo mradi uliowahi kupata ufadhili mkubwa zaidi katika Hostoria ya *MCC* yaani *Millennium Challenge*.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu ziara ya Mheshimiwa Kuwait, kufuatia ziara ya Mheshimiwa Rais nchini Kuwait; Kuwait *fund* walikubali kutoa kiasi cha

dola za Marekani laki mia tano thelathini elfu mia saba sabini na nane kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa barabara ya Chanya – Nyahuwa Mkoani Tabora na kuthibitisha kugharamia ujenzi na barabara hiyo kwa asilimia mia moja mara upembuzi yakinifu utakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kuwait *Fuel* ilitoa dola za Marekani milioni kumi kati ya dola milioni thelathini na tano kwa ajili ya awamu ya kwanza ya mradi wa maji wa Korogwe-Same-Mwanga. Wakati huo huo wameahidi kugharamia awamu ya pili ya mradi huo.

Waheshimiwa Wabunge mtaona na mmeona namna safari za Mheshimiwa Rais zinavyoleta tija katika maendeleo ya nchi yetu na si lazima tuone mara moja tija nyingine itakuja baada ya miaka miwili au baada ya miaka mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimalizie kwa kusema ameiletea sana heshima nchi yetu ya Tanzania, Mheshimiwa Rais jakaya Mrisho Kikwete, nasema hivyo, mtakuja kupata Rais ambaye hana sifa zozote za katika ulimwengu huu, si mtaona atakavyokaa mwaka mmoja au miaka miwili bila kutembea na heshima ya nchi hii itakavyokwenda chini. Tunapopata kiongozi wa aina hii aliyetukuka badala ya kumlaani tumpigie makofi kwa sababu anatusaidia kuleta maendeleo ya nchi yetu, nawashukuruni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu diplomasia ya uchumi. Waheshimiwa Wabunge, hiki ni kilio kikubwa. Diplomasia ya uchumi ni mkakati maalum ambao unaifanya Wizara pamoja na Balozi zake zote duniani zisaidie sekta muhimu za jamii na za uchumi katika nchi yetu ili kutangaza biashara, kutangaza uwekezaji, kutangaza shughuli za maendeleo ili kutafuta wawekezaji kule duniani na ku-*promote* utalii. Kazi hiyo, inafanywa. Wenzetu wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wametushauri kwamba pengine ni vizuri tukawa na *desk* maalum la *economic diplomacy*.

Kwa sasa hivi ni Idara ya Sera na Mipango ya Wizara ya Mambo ya Nje ndiyo inayoshughulikia na suala hili. Lakini tumesema tunauchukua uamuzi huo, pamoja na ushauri huo. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba kwenye Balozi zetu zote sasa tunapeleka wachumi, tunapeleka watu wa biashara, tunapeleka *promoters* wa kitaalii. Lakini ili kufikia hapo, kitu cha kwanza ndiyo hiki mnachotuona tunafanya, kununua majengo ambayo yanaweza ku-*accommodate* watu wa sekta mbalimbali, mbali ya Uhamiaji peke yake ili waisaidie nchi na Balozi zetu katika ku-*promote* biashara, ku-*promote investments*, ku-*promote tourism*, ku-*promote* na shughuli nyingine zozote za maslahi ya nchi yetu. Nami nina hakika tutafika huko.

Nafurahi sana Waheshimiwa Wabunge mnavyojikita katika suala zima la diplomasia la uchumi na tunachukua ushauri wowote mnaotupa ili mradi tu kwamba Balozi zetu sasa na sisi katika Wizara tujikite zaidi katika maendeleo ya yetu hasa katika kipindi hiki ambacho tunategemea kupata gesi na gesi itatupa mabilioni na tusingetaka tuwe na *dutch disease* ile ya kujisahau kutofanya jambo lolote lile tukidhani gesi peke yake inaweza ikaleta maendeleo ya nchi yetu. Tutajitahidi kwa pamoja na ninyi Waheshimiwa Wabunge kukuza diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la *diaspora* na uraia pacha. Swali limeulizwa nadhani na Mheshimiwa Lyimo. Kwanini tusilete Muswada Bungeni? Hii ilikuwa dhamira yetu kwanza lakini wakubwa walitushauri kwamba kwa kuwa tulikuwa na mjadala wa Katiba ndani ya Bunge hili, walidhani ni vizuri tukaleta kwanza mjadala huu humu, halafu baadaye tutaleta kiutaratibu tutakapokuwa tunapitisha zile sheria kuuleta Muswada humu ndani.

Naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wengi mnaozungumza mmeanza kutambua umuhimu wa raia wa Tanzania anayeishi nje kutokupata adhabu ya kuondolewa uraia wake pale anapopata nafasi ya kupata uraia wa nchi anayoishi. Ndiyo *theme* ya uraia wa pacha mbili. Kwamba inapotokea Mtanzania yoyote anayeishi nje kwa sababu yoyote ile ikatokea anapata uraia wa nchi ile asiadhibiwe na nchi hii kwa kumnyang'anya uraia wake wa kuzaliwa. Kwa kusema hivi, haina maana kabisa kwamba kesho tukipitisha Sheria ya Uraia Pacha, basi Watanzania wote watakuwa na uhuru wa kwenda kokote kule wakawa raia wa nchi ile, hapana. Kule unakokwenda utakutana na sheria zitakazokubana pengine usipate hata uraia wenyewe. Sisi tunachozungumzia, ukiupata tusikuadhibu kwa kukuondolea uraia wako wa kuzaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, Mheshimiwa Lyimo atajibiwa swali lake kwamba Watanzania watakapopata kibali cha kuingia nchini sasa kama raia, atapata nafasi pia ya kuleta pesa nchini kwetu, zinaitwa *remittances*. Sasa hivi kwa sababu Watanzania wamejilipua kule wanakoishi, hawezi kuleta pesa Tanzania kwa sababu ataulizwa kwamba wewe umesema unatoka Somalia, sasa mbona unapeleka Dar es Salaam hizi hela? Wanamkatalia kutokupeleka kwa sababu alishajilipua, akijiona ana pua ndefu kidogo, anajiita Msomali kumbe anatoka Dar es Salaam. Hasara yake ni kwamba hawezi kupeleka hela Dar es Salaam baada ya kujilipua. *(Makofi)*

Kwa kibali hiki cha kupata uraia pacha, sasa atakuwa huru kuleta pesa yeye mwenyewe bila kumtumia Membe, au bila kutumia njia za panya, kuleta pesa kwa shangazi yake, kwa ndugu yake au kwa mdogo wake, ataleta wazi

wazi nyumbani humu. Hizo zinaitwa *remittances,* wenzetu kote kule duniani wanazipata. *1.5 billion* Kenya peke yake; *3.2 billion* Nigeria; *2.5 billion,* Ghana kutoka kwenye *diaspora* hii na wanapata hivyo kwa sababu *Dual Citizenship.* Ukimpa mtu *citizenship* hii, anapata *white collar jobs.* Usipompa mtu *citizenship* hii, atakuwa anafanya kazi ya kufagia barabara, kusomba maji, kupika, kitu ambacho hakiwezi kumpa pesa za kutosha kuzileta nchini kwa ndugu zake.

Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tutakaposimama hapa kujenga hoja ya nguvu ya kutaka uraia wa pacha mbili, mtuunge mkono ili ndugu zetu walioko huko ughaibuni waweze kuleta maendeleo katika nchi yetu na fedha katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa lipo suala la Zanzibar, na ninakushukuru tena kwa kuliweka sawa hili. Nami naomba Waheshimiwa Wabunge tunapopata jazba wakati fulani na tukapiga *below the belt,* basi baada ya muda tutulie na tuyaache hayo pembeni. Mimi nina habari njema. Habari njema niliyonayo ni hii, kwamba Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sasa hivi ni kweli tuna Mabalozi watano, siyo wane. Mabalozi watano! Lakini kinachotokea, katika zile Balozi zetu 34 nyingine zina mapengo siyo kwamba zote zimejaa kwa sababu Mabalozi wanazidi kurudi nyumbani.

Nataka niwaambie leo kwamba tayari nimekwenda Zanzibar, kwa ruhusa ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nimeshapata majina mawili ya watu watakao-*replace* Mabalozi wa Zanzibar na kuongeza mmoja zaidi ili tuwe na Mabalozi sita. Lakini kutokana na siri za Taifa, siwezi kutoa majina hayo wala nchi wanazokwenda. Kwa hiyo, mtulie tu! *(Makofi)*

Narudia; nimekwenda Zanzibar, nimekutana na Makamu wa Pili wa Rais, nimeshapewa majina mawili, nimeshayapeleka kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *agreemwa* zimeshatumwa huko wanakotakiwa kwenda na pindi zikikamilika, mtasikia kwenye bomba tumeshawachagua wengine.

Mzale anapoondoka Sweden, pale Sweden siyo lazima aendee Mzanzibar na Zanzibar imeshachagua wapi tupeleke watu wake. Lakini kama hiyo haitoshi, tumeteua Manaibu Balozi wawili; mmoja anakwenda Oman na mwingine anakwenda India. Kama hiyo haitoshi, Wazanzibar 17 ambao tumewasomesha tayari kwenye Chuo cha Diplomasia, wale 17 katika kipindi cha mwaka 2013/2014 hatukuweza kuwaajiri kwa sababu utumishi na Serikali ilizuia ajira, sasa zimefunguliwa zile ajira. Kwa taarifa yenu, tumepata nafasi 19 tutashindwa vipi kuwaajiri Wazanzibar 17 wawepo pale? Hizo ndiyo habari njema nilizonazo, hatuna haja ya jazba na wala kugombana. Sisi Serikali tunaangalia *sensitivity* ya Muungano wetu na ningeomba mpoe kabisa na mtulie msubiri habari njema kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uboreshaji wa Balozi zetu, nafurahi kwamba Waheshimiwa Wabunge mmeona matatizo ya Balozi zetu. Sasa narudia kwamba inatokana na ufinyu wa bajeti. Namshukuru sana ndugu yangu Mheshimiwa Wenje, nimemsikia asubuhi akilitambua hilo kwamba sisi ndio tumeanza mwaka 2007/2008 kupewa kitu kinaitwa bajeti ya Maendeleo. Kabla yake katika kipindi chote cha miaka 1954, 1953 ya uhuru wetu Wizara ya Mambo ya Nje haikuwa inapata bajeti ya Maendeleo, haikuwa inapata kabisa! Tumeanza sisi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Tunapopata hizi pesa sasa, baadaye tunakuwa na ufinyu huu ambao huelezeki. Kwa hiyo, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 tumeanza kununua majengo Ufaransa, yale majengo pacha mawili; halafu katika kipindi hiki hizi pesa tulizoomba tutakarabati majengo yetu ya Geneva, tutakarabati majengo yetu ya Sudan, maana tuna majengo pale yanachakaa pamoja na *New York*. Sasa hivi tunakarabati majengo ya Msumbiji, jengo la ubalozi kama wengine mlivyosema, jengo lenyewe la *residence,* yaani nyumba ya Balozi, nalo tunataka kulikarabati, lakini wakati huo huo tunanunua majengo yale ya Paris.

Kwa hiyo, kutokana na ninyi Waheshimiwa Wabunge kutupa bajeti ya maendeleo, ndiyo sasa tumeanza kabisa kukarabati majengo yetu. Kama tutapata pesa hizi kama tulivyoomba, tutazidi kukarabati majengo kama nilivyosema katika kipindi cha mwaka 2014/2015. Nawashukuru sana kwa kutuunga mkono kwa hilo na nina hakika tutakapopata pesa zetu tutakuwa tunaifanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Kombo aliniuliza kwamba Mheshimiwa Membe, hivi muhogo huu nini? Wakikusikia watu wa Mtwara na Lindi, watakasirika. Mzee George Mkuchika akanionyesha kidole pale! Lakini nataka niseme kwamba katika Mikoa ya Mtwara na Lindi zao la muhogo usilisemee vibaya Mheshimiwa Kombo. Kule zao la muhogo ni kubwa mno. Mzee Mkuchika akaniambia, huyu anataka kuniua! Maana mimi nataka kustaafu na nataka kulikazania suala la zao la muhogo.

Kwa hiyo, ningependa kuwaambia wakulima wa muhogo kwamba soko kubwa liko China na kule wanataka wanga na bei ni ya kutupa. Ni nzuri mno! Napenda wanaonisikia wapate taarifa hii. Sasa hivi tupate wawekezaji kutoka sehemu zozote zile ili waweze kwenda kwenye Mikoa ya Kusini ambako kuna muhogo na hiyo haina maana ya kudharau biashara zilizopo kwenye maji na kwenye maji pia na baharini tutakuwa tunazishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni Rwanda. Naomba nizungumze suala la Rwanda. Nianze kwa kusema hivi, kwamba uhusiano kati ya Tanzania na

Rwanda siyo mzuri. Siyo mzuri kwa sababu mbili; kabla sijaenda kwenye *details*. Siyo mzuri kwa sababu; moja kuna kutoaminiana kati yetu na Serikali ya Rwanda. Kinachotokea ni nini? Ni kwamba hatuaminiani kwa sababu kila upande unadhani unapozungumza na mtu ambaye sio rafiki au siyo mwenzao wanadhani kwamba unapozungumza na adui yao mnakula njama au mnapanga njama za kuiondoa Serikali.

Kwa hiyo, inapotokea kwamba Membe kaongea na Mnyarwanda ambaye ni adui wa Serikali ya Rwanda, *immediately* mtu anaanza kutokuamini, anadhani unakula njama za kuiondoa Serikali ya Rwanda. Hivyo hivyo ndivyo tunavyoona Serikali ya Wanyarwanda inaongea na Wapinzani wetu au maadui tu wa Tanzania kuna sura inajitokeza tunadhani kwamba kwa kufanya hivi huenda wanakula njama za kuiondoa Serikali. Kuna kutokuaminiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ipo sababu ya pili. Sababu ya pili, ni wachonganishi, wanapoona kwamba kuna kutokuelewana kati ya watu wawili hawa kwa sababu yoyote ile. Wachonganishi wanatumia mwanya huo kupeleka taarifa za uwongo za kuchonganisha ili nchi mbili hizi ziwe kwenye *collision cause,* yaani ziwe kwenye mapambano ili vita ikishatokea, wale wachonganishi wapate faida ya kuchukua Serikali hizi. *(Makofi)*

Ningependa kuchukua nafasi hii kuonya kwamba wale wanaodhani kwamba kutokana na mgogoro huu ambao tunajua utaisha, wanachukua nafasi hiyo kupenyeza *propaganda* za fitina na uchonganishi kati ya Serikali mbili hizi, tukiwagundua tutawachukulia hatua za kisheria na tunawaonya wawe Watanzania, wasiwe Watanzania waache tabia ya kipumbavu ya aina hiyo. *(Makofi)*

La pili, nakuja kwenye bajeti ya leo. Ndugu zangu historia fupi sana, *Kongo DRC* mwaka 1956 mpaka mwaka 1959 Wanyarwanda wa upande wa Watutsi waliondoka kwenda *South* Kivu kwa ajili ya shughuli za kazi. Walipofika kule wakwenda kwenye Mlima Mlenge wakawa wanaitwa Banyarwanda au Banyamulenge. Ni Wanyarwanda *hundred percent* wanaoishi kule na wakawa wanafanya kazi na wakalowea pale. Hawa ndio wanaoitwa Banyamulenge. Ile M23 iliyoanzia kwa Laurent Nkunda, Kiongozi wao wa kwanza, iliundwa na kundi lile la Banyamulenge *by hundred percent,* walikuwa 6000.

Sasa mwaka 1994 baada ya ndege ya Rais wa Rwanda kupigwa ya Habyarimana, mtakumbuka na mnajua, Askari wote pamoja na familia zao wakakimbia Rwanda kwenda Kongo. Hawa ndio waliounda Jeshi la *FDLR,* maana yake ni Jeshi na familia zao. Jeshi lote lilikimbilia kule! Walipokimbilia kule, ndiyo wakaunda kundi la pili la Wanyarwanda linaloitwa *FDLR*. Kwa hiyo, nilipohojiwa na Mwamerika Yule, nilipomwambia kwamba makundi yote mawili

ya Rwanda yako Kongo, wame-*export* vita kule, yanapigana, nilikuwa sahihi kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Ni kundi la *FDLR* ambalo ni Askari wa Habyarimana na walikuwa milioni mbili jumla na familia zao. *Two million*, wanapigana sasa na Banyamulenge ambao wameunda *force* na wenye asili ya Kitutsi, maana yake ni *the Congolise Tutsies,* ndiyo waliounda kikundi kile cha Laurent Nkunda ambaye sasa yuko Rwanda baada ya kukimbia. Akaja John Bosco Ntaganda, naye ni Mrundi. Wakaja hao wengine tuliowafyeka, wote wale ni Warundi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mapambano, Rwanda *it is very smart,* hakuna kupigana vita ndani ya Rwanda. Unakwenda Congo kwa sababu kuna *arid land* na *no man's land* wanakwenda kupigana kule. Ni taarifa siyo ya Tanzania, ni taarifa ya Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni taarifa ya Umoja wa Mataifa ambayo nipo tayari kuileta kwenye meza yako Tukufu. Humu ndimo mwenye ukweli, siyo mimi Membe! Hii taarifa ya *expert* iliyokwenda kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Taifa. *Review* ya mwaka 2009 na *review* ya mwaka 2012. Imegawiwa kwa Viongozi wote wa Umoja wa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni *common knowledge* kwamba tunapozungumzia Banyamulenge ni Watutsi wa Kongo; tunapozungumzia *FDLR,* ni majeshi ya Marehemu Habyarimana ambayo yameua kweli! Mheshimiwa Keissy aliposema kwa kesi ile, waliua milioni saba, ni ripoti, ipo! Wameua North Kivu! Wale waliokwenda kwenye vijiji, naomba nikitamke kijiji kimoja ambacho *massacres* zilifanyika vibaya mno! Vibaya sana! Makobola; waulizeni watu wote wanaotoka Kongo; Makobola ndiko akina mama wote wenye mimba pamoja na ile *FDLR* walipasuliwa na *bat stock* pamoja na sime, bunduki zile, mimba zao zote na waliuawa na watoto wote. Ndiyo sehemu ambayo ilitokea *massacre* kubwa kuliko *massacre* nyingine zote. Makobola, *Northern Kivu*, iliyofanywa na majeshi ya Habyarimana. Ndiyo maana Kagame alipeleka *force* kuwasaidia M23 ili kuwawinda *FDLR* kwa sababu ni Wahutu tupu na wameua kweli!

Kwa hiyo, alichokisema Mheshimiwa Keissy pale ilikuwa sahihi kwa sababu ni ripoti ya Umoja wa Mataifa, ni ripoti ya dunia, ni ripoti ya *AU* na nilimshangilia pale kuwaambia wenzangu kwamba nakuja kuwapeni ukweli. Sasa mimi mzigo namna gani? Ndiyo maana namuunga mkono ndugu yangu Mheshimiwa Mtutura, aliposema, kama ni mzigo kutoa ukweli kuhusu *DR Congo,* basi mzigo huu nitaendelea nao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme, sisi Watanzania *we are a Nation*. Sisi sio kabila tu ambalo tulikutwa siku moja, halafu baadaye tukajiita

nchi. *We are a Nation* ya makabila zaidi ya 129. Tuna mipaka inayoeleweka, tuna heshima yetu kubwa sana ukilinganisha na nchi nyingine ambazo una-*question* kama ni nchi au pengine ni *conglomeration* ya watu tu. *We are a Nation, a very big Nation. As a nation*, ni lazima tui-*protect* nchi yetu. Lazima tuipende nchi yetu. *(Makofi)*

Nawaambia leo Watanzania, hata siku moja kwenye Bunge lolote duniani, iwe Uganda, iwe Kenya, iwe Rwanda, iwe Burundi hutakuta Mbunge ndani ya Mabunge yale atakayesimama kwa niaba ya nchi nyingine yoyote jirani kuisemea nchi hiyo pale. Hutakuta! *Patriotism* ndugu zangu ina-*demand* wewe utaifa wako kuilinda nchi yako. Hivi siku moja tungeamua kwenda vitani humu, kuna watu wangekwenda kutoa siri kule! Hatupigani vita namna hiyo! Utaifa ni uchungu wa nchi yako! Kila binadamu ana sira za nchi, ziwe nzuri zisiwe nzuri. Huwezi kusimama kwenye Bunge hili kwa niaba ya Serikali ya Rwanda ukaisemea bila aibu ya aina yoyote ile! Hata kidogo! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo mambo yanayoweza kuchonganisha nchi hii tukaenda vitani. Unapoona Mtanzania mwenzetu anasimama, macho yamemtoka kabisa, anailaumu Serikali yake na kuipendelea Serikali ambayo mna matatizo nayo, mnaweza kuchonganisha na tukaenda vitani. *(Makofi)*

Mimi ningeomba, *this is the big Nation!* Tunapopata heshima hii ya wananchi kuja kwenye jengo hili jekundu, unakuja hapa kutetea Jimbo lako kwanza; pili utatea nchi yako; utatea Chama chako! Siyo Rwanda! Huwezi kutetea Rwanda! Huwezi kutetea Rwanda hata kidogo! Wala hatuoni haya kusema hivyo! Tunaheshimiana tu! Lakini huwezi kuja hapa ukatulaumu sisi kwamba tunachonganisha, au ni mizigo, lakini wakati huo huo unasimama rasmi hapa kana kwamba umetumwa na Serikali ile kuja kui-*defend* ndani ya Bunge hili! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sitaki kabisa kuamini kwamba ni msimamo wa Chama cha CHADEMA. Mheshimiwa Mbowe, ulikuwa wapi mchana? Labda asingesema mambo hayo! Siwezi kuamini kwamba maneno aliyoyasema ndugu yangu Mheshimiwa Wenje ni msimamo wa CHADEMA! Ni hatari mno! Haiwezekani hata siku moja ukawa ni msimamo wa CHADEMA, kwa sababu Watanzania wakijua kwamba msimamo wenyewe ni huu, kwamba unaweza ukasimama kwenye Bunge hili kuitetea nchi nyingine kana kwamba ulizaliwa kule, kana kwamba unalipwa mishahara ya kule, kana kwamba unalitumwa kule, huwezi kushinda hii nchi! Hata kidogo! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatoa wapi ujasiri wa aina hii? Tunatoa wapi Watanzania ujasiri wa aina hii kwamba tunafika mahali ndani ya Bunge

unaitetea Rwanda! Wanajeshi wetu wanakufa kule, tumepoteza damu ya Wanajeshi wetu, wanakesha wanaumwa mbu kule, wanaumwa na wanakufa! Leo unasimama unalaumu yote haya na unasema vitu vinavyoendelea *DRC Congo* sio Wanyarwanda, ni M23 wale, sio Wanyarwanda. Huhitaji kusoma wala kuwa Mbunge kuelewa, narudia.

Sasa mimi nataka nimtege ndugu yangu. Nakutega, kama unadhani kwamba wewe uliyoyasema ni sahihi, lete *documents* hapa mimi niko tayari kujiuzulu Uwaziri wangu wa Mambo ya Nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinyume chake pia ki-*prevail* kwamba nikiweza kuleta *documents* za ku-*prove* kwamba unaposikia M23 ni Watutsi wa Rwanda; unaposikia *FDLR* ni Majeshi ya Habyarimana ya mwaka 1994. Nikiweza kuleta *documents* zote hizo *intangible* nakuuliza kama uko tayari na wewe kuwajibika kama mimi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema haya kwa nini? Nasema kwa sababu sisi ni viongozi jamani! Uongozi wa nchi unatoka humu! Hatuwezi kuzungumza maneno ya dhihaka wala ya uchinganishi, kesho ni sisi! Vijana hawa mnawaona wako kule mbele wanazungumzia masuala ya *International Relations*. Wanaposikia kwamba watu tunaweza kusimama humu ndani ku-*defend interest* za nchi nyingine na siyo *interest* za nchi yetu, tunawaambia nini kuhusu uzalendo na *patriotism*? Sisi ndiyo Viongozi! *What message are we trying to send to these boys there*? Hatuwezi kupeleka *message* nzuri.

Upinzani, zungumza! Lakini yako mambo *of national interest,* hata kama unayoanaje, huwezi ukayazungumza hadharani. *(Makofi)*

Ndiyo maana napenda sana kuishukuru Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa sababu Kamati ile ipo kule kuondoa aibu hizi nyingine, hatuzisemi; tunakwenda tunakutana kule tunaambiana. Wakija humu wanasema, hiyo ipite; na wanailewa vizuri! Jamani Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ina unyeti wake. Tunapozungumzia uhusiano na nchi hizi, ni lazima tuwe waangalifu mno. *(Makofi)*

Narudia tena, narudia tena, narudia tena kwa Watanzania; sisi humu ndani ndio Viongozi, na siyo vizuri kama sisi Viongozi kusimama humu na kutetea nchi nyingine. Tetea kimya kimya! Ukitetea waziwazi utaanza kuleta fikra, baadhi ya watu wakawafikirieni vibaya kwamba labda unatumiwa. Kumbe masikini ya Mungu, unampinga Membe tu! Lakini *your creating a picture* kana kwamba umetumwa au pengine umetumiwa! Tusiende hivyo! *(Makofi)*

Tuna Majimbo ya kuyatetea, tuna nchi ya kuitetea na tuna Chama cha kukulinda na kukutetea. Huo ndiyo uzalendo, na ndiyo *three whip* tuliyoiapia tulipokuwa tunaingia kwenye Bunge hili. Nawaomba lazima tu *up-hold* hili. *(Makofi)*

Naomba niwakumbushe tena, katika Afrika Mashariki, katika *region* ya *SADC, we have power. Power* yetu sisi siyo ya uchumi. *Power* yetu sisi siyo ya uchumi, lakini tuna *power* ya *persuasion*, *power ya conflict management,* tuna *power* ya *resolution.* Nchi zote hizi tunazozisema sasa tulizisaidia kwa namna moja au nyingine walivyokuwa wanapata uhuru wao. Tulikuwa kwenye *front line* ya *liberation.* Kwa kufanya hivyo, tusijidharaulishe sisi wenyewe tukajiona kana kwamba tumepindua hii nchi juzi au tumepita katika madaraka jana, hapana. Wenzetu wanajifunza kutoka Tanzania! Lazima pia wajifunze na masuala mazima ya uzalendo. *(Makofi)*

Nimeishiwa muda? Ah, zimebaki dakika tano! Kwa hiyo, ningependa nimalizie na Malawi.

Waheshimiwa Wabunge, kinachoendelea Malawi, asubuhi nimekisema na *up date* ya sasa kwa wale mnaotaka ni kwamba sasa uhesabuji wa kura zote umekwisha na mchana huu Tume imekwenda Mahakamani kuomba nyongeza ya siku 30 ili waone tu namna ya ku-*compile* zile *results,* lakini mshindi wameshampata tayari. Masaa mawili yaliyopita, makundi manne sasa ya Vyama vya Upinzani ikiwemo *DPP* na wenyewe wamekwenda Mahakamani kutoa katazo kwamba Tume isikubaliwe kupoteza siku 30 zaidi lakini matangazo hayo yatangazwe leo usiku, na kama wamechelewa sana watangaze kesho asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokisema hapa ni nini? Sehemu inayotuhusu sisi kama Watanzania ni kwamba na ningependa *message* hii iwafikie Watanzania. Sisi Watanzania tutakuwa tayari kushirikiana na Serikali yoyote ambayo itakuwa imechaguliwa na wananchi wa Malawi. Kama ndugu zetu, tutaendelea kushirikiana nao na tutaendeleza mazungumzo yetu ya amani katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo la mpaka kati yetu na Malawi. Tupo tayari kuwa wavumilivu mpaka pale Serikali yao itakapopatikana na kutengamaa ili Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje anayekuja pamoja na Timu yake nyingine tuweze kuendeleza mazungumzo yetu pale tulipoishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard Membe nakushukuru sana hoja imetolewa na hoja imeungwa mkono, nakushukuru sana kwa maelezo uliyoyatoa. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wenje ni kitu gani tena? Ni kanuni gani?

**MHE. EZEKIAH D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ieleweke wazi kwamba taarifa iliyosomwa hapa Bungeni ni ya Kambi Rasmi ya Upinzani na Msimamo tuliotoa…

**NAIBU SPIKA:** Ni kanuni gani? Ni kanuni gani unatumia? Ni jambo gani unafanya? Sijaelewa, unanihutubia au unafanya nini?

**MHE. EZEKIAH D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni taarifa, chini ya kanuni ya 68.

**NAIBU SPIKA:** Ameshakaa, sasa taarifa ya nini tena?

**MHE. EZEKIAH D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimevumilia sana kwa maana ya kwamba Waziri amalize nilitoa heshima ili baadaye nitoe taarifa, sikutaka ku-*interrupt*. Nimesimama kipindi ana *wind-up*. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Nakupa dakika mbili!

**MHE. EZEKIAH D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa tuliyotoa ya Kambi Rasmi ya Upinzani na kuhusu uhusiano wetu na Rwanda, sisi Kambi Rasmi ya Upinzani kazi yetu ni ku-*check*. *Check and balance* ya Serikali. Kama Serikali mbadala, tunataka kujenga taswira ya Serikali itakayoheshimu *sovereignty* ya nchi zote duniani kulingana na Kikataba ya Kimataifa ikiwemo *Vienna Convention*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni suala la kusikitisha sana, kama Mheshimiwa Waziri kwa mimi kutoa *position* yangu kama Upinzani anafikiria kwamba natumiwa na nchi nyingine kwamba mimi ni msemaji wa nchi ya Rwanda, naomba kusema kwamba duniani pia haijawahi kutokea katika historia ya dunia, Rais yeyote wa dunia yoyote kuwa msemaji wa waasi katika Mkutano wowote duniani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa kuwa umechokoza mwenyewe na mimi niseme yafuatayo:- *(Kicheko)*

Nilisikiliza kwa makini sana hotuba yako, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. Kwa mtu yeyote mwenye uelewa wa kawaida, ataona kwamba hotuba hii haikuandikwa na Kambi hii. Lazima asilimia 90 au zaidi ya Wajumbe hawa waliokaa hapa watanyamaza, hawakushiriki katika kuandika hotuba hii. Kama wangeshiriki, isingekuwa hivi. Haiwezekani! *(Makofi)*

Mchungaji Peter Simon Msigwa nakuheshimiwa sana. Utaratibu mmoja mzuri katika Bunge lolote lile; kazungumza, tumenyamaza; na mtu mwingine anapozungumza, na nyie mnafanya nini? Ndiyo Bunge lilivyo! Hakuna atakayekusemea! Haiwezekani! Nasema, mimi nawachukulia kama ni watu waelewa, ni watu wazuri sana, ndiyo maana nikasema hivyo. Kama ni kinyume chake, hayo unasema wewe. Nawasemea kwamba ni watu wazuri kiasi ambacho hatuwezi kuisemea nchi jirani tukaisaliti nchi yetu wenyewe, ndiyo maana yangu mimi. Kama ninyi ni kinyume chake, thibitisha hayo! *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, hili ni la kujifunza na ni ushauri wa bure kwenu kwamba tunapotengeneza hotuba ya kundi kama tunavyofanya kwenye Kamati, sisi ni Wabunge wote, tunatengeneza hotuba ya Kamati. Wanakamati tunashiriki kutengeneza hotuba. Mwenyekiti wa Kamati akija kusoma hapa, anasoma kitu ambacho Wanakamati tulikipitia. Sasa ushauri ambao nautoa katika kumalizia suala la Mheshimiwa Wenje, kwa siku zijazo ni vizuri Kambi Rasmi ya Upinzani kweli tukakaa, tukapitia hotuba zetu ili ziwe zetu kweli. Baada ya hapo Katibu tuendelee!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Katibu tuendelee!

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**TAARIFA**

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kidogo! Wabunge wawili hawakusimama!

**MWENYEKITI:** Hapana, hapana! Mheshimiwa Keissy nakuomba tafadhali! Mheshimiwa Keissy nakuomba ukae chini! Katibu tuendelee!

**Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa**

Kif. 1001 - *Admin. and HR Mgnt ... ... ... ... ...* 10,937,135,000/=

**MWENYEKITI:** Sijapata majina ya Upinzani. *(Minong'ono)*

Naomba aseme mmoja. Nani ameandika na mmempa nani?

**MHE. EZEKIAH D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja niliandika nikakuletea na nyingine sasa hivi pia nimeijibu hapo, nimeleta *note*.

**MWENYEKITI:** Kwamba umemteua nani?

**MHE. EZEKIAH D. WENJE:** Kwamba mimi ndio nitasimama kwa niaba ya CHADEMA, Mheshimiwa Moses Machali kwa niaba ya *NCCR* na Mheshimiwa Rajab Mborouk Mohamed kwa niaba ya *CUF*.

**MWENYEKITI:** Sasa kama hivyo ndivyo, basi wengine kaeni. *(Kicheko/Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Haoooo! *(Makofi/Kicheko/Minong'ono)*

**NAIBU SPIKA:** Wanaongea kitu gani?

**ND. JUSTINA SHAURI - KATIBU MEZANI:** Hawajaitwa majina.

**NAIBU SPIKA:** Majina yao ninayo. Ndiyo maana nikauliza, sijapata upande huu! Ya hawa nilishapata tayari.

Tunaendelea! Mheshimiwa Stephen Ngonyani, hayupo. Mheshimiwa Rajab Mborouk Mohamed!

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuzingatia Sheria ya Umma na Sera ya Manunuzi ya Umma, katika mchango wangu nilizungumzia suala zima la ukosefu wa kutumia Sheria za Manunuzi ambalo linafanywa na Maofisa wa Wizara hii hususan katika suala zima la safari za nje. Niliweza kubainisha baadhi ya fedha ambazo zimetumika na Maofisa hawa kwa ajili ya safari za kwenda nje kama ambavyo nimezipakuwa katika tovuti ya Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali; nikatoa mifano miwili ya safari za Maofisa ambao walitumia Shilingi

milioni 44 kwa ajili ya ununuzi wa tiketi, tiketi ambazo uhalisia wake ulikuwa ni Shilingi milioni 23.

Vilevile nikazungumzia tiketi ambazo zimenunuliwa kwa Shilingi milioni 70.8 ambazo uhalisia wake ulikuwa ni Shilingi milioni 18.4. safari hizi za Maofisa wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje liliwahi kujitokeza hata mwaka 2013, na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake mwaka 2012 na mwaka 2013 alisema kama kuna kitu ambacho vilevile atakishughulikia ni suala zima la safari za nje, ama kwenda *group* kubwa ama kuzipunguza ili kuoana na hali halisi ya mapato ambayo anayapata katika Wizara yake.

Katika eneo hili, inaonekana kwamba Waziri bado hajachukua hatua ambazo ameziahidi hapa Bungeni. Naomba nipate maelezo ya kina kutoka kwa Waziri juu ya ufisadi huu ambao unafanywa na Maofisa wake ndani ya Wizara yake. Kama sitapata jibu la kuridhisha, basi nina nia ya kuondoa Shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi!

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Rajabu kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa mwaka 2013 Mheshimiwa Rais aliniagiza kutengeneza timu ya kuangalia orodha ya watu wanaokwenda nje. Wakati ule wastani wa safari za Mheshimiwa Rais na Viongozi kwenda nje ilikuwa ni watu 68. Tulichokifanya cha kwanza, ni mimi mwenyewe katika Wizara yangu ku-*cut* kutoka watu 12 hadi kufikia watu wanne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kila safari anayofanya Mheshimiwa Rais sasa, ni watu wanne tu kutoka Wizara ya Mambo ya Nje ndiyo wanaosafiri.

Pia tulijaribu kuangalia kama nilivyosema na nitazungumza hili *in confidence* kwamba safari ya Mheshimiwa Rais ina Ofisi ya Rais, ina watu wa Usalama wa Taifa, ina watu wa uchumi halafu ina watu wa Mambo ya Nchi za Nje. Wote walijaribu kujibana na ndiyo maana tukafikia orodha ya wastani wa watu 50 na wale watu 50 ukienda kwenye Mikutano, watu 14 hutawaona kwa sababu ya kazi maalum wanazozifanya. Utakaowaona pale ni watu 36 na katika wale watu 36, kila kundi lina kazi yake maalum unapofuatana na Mheshimiwa Rais. Tusingeweza kujinyima zaidi. Kwa hiyo, naomba mwenzangu uyakubali hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo swali kuhusiana na suala la *tickets* ambalo alizungumza *very passionately.* Kinachotokea ni hivi; moja, unapokwenda kwa *travel agent*, wiki mbili kabla ya safari au wiki tatu kabla ya safari, unapata *a very cheap ticket,* kama unatoa *advance notice* ya safari. Lakini kwa mfano kama kifo kimetokea ghafla, au kuna Mkutano umekuja wa dharura unatakiwa kwenda au Rais anatakiwa kwenda, huna ujanja tena. Pale *travel agent* ataku-*charge* mara mara tatu au mara nne zaidi. Ndiyo dunia nzima ilivyo.

Kwa hiyo, tunachokifanya kwenye Wizara ni nini? Pale tunapopata kalenda ya Mikutano kama ya *UN* au ya Uingereza sasa au Mwezi *August* Marekani Obama ameitisha Viongozi wote wa Afrika na yeye; ile mikutano ambayo kalenda zake zinajulikana, *tickets* zinakuwa *cheap*. Hizi ni safari za ghafla ambazo zinatokea chini ya wiki mbili na wenzangu wote mtaunga mkono, gharama ya *ticket* inakuwa kubwa zaidi. Hili ndilo linalotukuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili hatuwezi kulikwepa, kwa sababu safari za ghafla ni za Mwenyezi Mungu, hazipangi binadamu. Ningependa kwa maelezo hayo, twende pamoja. Nashukuru.

**MHE. RAJAB M. MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na majibu ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa. Amejielekeza zaidi katika safari za Rais, lakini vilevile katika safari za ghafla. Hili mimi nalijua sana kuhusiana na suala la safari za ghafla. Nilichokizungumzia mimi, ni kuzingatia Sheria za Manunuzi na Sera ya Manunuzi ya nchi kwamba inakiukwa! Hilo ndilo ambalo nimelizungumizia na nimetoa mifano miwili ya safari ambazo zimefanywa na Maofisa wake, na hazikuwaza za kushtukiza, ambazo zimetumia fedha nyingi, tofauti na zile ambazo zilitakiwa kutumiwa katika uhalisia wake.

Wakati nachangia hapa, nikamwambia Mheshimiwa Waziri, kwamba ni kwa nini sasa Mheshimiwa Waziri, usitumie *ATCL* kwa ajili ya ku-*order* hizi *tickets?* Kwa nini utumie mashirika mengine ambayo kwa kweli unawapa fadia wao badala ya kupeleka faida katika Shirika letu.

Mheshimiwa Waziri, lakini katika Sheria ya Manunuzi, tuna kitu kinaitwa *JPSA*, hii imeweka viwango. Kwa hiyo, bado suala langu hajalitolea majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nang'ang'ania Shilingi ya Waziri, nataka *commitment* ya Serikali, juu ya namna ya kushughulikia ufisadi huu ambao unafanywa na Maofisa wake ndani ya Wizara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wenzangu ambao wataweza kulichangia hili waweze kulichangia.

**MWENYEKITI:** Kabla hatujakwenda huko, Mheshimiwa Rajab, kama nilikusikia vizuri asubuhi, utufafanulie tu. Ulisema kwamba taarifa hii umeipata kwenye *CAG report,* ipi? Asubuhi nilikusikia kama unasema kwamba taarifa hii uliyoizungumza umeipata kutoka kwenye *CAG report*. Ni *CAG report* ipi?

**MHE. RAJAB M. MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii nilisema nimeipakua katika tovuti ya *CAG*, lakini vilevile nimeangalia katika vitabu vya *CAG* kwa taarifa ya mwaka 2011/2012 na 2012/2013.

**MWENYEKITI:** Sasa kama unatuletea mambo ya mwaka 2011/2012, na sisi bajeti tunayoizungumzia ndiyo hii, kwa maana ya matumizi haya tunayoishia ya mwaka mmoja, wewe unatuletea kitu cha miaka kadhaa iliyopita; nawaomba sana Waheshimiwa tuwe tunapeana nafasi, tunazungumza. Hii habari ya kushambulia kwa pamoja na nini, ni utaratibu ambao siyo mzuri sana.

Mchungaji Msigwa kwa mara ya pili, mimi nakusikia; mimi ndiyo Mwenyekiti. Kanuni zinaniambia kwamba, ninayemsikia nimtaje jina. Kaa chini tafadhali! Nimekusikia ukiongea, tafadhali kaa chini. Ahsante sana. Tuendelee! Ni onyo la pili nakupa Mheshimiwa Msigwa, usiendelee kusema namna hiyo. Mheshimiwa Rajab!

**MHE. RAJAB M. MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya kudadavua katika tovuti niliyokwambia, hii ni taarifa iliyoishia tarehe 31 Machi, 2014 ndiyo ambayo imetoa taarifa hizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tupate ufafanuzi kidogo Mheshimiwa Waziri kwanza.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka tu nimshauri mwenzangu, kwa kuwa ni kitu *specific* cha watu inaowahusu, kwa nini asitupe muda sisi, twende tukalifanyie kazi. *This is not a big deal!* Siyo suala la *policy*, ni watu mafisadi kama anavyowaita, wako mle. Tutakwenda kuchunguza, tutaomba na wenzetu wa TAKUKURU waliangalie, halafu mambo yakienda vizuri nitakuja kulitolea taarifa hapa. Nirudishie Shilingi yangu tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** *Actually*, kabla hujaongea Mheshimiwa Rajab, ushauri wangu pia ulikuwa ni huo, ndiyo maana nikauliza habari ya *CAG report*. Kwa sababu wewe ni Mwenyekiti mmojawapo wa Kamati za Fedha, ambazo kwa kweli zinashughulikia mambo haya yanayotokana na *CAG*, kama kuna wizi, kama kuna ufisadi.

Kwa hiyo, nakuomba kama Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, baada ya kuligundua jambo hili ambalo inaelekea ni la kweli, basi tutoe nafasi kwa

kutumia Ofisi yenu, zile Ofisi zetu za Kamati za Fedha, na kama sisi ndio wasimamizi wenyewe hasa, tuli-*persue* hilo jambo tuone tutafika wapi. Ni ushauri tu kama utaukubali, Mheshimiwa Rajab.

**MHE. RAJAB M. MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na ushauri wako. Mheshimiwa Waziri, Shilingi naiacha. Unajua mimi nakuamini sana, kwa sababu una malengo mazuri ya mwaka 2015, sawa! *(Makofi/Vigelegele)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rajab, malengo gani hayo tena? Mheshimiwa Machali! *(Kicheko)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, wakati nachangia, nilijielekeza kwenye ukurasa wa 24 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nilizungumzia suala la mikataba mbalimbali ambayo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesaini. Nikaomba kwamba pengine itakuwa ni vizuri wakati Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wana-*wind up* basi waweze kutusaidia, angalau watueleze hii mikataba ambayo imesainiwa halafu mpaka leo haijaletwa ndani ya Bunge lako Tukufu ili iridhiwe; ni sababu gani ambazo zinapelekea mikataba hii kuendelea kuchelewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, ukijaribu kuangalia, kwa *records* za Bunge letu, iko mikataba ambayo tumepata kuiridhia ilisainiwa miaka ya 1980, miaka ya 1990, ikaja ikaletwa miaka hii ya 2000 na kitu, nakumbuka na mimi nikiwa ni Mbunge na hata mingine kabla sijawa Mbunge, Serikali imekuwa ikisaini mikataka kwa muda mrefu.

Sasa *issue* ni moja, kuna tatizo gani kwa Serikali kutokuharakisha kuleta mikataba hii ili tukajua? Kama pengine kuna upungufu fulani, Bunge ambalo ndilo pengine lina watu ambao wanawakilisha wananchi, wataishauri Serikali kuweza kufanya *review* juu ya mikataba hii na hatimaye pengine hatua ambazo ni *appropriate* zinaweza zikaja zikachukuliwa.

Vile vile nilisema, hata Rais wa China wakati anafanya ziara mwaka 2013 iko mikataba iliyosainiwa. Wananchi wanauliza, ile mikataba ina maslahi mapana kiasi gani kwa nchi yetu? Mikataba mingine tena tunaona imetolewa hapa mikataba 13, hatujui! Kuna tatizo gani kwa Serikali kutokuleta mikataba hiyo haraka ndani ya Bunge hili? Pengine itakuwa ni vizuri hata mikataba mingine kabla hamjasaini, kwa nini msilete pengine kuja kuliomba Bunge kuweza kupata mawazo yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nitakuwa sijapata maelezo ya kutosha, nitatoa Shilingi. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mbona unawahi kwenye Shilingi jamani! Mtu mwema anasubiri maelezo, lakini ukiona mtu asubuhi asubuhi kesha…! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri tafadhali, maelezo!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Machali anachanganya mambo mbalimbali. Ni utaratibu wetu na kusema kweli ni utaratibu wa nchi nyingi za *Common Wealth* kwamba mikataba ambayo inapelekwa Bungeni kuridhiwa ni ile ambayo tunaiita *multilateral*. Ni ile mikataba ambayo inahusisha nchi nyingi, na kwa asili yake huwa inahitaji ridhaa ya Bunge.

Mikataba ambayo imetajwa hapa, hii ni mikataba ya nchi mbili *(bilateral)* ambayo mara nyingi huwa inaishia katika Serikali tu. Isipokuwa taarifa pia huwa tunatoa katika Kamati ya Bunge, na hii haihitaji ridhaa ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sehemu ya pili ambayo nimesema amechanganya ni kwamba, ni kweli kuna mikataba ambayo inahitaji ridhaa, na nchi inakuwa tayari imesaini lakini huwa inachelewa kuletwa Bungei kwa ajili ya ridhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili ingawa kama Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, sisi ndio waratibu, lakini kutegemea na *subject matter* ya ule mkataba ni Wizara husika ndiyo yenye jukumu la kuleta mkataba ule kwenye Bunge kwa ajili ya ridhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, mikataba unayoongea ni mingine.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa tafsiri nyingine ni kwamba, kama wao wanasema wanaripoti kwenye Kamati ya Bunge, na Kamati za Bunge hazijaweza kulipatia Bunge lako taarifa hizi, na hata ukienda *library* ya Bunge, hii mikataba haionekani. Basi ina maana tatizo litakuwa kwetu kwenye Taasisi ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nikuombe tu mwongozo wako, kama *in case* ni kama ambavyo anatuambia hii mikataba iliyoorodheshwa mahali hapa ipo, hivi sasa wamesharipoti kwenye Kamati, labda sijui utusaidie wewe sasa, maana yake inaonekana kuna Kamati ambazo mmesha-*discuss.* Kama bado, basi watusaidie maelezo, kama ipo au haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa Shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, utaratibu wetu wa kawaida tulishaambiana sisi Wabunge kwamba kama Mbunge yeyote anahitaji mkataba wa aina fulani Serikalini, anawasiliana na Katibu wa Bunge, utaratibu unawekwa ili Mbunge huyo aweze ku-*access* mkataba maalum. Wabunge wote mmeshaambiwa jambo hili, mnalifahamu. Kwa hiyo, kama una *interest* na mkataba fulani, utaratibu wetu ndiyo huo. *(Makofi)*

Nadhani tuendelee, kwa sababu una uhuru huo wa kupata mkataba kwa kweli, labda kama ungeripoti kwamba nimetaka mkataba fulani, nimenyimwa! Hiyo ndiyo ingekuwa *issue*.

Mheshimiwa Abas Mtemvu!

**MHE. ABAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia masuala ya ajira na nilimpongeza sana Waziri wa Kazi na Ajira kwa ushirikiano, pamoja na yeye mwenyewe Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Nikaelezea kwamba mimi ni Mwenyekiti wa *Bravo Job Center,* tunafanya kazi na Dubai, tunafanya kazi na Muscat, tunatoa ajira nyingi za madereva, ajira nyingi za Manesi, ma-*housemaids* na ulinzi.

Hata hivyo, nikamwuliza Mheshimiwa Waziri, nilikwenda *Qatar*, nikakutana na Waziri wa Kazi, tukapata kampuni moja kubwa tukaingia nayo mkataba kufanya kazi Qatar na Saud Arabia. Nikaenda Saud Arabia, nikakutana na Balozi. Balozi wa Saud Arabia hadi leo kazuia Watanzania kwenda kufanya kazi kule. Nimekuletea maandishi, nimekuleta *copies* za *Visa*.

Sasa Mheshimiwa Waziri, nilikuwa naomba, unifahamishe, kuna tatizo gani Saud Arabia mpaka Watanzania wanazuiwa kwenda kufanya kazi? Sina dhamira, lakini nimekwambia nitatoa Shilingi, lakini sina dhamira kwako kutoa Shilingi. Nimeleta barua karibu tano kwenye Wizara yako, hata barua moja sijapata jibu.

Mara ya mwisho niliongea na wewe tukiwa kwenye *Jet* na Waziri wa Fedha na Makamu Mwenyekiti wa Mambo ya Nje, ukaniahidi, Mtemvu haraka sana na Balozi hana uwezo wa kuzuia Watanzania wasiende kufanya kazi. Tatizo ni nini?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mheshimiwa Abas Mtemvu kwa moyo wake mzuri wa kutafuta ajira nje ya nchi kwa Watanzania ambao wanashindwa kupata ajira hapa. *(Makofi)*

Yote aliyoyasema ni sahihi kabisa! Nimemwita Balozi wetu, na hata hivi ninavyozungumza yuko Dar es Salaam. Nimepata nafasi ya kuzungumza naye kuhusu suala hili. Kwanza niseme kwamba *Bravo Job Center* imesaidia kuwapeleka wafanyakazi wengi sana kule.

Kilichomfanya Mheshimiwa Balozi ashindwe kuwaruhusu *housemaids*, yaani wasichana wa ndani kuingia kule, ni kwa sababu ya matukia yasiyopungua matano ambayo yalitokea kwa wasichana wa kazi ambao walikwenda Saud Arabia. Walipokwenda kule, wengine walijikuta wanapelekwa jangwani kwenye mahema, kwenye *summer jobs*. Wanapokwenda kule, wanakaa baada ya miezi sita, tukiuliza wako wapi? Hawapo, na wengine wanarudi wanajuta kupigwa na wengine kufanyiwa vitendo ambavyo kwa kweli siyo vya kibinadamu.

Kutokana na hali hiyo, aliomba kwamba, linapofika suala la *housemaids*, kwa sababu wanaweza kutumiwa na watu ambao wana nia mbaya, asitishe kwanza upelekaji wa watu hawa ili kuwe na utaratibu mzuri sana wa kujaribu kuwa na uhakika wa wapi wanakwenda, mwajiri anakuwa nani? Tusije tukawapoteza wasichana hawa, wasije wakapata matatizo wasichana hawa, tukapata matatizo makubwa! *(Makofi)*

Hiyo ndiyo ilikuwa busara ya Mheshimiwa Balozi. Lakini nimemhakikishia Mheshimiwa Mtemvu kwamba wasichana wa kazi watakwenda, lakini watupe muda, sisi pamoja na Wizara inayohusika na ajira ili kuweza ku-*cross check* na ku-*counter check* kwa kushirikiana na *Bravo Center*. Wale wanaume hawana matatizo kabisa, tatizo tunalo kwa hawa wasichana. Namhakikishia tena ndugu yangu na kaka yangu; Bwana Zuberi, atupe muda, tuweke utaratibu mzuri tu. Tutakushirikisha, kwa sababu nia yako ya kusaidia Watanzania iko palepale, lakini tuwe tunakwenda polepole, tukizingatia pia usalama wao. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri anasema wale wanaume hakuna shida, lakini habari zisizothibitishwa zinasema hao pia nao kuna matatizo kidogo kidogo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa mtemvu!

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Sikuleta kwako *sample* ya *housemaids*, nimekuletea *sample* ya madereva ambao wamepata nafasi kule lakini Balozi amezuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikuhakikishie, wale wanaopelekwa jangwani ni watu wanaokwenda hawana *security*. Sisi Dubai pale, ukiongea na

Balozi; wa kwanza, Maharage, *Chief of Protocol* na wa sasa, watakwambia; tuna Ofisi, tunawakagua watu wetu wote, wanaume na wanawake. *Muscat* hivyo hivyo, tumefungua Ofisi. Utakapojaliwa kwenda kule wewe uliza tu, Ofisi ya *Bravo Job Center.* Siyo hilo tu, pale tunatafuta masoko. Sasa tuna masoko ya korosho, tuna masoko ya mbuzi, tuna masoko ya vitu vingi. Tunataka tuwaambie Watanzania wanaoweza kufanya ili wafanye.

Mheshimiwa Waziri, mimi nafikiri Saudi Arabia liko tatizo. Tazama hilo tatizo, tunahitaji ajira. Tunahitaji Watanzania wakafanye kazi nje. Nchi za kiarabu kuna ajira kubwa na mshahara mzuri. Nakushukuru, siondoi Shilingi yako, lakini nakuomba ulitazame, Watanzania wapate ajira. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu!

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Sina nia ya kutoa Shilingi. Kwenye *speech* hii ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 19, *section 58* inasema: "Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Shirika la *Emirates*, limekubali kuanzisha safari za ndege za Shirika lake lingine la *Fly Dubai* kutoka Dubai kwenda Kilimanjaro, Dar es Salaam na Zanzibar. *Fly Dubai* ni Shirika lenye bei nafuu kwa wateja."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika hili liko *affiliated* na *Emirates. Emirates* wana *policy* ya kutoa ajira kwa kila ambapo wanakwenda kutua, kwa mfano hapa kwetu. Sasa hili suala ambalo tumewahi kuzungumza na Mheshimiwa Waziri: Je *quarters* za Tanzania kupata ajira kwenye *emirates*, bado hatuzichangamkii; na hatuzichangamkii kwa sababu *emirates* kuna sintofahamu. Nilitaka kujua sasa Wizara, na kwa utalaam aliokuwa nao yeye, ni juhudi zipi sasa za Wizara kuwabana *emirates*? Ni lazima Watanzania wapewe *quarters* zao ili na wao wafanye kazi *Emirate* kwenye ndege na kwenye vituo vingine ambavyo wana *services* zao ambazo wanazo katika uwanja wa ndege pale Dubai na maeneo mengine katika Shirika la Ndege hili la *Emirates*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ufafanuzi Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba nijibu swali la Mheshimiwa Azzan Zungu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Ni kweli kabisa kwamba tumepata taarifa za kauminika, jambo ambalo hatukuwa tumelijua mpaka alipokuwa ametushtua, kwamba kumbe *emirates* kila inakotua, na kama inakwenda mara mbili, au kila siku; mara saba, yaani

mara saba kwa wiki, kuna *quarter*. Yaani kuna idadi ya wafanyakazi ambao *Emirates* watatakiwa kuwaajili kutoka kwenye ile nchi.

Tumemwagiza Naibu Balozi wetu Dubai, na taarifa za awali tulizopata ni kwamba wanatakiwa waajiri Watanzania wasiopungua 50. Kuna Mkutano utafanyika Shirika la *Emirates* kama nilivyoeleza kwenye kitabu, tutafuatilia sana suala la *quarters* zetu pamoja na mashirikia mengine ikiwemo *Air Oman,* pamoja na *Turkish airlines,* na *airlines* nyingine zote ambazo zinakuja Dar es Salaam ili tujue *quarters* zetu kama zipo na ili tuwaombe Watanzania wenye elimu inayolingana na sifa hizo, waombe na tupo tayari kuwasaidia ili tuweze kuzioshika *quarters* zetu na hivyo kuwa na wafanyakazi wengi kwenye ajira hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Mheshimiwa Wenje, dakika zangu karibu zinaisha kabisa, jaribu kuzitumia zilizobaki.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ni dhahiri kwamba misaada haiwezi ikatusaidia kuendesha nchi yetu na tukawa na uchumi thabiti. Ndiyo maana suala la diplomasia ya kiuchimi, tunatakiwa tuitilie mkazo ili ituletee tija ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *votes* katika hiki kitabu cha mipango ya maendeleo imeweka fedha kwa ajili ya *acquisition*, *expansion* na *rehabilitation* ya majengo, lakini haijazungumzia kabisa ni namna gani tutapata fungu kwa ajili ya diplomasia ya kiuchumi ili tuweze kufanya matangazo ya fursa tulizonazo Tanzania, lakini pia ili tuweze kusafirisha, hata kama kuna mtu yuko Washington, asafiri kwenda mpaka New York, afanye hata Kongamano kueleza wafanyabiashara huko ni fursa zipi tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni kweli kwamba ili tufanye diplomasia ya kiuchumi, tunahitaji vitu viwili vikubwa. Moja, tunahitaji mahusiano mema na nchi ambazo tunahusika nazo, majirani zetu, lakini pia tunahitaji fedha kwa ajili ya kutekeleza haya masuala ya diplomasia ya kiuchumi. Kwa hiyo, kwa sababu hakuna *vote* maalum inayohusu *economic diplomacy* nataka Waziri atupe *commitment*, mafungu yaliyoko hapa hakuna hata moja litakalosaidia, kwa sababu suala la uchumi ni suala la matangazo, ndiyo utatangaza fursa ulizonazo ili watu waje wawekeze; ili tutokane na hii diplomasia ya ombaomba; kuombaomba ni aibu. Suala la kwenda kuombaomba huko halafu tunakuja kupiga kifua hapa kwamba sisi ni waombaji hodari, imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atupe *commitment*, pesa inakwenda kupatikana wapi kwa ajili ya *economic diplomacy*? Atupe *commitment!* Hivi hivi tusipopata *commitment* vizuri, nitakamata Shilingi ya rafiki yangu, Mheshimiwa Membe.

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Mheshimiwa Mahadhi!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wakati alipokuwa akitoa maelezo ya hoja mbalimbali alieleza kwa upana jinsi diplomasia ya uchumi inavyotekelezwa. Moja, alieleza kuwa katika hatua za awali ambazo tunazifanya ni pamoja na kuwa na majengo na Ofisi nzuri ili pia tuweze kuchukua Maafisa wa ziada watakaoshughulikia sekta maalum katika Balozi zetu huko.

Pia tulieleza kwamba suala la diplomasia ya uchumi linajumuisha watu wengi, linajumuisha sekta nyingi, linajumuisha sekta nyingi, linajumuisha Wizara zote. Kwa hiyo, siyo lazima kuwe na kifungu maalum wakione, lakini vifungu vyote vilivyopo hapa kwa ujumla wake pia vinatekeleza suala la diplomasia ya uchumi. Vile vile tumekuwa mfano katika suala la matangazo na labda vipeperushi. Tumekuwa tukishirikiana pia na Taasisi nyingine ambazo zinashughulikia mambo hayo moja kwa moja kama *TIC, TANAPA*, wamekuwa wakitengeneza na kuwapa Balozi zetu kwa ajili ya kutangaza sekta hizo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Waziri kivuli kwamba katika bajeti hii tayari kuna vifungu vya kutosha vya kuweza kushughulikia diplomasia ya uchumi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wenje!

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kweli kwamba kuna kifungu hata kimoja hapa kinachoshughulikia diplomasia ya kiuchumi. Kuongeza idadi ya watumishi kwenye Mabalozi; kila nikisafiri, nchi yoyote nikienda, nakwenda kwenye *Embassy*.

Nimewahi kwenda Marekani, tunaye *Economic Attache*, hana fungu hata moja linaloweza kumsaidia kusafiri kwa mfano kutoka Washington afike hata New York akaitisha kikao, atafute wafanyabiashara ambao wako kule, aeleze fursa zilizopo Tanzania ili watu waje wawekeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia vifungu hivi vyote ambavyo vipo hapa kwenye kitabu cha matumizi, hakuna kasma hata moja inayoshughulikia masuala kama haya. Kuna nchi nyingine unakuta kuna matangazo yapo hata kwenye *CNN*, wanatangaza utalii kwenye nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijawahi kuona tangazo hata moja kwenye *CNN*; *Economic Attaches* tulizonazo kwenye Mabalozi hawana fungu hata moja linalowawezesha kufanya hata kongamano moja la kiuchumi ya kueleza fursa tulizonazo. Tuchukue kitu hiki *serious*! Hii ndiyo fursa peke yake ya sisi

kuondokana na diplomasia ya ombaomba! *This begging diplomacy is enough*! Tusipo-*strengthen economic diplomacy* kwa maana ya mafungu, *we are going no where*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa Shilingi, naomba Mheshimiwa Waziri atupe *commitment* fungu liko wapi la ku-*strengthen economic diplomacy?* Naomba wenzangu wanisadie.

**MWENYEKITI:** Kwa sababu ya muda, muda wa zile dakika za Mheshimiwa Waziri kwa kweli karibu zimekwisha kabisa. Basi niwape watu wawili kuchangia; Mheshimwa Mbowe na Mheshimiwa Mnyika. Upande huu sioni mtu. *(Kicheko/Mionong'ono)*

Wako wapi? Mheshimiwa Lusinde na Mheshimiwa Kigwangalla. Tuanze na Mheshimiwa Mbowe!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Wenje kwamba unapozungumzia *Economic Diplomacy* ni lazima uzungumzie na *component* ya usalama na *component* ya kuaminika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuzungumza kwa kifupi sana kwamba hoja aliyoizungumzia Mheshimiwa Wenje ni *valid* na hotuba aliyoizungumza Mheshimiwa Wenje leo wakati akiwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani ni maoni ya Kambi. *(Makofi)*

Mimi namwelewa sana Mheshimiwa Membe na ninamheshimu sana utendaji wake wa kazi. Lakini vile vile ninaamini kwamba alivyozungumza Mheshimiwa Membe ni sifa muhimu sana kwa nchi yetu kuwa ni nchi ya upatanishi.

Tanzania tumekuwa ni kiungo cha upatanishi, Tanzania tumekuwa ni kiungo cha kuunganisha mataifa mbalimbali, na Tanzania tumekuwa ni kimbilio wakati wowote panapotokea matatizo katika ukanda wetu wa Maziwa Makuu, Tanzania tumeonekana kama ndio watu wa kukimbilia kutafuta usuluhisho na sio watu wa kukimbilia kuongeza mgogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli vile vile kwamba kila nchi ina *foreign policy* yake. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri alipozungumza hapa kwamba hakuna nchi yoyote duniani ambako wanaweza kupingana kuhusu *foreign policy,* taarifa zile zilikuwa kidogo siyo za kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme tu kwamba unaweza kukumbuka mfano, kwamba katika katika Bunge la Uingereza walivutana sana katika *House of Commons* kuhusiana na maamuzi ya Waziri Mkuu wa Uingereza, Tony Blair kupeleka majeshi katika nchi ya Iraq na akatoa taarifa ambazo hazikuwa sahihi sana, jambo ambalo lilipelekea kuanguka kwa utawala wa Tony Blair kama Waziri Mkuu wa Uingereza.

Aidha, tunakumbuka mgogoro mkubwa sana uliokuwa katika *Congress* Marekani, ikiwa sehemu zote mbili za Bunge la Marekani zikimshambulia Rais wao wakati ule George Bush kwa namna alivyoweza kupeleka majeshi katika nchi za nje katika *foreign policy* yake, jambo ambalo Wamarekani wengi waliona halina maslahi mapana kwa nchi yao. Aidha, Kenya kabla ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika mara ya mwisho kulikuwa kuna mvutano mkubwa sana katika Bunge la Kenya kuhusu upelekaji wa majeshi ya Kenya nchini Somalia, jambo ambalo limesababisha matatizo makubwa sana kwa wanachi wa Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba CHADEMA kama Kambi ya Upinzani tutaiunga mkono Serikali wakati wowote bila kujali ni Serikali ya Chama gani, pale ambapo itakuwa inatoa misimamo ambayo na sisi tunafikiri ina maslahi mapana kwanza kwa Taifa letu, na vile vile ina maslahi mapana kwa nchi za jirani kwa sababu wote tunawahitaji, sisi ni watu wapatanishi na siyo watu wa kugombanisha Mataifa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, niseme kwamba tunaweza tukafanya maamuzi mengine kwa nia njema, lakini tukawaumiza askari wetu. Tunaweza tukashabikia kwa upande mmoja, tukafanya maamuzi ambayo katika *long run* yakawa na madhara makubwa kwa Taifa letu. Namwombe Mheshimiwa Waziri, huu mgogoro wa Afrika ya Mashariki, huu mgogoro wa Tanzania na Rwanda, siyo mgogoro wa kistaarabu, tutafute utaratibu wa kuumalizia. *(Kicheko/kelele)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbowe umeshatoka kwenye hoja ya *economic diplomacy!*

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Ndiyo diplomasia yenyewe, masuala ya usalama.

**MWENYEKITI:** Tupo kwenye uchumi wa kidiplomasia, halafu dakika zako pia zimekwisha. Malizia tu Mheshimiwa.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Nimalizie kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri… *(Minong'ono)*

**MWENYEKITI:** Tuvumiliane tafadhali! Ndiyo ule uvumilivu niliokuwa nasema tangu mwanzo.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Nasema nimshauri Mheshimiwa Waziri, kwa nafasi ambayo Tanzania imejizolea sifa kwa kuwa nchi patanishi, na ninaomba Waheshimiwa Wabunge mnielewe, siyo sifa kwa sisi Tanzania kugombana na wenzetu. Tunapoweza kutumia diplomasia kumaliza matatizo yetu…

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Rwanda iendelee kuiba Kongo?

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Tumalizeni matatizo yetu! Malizeni matatizo ukanda wa Maziwa Makuu kwa kutafuta diplomasia ya kutatua migogoro, tusiendekeze kuwa na ushabiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Mbowe. Tayari, nakushukuru sana.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, kwa kifupi sana!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Wenje kwamba kwenye kitabu cha maendeleo hakuna mradi wowote wa diplomasia ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunaweza, kwenye kitabu cha matumizi ya kawaida kuongeza fungu la safari kutoka Shilingi bilioni 9.3 zilizotengwa mwaka 2013, kuwa Shilingi bilioni 23.8 kwa ajili ya safari za viongozi nje; tuna uwezo kabisa wa kutenga pesa za miradi ya maendeleo inayohusu diplomasia ya kiuchumi. *(Makofi)*

Vile vile ndugu zangu, niseme kwamba jambo hili Mheshimiwa Waziri ni vizuri akalichukulia kwa uzito unaostahili. Bado tunafikiria diplomasia ya ombaomba. Wenzetu wa India, China, Marekani na Afrika ya Kusini, wanafikiria diplomasia za kibiashara, sisi bado tunafikiria diplomasia ya kuombaomba.

Naomba kuunga mkono hoja hii kwamba tunahitaji kupanua wigo wa uwezo wetu wa diplomasia ya kimataifa, tuelekeze nguvu kwenye Balozi zetu, kwenye masuala ya kiuchumi kudhibiti utoroshaji wa pesa nje kwenye masuala ya ufisadi, kurejesha pesa kutoka nje, kudhibiti ukwepaji mkubwa wa kodi wa Makampuni ya Kimataifa kama tutaweka mfumo vizuri zaidi wa Balozi zetu kushauri mazingira ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwamba tatizo letu, tunazungumza sana diplomasia ya kiuchumi, lakini ukweli ni kwamba tunaweka kipaumbele zaidi diplomasia ya kijeshi. Kuna mtu amezungumza hapa akirushia neno kwenye jambo hili kuhusiana na *DRC* kwamba tuwaache Warwanda wapiganishe vita Kongo? Nchi hii imeingia kwenye kashfa ambayo kila mwaka wa fedha nimekuwa nikimwuliza Waziri wa Fedha; kashfa ya Meremeta ni kwa sababu Tanzania ilikwenda kupiganisha vita kule *DRC*…

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Siyo kweli! Siyo kweli!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Nasema hivi, kama siyo kweli nitakiwe kuleta ushahidi, na nitaleta ushahidi.

**MJUMBE FULANI:** Rwanda inaiba Kongo mpaka kuku! *(Kicheko)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema ni nini? Tanzania kama Taifa tutangulize mbele diplomasia ya kiuchumi badala ya kupenyeza chini kwa chini diplomasia ya kijeshi ambayo inatuingiza kwenye migogoro na tuhuma zisizo za maana. Ni hii rai yangu kwa Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nawaomba utulivu. Pande zote, zinazotetea Rwanda na zinazopinga Rwanda na kadhalika, tujue tu kwamba mambo haya yana gharama kubwa kisiasa. Tunaweza tukaona kama ni mambo ya kubishana bishana hapa Bungeni, iko misimamo ambayo gharama yake ni kubwa sana kisiasa. Ningeomba wanasiasa tuwe makini kabla ya kuchukua misimamo ya kujaribu kujitambulisha na vitu fulani fulani. Ni ushauri tu! Mheshimiwa Lusinde. *(Makofi)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kupata fursa ya kumsaidia Waziri kivuli, Mheshimiwa Wenje.Siku zote huwa nasema, vivuli havina hakika sana, kwa sababu saa 6.00 kinakuwa kiko sehemu nyingine na saa 12.00 kinakuwa kirefu kuliko mtu mwenyewe. Kwa hiyo, kivuli siyo kitu cha kuamini sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiisoma vizuri hotuba imeeleza. Hotuba imeeleza namna ambavyo ajira mpya zinatangazwa, kuimarisha Ofisi zetu nje ya nchi, mpaka hata kufikia kuzungumzia Ofisi ya Guang zhou na maeneo mengine ya Schengen ili kuweka biashara vizuri, kutangaza vivutio muhimu vya nchi yetu. Unataka *diplomacy* ya uchumi upi kama ukishakuwa umetangaza, ukishakuwa umeimarisha mahusiano? Lakini hata haya yote yanayozungumzwa, tuwe wakweli! Ni kweli diplomasia ya usuluhishi ni muhimu sana mahali pote; kuanzia kwenye nyumba zetu, kwenye Serikali na maeneo

mengine. Lakini hata rafiki yangu Kiongozi Mkuu wa Upinzani Bungeni, amejaribu kweli kusuluhisha imeshindikana, wameamua kuchukua hatua za kufukuza baadhi ya watu wengine. *(Kicheko/Makofi)*

Hiyo ni kuonesha kwamba diplomasia nayo ina mipaka yake. Huwezi tu ukaenda unasuluhisha kitu; ukishaona inashindikana wengine una-*divorce*. Nao wamefanya, na wamesema ni maamuzi ya kishujaa. Sasa yanapofanyika maamuzi ya kishujaa, tusiwe tunaanza tena kusema lazima turudi kwenye diplomasia. Diplomasia ina mipaka yake. Mnafanya, mkiona hapa imezidisha, nanyi kidogo mnaweka kigingi kama ambavyo ninyi mmechukua uamuzi mgumu hivi karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niunge mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri, iko vizuri. Kwa hiyo, kwa kweli wala tusipoteze muda, tumpongeze Waziri wetu na tuhakikishe kwamba mambo haya machache aliyoyasema yataongezewa, isipokuwa mwakani sasa, kwa maana wakati mwingine tusiangalie tunapoangukia, tuangalie tunapojikwaa; mwakani bajeti yao tuwaongeze kwa nguvu zetu zote ili waweze kufanya mambo makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru, ahsante sana Mheshimiwa Lusinde. Wa mwisho, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote nitumie fursa hii kusema kwamba diplomasia ya kiuchumi katika ukanda huu wa maziwa makuu kwa kiasi kikubwa itaendelea kudumu kama diplomasia ya ulinzi na usalama katika maeneo haya itaendelea kudumu. Kwa maana hiyo, niwapongeze sana Wanajeshi wa vikosi mbalimbali vya Tanzania ambao wamekuwa wakishiriki kulinda amani katika Maziwa Makuu katika *mission* mbalimbali ikiwepo ile ya *MONUSCO* kule Kongo na nyinginezo. Nahamu kuna mdogo wake Mbunge mmoja kutoka Kambi ya Upizani, rafiki yangu, alikuwa mstari wa mbele katika *mission* ya *MONUSCO* kule Kongo.

Vijana hawa wanafanya kazi nzuri sana, ni wazalendo, wana mapenzi ya dhati na Taifa letu na wanaendelea kusumisha amani katika ukanda wa Maziwa Makuu, amani ambayo itatuwezesha kuendelea kudumisha diplomasia ya uchumi, ukizingatia kwamba Tanzania imekaa kimikakati sana katika ukanda huu katika dhana hii ya diplomasia ya uchumi katika Maziwa Makuu. Kwa maana hiyo, inasikitisha sana kuona leo hii Mbunge wa Bunge hili la Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania anaweza kukubali kuwa kuwadi wa kuwasaidia maadui zetu na kuwasemea maadui zetu ndani ya Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tuwe na mapenzi mema na Taifa letu, tuwe wazalendo, tuendelee kuchunga ndimi zetu, kuchunga kauli zetu kwenye mambo *sensitive* kama usalama na ulinzi wa Taifa hili, hususan katika diplomasia nzima ya ukanda wa Maziwa Makuu. Eneo hili sasa hivi ni tete sana, na kwa namna yoyote ile kauli zetu sisi wanasiasa inapaswa kuwa ni zenye kuchagua maneno sana unapozungumzia migogoro hii ya Maziwa Makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Daktari, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE YA NCHI NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kubwa lililojitokeza hapa ni *la Economic Diplomacy.* Ningependa kusema hivi, ukiangalia jumla ya bajeti iliyotengwa kwa Balozi zetu zote ni Sh. 78,288,000,000/= hiyo ndiyo bajeti ya Balozi zetu zote.

Katika hizi, Sh. 73,288,000,000/= zimetengwa kwa ajili ya maeneo maalum, tunaita *ring fence*, kwa mfano ulipaji wa nyumba, mishahara na mambo mengine yote. Sh. 2,000,000,000/= ndizo zimetengwa kwa ajili ya *economic diplomacy*. Kwa hiyo, siyo kwamba hatukutenga, semeni tu kwamba hazitoshi. Kwa sababu mmetoa *drive* hii, kwamba ni vizuri tukatenga; labda ni pesa nyingi zaidi, basi mwakani katika mwaka wa fedha unaokuja wa 2015/2016 nitaleta fungu kubwa zaidi ili tusaidiane katika diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hiyo diplomasia ya ombaomba toka niingie kwenye Wizara na wenzangu, haipo. Mheshimiwa Rais anapoleta wawekezaji ndani ya nchi, anapoleta wafanyabiashara ndani ya nchi, hujapata hela hapo za ombaomba! Wanaleta wawekezaji, wanakuja nchini, wanakuja kuangalia miradi ya kuwekeza kwenye biashara, kwenye utalii na kwenye shughuli nyingine wanaondoka. Hatujaomba senti yoyote!

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo kama ya zamani ya kuomba hela ukapewa, hayapo tena. Kama ingekuwa biashara yenyewe ni ya kuombaomba, tusingekuwa hapa. Sasa hivi ni *business partnership*! Unaomba wawekezaji, wafanyabiashara, na watu wengine wanakuja nchini. Huendi na bakuli tena. *Unless* kuna *drought* kama ilivyokuwa Somalia, *unless* kuna vita halafu Shirika la Wakimbizi linakuja kusaidia.

Nchi ambayo ipo huru, *sovereign state*, na ina *resources* zake kama Tanzania, historia ya kuombaomba tena haipo. Kama unadhani sisemi kweli, nendeni mkajaribu kuomba nje kama mtapata hela! *There is no that money!* Ni *partnership*!

Kwa hiyo, ningependa niseme, tutaongeza kiwango *cha economic diplomacy* katika maana ya utendaji, tutashirikiana na Wizara husika kutupa *brochures*, tutaongeza kiwango cha *two billion* ambacho kinaonekana hakitoshi, lakini baada ya kufanya hivyo, iwe hiyo sasa kwenye *financial year* inayokuja. Lakini mpaka hapo itakapofika, tutashirikisha Wizara zote hasa zile za Sekta za Uchumi kuwasiliana nasi ili waweze kutusaidia kusukuma gurudumu la *economic diplomacy*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wenje!

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi Shilingi bilioni mbili anazungumza Mheshimiwa Waziri za *Economic Diplomacy* katika vitabu hivi vyote, hakuna sehemu ambapo iko *indicated unless* kama kuna kitabu kingine ameacha nyumbani. Katika vitabu hivi, hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili suala la misaada, Mheshimiwa Waziri alivyokuwa anajibu hapa amejibu sana akisema kwamba Rais alikwenda Marekani akapata misaada *Millennium Challenge Account,* alienda Kuwait akapata misaada, hii yote ni misaada ambayo sasa hivi anasema tena hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *anyway,* mimi nachotaka kusema ni kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri wewe mwenyewe unajua kwamba hata pesa ulizotengewa mwaka jana *about* 30 *billion* mpaka sasa mwaka wa fedha unaisha una 6.5 *billion* peke yake. Sisi hapa tunachojaribu kufanya ni kukusaidia ku-*strengthen* Wizara yako ili *deliverables* ziwepo siku moja uache *legacy* isiwe kwamba na wewe ulipita tu kama wengine walivyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Serikali imeishazoea sana diplomasia ya ombaomba, naomba nimrudishie shilingi yake ili waendelee kuombaomba. Nashukuru sana. *(Kicheko)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* … .........Tshs. 820,086,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 – *Foreign Affairs Office Zanzibar* ...Tshs.598,559,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba niko kwenye *subvote* 1003, kasma 221300 – *Education Material, Supplies and Services.* Hapo tunaona kuna Sh.500,000/= hivi kweli hiyo ni fedha kiasi gani ambayo inaweza kutosha kwa shughuli hizo za vifaa vya mafunzo katika ofisi hii? Hilo ni fungu muhimu sana na naliona limetengewa fedha kidogo sana na umekuwa ni uzoefu wa kawaida kutengewa fedha kidogo. Mwaka 2012/2013 zilitengwa Sh.200,000/=, halafu mwaka 2013/2014 walitengewa Sh.500,000/= na safari hii Sh.500,000/= sijui inakuwaje, naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Umepapata Mheshimiwa Waziri? Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu anachokizungumzia cha *Education, Materials, Supplies and Services,* kimepangiwa fedha hizo ambazo kweli ni kidogo lakini ni kutokana na ufinyu ya bajeti yenyewe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haroub.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimwia Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nimesimama katika *Suvote 1003, item* 220900 – *Training Foreign.* Tumeona hapa katika kifungu hicho zimetengwa Sh.4,143,000/= kwa ajili ya mafunzo nje ya nchi na hapa zinapigwa kelele kwamba wafanyakazi wa ofisi hii wawe na uwezo ili tuweze kupata *economic diplomacy.* Sasa fedha hizi Sh.4,000,000/= zinakwenda kuwasomesha kozi gani huko nje ya nchi na ni nchi gani ambayo watasoma watu kwa Sh.4,000,000/= waweze kupata ujuzi na utaalam wa kuweza kusaidia Wizara hii na kuleta manufaa katika mahusiano ya Kibalozi yenye tija za kiuchumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NAUSHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kiwango anachokisema hakitoshi kwa ajili ya

mafunzo nje ya nchi lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nafasi nyingi ambazo tumekuwa tukipeleka Maafisa wetu ni zile ambazo tumepata nafasi maalum za mafunzo bila ya gharama zozote.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 – *Policy and Planning* …………Tshs.2,017,703,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rukia.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko katika *subvote* hiyo 1004, kasma 221400 – *Hospitality Supplies and Services.* Mwaka 2012/1013 kulikuwa hakuna matumizi yoyote, mwaka 2013/2014 kuna Sh.1,800,000/= lakini mwaka huu kuna Sh.234,675,000/=. Ilikuwaje mbona imepanda gafla, matumizi haya yametokea wapi tena wakati miaka iliyopita hayakuwepo?

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya hapa ni kwamba kasma hii siku za nyuma ilikuwa haina pesa kabisa, kwa hiyo, kulikuwa na malimbikizo ya madeni na malalamiko kutoka kwenye Balozi karibu zote. Ndiyo maana katika *Policy Planning* wakaona sasa waombe pesa kwa sababu tulikuwa na malimbikizo ya madeni na *Treasury* ikakubali kwamba tuombe kiasi hiki iili kulipa madeni ya nyuma kama anavyosema dada yangu kwenye hivi hazikuwepo pesa halafu baadaye zinazobakia zitumike katika *financial year* hii. Kwa hiyo, ni malimbikizo ya madeni ya nyuma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kasma 229900 - *Other Operating Expenses* ambayo mwaka jana haikutengewa pesa, mwaka huu imetengewa Sh.111,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba fedha hizi ni kwa ajili ya kumlipa Mtaalam Mwelekezi wa kufanya mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje pamoja na Mpango Mkakati wa Wizara. Hata hivyo, napenda kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kwa sababu kwenye hotuba yake na hata kwenye randama, inaonesha Wizara imeshindwa kwa mwaka wa fedha uliopita kufanya mkutano na Mabalozi wote, kwa ajili ya kuwapa mikakati na mwelekeo wa pamoja kwa sababu ya uhaba wa pesa. Mwaka huu zimetengwa Sh.200,000,000/= kwa ajili ya kazi hiyo na Wizara inasema kwamba hizo pesa

hazitoshi lakini kumetengwa hii pesa hapa ya Mshauri Mwekelezi kwa ajili ya kutengeneza au kufanya mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje pamoja na Mkakati wa Wizara na mara zote Wizara imekuwa ikisema inao wataalam wengi wa ndani wa kufanya kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nipate ufafanuzi kutoka kwa Mheshimwia Waziri, ni kwa nini wameona haja ya kutenga kiwango kikubwa hicho cha pesa kwa ajili ya Mshauri Mwelekezi wakati ambapo kwenye kazi muhimu kama hiyo ya kufanya mkutano na Mabalozi wote kuna tatizo kubwa la pesa. Kwa hiyo, napenda kushauri tu kwenye ufafanuzi huo kama atakubali kufanya mabadiliko ikiwemo kwenye ile kasma ya juu ile ya fedha za nje na yenyewe vilevile imeongezeka sana ili kupata pesa za kuufanya huu mkutano muhimu sana na Mabalozi wote katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tumetenga fedha hizo kwa ajili ya ku-*review* Sera yetu ya Mambo ya Nchi za Nje lakini siyo kama ilivyoelezwa kwamba fedha hizi ni kwa ajili ya Mtaalam Mwelekezi tu. *Review* ya Sera hiyo inajumuisha pia mikutano na vikao mbalimbali ambavyo vitajumuisha sekta nyingi ukiachilia Wizara yetu. Kwa hiyo, ndiyo maana tumetenga fedha hizo. Pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kikao cha Mabalozi mwaka huu kitafanyika na asiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna jambo ambalo amelieleza kimakosa kwamba kifungu hiki ni pamoja na kulipia kumbi za mikutano kwa ajili ya mapitio ya Sera. Mheshimiwa Naibu Waziri akitazama kwenye kasma 220700 – *Rental Expenses,* kwa mujibu wa randama ya Wizara gharama hizi ni za kukodi kumbi za mikutano na magari kwa ajili ya mapitio ya Sera ikiwa ni pamoja na Mpango Mkakati. Kwa hiyo, naomba kusisitiza kwamba hii Sh.111,000,000/= iliyotengwa hapa ni kwa ajili ya kumlipa Mtaalam Mwelekezi. Kwa hiyo, sioni sababu kama Wizara inasema ina wataalam na kadhalika kutumia kiwango kikubwa namna hii wakati ambapo kwenye vifungu vingine kuna matatizo makuwba. Kwa hiyo, bado napenda kuishauri Wizara kama wanaweza kupata Mtaalam Mwelekezi kwa gharama ya chini zaidi, hizo pesa zikaelekezwa kwenye maeneo ambayo Wizara yenyewe inakiri kwamba kuna matatizo makubwa ya pesa.

**MWENYEKITI:** Ni ushauri tu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE YA USHIRIIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachukua ushauri huo lakini pia napenda nimhakikishie tena Ndugu yangu Mheshimiwa Mnyika kwamba katika kipindi kilichopita, tulishatenga Sh.200,000,000/= kwa ajili ya mkutano wa Mabalozi na safari hii tumeomba tena Sh.200,000,000/= kwa ajili ya mkutano huo basi tukiweza ku-*serve* kwenye *consultancy fees* hizi, tukaongezea pale tutakualika na kikao chenyewe cha Mabalozi. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mangungu.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia matumizi ya Kanuni za Uendeshaji bora, kifungu hicho kimeshahojiwa, ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na muda wetu sasa ni wakati wa *guillotine*.

Kif. 1005 – *International Cooperation* .....Tshs. 2,314,466,000/=
Kif. 1006 – *Europe and America* .................Tshs.665,918,000/=
Kif. 1007 – *Asia and Australia* ...............Tshs. 583,984,000/=
Kif. 1008 – *Africa* ................................Tshs. 4,882,235,000/=
Kif. 1009 – *Regional Cooperation* ...........Tshs.5,448,506,000/=
Kif. 1010 – *Protocol* ...................................Tshs.50,435,350,000/=
Kif. 1011 – *Legal Services* ........................Tshs. 1.932,271,000/=
Kif. 1012 – *Government Communication Unit* ...............................................Tshs.455,760,000/=
Kif. 1013 – *Middle East Division* ..............Tshs. 639,692,000/=
Kif. 1014 – *Internal Audit Unit* ...................Tshs.307,362,000/=
Kif. 1015 – *Procurement Unit* .....................Tshs.721,458,000/=
Kif. 1016 – *Information and Communication Technology*....... Tshs.560,312,000/=
Kif. 1017 – *Diaspora Engagement and Opportunity* ....... ...............Tshs.320,427,000/=
Kif. 2001 – *Embassy of Tanzania – Addis Ababa* ............................Tshs. 2,058,322,000/=
Kif. 2002 – *Embassy of Tanzania - Berlin* …Tshs. 3,959,449,000/=

Kif. 2003 – *Embassy of Tanzania – Cairo* …Tshs.1,436,028,000/=
Kif. 2004 – *Embassy of Tanzania– Kinshasa*......................................Tshs.1,289,286,000/=
Kif. 2005 – *High Commission of Tanzania – Abuja* …………….................. Tshs.1,633,211,000/=
Kif. 2006 – *High Commission of Tanzania – London* …………….................. Tshs.3,762,094,000/=
Kif. 2007 – *High Commission of Tanzania – Lusaka* …………..... Tshs.1,241,082,000/=
Kif. 2008 – *High Commission of Tanzania – Maputto* ………..... Tshs.1,530,037,000/=
Kif. 2009 – *Embassy of Tanzania – Moscow* .....................................Tshs.2,530,735,000/=
Kif. 2010 – *Embassy of Tanzania – New Delhi* ………………… ...... Tshs.1,940,774,000/=
Kif. 2011 – *Permanent Mission of the UN-New York* ……...............Tshs.3,882,610,000/=
Kif. 2012 – *High Commission of Tanzania – Ottawa* …………... Tshs.1,904,933,000/=
Kif. 2013 – *Embassy of Tanzania – Paris* ………… .......Tshs. 3,225,186,000/=
Kif. 2014 – *Embassy of Tanzania – Beijing* …………….................. Tshs.2,758,681,000/=
Kif. 2015 – *Embassy of Tanzania – Rome* ……………………..........Tshs.3,324,336,000/=
Kif. 2016 – *Embassy of Tanzania – Stockholm* ………………...... Tshs.2,418,267,000/=
Kif. 2017 – *Embassy of Tanzania – Tokyo* …………….................. Tshs.2,962,497,000/=
Kif. 2018 – *Embassy of Tanzania – Washington* ………………...... Tshs.3,400,635,000/=
Kif. 2019 – *Embassy of Tanzania - Brussels* ……………………..........Tshs.2,780,966,000/=
Kif. 2020 – *Permanent Mission to the UN – Geneva* ……… ........ Tshs.3,333,553,000/=
Kif. 2021 – *High Commission of Tanzania – Kampala* ……….................. Tshs.1,311,130,000/=
Kif. 2022 – *High Commission of Tanzania – Harare*…………..... Tshs.1,668,641,000/=
Kif. 2023 - *High Commission of Tanzania – Nairobi* ………… ........................Tshs.3,506,346,000/=
Kif. 2024 – *Embassy of Tanzania – Riyadh* …………….................. Tshs.1,739,847,000/=

Kif. 2025 – *High Commission of Tanzania*
– *Pretoria* ……………..................Tshs. 2,478,312,000/=
Kif. 2026 – *Embassy of Tanzania*
- *Kigali* …………………….............Tshs.1,428,300,000/=
Kif. 2027 – *Embassy of Tanzania –*
*Abu-Dhabi* ………………........Tshs. 2, 548,291,000/=
Kif. 2028 – *Embassy of Tanzania –*
*Bujumbura* …………………..... Tshs.1,319,780,000/=
Kif. 2029 – *Embassy of Tanzania – Muscat*
.....................................................Tshs.2,132,770,000/=
Kif. 2030 – *High Commission of Tanzania*
– *Lilongwe* ……….........................Tshs.1,085,312,000/=
Kif. 2031 – *Embassy of Tanzania–Brasilia* ...Tshs.2,415,119,000/=
Kif. 2032 - *High Commission of Tanzania*
– *Kuala Lumpa* .................. Tshs.2,077,525,000/=
Kif. 2033 – *Embassy of Tanzania*
– *The Hague* …………........ Tshs.1,719,887,000/=
Kif. 2034 – *Embassy of Tanzania*
– *Moroni* ……………….......... Tshs.1,474,582,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa**

Kif. 1004 – *Policy and Planning* …………Tshs.30,000,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka

wa Fedha wa 2014/2015 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Makadirio haya sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikano wa Kimataifa kwa mwaka wa Fedha 2014/2015 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba tukushukuru sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wataalam wote, Waheshimiwa Mabalozi wote na watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kazi nzuri ambayo mnafanya. Tunajua fedha tulizowapa hazitoshi lakini mjitahidi kuzitumia. Matumaini yetu ni kwamba tukikutana mwakani kutakuwa na tofauti kubwa katika maboresho ya utendaji kazi. Tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa bajeti hii ya mwaka 2014/2015. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na hatua inayofuata, naomba niwatambue wageni walioko Bungeni jioni hii, ni wageni 62 wa Mheshimiwa Anna Tibaijuka, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi na Maafisa kutoka Wizarani, wakiongozwa na Alphayo Japani Kidata, Katibu Mkuu wa Wizara na Ndugu Dkt. Selassie D. Mayunga, Naibu Katibu Mkuu. Ahsanteni sana na karibuni sana Bungeni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Anna Tibaijuka, ni viongozi watano kutoka Chama cha Wapangaji Tanzania, wakiongozwa na Ndugu Ndumeyi Mukama ambaye ni Katibu Mkuu, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wa Mheshimiwa Waziri Tibaijuka na Mheshimiwa Charles Mwijage ni Madiwani 53 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Muleba wakiongozwa na Ndugu Muhayi Boshoko – Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Muleba na Ndugu Christopher Kilaja, kutoka CCM Muleba. Wale wageni wa kutoka Muleba, bado hawajafika. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ni wanafunzi saba kutoka vyuo vikuu mbalimbali, karibuni sana wanafunzi. *(Makofi)*

Wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa George Simbachawene, Naibu Waziri, kutoka *Tourist Safaris Arusha,* wakiongozwa na Ndugu Ricky Thomson – Mkurugenzi, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Halima Mdee, ambao ni wajasiriamali kutoka Dodoma wakiongozwa na Ndugu Musa Kajanja na Bi. Getrude Ndibalema. Karibuni sana popote pale mlipo. *(Makofi)*

Sasa moja kwa moja naomba nimwite Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, Waziri Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Tufanye mwisho kabisa Mchungaji.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** *Please* nakuomba.

**NAIBU SPIKA:** Baada ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri nitakupa nafasi, Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 - Wizara ya Nyumba, Ardhi na Maendeleo ya Makazi kama ilivyosomwa Bungeni

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, naomba kutoka hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya mwaka wa fedha 2013/2014 na malengo ya Wizara katika bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia Waheshimiwa Wabunge kuwa na afya njema na hivyo kuweza kushiriki Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia nampongeza Dkt. Asha Rose Migiro, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge lako na Waziri wa Katiba na Sheria. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Ridhwani Kikwete na Mheshimiwa Godfrey Mgimwa kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu na kuimarisha safu ya Wabunge vijana wa CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitangulize dua zangu kwa Mwenyezi Mungu kuwa azipokee na kuzilaza mahali pema peponi roho za Marehemu Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mbunge wa Jimbo la Kalenga na Mheshimiwa Said Bwanamdogo aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Chalinze. Vilevile kwa namna ya pekee, natoa pole kwa Watanzania wenzangu walioathirika na majanga mbalimbali likiwemo la mafuriko yaliyotokea sehemu mbalimbali nchini kati ya mwezi Machi na Aprili 2014.

Mhesbhimiwa Naibu Spika, sina budi kuwalilia na kuwakumbuka wananchi kadhaa wa Wilaya ya Muleba, Kata ya Mazinga, Nyakabango, Kimwani la Lulanda, waliouliwa na mamba na viboko kutoka Hifadhi ya Taifa ya Rubondo. Maisha yao hayakupotea bure, nimetoa taarifa kuepusha mashambuzi mengine.

Aidha, kuna wananchi ambao wamepoteza maisha yao katika migogoro ya ardhi sehemu mbalimbali nchini. Nichukue nafasi hii kuwapa pole wafiwa. Njia peke ya kuwaenzi ndugu zetu hao ni kumaliza migogoro hii tukawa Taifa na jamii inayomaliza tofauti kwa majadiliano *(dialogue and not confrontation)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mohammed Ghalib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa uongozi wao mahiri. Nawashukuru kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano wanaonipa ulioniwezesha kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa ya kuongoza sekta hii mtambuka na muhimu katika maendeleo ya Taifa letu. Nawapongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Ally Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, pia Mheshimiwa Maalum Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mheshimiwa Balozi Ally Idd Seif, Makamu wa Pili wa Rais,

kwa mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar na za miaka 50 ya Muungano zilionyesha jinsi gani Taifa hili linasonga mbele kwa amani, mshikamano na upendo. Tanzania imekuwa kisiwa cha amani si kwa kubahatisha bali kwa uongozi imara chini ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Spika kwa kuongoza shughuli za Bunge kwa ufanisi, Mwenyezi Mungu aendelee kumuongoza na kumpa nguvu, afya na hekima za kumudu zaidi majukumu yake. Pia nakupongeza wewe Mheshimiwa Naibu Spika sasa hivi una kofia mbili, Mbunge wa Kongwa kwa kazi nzuri unayofanya na utendaji wako mahiri kuongoza Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini kwa kunipa ushirikiano wa karibu katika kutimiza majukumu yangu nikiwa Mbunge wao. Pamoja na kuwa na kazi nyingi za kitaifa, wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini wamekuwa wakinipa ushirikiano mzuri na kujitahidi kukutana nami napopata nafasi Jimboni kwa kuhudhuria vikao na mikutano mbalimbali tunayopata nafasi kufanya kwa pamoja. Kama Waziri tena wa Ardhi, muda wa kuwa Jimboni ni mdogo, pamoja na hayo wananchi wa Muleba wamekuwa wakijitokeza kwa wingi katika mikutano ya Kata ninapofika ili tutathmini maendeleo, kujipanga vizuri na kula na kunywa pamoja. Muleba tunasema 'Ibitaina Mayoti Byera" yaani kazi bila pongezi haiendi. Nawashukuru sana na kwa leo Mheshimiwa Naibu Spika umeshuhudia mwenyewe Madiwani wamekuja kushuhudia hapa kuniunga mkono, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawashukuru ndugu, jamaa na marafiki wanaonisaidia na kunipa ushirikiano wa karibu katika kutimiza majukumu yangu. Nawashukuru wananchi na kuwahakikishia popote pale walipo iwe ni Nshamba, Kimwani au Muleba kwamba tutayalinda mafanikio tuliyofikia na kuongeza kasi zaidi za kufikia malengo ya kulinda amani, utulivu na kufikia maisha bora. Namwomba Mwenyezi Mungu amwezeshe kila mwananchi kulitambua hili na kuchangia katika nafasi yake kwa kadri ya uwezo wake kufikia maisha bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, natuma salamu kwa Mama yangu Mzazi, Mauleria Kajumulo hapo Muleba, sala zake za kila siku zinaendelea kuniimarisha. Naomba alijue hilo na leo naamini mambo yangu yatakwenda vizuri hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi ambao wamenisaidia katika kutekeleza majukumu yangu magumu na hasa katika utatuzi wa migogoro ya ardhi sehemu mbalimbali nchini. Hii imenipa nguvu mpya katika kutekeleza ilani ya CCM. Aidha, sina budi kutambua mchango wa viongozi wa dini na vyama vya hiari ambao nimeshirikiana nao katika kazi zangu za kutatua migogoro na changamoto nyingi za sekta ya ardhi ambazo zinahitaji ushiriki wao, busara zao na kutambua na kutofautisha sheria na haki na uhusiano wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, kwa ushirikiano mkubwa na ushauri wao ambao uliiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Natoa shukrani za pekee kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kwa ushirikiano na umoja tuliojenga katika kutekeleza majukumu yetu tena katika muda mfupi. Namshukuru pia Katibu Mkuu, Bwana Alfayo Japani Kidata, Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Selassie David Mayunga, watendaji katika Idara, Vitengo, Shirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushauri na mshikamano wao katika kupanga na kutekeleza mipango ya Wizara yetu. Zipo changamoto nyingi zinazoikabili sekta yetu, lakini kwa mshikamano na umoja wao, naamini tumeweza kuendelea kukabiliana nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zinazoikabili sekta ya ardhi. Hizi kwa ufupi tu niseme zipo katika mafungo manne.

(i) Uelewa usiotosheleza wa wananchi kuhusu sekta yenyewe hasa sheria zake, taratibu na miongozo iliyopo, haki na wajibu wao. Ni sekta kubwa na mtambuka inatakiwa mtu ajue amesimama wapi kisheria.

(ii) Nafasi ya vyombo mbalimbali vya usimamizi na utendaji wake.

(iii) Vitendea kazi vilivyopo na vinavyohitajika ili kukidhi mahitaji ya sekta nyeti ya ardhi ambayo ni kiungo muhimu katika maendeleo.

(iv) Mazingira ya utendaji yaliyopo nje ya uwezo wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeongeza utoaji wa elimu kwa umma kuhusu Sheria za Ardhi, Kanuni na Taratibu pamoja na kuandaa miongozo mbalimbali. Kupunguza kwa kiasi kikubwa ukosefu wa vitendea kazi katika sehemu za kazi kwa mfano ununuzi wa mtambo mpya wa uchapaji wa ramani na nyaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongea mahusiano na wadau wake na kuboresha mazingira ya utendaji yaliyopo nje ya uwezo wa Wizara, Wizara iliweza kuwashawishi wahisani wa maendeleo ambao tayari wameanza kuipatia Wizara rasilimali fedha za kutekeleza Mpango Mkakati wa utekelezaji wa Sheria za Ardhi. Pia Wizara ipo katika hatua za kurekebisha muundo wake ili watumishi wa sekta ya ardhi waliopo Halmashauri wawajibike moja kwa moja Wizarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nifanye mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014 na malengo ya mwaka 2014/2015. Kwanza, nianze na ukusanyaji, Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya shilingi bilioni 100 kutokana na vyanzo mbalimbali, hadi kufikia Aprili, 2014 tulikuwa tumekusanya shilingi bilioni 37 na sasa hivi bado makusanyo yanaendelea. Pamoja na kwamba bado tupo chini ya kiwango chetu lakini kiutendaji tumeweza kuongeza tija kutoka shilingi bilioni 14.27 za mwaka 2012/2013. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 baada ya kurekebisha uhalisia wa vyanzo vya walipa kodi tofauti na walipa tozo, Wizara imeweka lengo la kukusanya shilingi bilioni 61.32. Nitumie fursa hii kuwakumbusha wananchi kutimiza masharti ya umiliki wa ardhi ikiwa ni pamoja na kulipa kodi ya pango la ardhi, ada na tozo nyingine kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa matumizi, tuliidhinishiwa shilingi bilioni 108.3 hadi Aprili, 2014 jumla ya fedha zilizopatikana ni shilingi bilioni 47.94 sawa na 44.25% ya fedha zilizoidhinishwa. Jumla ya shilingi shilingi bilioni 38.8 sawa na 81% ya kiasi kilichotolewa zilikuwa zimetumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala wa ardhi. Usimamizi wa ardhi nchini unahusisha mamlaka kuu tatu ambazo ni Halmashauri za Vijiji, Halmashauri za Wilaya na Miji na Wizara chini ya Ofisi ya Kamishna wa Ardhi. Majukumu na mamlaka za usimamizi yameainishwa vema katika Sheria za Ardhi, lengo la sheria ni kuhakikisha kuwa wananchi wanashirikishwa ipasavyo katika suala zima la usimamizi wa rasilimali ardhi kuanzia ngazi ya Kijiji hadi Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ofisi za Ardhi za Kanda. Kwa sababu muda si rafiki na kwa sababu sekta yangu ni mtambuka na ina vipengele vingi, hapa nitaanza sasa kusoma tu kwa ufupi ili kusudi wale ambao tunafuatana twende kwa vichwa vya habari. Kwa hiyo, tuna ofisi saba za Ardhi za Kanda, ofisi hizo zipo katika kanda saba, zilizoka sita sasa zimekuwa saba kwa sababu Kanda ya Dar es Salaam imeundwa rasmi na imetenganishwa na Mkoa wa Pwani na Morogoro ambao unaitwa Kanda ya Mashariki. Kwa hiyo, huduma zimesogezwa karibu na wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale wanaonifuata sasa nimekwenda mpaka Ibara ya 18. Mkakati wa kupima kila kipande cha ardhi. Wizara imeweka mkakati wa kuhakikisha kuwa kila kipande cha ardhi nchini kinapangwa, kinapimwa, kinamilikishwa na kinasajiliwa kisheria. Mkakati huu ambao umeanza kutekelezwa katika Wilaya ya Mvomero katika Mkoa wa Morogoro utasaidia kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilipata nafasi ya kushiriki Turiani ambapo niliweza kutoa hati miliki za kimila kwa wale ambao wamepimiwa. Ndiyo njia pekee katika kujaribu kuondokana na migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, utekelezaji utaendelea katika Wilaya za Kilosa na Kilombero, Mkoa wa Morogoro. Natoa rai kwa wananchi na Halmashauri zote ambazo maeneo yao yatahusika katika kufanikisha utekelezaji wa mkakati huu kutoa ushirikiano wa dhati mara zitakapofikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Sheria ya Ardhi. Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 inatoa fursa ya kuhakikisha kuwa ardhi yote nchini inamilikiwa kisheria. Hadi Aprili, 2014, vijiji 20 vimewezeshwa kuandaa mipango shirikishi ya matumizi ya ardhi ya kijiji. Vyeti vya Ardhi vya Kijiji 972 vimetolewa kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali. Hatimiliki za Kimila 24,945 zimetolewa na hatimiliki 24,651 pia ziliendelea kupatikana. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara yangu itaendelea na kazi ya uhakiki na upimaji wa vipande vya ardhi Wilayani Mvomero na inatarajia kupima na kuandaa hatimiliki za kimila 70,000 na hatimiliki 40,000. Halmashauri zote nchini zinaombwa kuhakikisha kuwa zinapanga, zinapima na zinamilikisha viwanja na kuandaa hati ili wananchi waweze kuwa na miliki salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina jukumu la kushughulikia uteuzi wa Wajumbe wa Kamati za Ugawaji Ardhi katika ngazi ya Taifa, Miji na Wilaya. Kamati hizi ni vyombo muhimu katika kushughulikia ugawaji wa ardhi nchini. Naomba nitoe rai na nihimize Halmashauri ambazo hazina Kamati za Ugawaji Ardhi za Wilaya na Miji kuwasilisha mapendekezo ya majina ya Wajumbe wa Kamati hizo Wizarani ili uteuzi uweze kufanyika. Naomba katika kufanya hivyo walete watu ambao wana mahusiano na sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara iliahidi kushughulikia maombi ya uhamisho wa miliki 1800. Hadi Aprili, 2014, Wizara imeshughulikia maombi ya uhamisho wa miliki 3,079. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara itashughulikia maombi ya uhamisho wa miliki 3,500. Napenda kuwashauri wananchi wote wanaonunua miliki za ardhi kuhakikisha wanafanya uhamisho wa miliki na kuzisajili. Nifafanue tu kwamba usiposajili miliki yule aliyekuuzia ndiye anabaki mmiliki kisheria wa hiyo nyumba au ardhi.

Hili nalo lieleweka kwa sababu inaleta migogoro hasa katika usimamizi wa mirathi. Kama umenunua mali na haijahamishiwa kwako kimsingi mbele ya sheria ni sawa na huna chochote inabaki mali ya yule aliyekuuzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunashughulika na kuboresha kumbukumbu za ardhi na teknolojia ya habari na mawasiliano, kazi hii tunaendelea nayo na Waheshimiwa Wajumbe wanaweza kuiona mpaka Ibara ya 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kazi zetu nyingine pia tuna uthamini wa mali ikiwemo ardhi, nyumba na mali zote zisizohamishika. Kazi hii imeendelea na imeainisha vizuri kuanzia Ibara ya 25,26, 27 na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba Wathamini wa Halmashauri zote nchini wamepatiwa mafunzo na miongozo ya utaratibu wa kufanya uchambuzi wa takwimu za bei ya soko na kuweka viwango vya thamani ya ardhi na majengo. Mfumo endelevu wa uhuishaji viwango vya thamani kadri ya mabadiliko ya bei ya soko vinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara imepanga kuimarisha mifumo ya kielektroniki ya uwekezaji na uhuishaji viwango vya thamani ya ardhi, majengo na mazao. Nawaagiza Waatalam wa Uthamini nchini kushiriki kikamilifu kuhuisha viwango vya thamani ili viendane na mabadiliko katika soko la mali kwenye maeneo yao. Nahimiza wananchi wawe macho kwamba uthamini unakwenda na viwango ambavyo vinakuwa vimepitishwa na Wizara baada ya kuangalia bei ya soko kama sheria inavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyohivyo, nawaagiza wataalam na wadau wa uthamini kuzingatia yaliyomo kwenye miongozo tofauti ambayo tunatoa kuhusu uthamini kwani ni kazi ambayo inatakiwa ifanyike kwa maadili. Ninawataka Wathamini kutambua kwamba baadhi yao wamekuwa chanzo cha migogoro kwa kujihusisha na vitendo visivyofaa kama kudai rushwa na hongo badala ya kuthamini mali za wananchi kwa ukweli na haki. Aidha, kumekuwa na migogoro mingi baada ya shughuli za uthamini ikiwa ni pamoja na uthamini hewa. Wizara tayari imeweka mikakati ya kuziba mianya hiyo kwa kutumia upimaji wa kielektroniki wa kila kipande cha ardhi na pia kutaka malipo ya uthamini yafanyike kupitia benki teule na hivyo kuwabana wale wanaotumia ujanja wa malipo kwa wathaminiwa hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba wananchi watupe ushirikiano katika utekelezaji wa mfumo huu ambapo tunawataka wafungue akaunti za

benki tunapowalipa. Namna hii ndiyo tutaweza kutekeleza kazi zetu kwa ufanisi zaidi na wenyewe kupata haki yao bila mtu yeyote kuwaibia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, hii ni kazi ambayo tunaendelea nayo. Wizara yangu itaendelea kushughulikia utatuzi wa migogoro ya ardhi na nyumba kupitia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Tulikuwa tumeahidi kuamua mashauri 11,000. Kuanzia Julai 2013 yalikuwepo mashauri 18,328 na hadi kufikia Aprili, 2014 mashauri mengine 11,548 yalifunguliwa. Katika kipindi hicho jumla ya mashauri 11,432 yaliamuliwa na hivyo mashauri 18,448 yaliyobaki na yaliyofunguliwa yataendelea kushughulikiwa katika mwaka mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, niliahidi kuendelea kufuatilia utendaji kazi wa Wenyeviti ili kuhakikisha kuwa wanazingatia maadili ya kazi zao. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imeandaa Mwongozo wa Maadili ya Kazi wa Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya *(Code of Conduct)* itakayotumika kufuatilia utendaji wao wa kazi. Wananchi nawashukuru kwani wamekuwa tayari kutoa taarifa pale ambapo Wenyeviti wengine wamekuwa hawana maadili na tumewashughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 32 na kuendelea nazungumzia huduma za upimaji na ramani, huwa tunatayarisha ramani, tunapima maeneo, ni kazi ambayo nimeifafanua katika hotuba yangu kwa kirefu kwenye *Hansard* mtaipata mpaka Ibara ya 34. Kwa muda tulionao sasa hivi ninasonga mbele kuzungumzia mipaka ya kimataifa katika Ibara ya 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ina jukumu la kuweka na kutunza alama za mipaka kati ya Tanzania na nchi za jirani. Hadi Aprili, 2014, uwekaji wa alama za mipaka wa eneo la kilomita 51 za nchi kavu kati ya Tanzania na Msumbiji umekamilika. Mpaka kati ya Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa mazungumzo yanaendelea na tena yanaendelea kwa utulivu na amani. Vilevile, uwekaji wa alama 78 za mpaka kati ya Tanzania na Zambia umefanyika katika eneo la Tunduma na Konde lenye urefu wa Kilomita 46. Uwekaji wa alama 70 za mpaka kati ya Tanzania na Kenya umefanyika katika eneo la Sirari lenye urefu wa kilomita 14.8. Uwekaji wa alama za mpaka kati ya Tanzania na Burundi umeanza katika Wilaya ya Ngara hadi Aprili, 2014 alama 149 zimesimikwa na kazi inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwa wale wanaonifuata naomba niende Ibara ya 39. Ili kurahisisha upimaji wa ardhi na kupunguza

gharama za upimaji kwa wananchi, hadi Aprili, 2014, Wizara imeweza kusimika na kupima alama za misingi za upimaji *(control points)* 104 katika miji saba ambayo imetajwa katika hotuba, mtaiona. Utaona kwamba shughuli hizi ni nyingi, ni tofauti na ziko katika Idara mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji wa ardhi chini ya maji, bado niko kwenye Idara yetu ya Upimaji. Jukumu mojawapo la Wizara ni upimaji wa ardhi chini ya maji na kutayarisha ramani zinazoonesha umbile la ardhi chini ya maji hususan milima, mabonde, miinuko na kina cha maji. Wizara yangu imenunua kifaa kiitwacho *echo sounder* ili kuwezesha kazi ya upimaji vina vifupi iweze kufanyika. Kazi hii ni muhimu sana hasa kwa usalama wa vyombo vyetu majini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Kupima Viwanja. Wizara inaendelea kusimamia Mfuko wa Mzunguko wa Kupima Viwanja (*Plot Development Revolving Fund – PDRF)* ambao huzipatia mikopo Halmashauri mbalimbali nchini kwa ajili ya kulipa fidia, kupima viwanja na kuvimilikisha kwa wananchi na taasisi mbalimbali. Hadi Aprili, 2014, madeni kwa Halmashuri mbalimbali yamepungua kutoka shilingi milioni 633.6 hadi kufikia shilingi milioni 325.5. Hadi Aprili, 2014, Halmashauri nne (4) zilizokopa fedha kutoka kwenye mradi huo zilirejesha sehemu ya mikopo yao na kufanya deni hilo kupungua kutoka shilingi bilioni 1.87 hadi kufikia shilingi milioni 780.39. Wizara itaendelea kufuatilia Halmashauri ambazo zinadaiwa ili ziweze kurejesha fedha hizo. Nahimiza Halmashauri zinazodaiwa kulipa madeni haya ili fedha hizi zikopeshwe katika Halmashauri zingine kusudi ule mzunguko uwe na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mipango Miji na Vijiji. Katika Idara hii ya Mipango Miji na Vijiji, tumeendelea kufanya kazi mbalimbali. Katika kipindi cha muongo mmoja tumeshuhudia ongezeko la watu na kasi ya ukuaji wa miji na vijiji hapa nchini. Ongezeko hili linajidhihirisha katika takwimu za Sensa ya Taifa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012. Wakazi wa mijini waliongezeka kutoka milioni 7.9 sawa na asilimia 23.1 mwaka 2002 na hivi sasa wakazi wa mijini ni milioni 12.7 sawa na asilimia 29.1 mwaka 2012. Ongezeko hili limekuwa changamoto kubwa kwa Mamlaka za Upangaji Miji kushindwa kutoa huduma za kiuchumi na kijamii kwa kiwango stahiki na kufanya miji yetu kukua kiholela.

Mheshimiwa Naibu Spika, uandaaji na utekelezaji wa mipango ya jumla ya uendelezaji miji ni kitu muhimu sana na naomba nikizungumzie. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam ziliendelea kukamilisha maandalizi ya Mpango Kabambe wa Jiji la Dar es Salaam ambapo rasimu ya mwisho iliwasilishwa kwa wadau na Mtaalam Mwelekezi anaendelea kuiboresha kwa kutumia maoni na mapendekezo yaliyotolewa na wadau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba Jiji la Dar es Salaam lenyewe sasa hivi lina wakazi takribani milioni 4.55 na linakuwa kwa kasi ya asilimia 5.7 kila mwaka. Kwa hiyo, mambo yasipobadilika, Jiji la Dar es Salaam litakuwa na wakazi milioni 9 ifikapo mwaka 2025. Kwa hiyo, katika miaka 13 inayokuja Dar es Salaam itakuwa na watu milioni 9 mambo yakiendelea kama yalivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji Mdogo wa Bagamoyo imekamilisha maandalizi ya Rasimu ya awali ya Mpango Kabambe wa mji huo ambao nao unakuwa kwa kasi sana. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mafia ilikamilisha maandalizi ya Rasimu ya Mpango wa Muda wa Kati wa Matumizi ya Ardhi kwa mji wa Kilindoni. Rasimu za mipango hiyo ziliwasilishwa kwa wadau wa Halmashauri husika kwa ajili ya kuzitolea maoni. Wizara inaendelea kushirikiana na Halmashauri za Manispaa ya Sumbawanga na Mji wa Bariadi kuandaa Mipango Kabambe ya miji hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Manispaa ya Sumbawanga, Wilaya ya Mafia, Mji Mdogo wa Bagamoyo na Bariadi itakamilisha kuandaa mipango ya jumla ya miji hiyo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Arusha na Halmashauri za Arusha na Meru, itaanza maandalizi ya mipango kabambe ya Jiji hilo na viunga vyake kwa kutumia Mtaalam Mwelekezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Manispaa za Lindi na Mtwara zitaanza maandalizi ya Mipango Kabambe ya Miji hiyo. Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini ambazo hazina mipango ya jumla kutenga fedha za kuandaa mipango hiyo. Natoa wito pia kwa Halmashauri ambazo sikuzitaja ni ruksa kabisa kutualika kushirikiana nao kuendelea kuweka hiyo mipango kabambe.

Mheshimiwa Naibu Spika, uandaaji na utekelezaji wa mipango ya kina ya uendelezaji miji, kazi hii nayo tumeendelea kuitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirejea Ibara ya 49, inayohusu uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni. Naomba nitue hapo kidogo nizungumzie kazi hii muhimu ambayo tunaendelea nayo. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara yangu iliahidi kuendeleza Mji wa Kigamboni; kuingia mkataba na makampuni mawili ya kujenga nyumba, kufanya uthamini wa mali na kulipa fidia kwa wananchi ili kupisha utekelezaji wa mradi na kujenga uwezo wa Wakala wa Uendelezaji wa Mji Mpya Kigamboni ili iweze kutekeleza majukumu

yake ipasavyo. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu haikuweza kutekeleza kazi hizo kama ilivyoahidi kutokana na ukosefu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Wizara yangu imekamilisha uandaaji wa Rasimu ya Muundo wa Wakala wa Uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni na kuanzisha ofisi yake katika eneo la mradi. Kwa hiyo, Wanakigamboni sasa hivi hawana haja ya kupanda feri kuja Wizarani, mambo yote yanamalizika huko huko Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulitokea ucheleweshwaji katika kumteua Mtaalamu wa Fedha *(Transaction Adviser and Fund Raiser)* kwa sababu ya kukidhi matakwa ya Sheria ya Manunuzi. Naomba niseme kwamba, hapa nilikwama karibu miezi tisa nikisubiri tuweze kufuata utaratibu na hatimaye mwezi Machi, 2014 Mtaalam aliteuliwa na sasa ameanza kazi. Jambo hili linatarajiwa kuongeza kasi kubwa katika kupata fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Nifafanue tu kwamba, Mji Mpya wa Kigamboni Serikali inawezesha fedha za kuupanga lakini Mji Mpya utajengwa na sisi Watanzania wenyewe na wadau wengine na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara yangu itakamilisha *public hearing* (mkutano wa wadau) ili uweze kuidhinisha mpango, kuandaa mipango ya kina ya maeneo yaliyopo ndani ya Mpango Kabambe wa Mji Mpya wa Kigamboni, kuainisha kulipa fidia na kupima maeneo ya miundombinu na umma katika eneo la mradi na kusimamia utekelezaji wa mpango kabambe kupitia Wakala wa Uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni. Natoa rai tena kwa wananchi wa Kigamboni kuwa na imani na mradi huu. Nawashukuru kwa uvumilivu na ushirikiano wao na kutambua azma ya Serikali kujenga mji mpya wenye viwango (mji wa kisasa) na sisi tufananefanane na wenzetu, siyo kubakia tu kwenda Dubai na kushangaa. Jambo hili ni gumu na linachukua muda lakini hatua iliyofikiwa si haba kwa zoezi lenyewe kwa mtu anayeelewa kazi tunayoifanya. Niondoe wasiwasi kwa wale ambao wanadhani kwamba kazi hii imeshindikana kwa hiyo tuondokane nayo. Mradi huu umetajwa kwa jina katika Ibara ya 60(b)(iv) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 ambayo inasema na ninanukuu:-

"Kuanzisha Mji Mpya wa Kisasa wa Kigamboni *(Kigamboni New City)"*, mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii pekee ni ishara tosha kuonesha wajibu wa Serikali katika kutoa kipaumbele kutekeleza kazi hii. Kwa hiyo, mimi nasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kuanzisha mji ilianza kwa Serikali kuunda chombo cha *Kigamboni Development Agency - (KDA)* ambao ni Wakala wa kuendeleza Mji Mpya na kama nilivyosema *KDA* yuko kule anachapa kazi. Miaka 50 baada ya Uhuru, *KDA* ni Wakala wa pili kuundwa baada ya *CDA* kwa ajili ya kuendeleza mji. Kwa hiyo, kwa wale ambao wanafikiria kwamba hakuna maendeleo ambayo tumefanya, tumepiga hatua kwa sababu lazima nikiri kwamba kujenga mji ni mchakato na siyo tukio, hivyo inabidi twende hatua kwa hatua lakini tunasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawahimiza wananchi wa Kigamboni kuendelea kuwa wavumilivu na kutokubali kurubuniwa kwa kuuza maeneo yao kwa wajanja ambao baada ya viwango vya fidia kutajwa, wamejitokeza wakitaka kununua ardhi za wananchi kwa bei poa ili wao baadaye wafidiwe na *KDA*. Wananchi muwe macho na kwa wale wapiga porojo wanaosema mimi ni Wakala wa Ardhi kule Kigamboni, mimi ni Waziri wa Ardhi Tanzania, sina muda na wala sikuja hapa kupoteza muda wangu kuwa Wakala wa Viwanja kule Kigamboni. Kwa hiyo, watu wanaowaibia wananchi wakidai kwamba na fedha za Waziri zipo hao ni waongo msiwasikilize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, itambuliwe kuwa viwango vya fidia katika Awamu ya Kwanza ya Mradi ni shilingi 35,000 kwa mita moja ya mraba, hii ni sawa na shilingi 141,645,000 kwa ekari moja. Katika soko binafsi hakuna mtu anayetoa fedha hizo. Sasa wale wanaozunguka kuwadanganya wananchi, unajua Serikali haitalipa, Serikali italipa ila inafanya kazi hatua kwa hatua. Kwa hiyo, wananchi wameisha– *support* mradi kwa hiyo wavumilie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kigamboni watambue mamlaka ya upangaji mji wao ni *KDA* na ofisi zake ziko Kigamboni na wasikubali na kuyumbishwa na wanaotaka kupima maeneo ya wananchi kabla ya fidia stahiki kulipwa. Pia nifafanue kwamba, wananchi wa Kigamboni wataendelea kubaki Kigamboni katika makazi yatakayojengwa Kata ya Kibada –Uvumba kwenye *resettlement city*. Ndani ya Kigamboni kuna miji ndani ya miji. Tunaanza na *resettlement city* ambayo iko Kibada - Uvumba. Wananchi watawezeshwa kutumia sehemu isiyopungua asilimia kumi ya fidia yao kununua hisa za *KDA* hivyo kuendelea kufaidi matunda ya Mji Mpya wa Kigamboni kwa vizazi vingi vijavyo. Ndivyo miji mnayoina hii iliyopangwa vizuri inakwenda hivyo. Wanasema *cities look like the way they were financed.* kama huna *financing mechanism* ya mji, huwezi kuujenga na mambo yatakuwa holela holela tu hivyo hivyo hivyo. Kwa hiyo, pale tunajipanga na wananchi wa Kigamboni wanabaki kwenye ardhi yao kwa mfumo wa kisasa wa hisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika fani ya kazi yoyote, hakuna viwango bila weledi na nidhamu, kwa hiyo hali hii inataka pia uzalendo. Nafurahi

kuwatangazia kuwa Mheshimiwa Rais ameomba msaada wa wataalam kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Jopo la wataalam wa Mipango Miji kutoka China litawasili mwezi ujao ili kushirikiana na wataalam wetu katika upangaji wa Mji Mpya wa Kigamboni, pia miji ya Lindi na Mtwara, kwa sababu pale tunakwenda kwa viwango na viwango ndugu zangu vinahitaji nidhamu. Wizara ina imani kuwa utaratibu wa kupata fedha za kuendeleza mji mpya wa Kigamboni sasa utashika kasi baada ya kupata Mtaalam Mwelekezi ambaye ndiye ataweza kututafutia fedha. Kwa hiyo, haya matatizo ya mwanzoni haya, wazungu wanaita *teasing problems,* ninaamini yatapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 55 ninazungumzia urasimishaji wa makazi holela. Hii ni kazi ambayo Wizara yangu imeendelea kuifanya. Kama nilivyosema miji yetu inatakiwa ipimwe, ipangwe, tuondokane na makazi holela maana yake mwisho wa siku makazi holela hayatusaidii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 57 usimamizi na udhibiti wa uendelezaji vijiji. Wizara ilitoa elimu ya mwongozo wa kupanga makazi ya vijiji kwa wataalam na wadau katika Mikoa iliyopo Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Iringa, Njombe, Rukwa na Mbeya) ili kwenda sambamba na Programu ya *Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT)*. Vilevile, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo na Mvomero zilijengewa uwezo wa kuandaa Mipango ya Makazi ya Vijiji vinne (4) vya Fukayosi na Kidomole Wilayani Bagamoyo; Lukenge na Hembeti, Wilayani Mvomero.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe rai kwa Halmashauri za Wilaya zote nchini, hasa katika maeneo ambapo elimu hii imetolewa, wasimamie na kuwezesha upangaji wa makazi ya vijiji vyao, ili kuwezesha vijiji hivyo kuwa na makazi yaliyopangwa na kuwa na maeneo ya huduma za jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi ni kazi ambayo tunaitekeleza. Serikali ilipitisha Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi na madhumuni ya mpango huo ni kuweka utaratibu wa kuongoza matumizi ya rasilimali za ardhi yenye usawa kwa ajili ya kuboresha maisha ya jamii, maendeleo ya kiuchumi na kijamii na uendelevu wa rasilimali za kimazingira nchini na hivyo, kuchangia katika jitihada za Serikali katika utekelezaji wa MKUKUTA. Hivi sasa marekebisho ya mwisho pamoja na kuhuisha takwimu vipo katika hatua za mwisho ili uchapishwe na kusambazwa kwa wadau. Utekelezaji wa programu za kipaumbele (kilimo, mifugo, maji, makazi, mipango ya matumizi ya ardhi) utaanza katika mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja Ibara ya 62, nizungumzie mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya na Vijiji. Hadi Aprili, 2014 jumla ya vijiji 94 vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi katika Wilaya mbalimbali. Pia, kazi ya kutekeleza mradi wa *SAGCOT* imeanza kwa Mkandarasi kupitia Mpango wa Matumizi ya Ardhi katika ukanda wa Reli ya Uhuru. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itawezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya Vijiji 200 pamoja na kuendelea na uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na wilaya katika ukanda wa *SAGCOT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya nyumba, niseme kwamba, kwa sababu ya umuhimu na hali ya makazi yetu inayozidi kuwa changamoto, nitatumia muda kidogo kuzungumza sekta hii ya nyumba. Mkataba wa mkopo wa *Tanzania Housing Finance* umerejewa upya ili kuipata kampuni ya *Tanzania Mortgage Refinancing Company*. Hadi Aprili, 2014 jumla ya benki 19 zilikuwa zinatoa mikopo ya nyumba kwa kati ya miaka 15 hadi 20, tofauti na benki 10 zilizokuwa zinatoa mikopo ya nyumba kwa kipindi kisichozidi miaka 15. Kwa hiyo, utaona kwamba kazi zetu zilizo nyingi ni muhimu lakini matokeo yake hayaonekani moja kwa moja. Hata hivyo, katika hili la kuhimiza benki kutoa mikopo ya nyumba ni kazi ambayo tunakwenda nayo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara yangu itatoa elimu kwa umma kuhusu utaratibu wa mikopo ya nyumba, ikiwa ni pamoja na haki na wajibu wa mkopaji na mkopeshaji kwa mujibu wa sheria. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania kuweka utaratibu utakaowezesha mikopo ya nyumba kutolewa kwa masharti nafuu kuliko mikopo ya kibiashara. Wizara itashirikiana na vyombo vya fedha kuweka mazingira ya kuvutia uwekezaji katika sekta ya nyumba ikiwa ni pamoja na kuvutia waendelezaji milki binafsi ili wajenge nyumba za gharama nafuu za kuuza na kupangisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu iliendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha pamoja na Benki Kuu ya Tanzania kukamilisha uundwaji wa Mfuko wa Mikopo Midogomidogo ya Nyumba. Mfuko huo umeanza kwa mtaji wa Dola za Marekani milioni 3 ambazo ni sehemu ya mkopo uliotolewa na Benki ya Dunia kupitia mradi wa kuendeleza sekta ya nyumba hapa nchini *(Tanzania Housing Finance Project)*. Aidha, Serikali iliendeleza mazungumzo na Benki ya Dunia kwa lengo la kupata fedha zaidi kwa ajili ya mfuko huo. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itatoa elimu kwa umma kuhusu mfuko huo na kuwahamasisha kutumia huduma zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara iliahidi kuandaa Sheria ya Kusimamia Sekta ya Nyumba ikiwa ni pamoja na

kuweka masharti ya uendelezaji nyumba, kuelekeza haki na wajibu wa waendelezaji nyumba, wanunuzi, wamiliki na wapangaji wa nyumba. Kazi hiyo itaendelea katika mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilizielekeza Halmashauri zote kutenga ardhi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kwa watumishi wa umma. Aidha, *Watumishi Housing Company (WHC)* iliyoundwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Shirika la Nyumba la Taifa, itasimamia utekelezaji wa mpango huo. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara itaendelea kuwezesha utekelezaji wa mpango huo ikiwa ni pamoja na kuunda Mfuko wa Dhamana ya Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mengi sana katika sekta ya nyumba, lakini nitakwenda moja kwa moja sasa hivi katika kitovu chetu muhimu katika sekta hii ambacho ni Shirika la Nyumba la Taifa kuanzia Ibara ya 70. Wizara iliendelea kusimamia Shirika la Nyumba la Taifa *(National Housing Corporation)* katika utekelezaji wa malengo ya Mpango Mkakati wake wa kipindi cha mwaka 2010/2011 hadi 2014/2015 ikiwa ni pamoja na kuimarisha utendaji kazi. Shirika limeendelea kuboresha utendaji kazi wake kwa kuajiri wataalam wa fani mbalimbali wapatao 31 kwa ajili ya kuongeza ufanisi na tija. Ajira hizi zimepandisha uwiano wa wafanyakazi wenye taaluma na wasiokuwa na taaluma kufikia asilimia 51 kwa 49 dhidi ya lengo la asilimia 70 kwa 30 ifikapo Juni, 2015. Pia, watumishi wa ngazi zote walipatiwa mafunzo ya utambuzi na ulezi wa vipaji pamoja na ushirikiano kati ya sekta za umma na sekta binafsi *(public – private partnership)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iko kwenye mchakato wa kurekebisha Sheria Na. 2 ya Shirika la Nyumba la Taifa ya mwaka 1990 iliyoliunda upya Shirika hilo. Lengo la marekebisho haya ni kuliwezesha Shirika kufanya yafuatayo: Kupanua wigo wa shughuli za Shirika ili liweze kuwa mwendelezaji milki mkuu; kuliwezesha Shirika kuendesha shughuli zake katika mazingira shindani na kuoanisha Sheria ya Shirika na Sheria zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Hadi Aprili, 2014, Shirika lilifanikiwa kununua ardhi yenye ukubwa wa ekari 3,686 na viwanja 464. Kwa hiyo, Shirika lenyewe tayari lina *land bank* wakati sisi Serikalini lazima nikiri kuwa bado tunalizungumzia, Shirika la Nyumba lenyewe tayari lina *land bank* na linaendelea vizuri katika kazi hii. Shirika limeendelea na mchakato wa ununuzi wa ardhi yenye ukubwa wa ekari 2,627.5 iliyoko kwenye maeneo mbalimbali nchini. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Shirika litaendelea na ununuzi wa ardhi ambao kwa sasa umefikia hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa nyumba za makazi na majengo ya biashara. Hadi Aprili, 2014, Shirika liliendelea na utekelezaji wa miradi 26 ya ujenzi wa nyumba za makazi yenye jumla ya vyumba 1,947. Miradi hii, ililiwezesha Shirika kuifikia Mikoa 14 kwa kujenga nyumba za gharama nafuu 921 na nyumba za gharama ya kati na juu 978 katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Dodoma. Kati ya nyumba hizo, nyumba 697 zilikamilika ambapo 193 ni za gharama nafuu na 504 ni za gharama ya kati na juu. Shirika pia linaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi wa miradi 31 yenye jumla ya nyumba za gharama nafuu 1,717 na miradi 18 yenye nyumba 3,493 za gharama ya juu na kati zitakazojengwa katika Mikoa 17. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Shirika litaendelea kukamilisha miradi inayoendea; kuanza miradi mingine mipya ya nyumba za gharama ya juu, kati na nafuu na hivyo kuifikia Mikoa yote ya Tanzania Bara kwa kujenga nyumba zisizopungua 50 kwa kila Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Aprili, 2014, Shirika limefanikiwa kuuza nyumba 456 katika miradi yake na kupata kiasi cha shilingi bilioni 43.95 kati ya shilingi bilioni 67.05 zilizotarajiwa. Hadi Aprili, 2014, Shirika liliweza kukamilisha mradi wa jengo moja la ghorofa 10 lililojengwa kwenye Kiwanja Na. 1, Barabara za Ufukoni na Ali Hassan Mwinyi, Upanga - Dar es Salaam ambalo ni Makao Makuu mapya ya Shirika. Mheshimiwa Naibu Spika nakukaribisha wewe na Bunge lako Tukufu kutembelea Makao Makuu mapya ya *National Housing,* ni makao ya viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika lilianza ujenzi wa majengo manne (4) ya biashara ambayo ni jengo la ghorofa tano (5) lililoko Kiwanja Na. 2, Barabara ya *Old Dar es Salaam* Mkoani Morogoro; jengo la ghorofa moja (1) katika Mtaa wa Kitope, Manispaa ya Morogoro; jengo la ghorofa tano (5) lililoko Mtaa wa *Lupa Way*, Manispaa ya Mbeya; na jengo la ghorofa tatu (3) lililoko Mitaa ya Mkendo na Kusaga Mjini Musoma. Aidha, Shirika kwa kushirikiana na wabia wake liliweza kukamilisha miradi ya majengo 57 na miradi mingine 27 ya biashara ilikuwa katika hatua mbalimbali za matayarisho ya kuanza ujenzi. Vilevile, Shirika lilikamilisha miradi 16 ya ubia iliyotekelezwa kwa kushirikiana na sekta binafsi na kuendelea na ujenzi wa miradi mingine minne (4). Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Shirika litaendelea na utekelezaji wa jumla ya miradi ya majengo ya biashara 30 ikiwemo inayoendelea na ile ambayo kwa sasa iko katika hatua za maandalizi pamoja na kukamilisha miradi minne (4) ya ubia.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelelezaji wa vituo vya Miji Midogo *(Satelite Cities)*. Shirika limeendelea na matayarisho ya kuanza jukumu lake jipya la kuendeleza vituo vya Miji Midogo kama mwendelezaji miliki mkuu *(master developer)*. Wizara ililikabidhi rasmi Shirika eneo la Luguruni lenye ekari 156.53 na

eneo la Kawe lenye ekari 267.71 kwa ajili ya kuyaendeleza. Aidha, Shirika kwa niaba ya Serikali liliingia Mkataba wa Makubaliano *(Memorandum of Understanding)* na kampuni ya *Surbana International Consultants* ya Singapore kwa ajili ya kulipanga upya eneo la Luguruni. Pamoja na juhudi hizo, Shirika pia lilikamilisha matayarisho ya mipango ya kina *(detailed plans)* ya kuendeleza maeneo linayoyamiliki ikiwa ni pamoja na eneo la Burka/Matevesi – Arusha lenye ekari 579.2 na eneo la Usa River - Arusha lenye ekari 296 na pia kuendelea na matayarisho ya mipango hiyo kwa maeneo ya Uvumba, Kigamboni (ekari 202) na Kawe. Shirika litaanza uendelezaji wa eneo la Burka/Matevesi kwa kujenga miundombinu pamoja na nyumba za gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafutaji wa mitaji kwa ajili ya miradi na mikopo ya ununuzi wa nyumba. Kitu ambacho Shirika limekamilisha cha kujivunia ni kuingia mikataba ya mikopo ya kiasi cha shilingi bilioni 210 na kuweza kutumia kiasi cha shilingi bilioni 124. Hadi Aprili, 2014, wanunuzi wapatao 89 waliweza kupata mikopo ya nyumba yenye jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 12.2 na wengine wanaendelea na mchakato wa kupata mikopo hiyo. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara kupitia Shirika itaendelea na juhudi za kupata mikopo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi na majengo ya biashara pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi katika Ibara ya 80, ninazungumzia mapato ya Shirika. Hadi Aprili, 2014, mapato ya Shirika yalifikia shilingi bilioni 55.63 sawa na asilimia 98 ya lengo la kipindi cha Julai 2013 hadi Aprili, 2014, kati ya shilingi bilioni 68.2 ya lengo. Mapato hayo yaliliwezesha Shirika kuchangia mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 10.02. Kwa mwaka 2014/2015,, Shirika linategemea kuingiza kiasi cha shilingi bilioni 70.1 kutokana na kodi za pango la nyumba na hivyo kuendelea kuchangia mapato ya Serikali. Niseme tu Shirika hili linajiendesha lenyewe, Serikali ilitoa mtaji kwa namna ya nyumba lakini lenyewe sasa hivi unaona kwamba na lenyewe linachangia. Matengenezo ya nyumba na majengo na yenyewe yameendelea ndani ya Shirika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 82, sasa nizungumzie kidogo kazi zingine za Wizara yangu, kuna huduma na kisheria. Kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, huduma mbalimbali za kisheria zimeendelea kutolewa na Wizara. Huduma hizo zinajumuisha kutunga sheria mpya, kuhuisha sheria na kusimamia mashauri yanayohusu Wizara na migogoro mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 83, 84, 85 na 86, nazungumzia kazi zingine za Wizara. Ibara ya 85 ni mawasiliano Serikalini ambayo yameandikwa vizuri na ni sehemu ya rekodi yangu lakini muda siyo rafiki, naomba niende moja kwa moja mpaka Ibara ya 87.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara itakamilisha kuhuisha mkakati wa mawasiliano wa Wizara; kuratibu mawasiliano kati ya Wizara na wadau wake; kuandaa na kurusha vipindi vya televisheni na redio na kuboresha mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 88 ninazungumzia huduma za utawala wa rasilimali watu kazi ambayo tunaendelea nayo. Kwa mfano, kuhakikisha kuwa watendaji wetu wanakingwa dhidi ya UKIMWI na magonjwa mengine. Wizara yangu imekamilisha ujenzi wa kituo cha kuhudumia wateja *(customer service centre)*. Kituo hiki kitaanza kutoa huduma katika mwaka wa fedha 2014/2015. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara itaendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa kusimamia mifumo ya utendaji kazi, kuboresha mazingira ya ofisi na kutoa stahili kwa watumishi zinazoendana na masharti ya ajira zao. Jumla ya watumishi 166 walihudhuria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara 91, 92, inaendelea kuzungumzia kazi zetu, kuweka mazingira mazuri kwa watendaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna vyuo vya Ardhi, hivi navizungumzia katika Ibara ya 97, tuna Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro na vyenyewe vimeendelea kufanya kazi zake na vinaendelea kufanya kazi vizuri. Nitoe wito kwa Halmashauri kuajiri wataalam ambao wanatokana na vyuo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto maalum. Mimi kama Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, wengine wananiita Waziri wa Migogoro najua na hiyo ndiyo hali halisi. Utatuzi wa migogoro ni kazi ambayo inachukua muda wangu mwingi. Katika kazi zote tunazotekeleza, changamoto na kero kubwa inaendelea kuwa ni ongezeko la migogoro ya ardhi inayoibuka sehemu mbalimbali nchini. Nachukua nafasi hii kueleza Bunge hili Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba kimsingi hakuna migogoro ya ardhi bali ni "migogoro ya watumiaji wa ardhi". Ili kuondokana na migogoro hii, ni muhimu kwa watumiaji wa ardhi ambao ndiyo wako kwenye migogoro, ardhi yenyewe imetumia shwari wala haina ugomvi na mtu inasubiri siku ikifika inakupokea mambo yanakwisha lakini sasa sisi juu ya ardhi ni sokomoko ndani ya nyumba. Kwa hiyo, nataka mtambue ukweli huu kwamba sisi ndiyo tunagombana juu ya ardhi, migogoro ni ya sisi watumiaji wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondokana na migogoro hii, ni lazima tuelewe sura ya migogoro hii. Kuna aina kuu sita za migogoro, kwa ufupi kabisa katika hotuba yangu nimewawekea na jedwali mtaona ikoje, migogoro kati ya wakulima na wafugaji, migogoro kati ya wafugaji na hifadhi, migogoro kati ya wanavijiji na wamiliki wa migodi, migogoro kati ya wanavijiji na wamiliki wa

mashamba makubwa au wawekezaji, migogoro ya mipaka kati ya vijiji na Wilaya na migogoro ya wanavijiji na miji inayopanuka. Kwa hiyo, hii *typology,* kuelewa migogoro inahusu nini, huwezi kutatua migogoro kama huelewi inatokana na nini. Kwa hiyo, katika hotuba yangu kwa sababu muda hauruhusu nimejaribu kuanisha namna ya kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inashughulikia majukumu mbalimbali ambayo ni mtambuka na unaona kwamba ni mtambuka. Niseme tu kwa ufupi kwamba Wizara yetu inafanana kama figo, ni nani ameona yake lakini ikiharibika au ikapata mushkeli unakuwa katika shida kubwa. Kwa hiyo, tunafanya mambo mengi lakini hayaonekani na watu wengine wanafikiria siyo muhimu, ni figo ya Taifa. Ni mategemeo yangu kwamba Bunge litaendelea kuwa na mtazamo chanya na kuipa kipaumbele sekta ya ardhi kwa ujumla ili kuiwezesha kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya Wizara yangu yametokana na kuwepo kwa ushirikiano kati ya Serikali na Wadau wa Maendeleo zikiwemo taasisi za fedha za kimataifa, nchi wahisani, taasisi zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini. Wadau hao ni pamoja na Benki ya Dunia, Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa *(UN-HABITAT),* Shirika la Maendeleo la Ujerumani na Serikali za Denmark, Uholanzi, Uingereza na Sweden. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa George Simbachawene, kwa kunisaidia katika kutekeleza majukumu yangu. Pia napenda kumshukuru Katibu Mkuu Bwana Alphayo Kidata na Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Selassie David Mayunga na wafanyakazi wote ambao wanafanya kazi ngumu kama nilivyosema kazi ya figo siyo mchezo. Nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo kwa kazi nzuri wanayoendelea kufanya katika mazingira magumu lakini tunasonga mbele. Naomba nihitimishe kwa kusema kwamba kila mmoja wetu asikate tamaa kwa sababu mwisho wa siku watu ni waelewa na mambo muhimu tunayofanya yataweza kutambulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara imeazimia kutekeleza Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Sheria za Ardhi uliohuishwa mwaka 2013 (*SPILL* 2013) na Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano (2012/2013 - 2016/2017) ili kufikia malengo yaliyoainishwa kwenye Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na MKUKUTA II ambayo kwa pamoja yanalenga kufikia malengo makuu ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha. Ili Wizara yangu iweze kutekeleza kazi zake kama nilivyozianisha, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kama ifuatavyo:-

Mapato ya Serikali ni Sh.61,320,005,000/=, matumizi ya mishahara ni Sh.11,536,899,480/=, matumizi mengineyo ni Sh.42, 933,854,000/=. Jumla ya matumizi ya kawaida zinakuja Sh.54,470,753,480/=. Fedha za ndani ni Sh.21,000,000,000/=, fedha za nje ni Sh.13,379,977,000/=. Jumla ya matumizi ya miradi ya maendeleo Sh.34,379,977,000/=. Jumla ya matumizi ya kawaida na matumizi ya miradi ya maendeleo ni Sh.88,850,730,480/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru tena wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza kwa utulivu. Hotuba hii inapatikana kwenye tovuti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kama ilivyowasilishwa Mezani.**

**HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA PROF. ANNA KAJUMULO TIBAIJUKA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15**

**UTANGULIZI**

***1. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya mwaka wa fedha 2013/14 na malengo ya Wizara katika bajeti ya mwaka wa fedha 2014/15. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu

likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/15.

***2. Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia Waheshimiwa Wabunge kuwa na afya njema na hivyo kuweza kushiriki mkutano wa kumi na tano wa Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, nampongeza Mhe. Dkt. Asha Rose Migiro kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge lako na Waziri wa Katiba na Sheria. Aidha, nawapongeza Mhe. Ridhiwani Kikwete na Mhe. Godfrey Mgimwa kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu na kuimarisha safu ya Wabunge vijana wa CCM.

***3. Mheshimiwa Spika,*** naomba nitangulize dua zangu kwa Mwenyezi Mungu kuwa azipokee na kuzilaza mahala pema peponi roho za marehemu Mhe. Dkt. William Augustino Mgimwa aliyekuwa Waziri wa Fedha, Mbunge wa Jimbo la Kalenga na Mhe. Saidi Bwanamdogo aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Chalinze. Vilevile, kwa namna ya pekee natoa pole kwa Watanzania wenzangu walioathirika na majanga mbalimbali likiwemo la mafuriko yaliyotokea sehemu mbalimbali nchini kati ya mwezi Machi na Aprili, 2014. Sina budi kuwalilia na kuwakumbuka wananchi kadhaa wa Wilaya ya Muleba Kata ya Mazinga, Nyakabango, Kimwani na Rulanda waliouawa na mamba na viboko kutoka Hifadhi ya Taifa ya Rubondo. Maisha yao hayakupotea bure nimetoa taarifa kuepusha mashambulizi mengine. Aidha kuna wananchi ambao wamepoteza maisha yao katika migogoro ya ardhi sehemu mbalimbali nchini. Nichukue nafasi hii kuwapa pole wafiwa, njia pekee ya kuwaenzi ndugu zetu hao ni kumaliza migogoro hii tukawa taifa na jamii inayomaliza tofauti kwa majidiliano (*...dialogue and not confrontation*).

***4. Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mohammed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Mpanda Mashariki, kwa uongozi wao mahiri. Nawashukuru kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano wanaonipa, ulioniwezesha kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa ya kuongoza sekta hii mtambuka na muhimu katika maendeleo ya Taifa letu. Nawapongeza kwa dhati Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; pia, Mhe. Maalim Seif Shariff Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; na Mhe. Balozi Ali Idd Seif, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Zanzibar. Sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar na za miaka 50 ya Uhuru zilionesha jinsi gani taifa hili linasonga mbele kwa amani, mshikamano na

upendo. Tanzania imekuwa kisiwa cha amani si kwa kubahatisha bali kwa uongozi imara chini ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi.

***5. Mheshimiwa Spika,*** nakupongeza wewe kwa kuongoza shughuli za Bunge kwa ufanisi. Mwenyezi Mungu aendelee kukuongoza na kukupa nguvu, afya na hekima za kumudu zaidi majukumu yako. Pia, nampongeza Mhe. Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa na Naibu Spika wa Bunge letu kwa utendaji mzuri katika uendeshaji wa shughuli za Bunge.

***6. Mheshimiwa Spika,*** napenda nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini kwa kunipa ushirikiano wa karibu katika kutimiza majukumu yangu nikiwa Mbunge wao. Pamoja na kuwa na kazi nyingi za kitaifa, wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini wamekuwa wakinipa ushirikiano mzuri na kujitahidi kukutana nami ninapopata nafasi kufika jimboni kwa kuhudhuria vikao na mikutano katika tarafa zao au kupokea wageni na wataalaam waelekezi ninaowatuma kufika kusukuma maendeleo yetu. Kama Waziri, tena wa Ardhi, muda wa kuwa jimboni ni mdogo. Pamoja na hayo wananchi wa Muleba wamekuwa wakijitokeza kwa wingi katika mikutano ya Kata ninapofika ili tutathmini maendeleo, kujipanga vizuri na kula na kunywa pamoja. Muleba tunasema "Ebitaina mahyo tibyela". Au "Kazi bila pongezi haiendi". Ninawashukuru sana kwa moyo huo wa upendo ambao umewaumbua wanaodhani kuwa kukaa mbali ni kukosa mahusiano.

***7. Mheshimiwa Spika,*** aidha, ninawashukuru ndugu, jamaa na marafiki wanaonisaidia na kunipa ushirikiano wa karibu katika kutimiza majukumu ya Uwaziri na Ubunge. Nawashukuru wananchi na kuwahakikishia popote pale mlipo, iwe Tarafa ya Nshamba, Kimwani au Muleba yenyewe, kwamba tutayalinda mafanikio tuliyoyafikia na kuongeza kasi zaidi ili kufikia malengo ya kulinda amani, utulivu na kufikia maisha bora. Namuomba Mwenyezi Mungu amwezeshe kila mwananchi kulitambua hili na kuchangia katika nafasi yake kwa kadri ya uwezo wake kufikia maisha bora. Mwisho, ninatuma salamu kwa mama yangu mzazi Ma Aulelia Kajumulo hapo Muleba. Sala zake za kila siku zimeendelea kuniimarisha katika kutekeleza majukumu yangu. Nasimama hapa nikiwa mzima wa afya kwa sababu hiyo.

***8. Mheshimiwa Spika****,* napenda kuwashukuru kwa dhati viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi (CCM) ambao wamenisaidia katika kutekeleza majukumu yangu magumu hasa katika utatuzi wa migogoro ya ardhi sehemu mbalimbali nchini. Hii imenipa nguvu mpya katika kutekeleza ilani ya CCM. Aidha, sina budi kutambua mchango wa viongozi wa dini na vyama vya hiari ambao nimeshirikiana nao katika kazi zangu za kutatua migororo na changamoto nyingi za sekta ya ardhi ambazo zinahitaji ushiriki wao, busara zao na kutambua na kutofautisha sheria na haki na uhusiano wake.

***9. Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya kipekee natoa shukurani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama kwa ushirikiano mkubwa na ushauri wao ambao uliiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Natoa shukrani za pekee kwa Naibu Waziri, Mhe. George Bonifance Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe kwa ushirikiano na umoja tuliojenga katika kutekeleza majukumu yetu. Nawashukuru pia Katibu Mkuu Bw. Alphayo Japani Kidata; Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Selassie David Mayunga; watendaji katika Idara, Vitengo, Shirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushauri na mshikamano wao katika kupanga na kutekeleza mipango ya Wizara. Zipo changamoto nyingi zinazoikabili sekta yetu lakini kwa mshikamano na umoja wao naamini tumeweza kuendelea kukabiliana nazo.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SEKTA YA ARDHI**

***10. Mheshimiwa Spika,*** changamoto zinazoendelea kuikabili sekta yangu, kama nilivyoziorodhesha mwaka jana, zinagawanyika katika maeneo manne (4) makubwa kama ifuatavyo:

(i) Uelewa usiotosheleza wa wananchi kuhusu sekta yenyewe hasa sheria zake, taratibu na miongozo iliyopo; haki zao na wajibu wao;

ii. Nafasi ya vyombo mbalimbali vya usimamizi na utendaji wake;

(iii) Vitendea kazi vilivyopo na vinavyohitajika ili kukidhi mahitaji ya sekta nyeti ya ardhi ambayo ni kiungo muhimu katika maendeleo; na,

(iv) Mazingira ya utendaji yaliyopo nje ya uwezo wa Wizara.

***11. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara yangu iliahidi kuwa itaeleza jinsi ilivyojipanga kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa majukumu yake. Katika kutekeleza ahadi hiyo, Wizara imeongeza utoaji wa elimu kwa umma kuhusu sheria za ardhi, kanuni na taratibu pamoja na kuandaa miongozo mbalimbali; kupunguza kwa kiasi kikubwa ukosefu wa vitendea kazi katika sehemu za kazi kwa mfano, ununuzi wa mtambo mpya wa uchapaji wa ramani na nyaraka. Ili kuongeza mahusiano na wadau wake na kuboresha mazingira ya utendaji yaliyoko nje ya uwezo wa Wizara, Wizara iliweza kuwashawishi wahisani wa maendeleo ambao tayari wameanza kuipatia Wizara rasilimali fedha za kutekeleza Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Sheria za Ardhi. Pia, Wizara ipo katika hatua za kurekebisha muundo wake ili watumishi wa Sekta ya Ardhi walioko Halmashauri wawajibike moja kwa moja Wizarani.

***12. Mheshimiwa Spika,*** baada ya kueleza hayo, naomba sasa nieleze kwa kifupi utekelezaji wa Mpango wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/14 na Shabaha za Mpango wa mwaka wa fedha 2014/15. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa takwimu nyingi za utekelezaji zinaishia mwezi Aprili, 2014 na zitakuwa tofauti ifikapo mwisho wa mwezi Juni, 2014.

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2013/14 NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2014/15

### Ukusanyaji wa Mapato

***13. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya Shilingi **bilioni 100.05** kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato yanayotokana na Sekta ya Ardhi. Hadi Aprili, 2014 jumla ya Shilingi **bilioni 37.03** zilikusanywa. Makusanyo haya ni zaidi ya maduhuli yaliyokusanywa katika mwaka wa fedha 2012/13 kwa shilingi **bilioni 14.27**. Hata hivyo, mwenendo wa makusanyo kwa mwaka wa fedha 2013/14 ni hafifu yakilinganishwa na lengo la kukusanya shilingi **bilioni 100**. Sababu zilizochangia hali hiyo ni pamoja na kubainika kwamba makusanya ya nyuma yaliyopelekea malengo ya ukusanyaji mpya kuwekwa yalitokana na vyanzo visivyojirudia, yaani tozo kwa viwanja vipya wakati wa mradi wa viwanja elfu ishirini. Kwa hiyo pamoja na juhudi za kukusanya maduhuli kuongezeka na kupanda kwa viwango vya kodi, ada na tozo mbalimbali za ardhi bado malengo hayakufikiwa. Aidha utaratibu wa ulipaji wa kodi usio rafiki kwa wananchi, tabia ya kusubiri kulipa kodi dakika za mwisho wa mwaka wa fedha ambao bado unaendelea, na uelewa mdogo wa wananchi juu ya wajibu wao wa kulipa kodi pia umechangia kutokufikia malengo hadi sasa. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara inarekebisha viwango vya kodi, ada na tozo za ardhi pale ambapo zitadhihirika kuwa juu ya uwezo wa wananchi (*affordability test*); mazungumzo yamefanyika ili kuhakikisha utaratibu wa kufanya malipo unarahisishwa; na, kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa umma kuhusu wajibu wa wamiliki wa viwanja na mashamba kulipa kodi. Aidha wanaoshindwa kulipa kodi ya ardhi watachukuliwa hatua na kubatilisha milki zao kwa kukiuka masharti ya miliki.

***14. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15, baada ya kurekebisha uhalisia wa vyanzo vya walipa kodi tofauti na walipa tozo, Wizara imeweka lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 61.32.** Maduhuli haya yatakusanywa kwa kutumia mikakati ifuatavyo: kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi; kupanga, kupima na kumilikisha maeneo mapya; kuhamasisha wananchi kulipa kodi ya pango la ardhi; kurahisisha ulipaji wa kodi kwa kutumia teknolojia za

kisasa za malipo na kuhuisha viwango vya kodi ya ardhi. Aidha, Wizara yangu itaendelea kuwachukulia hatua za kisheria wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi. **Nitumie fursa hii kuwakumbusha wananchi kutimiza masharti ya umiliki wa ardhi ikiwa ni pamoja na kulipa kodi ya pango la ardhi, ada na tozo nyingine kwa mujibu wa sheria.**

**Matumizi**

***15. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya **Shilingi bilioni 108.3**. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 10.20** zilitengwa kwa ajili ya mishahara; **Shilingi bilioni 25.96** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo; na **Shilingi bilioni 72.17** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za miradi ya maendeleo **Shilingi bilioni 56.2** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 16** ni fedha za nje. Hadi Aprili, 2014 jumla ya fedha zilizopatikana ni **Shilingi bilioni 47.94** sawa na asilimia **44.25** ya fedha zilizoidhinishwa. Jumla ya **Shilingi bilioni 38.80** sawa na asilimia **81** ya kiasi kilichotolewa, zilitumika (**Jedwali Na. 1**). Ni matarajio yangu kwamba fedha zilizotolewa zitatumika hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2014.

**UTAWALA WA ARDHI**

***16. Mheshimiwa Spika***, Usimamizi wa ardhi nchini unahusisha mamlaka kuu tatu ambazo ni Halmashauri za Vijiji, Halmashauri za Wilaya na Miji na Wizara chini ya ofisi ya Kamishna wa Ardhi. Majukumu na mamlaka za usimamizi yameainishwa vema katika Sheria za Ardhi. Lengo la sheria ni kuhakikisha kuwa wananchi wanashirikishwa ipasavyo katika suala zima la usimamizi wa rasilimali ardhi kuanzia ngazi ya Kijiji hadi Taifa.

**Ofisi za Ardhi za Kanda**

***17. Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kusogeza huduma za ardhi karibu na wananchi, Wizara imeendelea kuanzisha na kuimarisha Ofisi za Ardhi za Kanda. Hadi sasa Wizara ina Ofisi za Ardhi za Kanda 7 ambazo ni Kanda ya Kusini (Mtwara), Ziwa (Mwanza), Mashariki (Dar es Salaam), Kaskazini (Moshi), Kati (Dodoma), Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) na Magharibi (Tabora). Wizara imepanga kupeleka huduma za Mipango Miji na Vijiji, Upimaji na Ramani na Uthamini wa Mali katika ofisi hizo katika mwaka wa fedha 2014/15.

***18. Mheshimiwa Spika,*** katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2013/14, Wizara yangu iliahidi kuanza kutoa huduma za ardhi katika ofisi ya ardhi ya Kanda ya Magharibi iliyopo mjini Tabora. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ofisi hiyo imeanza kazi rasmi na inahudumia mikoa ya Tabora, Shinyanga, Kigoma na Katavi, ambayo awali ilikuwa inahudumiwa na Kanda ya

Ziwa (Mwanza) na Nyanda za Juu Kusini (Mbeya). Ni matumaini yangu kwamba kwa kuanzishwa ofisi hiyo kutawawezesha wananchi kupata huduma za ardhi karibu na maeneo yao.

***19. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara yangu itaigawanya Kanda ya Mashariki kuwa Kanda mbili; Kanda ya Dar es Salaam na Kanda ya Mashariki. Kanda ya Dar es Salaam itahudumia Mkoa wa Dar es Salaam pekee kutoka makao makuu ya Wizara na Kanda ya Mashariki itahudumia Mikoa ya Pwani na Morogoro kutoka aidha mkoa wa Morogoro au Pwani kama itakavyoamuliwa na wadau. Kanda ya Mashariki itaanza kutoa huduma za ardhi kuanzia Julai, 2014. Hatua hii ni muendelezo wa kusogeza huduma za ardhi karibu na wananchi na kuongeza ufanisi.

**Mkakati wa Kupima Kila Kipande cha Ardhi Nchini**

***20. Mheshimiwa Spika***, Sheria za ardhi zinatoa miongozo muhimu ya kusimamia ardhi na fursa ya kuhakikisha kuwa ardhi yote nchini inamilikiwa kisheria. Wizara imeweka mkakati wa kuhakikisha kuwa kila kipande cha ardhi nchini kinapangwa, kinapimwa, kinamilikishwa na kinasajiliwa kisheria. Mkakati huu ambao umeanza kutekelezwa katika Wilaya ya Mvomero katika Mkoa wa Morogoro utasaidia kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi. Katika mwaka wa fedha 2014/15 utekelezaji utaendelea katika Wilaya za Kilosa na Kilombero, Mkoa wa Morogoro. **Natoa rai kwa wananchi na Halmashauri ambazo maeneo yao yatahusika katika kufanikisha utekelezaji wa mkakati huu kutoa ushirikiano wa dhati mara zitakapofikiwa. Aidha, ninawaomba wananchi pia kutambua ardhi ikishapimwa na kumilikishwa itakuwa haramu kuivamia na kuitumia kwa matumizi ambayo hayakupangwa. Migogoro haiwezi kuisha kama kila mwananchi hatii matumizi yaliyopangwa.**

**Utekelezaji wa Sheria ya Ardhi**

***21. Mheshimiwa Spika***, Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 inatoa fursa ya kuhakikisha kuwa ardhi yote nchini inamilikiwa kisheria. Hadi Aprili 2014, vijiji **20** vimewezeshwa kuandaa mipango shirikishi ya matumizi ya ardhi ya kijiji, Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **972** vimetolewa kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali, Hati za Hakimiliki ya Kimila **24,945** zimetolewa na Hati Miliki **24,651** zimetolewa (**Jedwali Na. 2**). Katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara yangu itaendelea na kazi ya uhakiki na upimaji wa vipande vya ardhi wilayani Mvomero na inatarajia kupima na kuandaa hatimiliki za kimila **70,000** na Hati Miliki **40,000**. **Halmashauri zote nchini zihakikishe kuwa zinapanga, zinapima, zinamilikisha viwanja na kuandaa Hati ili wananchi waweze kuwa na milki salama.**

***22. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kushughulikia uteuzi wa wajumbe wa Kamati za Ugawaji Ardhi katika ngazi ya Taifa, Miji na Wilaya. Kamati hizi ni vyombo muhimu katika kushughulikia ugawaji wa ardhi nchini. Katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara imefanya uteuzi wa Wajumbe wa Kamati za Ugawaji Ardhi katika Halmashauri za Magu, Musoma, Kigoma/Ujiji, Bukoba, Kilosa, Morogoro, Masasi, Tandahimba, Bariadi, Lindi, Mpanda, Same, Kilolo, Sengerema, Manispaa ya Morogoro na Manispaa ya Moshi. Aidha, Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi pamoja na majukumu mengine inalo jukumu la kugawa ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Katika mwaka wa fedha 2013/14 kamati hii ilipokea maombi **96** na kutoa ushauri wa kumilikisha viwanja **35** na mashamba **12** kwa ajili ya uwekezaji. **Nazihimiza Halmashauri ambazo hazina Kamati za Ugawaji Ardhi za Wilaya na Miji kuwasilisha mapendekezo ya majina ya wajumbe wa kamati hizo Wizarani ili uteuzi uweze kufanyika.**

***23. Mheshimiwa Spika***, mojawapo ya majukumu ya Wizara yangu ni kusimamia uhamisho wa milki za ardhi. Katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara iliahidi kushughulikia maombi ya uhamisho wa milki **1,800**. Hadi Aprili, 2014 Wizara imeshughulikia maombi ya uhamisho wa milki **3,079.** Kwa mwaka wa fedha 2014/15 Wizara itashughulikia maombi ya uhamisho wa milki **3,500**. Vilevile, Wizara inaendelea na jukumu la kusimamia masharti ya umiliki wa ardhi na kuhakikisha kuwa miliki zinaendelezwa ipasavyo. Hadi Aprili, 2014 ilani za ubatilisho **3,581** zilitumwa kwa wamiliki waliokiuka masharti ya umiliki wakiwemo wamiliki wa mashamba yasiyoendelezwa nchini. Kwa mwaka wa fedha 2014/15, Wizara itaendelea kushughulikia ubatilisho wa milki zote zinazokiuka masharti ya uendelezaji. **Napenda kuwashauri wananchi wote wanaonunua milki za ardhi kuhakikisha wanafanya uhamisho wa milki na kuzisajili.**

**Usajili wa Hati na Nyaraka za Kisheria**

***24. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara ilikuwa na lengo la kusajili hati za kumiliki ardhi pamoja na nyaraka za kisheria zipatazo **80,000**. Kati ya hizo hati za kumiliki ardhi ni **35,000** na nyaraka za kisheria ni **45,000**. Hadi Aprili, 2014 jumla ya hatimiliki na nyaraka za kisheria **50,592** zilisajiliwa. Kati ya hizo hatimiliki ni **21,285** na nyaraka za kisheria ni **29,307,** zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi Sura Na. 334 (**Jedwali Na. 3A)**. Aidha, nyaraka **5,072** zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka, Sura117 (**Jedwali Na. 3B)**. Pia, rehani ya mali zinazohamishika zipatazo **2,077** zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya Mali Zinazohamishika, Sura 210 (**Jedwali Na. 3C)**. Aidha, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara inakusudia kusajili Hatimiliki **42,000**, Nyaraka za Kisheria **45,000** na Hati ya Sehemu ya Jengo/eneo **2,000**.

**Kuboresha Kumbukumbu za Ardhi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

***25. Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imeendelea kutekeleza jukumu muhimu la utunzaji wa kumbukumbu za ardhi na kuzisimamia ipasavyo kwa kuweka na kuimarisha mifumo ya kielektroniki. Mifumo hiyo ni pamoja na mfumo unganishi wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi wa *Integrated Land Management Information System* (ILMIS) na mfumo wa kutunza kumbukumbu za kodi ya ardhi (*Land Rent Management System* - LRMS).

***26. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara iliahidi kuendelea na kazi ya kuweka mfumo unganishi wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi (*Integrated Land Management Information System* - ILMIS). Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imepata fedha za kujenga mfumo huo na ujenzi utaanza rasmi katika mwaka wa fedha 2014/15.

***27. Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imeendelea na kazi ya kusimika mfumo wa kielekitroniki wa kuhifadhi kumbukumbu na kukadiria kodi ya Ardhi. Katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara ilipanga kusimika mfumo huo katika Ofisi za Ardhi za Halmashauri 20. Hadi Aprili, 2014 mfumo huu ulisimikwa katika Ofisi za Ardhi za Halmashauri **75** (**Jedwali Na. 4).** Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara itaendelea na kazi ya kusimika mfumo wa kielekitroniki wa kuhifadhi kumbukumbu na kukadiria kodi ya ardhi katika ofisi za Ardhi za Halmashauri **30.**

## UTHAMINI WA MALI

***28. Mheshimiwa Spika***, Wizara yangu inalo jukumu la kuthamini na kuidhinisha taarifa za uthamini wa mali kwa madhumuni mbalimbali ya kuwezesha maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kuna aina kuu mbili za uthamini ambazo ni Uthamini wa Kawaida na Uthamini wa Kisheria.

### Uthamini wa Kawaida

***29. Mheshimiwa Spika***, Uthamini wa Kawaida hufanyika kwa kuzingatia misingi ya kitaaluma na hauna maelekezo maalum ya sheria. Uthamini huu hufanyika ili kuwezesha maamuzi mbalimbali kufanyika yakiwemo maamuzi ya mauzo au manunuzi ya mali, kuweka mali rehani, kuomba mikopo benki, dhamana ya mahakama, mizania na bima. Katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara iliweka lengo la kuthamini na kuidhinisha taarifa za uthamini wa mali **15,000**. Hadi Aprili, 2014, Wizara iliidhinisha taarifa za uthamini wa kawaida wa mali **7,904** (**Jedwali Na.5A)**. Kwa mwaka wa fedha 2014/15, Wizara itafanya na kuidhinisha taarifa za uthamini wa mali **10,000** kwa matumizi mbalimbali kadri maombi yatakavyowasilishwa.

**Uthamini wa Kisheria**

***30. Mheshimiwa Spika,*** Uthamini wa Kisheria hufanyika ili kuwezesha utozaji wa ada na ushuru wa Serikali kutokana na mauzo au uhamisho wa umiliki wa mali, utozaji malipo ya awali (*premium*) wakati wa kutoa milki, utozaji kodi ya pango la ardhi na ukadiriaji fidia za mali zinazoguswa na miradi mbalimbali inayotekelezwa nchini. Katika mwaka wa fedha 2013/14, Wizara ilipanga kufanya na kuidhinisha taarifa za uthamini wa fidia wa mali **40,000**. Hadi Aprili, 2014 Wizara iliidhinisha taarifa za uthamini wa mali **29,898** kwa ajili ya kulipa fidia **(Jedwali Na. 5B).** Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara itawezesha uthamini wa mali 30,000.

**Viwango vya Thamani**

**31. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea na zoezi la kuhakikisha uwepo wa viwango sahihi vya soko kwa ajili ya ukadiriaji thamani ya ardhi na mazao. Katika mwaka wa fedha 2013/14, Wizara ilipanga kuendelea kufanya uchambuzi wa takwimu za bei ya soko kwa lengo la kuhuisha viwango vya thamani sambamba na kuweka utaratibu endelevu wa kuhuisha viwango hivyo. Hadi Aprili 2014, Wizara imehuisha viwango vya thamani vya mazao mbalimbali katika Wilaya za mikoa ya Mwanza, Geita, Kagera, Mara, Shinyanga, Simiyu, Tabora na Kigoma kwa kushirikiana na Halmashauri za Mikoa hiyo. Aidha, Wizara imehuisha viwango vya thamani ya ardhi katika eneo la Makongo Juu Wilaya ya Kinondoni na Kata tatu (3) za Wilaya ya Temeke (maeneo ya Kimbiji, Pemba Mnazi na Kisarawe II).

Pia, Wathamini wa Halmashauri zote nchini wamepatiwa Mafunzo na Miongozo ya utaratibu wa kufanya uchambuzi wa takwimu za bei ya soko na kuweka viwango vya thamani ya ardhi na majengo. Lengo ni kuhakikisha mfumo endelevu wa uhuishaji viwango vya thamani kadri ya mabadiliko ya bei ya soko. Katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara imepanga kuimarisha mifumo ya kielektroniki ya uwekaji na uhuishaji viwango vya thamani ya ardhi, majengo na mazao. **Nawaagiza Wataalam wa uthamini nchini kushiriki kikamilifu kuhuisha viwango vya thamani ili viendane na mabadiliko katika soko la mali kwenye maeneo yao.**

***32. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ikiwa ni msimamizi wa taaluma ya uthamini imeandaa miongozo mbalimbali ya kuwajengea uwezo na weledi Wathamini wa kumudu majukumu yao kwa mujibu wa taratibu za kisheria na kitaaluma. Miongozo hiyo ni pamoja na; Mwongozo wa Utaratibu wa Uthamini wa Fidia; Mwongozo wa Uchambuzi na uwekaji viwango vya thamani ya soko la ardhi, majengo na mazao; na, miongozo ya ukadiriaji malipo ya *premium* wakati wa kumilikisha ardhi, kodi ya pango la ardhi na gharama za kuhamisha

makaburi pale ardhi husika inapotwaliwa kwa manufaa ya umma. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara itasambaza miongozo hiyo kwa wataalam na wadau wa uthamini nchini. **Hivyo, nawaagiza wataalam na wadau wa uthamini kuzingatia yaliyomo kwenye miongozo hiyo ili iwawezeshe kutimiza wajibu wao na kuleta tija kwa umma kiuchumi na kijamii. Ninawataka wathamini kutambua kwamba baadhi yao wamekuwa chanzo cha migogoro kwa kujihusisha na vitendo visivyofaa kama kudai rushwa na hongo badala ya kuthamini mali za wananchi kwa ukweli na haki. Aidha, kumekuwa na migogoro mingi baada ya shughuli za uthamini ikiwa ni pamoja na uthamini hewa. Wizara tayari imeweka mikakati ya kuziba mianya hiyo kwa kutumia upimaji wa kielektroniki wa kila kipande cha ardhi na pia kutaka malipo ya uthamini yafanyike kupitia benki teule na hivyo kuwabana wale wanaotumia ujanja wa malipo kwa wathaminiwa hewa. Ninawaomba wananchi watupe ushirikiano katika utekelezaji wa malipo kupita benki kwa kufungua akaunti katika benki teule inapohitajika kufanya hivyo.**

## MABARAZA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA

***33. Mheshimiwa Spika***, tangu Sheria ya Mahakama ya Ardhi Sura 216 ianze kutumika tarehe 1 Oktoba, 2003 jumla ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya 49 yameundwa. Kati ya hayo Mabaraza 42 yanafanya kazi. Mabaraza haya yanasikiliza na kuamua migogoro ya ardhi na nyumba kwa lengo la kudumisha haki, usalama na amani katika jamii.

***34. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara ilipanga kununua samani na vitendea kazi pamoja na kukarabati majengo ya Mabaraza saba (7) ili yaanze kufanya kazi. Aidha, Wizara ilikusudia kuunda Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika Wilaya tano (5) za Kilindi, Mbulu, Kahama, Sengerema na Kasulu. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Wizara imekamilisha ukarabati wa majengo/ofisi za Mabaraza sita (6) pamoja na ununuzi wa samani na vitendea kazi zikiwemo seti za kompyuta. Hata hivyo, Mabaraza matano (5) hayajaundwa kutokana na hitaji kubwa la kuboresha mabaraza **49** yaliyoundwa.

***35. Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliendelea kushughulikia utatuzi wa migogoro ya ardhi na nyumba kupitia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya na iliahidi kuamua mashauri **11,000**. Kuanzia Julai, 2013 yalikuwepo mashauri **18,328** na hadi kufikia Aprili, 2014 mashauri mengine **11,548** yalifunguliwa. Katika kipindi hicho jumla ya mashauri **11,432** yaliamuliwa hivyo mashauri **18,444** yaliyobaki na yatakayofunguliwa yataendelea kushughulikiwa katika mwaka wa fedha 2014/15 (**Jedwali Na. 6)**.

***36. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 niliahidi kuendelea kufuatilia utendaji kazi wa wenyeviti ili kuhakikisha kuwa wanazingatia maadili ya kazi zao. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imeandaa Mwongozo wa maadili ya kazi ya Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya *(Code of Conduct)* utakaotumika kufuatilia utendaji wao wa kazi.

***37. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara itaendelea kuimarisha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya 49 kwa kuyapatia vitendea kazi ili kuyawezesha kutatua migogoro kwa haraka na kufikia uamuzi wa haki. Aidha, Wizara itakarabati majengo/ofisi za Mabaraza ili kuboresha mazingira ya kufanyia kazi. Vilevile, Wizara itayapatia Mabaraza yaliyopo watumishi na kuendelea kuunda Mabaraza katika Wilaya zingine kwa lengo la kuharakisha utatuzi wa migogoro.

## HUDUMA ZA UPIMAJI NA RAMANI

***38. Mheshimiwa spika,*** upimaji ardhi na utayarishaji ramani za msingi ni moja ya majukumu ya Wizara. Ramani hizo ni chanzo muhimu cha taarifa zinazohitajika katika kubuni na kutayarisha Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa sekta mbalimbali.

### Utayarishaji Ramani

***39. Mheshimiwa spika***, katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara ilipanga kukamilisha kujenga na kuimarisha kanzi ya taarifa za kijiografia (*geodata base*) katika Wilaya mpya 19 za Mikoa mipya minne (4) ya Geita, Katavi, Njombe na Simiyu; pamoja na kuendelea na utekelezaji wa kazi hiyo katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera na Mara. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa kazi ya kujenga na kuimarisha kanzi katika Wilaya zote 19 katika mikoa mipya minne (4) pamoja na mikoa ya Kagera na Mara imekamilika. Kazi hiyo inaendelea katika Mikoa ya Shinyanga na Mwanza. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara itakamilisha kujenga na kuimarisha kanzi ya taarifa za kijiografia katika mikoa ya Shinyanga na Mwanza na itaanza kazi hiyo katika mikoa ya Kigoma, Tabora na Rukwa.

***40. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara yangu iliahidi kukamilisha kufunga mtambo mpya wa uchapaji ramani. Wizara imekamilisha ufungaji wa mtambo huo. Kuwepo kwa mtambo huo kunaiwezesha Serikali kuwa na uwezo wa kuchapa ramani zenye viwango stahiki kwa matumizi mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara itaandaa na kuchapa ramani za msingi za uwiano wa 1:2,500 kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam. Aidha, Wizara itandaa ramani za kuelekeza (*guide maps*) katika

jiji la Dar es Salaam na maeneo ya utalii kwenye mbuga za wanyama za Mikumi na Serengeti.

**Mipaka ya Ndani ya Nchi**

***41. Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imeendelea kushughulikia utatuzi wa migogoro ya mipaka ya kiutawala katika maeneo mbalimbali kwa mujibu wa Matangazo ya Serikali. Katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara iliahidi kujenga na kuimarisha taarifa za kijiografia kwa ajili ya kutafsiri Matangazo ya Serikali (GN) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Hadi Aprili, 2014 Wizara ilikamilisha kutafsiri Matangazo ya Serikali kwa Hifadhi za Taifa za Selous, Serengeti na Saadani. Aidha, alama za kudumu za mipaka kati ya Hifadhi ya Serengeti na vijiji vinavyopakana na hifadhi hiyo zimesimikwa na zinasubiri upimaji. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara itafanya kazi ya upimaji wa mipaka kati ya hifadhi ya Serengeti na vijiji inavyopakana navyo pamoja na kutafsiri Matangazo ya Serikali. Aidha, Wizara itahakiki na kupima mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro kwa kushirikiana na TANAPA, wanavijiji na wadau wengine. **Natoa rai kwa wapima wote nchini kutambua kwamba wanawajibu kuhalalisha upimaji wao kwa mujibu wa Sheria kwa kupata Baraka za Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani kwa kazi zao. Migogoro imeibuka kwa upimaji holela bila kuzingatia matakwa hayo ya sheria.**

**Mipaka ya Kimataifa**

***42. Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu ina jukumu la kuweka na kutunza alama za mipaka kati ya Tanzania na nchi jirani. Katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara iliahidi kuimarisha alama za mipaka saba ya kimataifa kati ya Tanzania na nchi za Msumbiji, Malawi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Burundi, Uganda na Kenya. Hadi Aprili 2014, uwekaji wa alama za mpaka wa eneo la kilomita **51** za nchi kavu kati ya Tanzania na Msumbiji umekamilika. Mpaka kati ya Tanzania na Malawi katika ziwa Nyasa mazungumzo yanaendelea. Vilevile, uwekaji wa alama **78** za mpaka kati ya Tanzania na Zambia umefanyika katika eneo la Tunduma/Nakonde lenye urefu wa kilomita **46.** Uwekaji wa alama **70** za mpaka kati ya Tanzania na Kenya umefanyika katika eneo la Sirari lenye urefu wa kilomita **14.8**. Uwekaji wa alama za mpaka kati ya Tanzania na Burundi umeanza katika Wilaya ya Ngara. Hadi Aprili 2014 alama **143** zimesimikwa na kupimwa. Mazungumzo ya upimaji wa mpaka kati ya Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo yamefanyika kwa nia ya kuanza upimaji.

***43. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara yangu itaendelea na kazi ya upimaji wa mipaka kati ya Tanzania na nchi za Kenya, Burundi, Zambia, Msumbiji na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo pamoja na

kuandaa kanzi ya mipaka hiyo. Aidha, kuhusu mpaka kati ya Tanzania na Uganda, Wizara inaendelea kuwasiliana na Serikali ya Uganda ili kuanzisha mazungumzo kwa ajili ya kukamilisha kazi zilizoanza kufanyika katika mwaka wa fedha 2001/02.

**Upimaji wa Mipaka ya Vijiji**

***44. Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imekuwa ikiendelea na upimaji wa vijiji vinavyoendelea kuzaliwa katika Halmashauri mbalimbali nchini. Katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara iliahidi kupima mipaka ya vijiji 100 katika wilaya za Songea, Tunduru, Nyasa, Namtumbo na Mbinga. Hadi Aprili 2014, Wizara imekamilisha upimaji wa vijiji **145** katika Wilaya za Nyasa (**29**), Mbinga (**68**), Wanging'ombe (**22**) na Bagamoyo (**26**).

**Upimaji wa Viwanja na Mashamba**

***45. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara yangu iliweka lengo la kuidhinisha ramani zenye viwanja **60,000** na mashamba **1,000**. Hadi Aprili 2014, Wizara imeratibu na kuidhinisha ramani za upimaji zenye viwanja **67,237** na mashamba **325** (**Jedwali Na. 7A)**. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara imepanga kuratibu na kuidhinisha ramani za upimaji zenye viwanja **70,000** na mashamba **500**.

***46. Mheshimiwa Spika***, ili kurahisisha upimaji wa ardhi na kupunguza gharama za upimaji kwa wananchi, Wizara katika mwaka wa fedha 2013/14 iliahidi kusimika na kupima alama za msingi za upimaji (*control points*) **300** katika miji **50**. Hadi Aprili, 2014 Wizara imeweza kusimika na kupima alama **104** katika miji saba (**7**) ya Sikonge (**15**), Kigoma Ujiji (**20**), Mbogwe (**10**), Karumwa (**10**) Katoro (**5**), Uvinza **(20)** na Bagamoyo **(24)**. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara itaendelea kukamilisha usimikaji wa alama **240** zilizosalia katika miji hiyo (**Jedwali Na. 7B**).

***47. Mheshimiwa Spika***, ili kuhakikisha kuwa huduma ya upimaji ardhi inasogezwa karibu zaidi na wananchi, Wizara yangu iliahidi kugatua Mamlaka ya kusimamia kazi za upimaji ardhi katika Kanda. Hadi Aprili, 2014 Wizara imefanya maandalizi ya kuhamishia huduma za upimaji na ramani katika ofisi za kanda sita zilizopo Tabora, Mwanza, Dodoma, Moshi, Mbeya na Mtwara. Katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara itaanza kutoa huduma za Upimaji Ardhi katika Kanda hizo.

***48. Mheshimiwa Spika,*** katika mkakati wa kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za Upimaji Ardhi, Wizara inaendelea na kazi ya kuzibadili kumbukumbu zilizopo kwenda katika mfumo wa kanzi ya kie-lektroniki (*Digital*

*Cadastral Database*) ili ziweze kuunganishwa na mfumo unganishi wa kutunza kumbukumbu za ardhi (*Integrated Land Management Information System – ILMIS*). Ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za upimaji ardhi na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, Wizara imebadilisha kumbukumbu za ramani **5,000** za Jiji la Dar Es Salaam na kuziweka katika ramani unganishi (*Cadastral Index Map*). Katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara itaandaa kanzi ya viwanja katika miji mbalimbali nchini na kutayarisha vipengele (*Modules*) vitatu vya Mfumo wa Utunzaji Kumbukumbu za Upimaji Ardhi (*Survey Registration System – SRS*) ili kuboresha utoaji wa huduma za Upimaji Ardhi nchini.

**Upimaji wa Ardhi Chini ya Maji**

***49. Mheshimiwa Spika,*** jukumu mojawapo la Wizara ni upimaji wa ardhi chini ya maji na kutayarisha ramani zinazoonesha umbile la ardhi chini ya maji hususan milima, mabonde, miinuko na kina cha maji. Katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara ilipanga kununua kifaa cha upimaji ardhi chini ya maji kijulikanacho kama *echo sounder* ili kuwezesha kazi ya upimaji vina vifupi iweze kufanyika. Kifaa hicho kimenunuliwa.

**Mfuko wa Kupima Viwanja**

**50. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kusimamia Mfuko wa Mzunguko wa Kupima Viwanja (*Plot Development Revolving Fund – PDRF*) ambao huzipatia mikopo Halmashauri mbalimbali nchini kwa ajili ya kulipa fidia, kupima viwanja na kuvimilikisha kwa wananchi na taasisi mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara iliahidi kuongeza juhudi za ufuatiliaji wa urejeshaji wa mikopo pamoja na Halmashauri sugu kukatwa madeni ya mikopo hiyo kutoka katika marejesho ya asilimia 30 ya fedha ambazo Halmashauri hurejeshewa baada ya makusanyo yake. Hadi Aprili, 2014 madeni kwa Halmashuri mbalimbali yamepungua kutoka Shilingi **milioni 633.6** hadi kufikia Shilingi **milioni 325.5 (Jedwali Na. 7C)**. **Nahimiza Halmashauri zinazodaiwa kulipa madeni haya ili fedha hizi zikopeshwe katika Halmashauri zingine.**

***51. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhimiza Halmashauri kurejesha fedha zilizokopeshwa kutoka kwenye mradi wa viwanja **20,000**. Hadi Aprili 2014, Halmashauri nne (4) zilizokopa fedha kutoka kwenye mradi huo zilirejesha sehemu ya mikopo yao na kufanya deni hilo kupungua kutoka shilingi **bilioni 1.87** hadi kufikia Shilingi **milioni 780.39** (**Jedwali Na. 7D).** Wizara itaendelea kufuatilia Halmashauri ambazo zinadaiwa ili ziweze kurejesha fedha hizo.

**MIPANGOMIJI NA VIJIJI**

***52. Mheshimiwa Spika,*** mojawapo ya majukumu ya msingi ya Wizara yangu ni usimamizi wa uendelezaji na udhibiti wa ukuaji wa miji na vijiji nchini. Jukumu ambalo hutekelezwa kwa mujibu wa Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali inayotolewa kuhusiana na masuala ya uendelezaji miji na vijiji nchini.

***53. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha muongo mmoja tumeshuhudia ongezeko la watu na kasi ya ukuaji wa miji na vijiji hapa nchini. Ongezeko hili linajidhihirisha katika takwimu za sensa ya Taifa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012. Wakazi wa mijini waliongezeka kutoka milioni **7.9** sawa na asilimia **23.1** mwaka 2002 hadi kufikia watu milioni **12.7** sawa na asilimia **29.1** mwaka 2012. Ongezeko hili limekuwa changamoto kubwa kwa Mamlaka za Upangaji miji kushindwa kutoa huduma za kiuchumi na kijamii kwa kiwango stahiki na kufanya miji yetu kukua kiholela. Suala la ukuaji wa miji endelevu ni kichocheo cha maendeleo hivyo tunahitaji kuwekeza katika ustawi wa miji kwa kizazi cha sasa na kijacho kwa kupanga na kusimamia uendelezaji wa miji hapa nchini.

**Uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Jumla ya Uendelezaji Miji**

***54. Mheshimiwa Spika,*** katika kupanga miji, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za miji nchini huandaa Mipango ya Jumla kwa ajili ya kusimamia uendelezaji na udhibiti wa ukuaji wa miji hiyo. Mipango hiyo iko ya aina mbili: Mipango Kabambe ambayo hutoa mwongozo wa uendelezaji miji kwa muda mrefu wa miaka ishirini na Mipango ya Muda wa Kati ya Matumizi ya Ardhi ambayo hutoa mwongozo wa uendelezaji miji kwa muda wa miaka kumi. Kazi ya uaandaaji wa Mipango hiyo hufanyika kwa kutumia dhana shirikishi ambapo Mamlaka zote za Upangaji zinazohusika na mchakato huo hujengewa uwezo.

***55. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam ziliendelea kukamilisha maandalizi ya Mpango Kabambe wa jiji la Dar es Salaam ambapo rasimu ya mwisho iliwasilishwa kwa wadau na Mtaalam Mwelekezi anaendelea kuiboresha kwa kutumia maoni na mapendekezo yaliyotolewa na wadau. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji Mdogo wa Bagamoyo imekamilisha maandalizi ya Rasimu ya awali ya Mpango Kabambe wa mji huo. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mafia ilikamilisha maandalizi ya Rasimu ya Mpango wa Muda wa Kati wa Matumizi ya Ardhi wa Mji wa Kilindoni. Rasimu za mipango hiyo ziliwasilishwa kwa wadau wa Halmashauri husika kwa ajili ya kuzitolea maoni. Wizara inaendelea kushirikiana na Halmashauri za Manispaa ya Sumbawanga na Mji wa Bariadi kuandaa Mipango Kabambe ya miji hiyo.

***56. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Manispaa ya Sumbawanga, Wilaya ya Mafia, Mji Mdogo wa Bagamoyo na Bariadi itakamilisha kuandaa Mipango ya Jumla ya miji hiyo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Arusha na Halmashauri za Arusha na Meru itaanza maandalizi ya Mipango Kabambe ya Jiji hilo na viunga vyake kwa kutumia Mtaalam Mwelekezi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Manispaa za Lindi na Mtwara zitaanza maandalizi ya Mipango Kabambe ya Miji hiyo. **Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini ambazo hazina Mipango ya Jumla kutenga fedha za kuandaa mipango hiyo.**

**Uandaaji na Utekelezaji wa Mipango ya Kina ya Uendelezaji Miji**

***57. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imeendelea na utekelezaji wa hatua ya awali ya uandaaji wa Mpango wa Uendelezaji upya eneo la Manzese. Uhamasishaji wa wadau katika ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na Mtaa pamoja na ukusanyaji wa taarifa na takwimu za hali halisi ya eneo hilo umefanyika. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Njombe imekamilisha maandalizi ya Rasimu ya Mpango wa Uendelezaji Upya Eneo la Kati la Mji huo. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni imeanza zoezi la kuhuisha Mpango wa Kina wa Makongo kwa kutumia dhana ya kuendeleza eneo na kudai tozo ya maboresho (*betterment fee*). Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa zoezi hili itahusisha upimaji wa barabara kuu.

***58. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara kwa kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni itaendelea na kazi ya kuchambua takwimu na kuandaa rasimu ya awali ya Mpango wa Uendelezaji Upya Eneo la Manzese. Wizara itaendelea na utekelezaji wa kuboresha Mpango wa Kina wa Makongo; zoezi ambalo litahusisha upimaji wa barabara za ndani (*access roads*) pamoja na kupima viwanja ndani ya eneo la Mpango. Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni itawezesha uboreshaji wa eneo la Mbweni JKT kwa kuweka miundombinu stahiki. Aidha, Wizara itaendelea na utekelezaji wa jukumu lake la kukagua, kuidhinisha na kuhifadhi michoro ya Mipangomiji **500** ya maeneo yaliyopangwa. Vilevile, Wizara itaandaa miongozo ya namna ya kupanga matumizi ya ardhi katika miji midogo nchini.

**Uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni**

***59. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara yangu iliahidi kuendeleza Mji wa Kigamboni; kuingia mkataba na makampuni mawili ya kujenga nyumba, kufanya uthamini wa mali na kulipa fidia kwa wananchi ili

kupisha utekelezaji wa mradi na kujenga uwezo wa Wakala wa Uendelezaji wa Mji Mpya Kigamboni ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu haikuweza kutekeleza kazi hizo kama ilivyoahidi kutokana na ukosefu wa fedha. Hata hivyo, Wizara yangu imekamilisha uandaaji wa rasimu ya muundo wa Wakala wa Uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni na kuanzisha ofisi yake katika eneo la mradi. Kulitokea ucheleweshwaji katika kumteua Mtaalamu wa Fedha (*Transaction Adviser and Fund Raiser*) kwa sababu ya kukidhi matakwa ya sheria ya manunuzi. Hatimaye mwezi Machi, 2014 mtaalam aliteuliwa na sasa ameanza kazi yake. Jambo hili linatarajiwa kuongeza kasi katika kupata fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

***60. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara yangu itakamilisha Mpango wa Mji Mpya wa Kigamboni kwa kufanya mkutano wa wadau *(public hearing)* ili uweze kuidhinishwa; Kuandaa mipango ya kina ya maeneo yaliyopo ndani ya Mpango Kabambe wa Mji Mpya wa Kigamboni; Kuainisha, kulipa fidia na kupima maeneo ya miundombinu na umma katika eneo la mradi na kusimamia utekelezaji wa Mpango Kabambe kupitia Wakala wa Uendelezaji wa Mji Mpya Kigamboni kwa kushirikiana na wananchi.

***61. Mheshimiwa Spika,*** ninatoa rai tena kwa wananchi wa Kigamboni kuwa na imani na mradi huu. Ninawashukuru kwa uvumilivu na ushirikiano wao na kutambua azma ya Serikali kujenga Mji Mpya wenye viwango. Jambo hili ni gumu na linachukua mda lakini hatua iliyofikiwa si haba kwa zoezi lenyewe. Niondoe wasiwasi kwa wale ambao wanadhani kwamba kazi hii imeshindikana kwa hiyo tuondokane nayo. Mradi huu umetajwa kwa jina katika Ibara ya 60(b)(iv) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010 ambayo inaahidi **"Kuanzisha Mji Mpya wa Kisasa wa Kigamboni (*Kigamboni New City*)".** Hii pekee ni ishara tosha kuonesha wajibu wa Serikali katika kutoa kipaumbele kutekeleza kazi hii.

***62. Mheshimiwa Spika***, kazi ya kuanzisha mji ilianza kwa Serikali kuunda chombo cha Kigamboni Development Agency - (KDA) ambao ni Wakala wa Kuendeleza Mji Mpya wa Kigamboni. Tayari Makao Makuu ya Wakala huo yamefunguliwa huko Kigamboni ambayo ni hatua kubwa na muhimu katika utekelezaji wa mradi huu. Miaka 50 baada ya Uhuru, KDA ni Wakala wa pili kuundwa baada ya CDA ambayo inajenga Makao Makuu yetu hapa Dodoma. Nirudie tena kwamba ili kulinda maslahi ya wananchi, viwango vya fidia vilivyopangwa ni endelevu na wakati ukifika umahiri na umuhimu wake utaonekana. Ninahimiza wananchi wa Kigamboni kuendelea kuwa wavumilivu na kutokubali kurubuniwa kwa kuuza maeneo yao kwa wajanja ambao, baada ya viwango vya fidia kutajwa, wamejitokeza wakitaka kununua ardhi za wananchi kwa bei poa ili wao baadaye wafidiwe na KDA. Itambuliwe kuwa

viwango vya fidia katika Awamu ya Kwanza ya Mradi ni shilingi 35,000 kwa mita mraba sawa na shilingi 141,645,000 kwa ekari moja. Hiki ni kiwango kwa mujibu wa sheria kulingana na soko na thamani ya ardhi itakavyokuwa katika mji mpya.

***63. Mheshimiwa Spika**,* wananchi wa Kigamboni watambue Mamlaka ya Upangaji Mji wao ni KDA na wasikubali na kuyumbishwa na wanaotaka kupima maeneo ya wananchi kabla ya fidia stahiki kulipwa. Pia nifafanue kwamba wananchi wa Kigamboni wataendelea kubaki Kigamboni katika makazi yatakayojengwa huko Uvumba- kata ya Kibada (*Resettlement City*). Wananchi watawezeshwa kutumia sehemu isiyopungua asilimia kumi ya fidia yao kununua hisa za KDA hivyo kuendelea kufaidi matunda ya mji mpya wa Kigamboni kwa sasa na vizazi vijavyo. Hii ndiyo njia ya kisasa kwa mwananchi kubaki kwenye ardhi yake katika soko huria wakati mji mpya wenye viwango unajengwa.

***64. Mheshimiwa Spika***, katika fani yoyote na kazi yoyote, hakuna viwango bila weledi na nidhamu kwa hiyo hali hii inataka pia uzalendo. Ninafurahi kuwatangazia kuwa Serikali imeomba msaada wa wataalam kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Jopo la wataalam wa Mipango Miji kutoka China litawasili Juni, 2014 ili kushirikiana na wataalam wetu katika Upangaji wa Mji Mpya wa Kigamboni, Miji ya Lindi na Mtwara. Wizara ina imani kuwa utaratibu wa kupata fedha za kuendeleza Mji Mpya wa Kigamboni ukikamilika mambo mengi ya mwanzo (*teething problems*) yatapungua na kasi utekelezaji wa mji huo itaongezeka.

**Urasimishaji Makazi Holela**

***65. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara ilishirikiana na Halmashauri ya jiji la Mwanza kurasimisha makazi holela. Hadi Aprili 2014, jumla ya makazi **3,008** yalirasimishwa na jumla ya viwanja **2,308** vimepimwa na Hati miliki za muda mrefu **911** zimetolewa katika Jiji la Mwanza. Aidha, elimu ya urasimishaji na mikakati ya kuzuia makazi holela mijini imetolewa kwa wataalam wa Halmashauri **25** katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ni Iringa, Mbeya na Rukwa. Katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia Programme ya Taifa ya kurasimisha na Kuzuia Makazi Holela kwa kutoa elimu ya urasimishaji na mikakati ya kuzuia makazi holela mijini kwa wataalam wa Halmashauri katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini ambayo ni Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

**Usimamizi na Udhibiti wa Uendelezaji wa Miji**

**66. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa elimu na kusambaza nakala za Sheria ya Mipangomiji Na.8 ya mwaka 2007 kwa wadau mbalimbali. Elimu ya Sheria hiyo imetolewa kwa wataalamu wa sekta ya ardhi katika mikoa ya Tabora, Shinyanga, Kigoma, Katavi, Singida na Dodoma. Lengo ni kuwajengea uwezo wataalamu wa Mipangomiji katika kutekeleza majukumu yao. Katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara itaendelea kutoa elimu ya Sheria hiyo na marekebisho yake kwa wataalam katika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Iringa, Mbeya, Njombe na Ruvuma.

**Usimamizi na Udhibiti wa Uendelezaji wa Vijiji**

**67. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara ilitoa elimu ya Mwongozo wa kupanga makazi ya vijiji kwa wataalam na wadau katika mikoa iliyopo Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Iringa, Njombe, Rukwa na Mbeya) ili kwenda sambamba na Programu ya *Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania* (SAGCOT). Vilevile, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo na Mvomero zilijengewa uwezo wa kuandaa Mipango ya Makazi ya Vijiji vinne (4) vya Fukayosi na Kidomole Wilayani Bagamoyo; Lukenge na Hembeti Wilayani Mvomero.

**68. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara itaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Upangaji zikiwemo Halmashauri za Wilaya na Vijiji ili kuziwezesha kuandaa Mipango ya Kina ya Makazi ya Vijiji kwa ajili ya vitovu vya huduma vya vijiji 10 vinavyokua kwa kasi. Vilevile, Wizara itaandaa na kutunza Mfumo wa Kitaifa wa kumbukumbu za vijiji; itaendelea kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mipango ya uendelezaji makazi vijijini katika wilaya zenye Mipango hiyo zikiwemo wilaya za Urambo, Manyoni, Bariadi na Babati. Aidha, elimu ya mwongozo wa uandaaji wa mipango ya makazi ya vijiji itatolewa na miongozo hiyo kusambazwa katika mikoa iliyopo katika Kanda ya Ziwa ambayo ni Kagera, Mwanza, Shinyanga, Mara, Geita na Simiyu. **Natoa rai kwa Halmashauri za Wilaya zote nchini, hasa katika maeneo ambapo elimu hii imetolewa; wasimamie na kuwezesha upangaji wa makazi ya vijiji vyao, ili kuwezesha vijiji hivyo kuwa na makazi yaliyopangwa na kuwa na maeneo ya huduma za jamii.**

## MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI

**Mpango wa Taifa wa Matumizi ya ardhi**

**69. *Mheshimiwa Spika*,** umuhimu wa ardhi ni wa kipekee. Nikimnukuu R. S. Simpson kwenye kitabu chake cha Land Law and Registration, 1976 alisema:-

*"ardhi ni chanzo cha utajiri wote. Kutokana na ardhi tunapata kila kitu tutumiacho chenye thamani iwe chakula, mavazi, nishati, makazi, vyuma au vito. Matumizi yote ya thamani yanatokana na ardhi yawe chakula, nguo, mafuta ya kuendeshea mitambo, hifadhi, chuma au mawe ya thamani (vito). Tunaishi juu ya ardhi na kutokana na ardhi na maiti au majivu yetu hurudi ardhini tunapokufa. Uwepo wa ardhi ni ufunguo wa uhai wa binadamu na mgawanyo na matumizi yake ni muhimu sana".*

***70. Mheshimiwa Spika**,* katika mwaka wa fedha 2013/14, Serikali ilipitisha Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi. Madhumuni ya Mpango huo ni kuweka utaratibu wa kuongoza matumizi ya rasilimali za ardhi yenye usawa kwa ajili ya kuboresha maisha ya jamii, maendeleo ya kiuchumi na kijamii na uendelevu wa rasilimali za kimazingira nchini; na hivyo, kuchangia katika jitihada za serikali katika utekelezaji wa MKUKUTA. Hivi sasa marekebisho ya mwisho pamoja na kuhuisha takwimu vipo katika hatua za mwisho ili uchapishwe na kusambazwa kwa wadau. Utekelezaji wa programu za kipaumbele (Kilimo, Mifugo, Maji, Makazi, Mipango ya Matumizi ya Ardhi) utaanza katika mwaka wa fedha 2014/15 kwa ushirikiano na wadau.

***71. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara iliahidi kutoa mafunzo kwa viongozi na watendaji wa Wilaya kuhusu sheria za ardhi na mbinu shirikishi za uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Newala, Tarime, Rorya na Maswa kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya. Hadi Aprili, 2014 Viongozi na watendaji wa Wilaya za Tarime, Rorya, Newala na Geita wamepewa mafunzo juu ya maudhui ya sheria za ardhi na sheria ya upangaji matumizi ya ardhi. Aidha, kazi ya kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya hizo inaendelea. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara itakamilisha kazi ya kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya za Tarime, Rorya, Newala na Geita pamoja na kutoa mafunzo kwa viongozi na watendaji wa Wilaya nne kuhusu sheria za ardhi na mbinu shirikishi za uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi pamoja na kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya husika.

***72. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara iliahidi kukamilisha uandaaji na uchapaji wa Kanuni za Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Mwaka 2007 na kuchapisha na kusambaza toleo la pili la Mwongozo wa Upangaji na Usimamizi Shirikishi wa Matumizi ya Ardhi ya Vijiji. Wizara imekamilisha uandaaji wa Kanuni za Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya mwaka 2007. Pia, Mwongozo wa Upangaji na Usimamizi Shirikishi wa Matumizi ya Ardhi umechapishwa na kusambazwa kwa wadau. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara itachapisha kanuni hizo na kuzisambaza kwa wadau na itatafsiri Mwongozo wa Upangaji na Usimamizi Shirikishi wa Matumizi ya Ardhi ya Vijiji katika lugha ya Kiswahili.

**Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya na Vijiji**

***73. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iliahidi kushirikiana na wadau kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **150** katika wilaya mbalimbali hususan za mipakani mwa nchi na zile zenye migogoro sugu  ya ardhi. Aidha, Wizara ilipanga kutekeleza mradi wa SAGCOT kwa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji ili kutenga maeneo yanayotosheleza mahitaji ya matumizi ya ardhi ya wananchi, kutenga maeneo ya vyanzo vya maji na ardhi inayofaa kwa uwekezaji. Hadi Aprili, 2014 jumla ya vijiji **94** vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi katika Wilaya mbalimbali (**Jedwali Na. 8).** Pia, kazi ya kutekeleza mradi wa SAGCOT imeanza kwa Mkandarasi kupitia Mpango wa Matumizi ya Ardhi katika ukanda wa Reli ya Uhuru. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itawezesha uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **200** pamoja na kuendelea na uandaaji wa mipango ya matumizi ya Ardhi ya vijiji na wilaya katika ukanda wa SAGCOT na kutenga maeneo ya uwekezaji.

**MAENDELEO YA NYUMBA**

***74. Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imeendelea kusimamia Sekta ya Nyumba ili kuwezesha upatikanaji wa nyumba na kuona kuwa sekta hii inachangia kikamilifu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara itaendelea kuweka sera na mikakati ya utekelezaji itakayowezesha wananchi kumiliki au kuwa na nyumba bora za gharama nafuu.

***75. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2013/14, Wizara yangu iliahidi kuendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha na Benki Kuu katika kuweka mifumo ya kifedha itakayowezesha upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa mkataba wa mkopo wa *Tanzania Housing Finance* umerejewa upya ili kuipata kampuni ya *Tanzania Mortgage Refinancing Company* iliyowezeshwa kutoa mikopo ya nyumba au mtaji kwa benki za biashara ili nazo zitoe huduma ya mikopo ya nyumba kwa wananchi hata kama benki hizo hazijaanza kutoa mikopo kwa wananchi wanaonunua nyumba (*Pre-financing*). Hadi Aprili, 2014 jumla ya benki **19** zilikuwa zinatoa mikopo ya nyumba kwa miaka **15-20**, tofauti na benki **10** zilizokuwa zinatoa mikopo ya nyumba kwa kipindi kisichozidi miaka **15**.

***76. Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara yangu itatoa elimu kwa umma kuhusu utaratibu wa mikopo ya nyumba, ikiwa ni

pamoja na haki na wajibu wa mkopaji na mkopeshaji kwa mujibu wa sheria. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania kuweka utaratibu utakaowezesha mikopo ya nyumba kutolewa kwa masharti nafuu kuliko mikopo ya kibiashara. Wizara itashirikiana na vyombo vya fedha kuweka mazingira ya kuvutia uwekezaji katika sekta ya nyumba ikiwa ni pamoja na kuvutia waendelezaji milki binafsi ili wajenge nyumba za gharama nafuu za kuuza na kupangisha.

***77. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara yangu iliendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha pamoja na Benki Kuu ya Tanzania kukamilisha uundwaji wa Mfuko wa Mikopo Midogomidogo ya Nyumba. Mfuko huo umeanza kwa mtaji wa Dola za Marekani milioni 3 ambazo ni sehemu ya mkopo uliotolewa na Benki ya Dunia kupitia mradi wa kuendeleza sekta ya nyumba hapa nchini (*Tanzania Housing Finance Project*). Aidha, Serikali iliendeleza mazungumzo na Benki ya Dunia kwa lengo la kupata fedha zaidi kwa ajili ya Mfuko huo. Katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itatoa elimu kwa umma kuhusu mfuko huo na kuwahamasisha kutumia huduma zake.

***78. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2013/14, Wizara iliahidi kuandaa Sheria ya kusimamia Sekta ya Nyumba ikiwa ni pamoja na kuweka masharti ya uendelezaji nyumba, kuelekeza haki na wajibu wa waendelezaji nyumba, wanunuzi, wamiliki na wapangaji wa nyumba. Kazi hiyo itaendelea katika mwaka wa fedha 2014/15.

***79. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2013/14, Wizara iliahidi kuwa mpango wa nyumba kwa watumishi wa umma ungeanza kutekelezwa. Katika kuwezesha utekelezaji wa mpango huo Wizara ilizielekeza Halmashauri zote kutenga ardhi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kwa watumishi wa umma. Aidha, *Watumishi Housing Company* (WHC) iliyoundwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Shirika la Nyumba la Taifa itasimamia utekelezaji wa mpango huo. Katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara itaendelea kuwezesha utekelezaji wa mpango huo ikiwa ni pamoja na kuunda Mfuko wa Dhamana ya Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Umma.

**Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi**

***80. Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA) una majukumu ya kutafiti, kukuza, kuhamasisha na kusambaza matokeo ya utafiti na utaalamu wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu nchini.

***81. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara kupitia Wakala imeendesha Semina na mafunzo kwa vitendo ambapo jumla ya washiriki **974** kutoka katika Wilaya za Sikonge (**100**), Biharamulo (**56**), Halmashauri ya Arusha (**160**) na Muleba (**550**). Aidha, mafunzo kwa vitendo yalitolewa kwa wakufunzi na wahitimu wa VETA (**47**), Tarime (**42**), Korogwe (**15**) na Mafundi sanifu (**4**) kutoka Manispaa ya Tabora. Vilevile, jumla ya mashine **250** za kufyatulia tofali zilizalishwa. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wakala utaendelea kuhamasisha na kueneza teknolojia ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu katika Wilaya za Nkasi, Kishapu, Chunya na Tandahimba.

***82. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14, Wizara iliahidi kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya kuimarisha vikundi vya ujenzi wa nyumba vilivyoanzishwa na kutangaza huduma zinazotolewa kupitia vyombo vya habari. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Wakala umeendelea kujitangaza kupitia vyombo vya habari. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wakala utaendelea kujitangaza kupitia vyombo vya habari na kushiriki maonesho mbalimbali ya kitaifa ili kusambaza huduma kwa wananchi wengi zaidi.

## SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

### Kuimarisha Utendaji Kazi wa Shirika

***83. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara iliendelea kusimamia Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) katika utekelezaji wa malengo ya Mpango Mkakati wake wa kipindi cha mwaka 2010/11-2014/15 ikiwa ni pamoja na kuimarisha utendaji kazi. Shirika limeendelea kuboresha utendaji kazi wake kwa kuajiri wataalamu wa fani mbalimbali wapatao **31** kwa ajili ya kuongeza ufanisi na tija. Ajira hizi zimepandisha uwiano wa wafanyakazi wenye taaluma na wasiokuwa na taaluma kufikia asilimia **51** kwa **49** dhidi ya lengo la asilimia **70** kwa **30** ifikapo Juni, 2015. Pia, watumishi wa ngazi zote walipatiwa mafunzo ya utambuzi na ulezi wa vipaji pamoja na ushirikiano kati ya sekta za umma na sekta binafsi (*public – private partnership)*.

***84. Mheshimiwa Spika,*** Wizara iko kwenye mchakato wa kurekebisha Sheria Na. 2 ya Shirika la Nyumba la Taifa ya mwaka 1990 iliyoliunda upya shirika hilo. Lengo la marekebisho haya ni kuliwezesha shirika kufanya yafuatayo:- kupanua wigo wa shughuli za Shirika ili liweze kuwa mwendelezaji milki mkuu; kuliwezesha Shirika kuendesha shughuli zake katika mazingira shindani; na, kuoanisha sheria ya Shirika na sheria zingine.

### Upatikanaji wa Ardhi kwa Ajili ya Ujenzi wa Nyumba

***85. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14, Shirika liliweka lengo la kuendelea na mchakato wa ununuzi wa ardhi katika Wilaya mbalimbali nchini. Lengo la ununuzi huu ni kuliwezesha Shirika kuwa na hazina ya ardhi *(land bank)* ya kutosha itakayoliwezesha kutekeleza jukumu lake jipya la kuwa mwendelezaji mkuu wa miliki. Hadi Aprili, 2014, Shirika lilifanikiwa kununua ardhi yenye ukubwa wa ekari **3,686.9** na viwanja **464 (Jedwali Na 9A).** Pia, Shirika limeendelea na mchakato wa ununuzi wa ardhi yenye ukubwa wa ekari **2,627.5** iliyoko kwenye maeneo mbalimbali nchini. Katika mwaka wa fedha 2014/15, Shirika litaendelea na ununuzi wa ardhi ambao kwa sasa umefikia hatua mbalimbali.

**Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Majengo ya Biashara**

***86. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14, Shirika liliweka lengo la kuendelea kukamilisha miradi iliyokuwa ikiendelea na kuanza miradi mingine mipya. Aidha, Shirika liliweka kipaumbele kwenye ujenzi wa nyumba za gharama nafuu zisizopungua **20** kwa kila mkoa. Hadi Aprili, 2014, Shirika liliendea na utekelezaji wa miradi **26** ya ujenzi wa nyumba za makazi yenye jumla ya nyumba **1,947**. Miradi hii, ililiwezesha Shirika kuifikia mikoa **14** kwa kujenga nyumba za gharama nafuu **921** na nyumba za gharama ya kati na juu **978** katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Dodoma. Kati ya nyumba hizo, nyumba **697** zilikamilika ambapo **193** ni za gharama nafuu na **504** ni za gharama ya kati na juu (**Jedwali Na. 9B)**. Shirika pia linaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi wa miradi **31** yenye jumla ya nyumba za gharama nafuu **1,717** na miradi **18** yenye nyumba **3,493** za gharama ya juu na kati zitakazojengwa katika mikoa **17.** Katika mwaka wa fedha 2014/15, Shirika litaendea kukamilisha miradi inayoendea; kuanza miradi mingine mipya ya nyumba za gharama ya juu, kati na nafuu na hivyo kuifikia mikoa yote ya Tanzania Bara kwa kujenga nyumba zisizopungua **50** kwa kila mkoa.

***87. Mheshimiwa Spika****,* kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa kipindi cha 2010/11 – 2014/15, Shirika linauza asilimia **70** ya nyumba za makazi zinazojengwa na kupangisha asilimia **30**. Hadi Aprili, 2014, Shirika limefanikiwa kuuza nyumba **456** katika miradi yake na kupata kiasi cha shilingi bilioni **43.95 kati** ya **Shilingi bilioni 67.05** zinazotarajiwa wakati miradi hii itakapokamilika.

***88. Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka wa fedha 2013/14, Shirika lilipanga kuendelea na utekelezaji wa miradi tisa (**9**) ya majengo makubwa ya biashara na majengo mengine **20** yanayojengwa kwa ubia kwa kushirikiana na sekta binafsi. Hadi Aprili, 2014 Shirika liliweza kukamilisha mradi wa jengo moja la ghorofa **10** lililojengwa kwenye Kiwanja Na. 1 Barabara za Ufukoni na Ali Hassan Mwinyi, Upanga - Dar es Salaam ambalo ni makao makuu mapya ya Shirika. Vilevile, Shirika lilianza ujenzi wa majengo manne (**4**) ya biashara ambayo ni

jengo la ghorofa tano (**5**) lililoko Kiwanja Na. 2 Barabara ya *Old Dar es Salaam* mkoani Morogoro; jengo la ghorofa moja (**1**) katika Mtaa wa Kitope Manispaa ya Morogoro; jengo la ghrofa tano (**5**) lililoko Mtaa wa Lupa Way, Manispaa ya Mbeya; na, jengo la ghorofa tatu (**3**) lililoko Mitaa ya Mkendo na Kusaga mjini Musoma. Aidha, Shirika kwa kushirikiana na wabia wake liliweza kukamilisha miradi ya majengo **57** na miradi mingine **27** ya biashara ilikuwa katika hatua mbalimbali za matayarisho ya kuanza ujenzi. Vilevile, Shirika lilikamilisha miradi **16** ya ubia iliyotekelezwa kwa kushirikiana na sekta binafsi na kuendelea na ujenzi wa miradi mingine minne (**4**).

***89. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15, Shirika litaendelea na utekelezaji wa jumla ya miradi ya majengo ya biashara **30** ikiwemo inayoendea na ile ambayo kwa sasa iko katika hatua za maandalizi pamoja na kukamilisha miradi minne (**4**) ya ubia.

**Undelezaji wa Vituo vya Miji Midogo (*Satellite Cities*)**

***90. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Shirika limeendelea na matayarisho ya kuanza jukumu lake jipya la kuendeleza vituo vya miji midogo kama mwendelezaji miliki mkuu (*master developer*). Wizara ilikabidhi rasmi Shirika eneo la Luguruni lenye ekari **156.53** na eneo la Kawe lenye ekari **267.71** kwa ajili ya kuyaendeleza. Aidha, Shirika kwa niaba ya Serikali liliingia Mkataba wa makubaliano (*memorandum of understanding*) na kampuni ya *Surbana International Consultants* ya Singapore kwa ajili ya kulipanga upya eneo la Luguruni. Pamoja na juhudi hizo, Shirika pia lilikamilisha matayarisho ya mipango ya kina (*detailed plans*) ya kuendeleza maeneo linaloyamiki ikiwa ni pamoja na eneo la Burka/Matevesi – Arusha lenye **ekari 579.2** na eneo la Usa River - Arusha lenye ekari **296** na pia kuendelea na matayarisho ya mipango hiyo kwa maeneo ya Uvumba, Kigamboni **(ekari 202)** na Kawe.

***91. Mheshimiwa Spika,*** Shirika litaanza uendelezaji wa eneo la Burka/Matevesi kwa kujenga miundombinu pamoja na nyumba za gharama nafuu **200** kabla ya Juni, 2014. Uendelezaji wa miradi hii ambao utakuwa na nyumba za makazi zisizopungua **15,000** pamoja na majengo ya biashara, utaishirikisha sekta binafsi kulingana na sera ya sasa ya Serikali ya ushirika wa sekta ya umma na sekta ya binafsi *(PPP)*. Katika mwaka wa fedha 2014/15, Shirika litaendelea na ukamilishaji wa mpango wa kina wa eneo la Luguruni, Kawe na Uvumba na kuendelea na uendelezaji wa maeneo ya Usa River na Burka/Matevesi.

**Utafutaji wa Mitaji kwa Ajili ya Miradi na Mikopo ya Ununuzi wa Nyumba**

***92. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14, Shirika limeendelea kutafuta mitaji kwa ajili utekelezaji wa miradi ya ujenzi. Hadi Aprili, 2014 Shirika limefanikiwa kuingia mikataba ya mikopo ya kiasi cha **Shilingi bilioni 210** na kuweza kutumia kiasi cha **Shilingi bilioni 124.** Aidha, Shirika limeendelea na juhudi za kuwahamasisha wanunuzi wa nyumba zake kutumia fursa za mikopo inayotolewa na benki za Azania Bank, Bank of Africa, CRDB - Bank, Exim Bank, KCB, NBC, Commercial Bank of Africa, NMB na Stanbic zilizoingia makubaliano ya kutoa mikopo ya ununuzi wa nyumba. Hadi Aprili, 2014, wanunuzi wapatao **89** waliweza kupata mikopo ya nyumba yenye jumla ya kiasi cha **Shilingi bilioni 12.2** na wengine wanaendelea na mchakato wa kupata mikopo hiyo. Katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara kupitia Shirika itaendelea na juhudi za kupata mikopo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi na majengo ya biashara pamoja na kuwahamasisha wananchi kuchukua mikopo kwa ajili ya ununuzi wa nyumba zinazojengwa na Shirika au wanazoweza kujenga wenyewe.

**Mapato ya Shirika**

***93. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Shirika lilitarajia kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 68.2** kutokana na kodi za pango la nyumba zake na hivyo kuendelea kuchangia mapato ya Serikali kwa kulipa kodi mbalimbali. Hadi Aprili, 2014, mapato ya shirika yalifikia **Shilingi bilioni 55.63** sawa na asilimia **98** ya lengo la kipindi cha Julai 2013 hadi Aprili 2014 (**Jedwali Na. 9C)**. Mafanikio haya yalitokana na juhudi za ukusanyaji wa kodi za pango pamoja na malimbikizo ya madeni. Mapato hayo yaliliwezesha Shirika kuchangia mapato ya Serikali kwa kiasi cha **Shilingi bilioni 10.02** kupitia kodi mbalimbali kama vile kodi ya pango la ardhi, kodi ya ongezeko la thamani, kodi ya majengo, kodi ya mapato, ushuru wa huduma za Halmashauri za Miji na Manispaa, kodi za mapato ya wafanyakazi, ushuru wa maendeleo ya taaluma na mchango wa pato ghafi kwa Serikali **Jedwali Na.9D.** Kwa mwaka 2014/15 Shirika linategemea kuingiza kiasi cha **Shilingi bilioni 70.1** kutokana na kodi za pango la nyumba na hivyo kuendelea kuchangia mapato ya Serikali.

**Matengenezo ya Nyumba na Majengo**

***94. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Shirika lilipanga kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 9.0** kwa ajili ya matengenezo makubwa ya nyumba na majengo yake. Hadi Aprili, 2014 Shirika lilitumia kiasi cha **Shilingi bilioni 4.2** kwa ajili ya matengenezo ya nyumba zipatazo **3,500.** Katika mwaka wa fedha 2014/15, Shirika litatenga kiasi cha **Shilingi bilioni 6.1** kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa nyumba na majengo ya yake.

**HUDUMA ZA KISHERIA**

**95. *Mheshimiwa Spika***, kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali huduma mbalimbali za kisheria zimeendelea kutolewa na wizara. Huduma hizo zinajumuisha kutunga sheria mpya, kuhuisha sheria na kusimamia mashauri yanayohusu Wizara.

**96. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara yangu iliahidi kuhuisha Sheria ya Ardhi, Sura 113; Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura 114; Sheria ya Mahakama za Ardhi, Sura 216 na Sheria ya Wapima Ardhi, Sura 324. Napenda kuliarifu bunge lako tukufu kuwa kazi ya kukusanya maoni ya wadau ili kuhuisha Sheria ya Ardhi, Sheria ya Ardhi ya Vijiji na Sheria ya Mahakama za Ardhi imekamilika na mapendekezo yatawasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua stahiki. Aidha, mchakato wa kuhuisha Sheria ya Wapima Ardhi utaendelea katika mwaka wa fedha 2014/15.

**97. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara ilipanga kuanza mchakato wa kutunga upya Sheria ya Utwaaji Ardhi. Kazi hii inaendelea na inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2014/15. Baada ya mchakato wa kutunga sheria hizo kukamilika, miswaada husika itawasilishwa katika Bunge lako tukufu. Aidha, Wizara yangu itaendelea na utaratibu wa kuzihuisha sheria mbalimbali za utawala wa ardhi kila mara inapolazimu ili kuzifanya ziendane na wakati na kukidhi makusudio ya kutungwa kwake.

## MAWASILIANO SERIKALINI

**98. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu inatoa elimu kwa umma kuhusu sera, sheria, kanuni na taratibu zinazo simamia Sekta ya Ardhi nchini. Katika mwaka wa fedha 2013/14 niliahidi kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa umma kwa kuanzisha mtandao rasmi wa kijamii (*official ardhi blog*); kuhuisha mkakati wa mawasiliano; na kuimarisha kitengo cha Mawasiliano cha Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ilianzisha mtandao rasmi wa kijamii unaopatikana kupitia anuani: www.ardhi.go.tz/blog; pia, kitengo cha Mawasiliano kilipatiwa vitendeakazi pamoja na kuongezewa rasilimali watu. Vilevile, Wizara imekamilisha mchakato wa kumpata mtaalam mwelekezi atakayehuisha Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara.

**99. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14, Wizara iliendelea kutoa elimu iliyolenga kuelimisha umma kuhusu sekta ya ardhi kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Wizara kwa kutambua umuhimu huo, iliendesha semina elekezi kwa wahariri wa vyombo vya habari nchini. Pia, wizara ilishiriki kwenye vipindi vinne (4) vya moja kwa moja (*live programmes*) vilivyorushwa kupitia runinga na redio. Pia, Wizara inakamilisha uandaaji wa vitabu vya sheria za Ardhi vitakavyosomeka kwa maandishi nundu, hii ni moja ya jitihada za

kuhakikisha wadau wote muhimu wa sekta ya ardhi (wakiwemo wenye ulemavu wa macho) wanapata elimu kuhusu Sekta ya Ardhi.

***100. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara itakamilisha kuhuisha mkakati wa mawasiliano wa wizara; kuratibu mawasiliano kati ya Wizara na wadau wake; kuandaa na kurusha vipindi vya televisheni na redio; na, kuboresha mawasiliano.

**HUDUMA ZA UTAWALA NA RASILIMALI WATU**

***101. Mheshimiwa Spika***, Wizara yangu inaendelea kuboresha mifumo ya usimamizi wa rasilimali watu na uendeshaji wa ofisi ili kuleta tija na ufanisi wa kazi. Hatua hii inajidhihirisha kutokana na hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa za kuboresha mifumo ya utendaji kazi na usimamizi wa rasilimali watu. Katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara imeendelea kutoa mafunzo, kuboresha mazingira ya ofisi, kutoa stahili kwa watumishi zinazoendana na masharti ya ajira zao, pamoja na kudumisha utawala bora. Msisitizo umelenga katika kutumia dhana shirikishi ya kupanga, kujenga uwezo, kutekeleza, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa majukumu ili kuboresha utendaji kazi na kusimamia nidhamu na watumishi. Vile vile Wizara inaendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kuhamasisha watumishi kujikinga na kupima afya zao.

***102. Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba yangu ya mwaka jana, nililifahamisha Bunge lako tukufu kuwa, wizara yangu ilikuwa inaendelea kujenga kituo cha kuhudumia wateja (*customer service centre*). Napenda kutoa taarifa kuwa Wizara imekamilisha ujenzi wa kituo hicho, na kwamba kituo hiki kitaanza kutoa huduma katika mwaka wa fedha 2014/15. Kituo hiki kitasaidia kuboresha utoaji wa huduma zinazotolewa na Wizara na kuleta ufanisi zaidi katika utendaji kazi wa pamoja na kuepusha mianya ya rushwa. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara itaendelea kuboresha utaoji wa huduma kwa kusimamia mifumo ya utendaji kazi, kuboresha mazingira ya ofisi, na kutoa stahili kwa watumishi zinazoendana na masharti ya ajira zao.

***103. Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa maendeleo ya rasilimali watu katika kufanikisha malengo yaliyopangwa, Wizara imeendelea kuwawezesha watumishi kuhudhuria mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuwajengea uwezo zaidi. Katika mwaka wa fedha 2013/14 jumla ya Watumishi **166** walihudhuria mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi nje na ndani ya nchi. Kati ya hao **36** walipatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi; **40** walipatiwa mafunzo yaliyohusu maadili katika utumishi wa umma; na, waajiriwa wapya **90** walipatiwa mafunzo ya awali (*induction course*). Katika kipindi hicho watumishi **88** wa taaluma mbalimbali waliajiriwa,

watumishi **13** walibadilishwa kazi baada ya kupata sifa na watumishi **8** walithibitishwa katika vyeo vyao.

***104. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara inatarajia kuwapatia mafunzo ya aina mbalimbali watumishi **250** wa kada mbalimbali**.** Aidha, kwa kutambua umuhimu wa michezo kwa afya za watumishi, Wizara katika mwaka wa fedha 2013/14 ilishiriki katika mashindano ya SHIMIWI na kufanikiwa kupata tuzo mbalimbali na pia iliandaa bonanza la michezo kwa watumishi wote. Vilevile viongozi wa michezo waliwezeshwa kuhudhuria mikutano na semina mbalimbali za michezo.

***105. Mheshimiwa Spika,*** ili kupambana na janga la UKIMWI katika sehemu ya kazi, Wizara imeendelea kuhamasisha watumishi kupima kwa hiari afya zao kwa kutumia utaratibu wa kuwaleta Wizarani wataalam wa huduma ya ushauri nasaha. Katika mwaka wa fedha 2013/14, watumishi 720 wa makao makuu walifanyiwa semina ya uhamasishaji, na watumishi **416** walipima na kufahamu hali za afya zao. Wizara imeendelea kuwapatia watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI msaada wa dawa na lishe. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara itaendelea kuhamasisha upimaji wa afya za watumishi kwa hiari na kutoa huduma stahiki.

**Vyuo vya Ardhi**

***106. Mheshimiwa Spika*,** Wizara ina vyuo viwili vya Ardhi vilivyopo Tabora na Morogoro. Vyuo hivi vinatoa mafunzo ya stashahada katika fani za Urasimu Ramani na Upimaji Ardhi; na, Cheti katika fani za Upimaji Ardhi, Umiliki Ardhi, Uthamini, Usajili na Uchapaji Ramani. Katika mwaka wa fedha 2013/14 idadi ya wahitimu ilikuwa **250** kati yao **178** walitoka Chuo cha Ardhi Morogoro na **72** walitoka Chuo cha Ardhi Tabora (**Jedwali Na. 10).** Katika mwaka wa fedha 2014/15 Chuo cha Ardhi Tabora kitaanzisha mafunzo ya stashahada katika fani ya Umiliki, Uthamini na Usajili wa ardhi ambayo itawapa wanafunzi sifa ya kujiunga na vyuo vikuu. Fani hizi ni muhimu kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la wataalam wa sekta ya ardhi. Aidha, Wizara itaendelea kuviimarisha vyuo hivi ili viweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. **Natoa wito kwa Halmashauri kuajiri wataalamu wanaohitimu katika vyuo hivi pamoja na kuwaendeleza watumishi wao kitaaluma kupitia vyuo hivi.**

## CHANGAMOTO MAALUM

**Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi**

***107. Mheshimiwa Spika*,** takriban katika kazi zote tunazotekeleza changamoto na kero kubwa imeendelea kuwa ni ongezeko la migogoro ya ardhi inayoibuka sehemu mbalimbali nchini. Ninachukua nafasi hii kuwaeleza

kwamba kimsingi hakuna migogoro ya ardhi bali ni "migogoro ya watumiaji wa ardhi". Ili kuondokana na migogoro hii ni muhimu kwa watumiaji wote wa ardhi kutambua ukweli huu na kujitathmini wenyewe pindi mgogoro unapoibuka.

Kuna aina kuu sita za migogoro ya watumiaji wa ardhi vijijini ambazo ni:-

i. Migogoro Kati ya Wakulima na Wafugaji;

ii. Migogoro Kati ya Wafugaji na Hifadhi;

iii. Migogoro kati ya Wanavijiji na Wamiliki wa Migodi;

iv. Migogoro kati ya Wanavijiji na Wamiliki wa Mashamba Makubwa (Wawekezaji);

v. Migogoro ya Mipaka kati ya Vijiji na Wilaya; na

vi. Migogoro ya Wanavijiji na Miji Inayopanuka.

Ufafanuzi wa kina wa migogoro hiyo na namna wizara inavyoishughulikia upo kwenye **Kiambatisho Na. 1.**

## SHUKRANI

***108. Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu inashughulikia majukumu mbalimbali ambayo ni mtambuka. Ni mategemeo yangu kwamba, Bunge litaendelea kuwa na mtazamo chanya na kuipa kipaumbele sekta ya ardhi kwa ujumla ili kuiwezesha kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

***109. Mheshimiwa Spika,*** mafanikio ya Wizara yangu yametokana na kuwepo kwa ushirikiano kati ya Serikali na Wadau wa Maendeleo zikiwemo taasisi za fedha za kimataifa, nchi wahisani, taasisi zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini. Wadau hao ni pamoja na Benki ya Dunia, Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa (UN-HABITAT), Shirika la Maendeleo la Ujerumani; na Serikali za Denmark, Sweden, Uholanzi na Uingereza kupitia Mradi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara.

***110. Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa George Simbachawene (Mb), kwa kunisaidia katika kutekeleza majukumu yangu. Pia napenda kumshukuru Katibu Mkuu Bw. Alphayo Japani Kidata, na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Selassie David Mayunga kwa ushirikiano mkubwa

wanaonipa. Nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Makamishna Wasaidizi na Wasajili Wasaidizi wa kanda, viongozi wa taasisi zilizo chini ya Wizara, watumishi na wataalamu wote wa sekta ya ardhi kwa kunisaidia katika kutimiza majukumu yangu kwa ufanisi. Naomba kila mmoja wetu aendelee kutekeleza majukumu yake kwa kujielekeza katika kuiwezesha ardhi kuwaondolea wananchi umaskini. Natambua kuwa Wizara yangu haina nyenzo na rasilimali za kutosha kutimiza matarajio ya Watanzania, lakini hata kwa kutumia rasilimali chache zilizopo kwa uangalifu tutatoa mchango mkubwa kwa Taifa.

**HITIMISHO**

***111. Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa fedha 2014/15 Wizara imeazimia kutekeleza Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Sheria za Ardhi uliohuishwa mwaka 2013 (SPILL 2013); na Mpango Mkakati wa Wizara wa miaka mitano (2012/13 - 2016/17) ili kufikia malengo yaliyoainishwa kwenye Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) na MKUKUTA II ambayo kwa pamoja yanalenga kufikia malengo makuu ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025.

***112. Mheshimiwa Spika,*** kwa hali hiyo Wizara imejipanga kutayarisha mipango ya kuendeleza miji na vijiji na kuisimamia, kupanga matumizi ya ardhi, kupima ardhi, kuhakiki milki, kusajili na kutoa hati ili kuwezesha kuwepo kwa usalama wa milki. **Natoa rai kwa mamlaka na asasi mbalimbali kutoa ushirikiano unaotakiwa kuhakikisha kuwa ardhi inaziwezesha sekta zote ili kufikia malengo ya maisha bora kwa kila Mtanzania.**

**MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2014/15**

***113. Mheshimiwa Spika,*** ili Wizara yangu iweze kutekeleza kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2014/15, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kama ifuatavyo:-

**Mapato ya Serikali Shilingi 61,320,005,000**

° Matumizi ya Mishahara Shilingi

° Matumizi Mengineyo (OC) Shilingi 42,933,854,000

**Jumla Matumizi ya Kawaida (A) Shilingi 54,470,753,480**

° Fedha za Ndani Shilingi 21,000,000,000
° Fedha za Nje Shilingi 13,379,977,000

**Jumla Matumizi ya Miradi ya Maendeleo (B) Shilingi 34,379,977,000**

Jumla ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Miradi ya Maendeleo (A+B) ni **Shilingi 88,850,730,480.**

***114. Mheshimiwa Spika,*** napenda kukushukuru tena wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara www.ardhi.go.tz.

***115. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Profesa Anna Tibaijuka kwa hotuba yako. Hoja imetolewa na imeungwa mkono ahsante sana. *(Makofi)*

Naliwatambua Madiwani wa Muleba lakini walikuwa hawajafika, kama mmefika, pale mlipo naomba msimame na wageni wengine wote kutoka Muleba. Karibuni sana, mmeona kazi nzuri inayofanywa na Waheshimiwa Wabunge wenu, Mheshimiwa Charles Mwijage na Profesa Anna Tibaijuka. Karibuni sana Dodoma, mtakaporudi Muleba msalimieni Mkuu wenu wa Wilaya, Mheshimiwa Kipuyo alifanya kazi nzuri sana Kongwa atawasaidieni pia. *(Makofi)*

Katika hatua hii, nilimuahidi Mheshimiwa Mchungaji Msigwa kwamba nitampa nafasi, muda wenyewe umeisha jaribu kutumia dakika moja au mbili.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) ambayo sina sababu ya kuisoma. Wakati wa uchangiaji wa Wizara ya Mambo ya Nje unaendelea hapa, Mheshimiwa Naibu Spika ulinituhumu kana kwamba nafanya jambo ambalo halistahili kufanyika ndani ya Bunge na kwa kweli kitendo kile kimeniletea usumbufu sana kwa familia yangu na wapiga kura wangu wa Iringa Mjini. Aliyekuwa anajaribu kukukemea wakati unajaribu kuitetea Serikali alikuwa ni Mheshimiwa Lema lakini ulinitaja mimi kwa makosa.

Naomba Mwongozo wako au usahihishe tu na Mheshimiwa Lema yuko hapa na *Hansard* iweke kumbukumbu sahihi mimi sikufanya kosa lolote, naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nikushukuru sana Mchungaji Msigwa kwa maneno uliyoyasema lakini nisahihishe neno moja kwamba nilikuwa nikitetea Serikali hapana, nilikuwa nafanya kazi yangu kama kiongozi wa mhimili huu wa

Bunge kuhusiana na ripoti iliyokuwa imesomwa mbele ya Bunge letu Tukufu na maudhui yake ambayo kimsingi hayakuwa sahihi kwa kweli na sote tunakubaliana katika hilo na nilikuwa natoa ushauri tu kwamba ni vizuri Kambi ya Upinzani inapoleta maoni yake au Kamati yakawa ni maoni kweli ya Kamati.

Nimewahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati najua maana ya maoni ya watu wengi. Mahali pa watu wengi huwezi kukuta mambo fulanifualni yakawepo, yuko mtu ataona tu atasema hapana, mbona hiki hakijakaa sawasawa lakini mkikaa wachache mara nyingi ni rahisi kupenyeza mawazo ambayo kumbe labda siyo sahihi sana kama ambavyo mngeshirikishana, huo ndiyo ulikuwa ushauri wangu wa ujumla.

Sasa wakati nikitoa ushauri huo, palikuwa na vurugu na kelele nyingi ambayo ni tabia ambayo imeanza kuzuka katika Bunge letu kwamba mtu fulani akiwa anaongea mambo ambayo mtu mwingine huyafurahii sana, unaanza kupiga kelele na kumzomea kama vile tuko sokoni, utaratibu ambao siyo mzuri sana, Wabunge ni kuvumiliana. Tumewahi kusema mara kadhaa kwamba ukiwa Mbunge ni lazima uwe na ngozi ngumu, ni lazima uweze kukaa na kusikiliza hata mawazo ambayo ni tofauti na ya kwako.

Nitoe mfano mdogo, asubuhi alisimama Mheshimiwa Kombo na yupo sasa hivi hapa, akasema ninyi Watanganyika, ninyi Watanganyika sitaki kurudia alisema nini. Baadaye alisimama Mheshimiwa Keissy akasema ninyi Wazanzibar, hakufika hata hatua mbili, kulitokea nini? Kwa hiyo, maana yake ni kwamba ukiwa unaweza kurusha madongo lazima uwe tayari na wewe wakati mwingine yanaporushwa kwako ukatulia, ukasikiliza, ndiyo maana ya Bunge. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nikuombe radhi Mheshimiwa Msigwa kwa yalitokea, vurugu hizi zilitokea katika mazingira hayo, sasa mimi kwa haraka haraka tu niliona kama ni wewe ndiye unayehusika na nikakuonya mara mbili maana Kanuni zinasema hivyo, Kanuni zinasema Spika ukiona kama kuna Mbunge anafanya fujo unamtaja kwa jina kwanza na unamtaja mara ya pili ikibidi, sasa ikifika mara ya tatu basi Kanuni zinachukua nafasi yake.

Kwa hiyo, tuwiane radhi na niwaombe tu wale ambao wanapenda kurusha maneno ambayo hayana sababu na kadhalika haifai, tusikilizane na tuchukuliane kwa upendo.

Hata nilipokwenda kutoa jezi hii ili kuja kwenye Kamati ya Bunge Zima, Mheshimiwa Lema hakusimama kama Wabunge wengine wote. Utaratibu huo pia ningependa kuukemea, siyo vizuri, tushirikiane na tufanye kazi vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hiyo, naomba niahirishe shughuli za Bunge sasa hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 2.00 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano, Tarehe 28 Mei, 2014, Saa Tatu Asubuhi)*